# JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## MKOA WA RUVUMA

## KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 20/02/2024

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Tunduru
S. L. P. 74,
57180 **Songea**

**Tel: +255 025-2602256 / 2602238**
**Fax: +255 025-2602144 / 2602128**
**Email**: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**Tovuti**: www.ruvuma.go.tz

**FEBRUARI, 2024**

**YALIYOMO**

YALIYOMO....2

3.0 MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28/12/2022 MKOA WA RUVUMA ....6

4.0 A. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28 DISEMBA 2022. ....27

MAPENDEKEZO YA KUGAWA HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU ILI KUPATA HALMASHAURI ZA WILAYA MBILI (2) YATAKAYOWASILISHWA KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC). ....39

6.0 MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025....81

7.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KISEKTA....88

7.1 UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA) ....88

7.1.1 SEKTA YA KILIMO ....88

7.1.2 SEKTA YA USHIRIKA....94

7.1.3 SEKTA YA MIFUGO ....100

7.1.4 SEKTA YA UVUVI....105

7.1.5 SEKTA YA MALIASILI NA UTALII ....109

7.2 VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI ....111

7.3 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE....118

7.3.10 HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024....129

7.4 ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI ....133

7.5 UTUMISHI NA UTAWALA....166

8.0 TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA ....168

8.1 WAKALA WA HIFADHI YA CHAKULA KANDA YA SONGEA (NFRA) ....168

8.3 SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ....199

8.5 WAKALA MAJI MIJINI NA VIJIJINI (RUWASA) ....................................................213

8.6 MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA (SOUWASA)..224

8.7 TAARIFA YA OFISI YA ARDHI MKOA WA RUVUMA. ..........................................226

8.8 MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA - MKOA WA RUVUMA ..................232

8.9 TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA OFISI YA AFISA MADINI MKAZI RUVUMA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DISEMBA, MWAKA 2023/2024 ..................233

8.10 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI - TAARIFA YA UMWAGILIAJI MKOA WA RUVUMA..........................................................................................................238

8.11 IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI - TAARIFA YA UTENDAJI KAZI JULAI MOSI, 2022 – JUNI 30, 2023 ..........................................................................248

8.12 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA BANDARI - BANDARI ZA ZIWA NYASA ..........................................................................................257

8.13 TAARIFA YA EWURA OFISI YA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI KIKAO CHA RCC RUVUMA. ........................................................................................262

8.14 WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI - TANZANIA (TARURA).......269

8.15 TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY- (TANROADS) – RUVUMA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ........................................................................277

8.16 WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA................................................284

I. MAOMBI YA UANZISHWAJI WA KONGANI YA VIWANDA VYA MAZAO YA MISITU MADABA.........................................................................................284

II. OMBI LA MISITU YA HIFADHI YA NAMATUI NA LIHUHU KUTANGAZWA KAMA MISITU YA LINDI MAJI (CATCHMENT FOREST)......................................286

III. OMBI LA KUREKEBISHA MPAKA WA HIFADHI YA LIHANJE ILI KUTOA ENEO KWA WANANCHI...........................................................................................287

9.0 TAARIFA ZA VIKAO VYA KAMATI ZA WILAYA (DCC) .......................................288

9.1 WILAYA YA NAMTUMBO ......................................................................................288

9.2 WILAYA YA SONGEA.............................................................................................296

9.3. WILAYA YA MBINGA..............................................................................................306

9.4 WILAYA YA NYASA................................................................................................320

## 2.0 AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 20 FEBRUARI, 2024

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 28/12/2022
4. Utekelezaji wa yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 28/12/2022.
5. Maombi ya kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.
6. Taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2022/2023, 2023/2024 kuishia tarehe 31, Desemba 2022.
7. Taarifa ya Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.
8. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kisekta
    - Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Maliasili na Ushirika)
    - Viwanda, Biashara na Uwekezaji
    - Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii
    - Elimu na Mafunzo ya Ufundi
9. Taarifa za Utekelezajai wa shughuli za Taasisi na Mashirika ya umma.
    - Wakala wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Songea (**NFRA)**
    - Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA)** Mkoa wa Ruvuma.
    - Benki Kuu ya Tanzania - Tawi La Mtwara Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Mkoa wa Ruvuma 2022/23
    - Shirika la Umeme Tanzania **(TANESCO)**
    - Wakala maji Mijini na Vijijini (**RUWASA**)
    - Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (**SOUWASA)**
    - Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.
    - Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - Mkoa wa Ruvuma
    - Taarifa ya Utendaji Kazi wa Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma kwa Kipindi cha Mwezi Julai Hadi Disemba, Mwaka 2023/2024
    - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Taarifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma
    - Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani
    - Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari **(TPA)** Ziwa Nyasa

- Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **(EWURA)** – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
- Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini **(TARURA)**
- Wakala wa Barabara Tanzania **(TANROAD)**
- Wakala Wa Huduma Za Misitu Tanzania **(TFS)**
    - Maombi ya Uanzishwaji wa Kongani ya Viwanda vya Mazao ya Misitu Madaba.
    - Ombi la Misitu ya Hifadhi ya Namatui na Lihuhu Kutangazwa Kama Misitu ya Lindi Maji (Catchment Forest).
    - Ombi la Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Lihanje Ili Kutoa Eneo kwa Wananchi.

10. Taarifa za Kamati za Ushauri za Wilaya **(DCC)**
    - Wilaya ya Namtumbo;
    - Wilaya ya Songea;
    - Wilaya ya Mbinga;
    - Wilaya ya Nyasa.
    - Wilaya ya Tunduru;
11. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
12. Kufunga Kikao.

**3.0 MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28/12/2022 MKOA WA RUVUMA**

**1.0 WALIOHUDHURIA**

| **NA.** | **JINA** | **WADHIFA** | **NAFASI** |
|---|---|---|---|
| 1. | Col. Laban Elias Thomas | Mkuu wa Mkoa | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Stephen M. Ndaki | Katibu Tawala Mkoa | Katibu |
| 3. | Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Nyasa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jonas W. Mbunda | Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Benaya Z. Kapinga | Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daimu Iddi Mpakate | Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama | Mbunge wa Jimbo la Madaba | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jackline Msongozi (Mb) | Mbunge Viti Maalumu | Mjumbe |
| 10. | Mhe.Vita R. Kawawa | Mbunge wa Jimbo la Namtumbo | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Dkt. Thea M. Ntara | Mbunge Mwakilishi Kundi la Vyuo | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Pololet K. Mgema | Mkuu wa Wilaya ya Songea | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dkt. Julius K. Ningu | Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Julius Sunday Mtatiro | Mkuu wa Wilaya ya Tunduru | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Aziza Mangosongo | Mkuu wa Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 16. | Dr. Louis K. Chomboko | Katibu Tawala Msaidizi Afya | Mjumbe |
| 17. | Ndg. Jumanne A. Mwankhoo | Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu | Mjumbe |
| 18. | Ndg Joel M. Mbewa | Katibu Tawala Msaidizi MMI | Mjumbe |

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 19. | Ndg. Bakari A. Mketo | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali watu | Mjumbe |
| 20. | Ndg. Eng. Gilbert D. Simya | Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu | Mjumbe |
| 21. | Ndg. Juma N. Fuluge | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Elimu | Mjumbe |
| 22. | Ndg. Joseph K. Martin | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi ITI | Mjumbe |
| 23. | Ndg. Onesmo Ngao | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Hairu H. Musa | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Michael L. Mbano | Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Stewart Nombo | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Teophanes T. Mlelwa | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Kelvin K. Mapunda | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Mbinga | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Desderius O. Haule | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Simon Kapinga | Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Juma Alfan Pandu | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |
| 32. | Dkt. Frederick Sagamiko | Mkurugenzi wa Manispaa Songea | Mjumbe |
| 33. | Ndg. Jimson Mhagama | Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Nyasa | Mjumbe |
| 34. | Ndg. Ambokile Paul | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 35. | Ndg. Chiza C. Marando | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | Mjumbe |
| 36. | Ndg. Juma Haji Juma | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 37. | Ndg. Khashim S. Lugome | Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Songea. | Mjumbe |
| 38. | Ndg. Grace S. Quintine | Mkurugenzi wa Mji Mbinga | Mjumbe |
| 39. | Adv. Sajidu I. Mohamed | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Mjumbe |
| 40. | Mhe. Hassan Zidadu Kungu (Mb) | Mbunge - Jimbo la Tunduru Kaskazini | Mjumbe |

### 1.1 WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA

| NA | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jenista Mhagama (Mb) | Mbunge – Jimbo la Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Judith Kapinga (Mb) | Mbunge Mwakilishi Kundi la Vijana Taifa | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Mariam M. Nyoka (Mb) | Mbunge Viti Maalum | Mjumbe |
| 4. | Ndg. Jeremiah Sendoro | Katibu Tawala Msaidizi – Uchumi na Uzalishaji | Mjumbe |

### 1.2 KAMATI YA ULINZI NA USALAMA MKOA:

| | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ajuaye W Mhowa | Kaimu Mshauri Jeshi la Akiba Mkoa | Mwalikwa |
| 2. | Ndg. Jones Mndeme | Kaimu Afisa Usalama Mkoa | Mwalikwa |
| 3. | Saci – Tununasya Adam | Afisa Uhamiaji Mkoa | Mwalikwa |
| 4. | SSP Kulwa Kabota | Kaimu Kamanda wa Magereza Mkoa | Mwalikwa |
| 5. | Ndg. Hamza Y. Mwenda | Kamanda Takukuru Mkoa | Mwalikwa |
| 6. | ACP Marco Chillya | Ag. Kamanda wa Polisi Mkoa | Mwalikwa |
| 7. | Iman Mwakingwe | S/O - RSO | Mwalikwa |

### 1.3 MAKATIBU TAWALA WA WILAYA:

| | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Ndg. Pendo Daniel | Katibu Tawala Wilaya Songea | Mwalikwa |
| 2 | Ndg. Paulo N. Lugongo | Kaimu Katibu Tawala wilaya Nyasa | Mwalikwa |
| 3 | Ndg. Augustino S. Maneno | Kaimu Katibu Tawala Wilaya Tunduru | Mwalikwa |
| 4 | Ndg. Aden H. Nchimbi | Katibu Tawala Wilaya Namtumbo | Mwalikwa |
| 5 | Salma A. Kipande | Kaimu Katibu Tawala Wilaya Mbinga | Mwalikwa |

### 1.4 WAALIKWA KUTOKA SEKRETARIETI YA MKOA:

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Theresia R. Mselenga | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi | Mwalikwa |
| 2. | Albano Midelo | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini | Mwalikwa |
| 3. | Ndg. Hakimu Mafuru | Afisa Elimu Taaluma | Mwalikwa |
| 4. | Ndg. Romanusi Komba | Mtaalamu wa TEHAMA | Mwalikwa |
| 5. | Ndg. Basil S. Amuli | Afisa Uvuvi | Mwalikwa |
| 6. | Dr. Magafu Majura | Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Songea | Mwalikwa |
| 7. | Ndg. Yahya A. Madenge | Afisa Tehama | Mwalikwa |
| 8. | Ndg. Walumbe Komba | Mkuu wa Kitengo TEHAMA | Mwalikwa |
| 9. | Ndg. Musa Nkolabigawa | Katibu wa Mkuu wa Mkoa | Mwalikwa |
| 10. | Ndg. Africanus Chale | Afisa Misitu Mkoa | Mwalikwa |
| 11. | Ndg. Mariam Juma | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mwalikwa |
| 12. | Ndg. Onesmo F. Gama | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mwalikwa |
| 13. | Ndg. Sunday S. Hebuka | Mtakwimu | Mwalikwa |
| 14. | Ndg. Adelini Komba | Mkaguzi wa Ndani Serikali za Mitaa | Mwalikwa |
| 15. | Ndg. Grace Mafuru | Afisa Tawala Mkoa | Mwalikwa |
| 16. | Ndg. Frank Hosea | Mkadiriaji Majenzi | Mwalikwa |
| 17. | Ndg. Onesmo Mpuya | Afisa Kilimo Mkoa | Mwalikwa |
| 18. | Ndg. Amandus Chilumba | Afisa Serikali za Mitaa | Mwalikwa |
| 19. | Ndg. Leonida Ngira | Mhasibu | Mwalikwa |
| 20. | Ndg. Leodigard Riziki | Afisa Manunuzi | Mwalikwa |
| 21. | Ndg. Humphrey Millanzi | Afisa Manunuzi | Mwalikwa |
| 22. | Issa O. Nyika | EDMO | Mwalikwa |
| 23. | Ndg. Upendo Kinemela | Afisa Hesabu | Mwalikwa |
| 24. | Ndg. Denis W. Chiwangu | Mtakwimu | Mwalikwa |
| 25. | Ndg. Amina Tindwa | Afisa Serikali za Mitaa | Mwalikwa |
| 26. | Ndg. Shadrack Mhina | Afisa TEHAMA | Mwalikwa |
| 27. | Ndg. Aniceth Gaima | Afisa Ugavi | Mwalikwa |
| 28. | Ndg. Beatrice Gauza | Afisa Ushirika | Mwalikwa |
| 29. | Ndg. Abdallah M. Saidi | Mchumi | Mwalikwa |

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 30. | Ndg. Godson Chale | Mhasibu | Mwalikwa |
| 31. | Ndg. Osmund Luoga | TEHAMA | Mwalikwa |
| 32. | Ndg. Atemista S. Ponera | RMA | Mwalikwa |
| 33. | Ndg. Geofrey Rwela | Afisa TEHAMA | Mwalikwa |
| 34. | Ndg. Christa Njerekela | LUCODIA | Mwalikwa |
| 35. | Ndg. Margareth S. Mvula | Msaidizi wa Ofisi | Mwalikwa |
| 36. | Ndg. Slivia Mgina | Msimamizi na Mwendesha Ofisi | Mwalikwa |
| 37. | Ndg. Jeni J Mkomwa | RMA | Mwalikwa |
| 38. | Ndg. Happfania Ndomba | RMA | Mwalikwa |
| 39. | Ndg. Mwaija A. Ponera | RMA | Mwalikwa |
| 40. | Ndg. Robert A. Luoga | RMA | Mwalikwa |
| 41. | Ndg. Hawa Selemani | RMA | Mwalikwa |
| 42. | Ndg. Seligius A. Ngahi | Kitengo cha Sheria | Mwalikwa |
| 43. | Ndg. Siwema M. Gama | RMA | Mwalikwa |
| 44. | Ndg. Marietha L. Komba | MMO | Mwalikwa |
| 45. | Ndg. Miraji Swedi | Mhasibu | Mwalikwa |
| 46. | Ndg. Philemoni Bossy | Mkaguzi wa Ndani | Mwalikwa |
| 47. | Ndg. Goretha Komba | MMO | Mwalikwa |
| 48. | Ndg. Schlostica Mahundi | MMO | Mwalikwa |
| 49. | Ndg. Mathias R. Tilia | Afisa Taaluma Mkoa | Mwalikwa |
| 50. | Ndg. Emmanuel R. Komba | Afisa Biashara | Mwalikwa |
| 51. | Ndg. Victory G. Nyenza | Afisa Ustawi wa Jamii | Mwalikwa |
| 52. | Ndg. Denis Luambano | Mhasibu | Mwalikwa |
| 53. | Ndg. Zuberi R. Msham | Afisa Utumishi | Mwalikwa |
| 54. | Ndg. Salumu Kateula | Afisa Utumishi | Mwalikwa |
| 55. | Ndg. Anthony Luoga | Kaimu Afisa Elimu | Mwalikwa |
| 56. | Ndg. Lydia A. Makua | Afisa Tawala | Mwalikwa |
| 57. | Ndg. Ahmad H. Namohe | Afisa Utumishi | Mwalikwa |
| 58. | Ndg. Benedicto G. Ndiyani | Mlinzi wa Mkuu wa Mkoa | Mwalikwa |
| 59. | Ndg. Musa Nkolabigawa | Msaidizi wa Mkuu wa Mkoa | Mwalikwa |

**1.5 VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA:**

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Komred Oddo Mwisho | Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi | Mwalikwa |
| 2 | Mohamed Rashid Lawa | Kaimu Katibu wa Chama cha Mapinduzi | Mwalikwa |
| 3 | Hemed Ahmad Chale | MNEC | Mwalikwa |
| 4 | Ndg. Richard Tawe | Katibu ACT | Mwalikwa |
| 5 | Ndg. Hamisi H. Kaisi | Katibu CUF | Mwalikwa |
| 6 | Ndg. Oswald A. Nyoni | Katibu TLP | Mwalikwa |
| 7 | Ndg. Paulo M. Geho | KATIBU TADEA | Mwalikwa |
| 8 | Ndg. Ally S. Mapunda | Mwenyekiti TADEA | Mwalikwa |
| 9 | Ndg. Ibrahimu M. Komba | Katibu UPDP | Mwalikwa |
| 10 | Ndg. Juma Mtokani Haule | Mwenyekiti NCCR Mageuzi | Mwalikwa |

**1.6 WAALIKWA:**

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Bosco Mwingira | Afisa Mipango - Tunduru | Mwalikwa |
| 2. | Ndg. Eliseus Mhelela | Meneaja TANESCO MKOA | Mwalikwa |
| 3. | Ndg. Baraka J Mungai | Mhandisi Miradi – White City | Mwalikwa |
| 4. | Ndg. Emanuel Snagalali | Meneja Consessions FDT Iringa | Mwalikwa |
| 5. | Ndg. Edmund Lubinga | Mjumbe Timu ya CSR | Mwalikwa |
| 6. | Ndg Prosper R Luambano | Afisa Mipango - Madaba | Mwalikwa |
| 7. | Ndg Elizabeth Ngongi | REO – TCCIA | Mwalikwa |
| 8. | Eng. Bathlomeo Matwiga | Ag. RM RUWASA | Mwalikwa |
| 9. | Ndg Seif A Mgonja | RRO – NIDA | Mwalikwa |
| 10. | Ndg Rose C Kangu | Mhifadhi – Makumbusho | Mwalikwa |
| 11. | Ndg.Josephine Bazombanza | Katibu Machinga | Mwalikwa |
| 12. | Ndg Kauli G Makasi | RPO – NIS | Mwalikwa |
| 13. | Ndg Paschal Masatu | Afisa Mipango – Mbinga TC | Mwalikwa |
| 14. | Ndg Jerome Asifiwe | Kaimu Afisa Mipango Nyasa | Mwalikwa |
| 15. | Ndg Edwin Msavangwa | Mneja PSSSF – Ruvuma | Mwalikwa |
| 16. | Ndg Rosemary Ngonyani | Mwenyekiti – TWCC Ruvuma | Mwalikwa |
| 17. | Ndg Osward Mfaeka | RM – SIDO | Mwalikwa |
| 18. | Ndg Clement Abadyawe | RM – TEMESA | Mwalikwa |
| 19. | Ndg Peter Stanslausi | Mchumi - BOT | Mwalikwa |
| 20. | Ndg Ngapona Israel | Ag RM – NHC | Mwalikwa |
| 21. | Ndg Oppurtuna Makero | Agg RPOCS | Mwalikwa |
| 22. | Ndg Magreth Salia | NFRA | Mwalikwa |
| 23. | Ndg Mwangapiti, Lusajo R | HRO – VETA | Mwalikwa |
| 24. | Eng. Patrick Kibasa | MD – SOUWASA | Mwalikwa |
| 25. | Ndg Ahmad Issa | MHANDISI - NAMIS | Mwalikwa |
| 26. | Ndg Simon Kinyunyu | Mhandisi - NAMIS | Mwalikwa |
| 27. | Ndg Imani Kalembo | MENEJA - ITMCU LTD | Mwalikwa |
| 28. | Ndg Musa A. Manjaule | M/ KITI - TAMCU LTD | Mwalikwa |
| 29. | Ndg Zainabu Mbaruku | DPLO - SONGEA DC | Mwalikwa |

| NA. | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 30. | Ndg Issa H. Mlela | DFC – SONGEA | Mwalikwa |
| 31. | Ndg Kamwanga Tamigwe | AG HOST | Mwalikwa |
| 32. | Ndg Zawadi H. Nyoni | DCDO - SONGEA DC | Mwalikwa |
| 33. | Ndg Devsdedith | GONELAMENDA - AFISA MAJI | Mwalikwa |
| 34. | Ndg Shabani J | MHIFADHI - SHAMBA LA MITI MPEPO TFS | Mwalikwa |
| 35. | Ndg Edwini Msavanawa | MENEJA - PSSSF | Mwalikwa |
| 36. | Ndg Sothery S. Nchimbi | Ag. DEO[P] - SONGEA DC | Mwalikwa |
| 37. | Ndg Ernest Nzunguru | MENEJA - BOT MTWARA | Mwalikwa |
| 38. | Ndg Lilian Ndunguru | Ag. DHRO - SONGEA DC | Mwalikwa |
| 39. | Ndg Dickson Mbugano | Ag. RMO - MADINI RUVUMA | Mwalikwa |
| 40. | Ndg Philipo B. Ndiwauru | M/KITI - MBIFACU LTD | Mwalikwa |
| 41. | Ndg Mollasco Ngowe | MENEJA - LIPARAMBA | Mwalikwa |
| 42. | Ndg Faustine J. Magafu | PP - LIPARAMBA GRHO | Mwalikwa |
| 43. | Ndg Howard Mwakalinga | GAMO - USIMAMIZI MALI ZA SERIKALI | Mwalikwa |
| 44. | Ndg Karim S. Ally | MENEJA KANDA - EWURA MBEYA | Mwalikwa |
| 45. | Ndg Archmoses. Mosdes | K/ MENEJA - TBA | Mwalikwa |
| 46. | Ndg Juma N. Mwanga | MENEJA - SONAMCU | Mwalikwa |
| 47. | Ndg Hance John | MENEJA - NHIF | Mwalikwa |
| 48. | Ndg Frank T. Kapinga | GAMO - USIMAMIZI WA MALI ZA SERIKALI | Mwalikwa |
| 49. | Ndg Ephatar Mlavi | MANAGER - TANROADS | Mwalikwa |
| 50. | Ndg Yasin Hamad | MANAGER - NAMIS | Mwalikwa |
| 51. | Ndg Faraja M Komba | AG. MANAGER - MBIFACU LTD | Mwalikwa |
| 52. | Ndg Amina Pilly | MGCO - SONGEA MC | Mwalikwa |
| 53. | Ndg Mwantumu Athmani | RSM. NBS | Mwalikwa |
| 54. | Ndg Asajile John | MENEJA - TCRA | Mwalikwa |
| 55. | Ndg Zabron Walwa | MENEJA - TRA | Mwalikwa |
| 56. | Ndg Herbert A. Mwoleka | Ag. ACL - ARDHI MKOA | Mwalikwa |
| 57. | Ndg Antony Mesebe | KAMANDA KITUO SONGEA TAWA | Mwalikwa |
| 58. | Ndg Obed B. Mwasomola | REV - NAMTUMBO DC | Mwalikwa |
| 59. | Ndg Kyomo A.B | MPCO - SONGEA MC | Mwalikwa |
| 60. | Ndg Epaphras Tengamamba | CA –HC SONGEA | Mwalikwa |

## 1.7 SEKRETARIETI YA KIKAO

| | JINA LA MJUMBE | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Deogratius Sibula | Afisa Mifugo | Sekretarieti |
| 2 | Paul Msemwa | Afisa Kilimo | Sekretarieti |
| 3 | Romanus F. Komba | Afisa TEHAMA | Sekretarieti |
| 4 | Sunday S. Hebuka | Mtakwimu | Sekretarieti |
| 6 | Sophia Gama | Katibu Muhtasi | Sekretarieti |
| 7 | Xaveria Mlimila | Afisa Maendeleo ya Jamii | Sekretarieti |
| 8 | Denis Chiwangu | Mtakwimu | Sekretarieti |

## 2.0 AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28 DESEMBA 2022

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021
4. Utekelezaji wa yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021.
5. Taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2021/2022, 2022/2023 kuishia tarehe 30, Novemba 2022 na Taarifa ya Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.
6. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kisekta
    - Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Maliasili na Ushirika)
    - Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Taarifa ya Timu ya Kuchambua, Kuandaa na Kuainisha Mfumo Mzuri wa Uwajibikaji Kwa Jamii (**CSR**) wa Wachimbaji wa Madini Mkoa wa Ruvuma
    - Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii
    - Elimu na Mafunzo ya Ufundi
    - Utumishi na Utawala
7. Taarifa za Utekelezajai wa shughuli za Taasisi na Mashirika ya umma.
    - Wakala wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Songea (**NFRA)**
    - Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA)** Mkoa wa Ruvuma.
    - Ofisi ya Taifa ya Takwimu **(NBS**) Mkoa wa Ruvuma - Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022.
    - Shirika la Umeme Tanzania **(TANESCO)**
    - Wakala maji Mijini na Vijijini (**RUWASA**)
    - Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (**SOUWASA)**
    - Wakala wa Misitu **(TFS)** - Taarifa ya Shamba la Miti Wino na Mpepo
    - Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – LIKUYU SEKAMAGANGA
    - Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.

- Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani
- Taasisi ya Kuzuia na Kupamaba na Rushwa **(TAKUKURU)**
- Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania **(TAA)** Mkoa wa Ruvuma
- Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **(EWURA)** – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
- Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari **(TPA)** Ziwa Nyasa
- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (**TCRA)**

**8.** Taarifa za Kamati za Ushauri za Wilaya **(DCC)**
- Wilaya ya Songea;
- Wilaya ya Tunduru;
- Wilaya ya Mbinga;
- Wilaya ya Namtumbo;
- Wilaya ya Nyasa.

9. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
10. Kufunga Kikao.

**3.0 MUHTASARI NA. RCC: 01/12/2022 KUFUNGUA KIKAO**

**UTANGULIZI**

Katibu Tawala wa Mkoa alianza kwa kuwakaribisha wajumbe na waalikwa wote katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa ni kikao kinachoendeshwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 iliyoanzisha Sekretarieti za Mikoa. Aidha alieleza kuwa kikao hiki ni muhimu kwani ndio kikao cha juu kabisa cha ushauri na maamuzi mbalimbali katika ngazi ya Mkoa. Baada ya utangulizi huo alifanya utambulisho kwa wajumbe na waalikwa wa kikao na kisha alimkaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa (Mwenyekiti) kwa ajili ya kufungua kikao.

**Kufungua kikao**

Katika hotuba yake ya ufunguzi Mwenyekiti alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki muhimu kwa maendeleo na ustawi wa Mkoa wetu. Pia aliwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuunga mkono juhudi za **Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Mwenyekiti

aliwajulisha wajumbe kuwa katika kikao hiki tutapata fursa ya kujadili masuala muhimu yaliyotokana na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichopita cha tarehe **29 Desemba, 2021**,taarifa mbalimbali zikiwemo za Utekelezaji na Mpango na Bajeti ya Mkoa kwa mwaka **2021/2022**, mwaka **2022/2023** kuishia **Novemba, 2022** pamoja na Maandalizi ya Bajeti ya Mwaka **2023/2024.**Taarifa nyingine ni Utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Ruvuma, shughuli za Uchumi na Uzalishaji, Shughuli za Biashara, Viwanda na Uwekezaji, Taarifa ya Timu ya Kuandaa, Kuchambua na Kuainisha Mfumo mzuri wa uwajibikaji kwa Jamii (CSR) kwa wachimbaji wa Madini Mkoa wa Ruvuma, Hali ya Elimu, Afya, Maji, Ardhi, misitu nk.

Mwenyekiti alieleza kuwa msimu wa kilimo wa 2022/23 umeshawadia, hivyo aliwasihi wananchi wote kuanza maandalizi mapema kwa kwa kuzingatia kalenda ya kilimo. Kwa upande wa Serikali ya mkoa wa Ruvuma tunaendelea na uratibu wa mfumo wa ugawaji na usambazaji wa Mbolea za Ruzuku kwa wakulima kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA). Mfumo huu unaenda sambamba na zoezi la kusajili wakulima wote, Mawakala na makampuni yanayoingiza mbolea. Wakulima waliosajiliwa tangu zoezi la usajili lilipoanza tarehe 15 Agosti 2022 kupitia vitabu ni wakulima **261,235** kati ya hao **250,493** wameshaingizwa kwenye mfumo na wameanza kupata mbolea, aidha zoezi la Usajili linaendelea.

Natoa wito kwa Viongozi wa ngazi zote kuhakikisha wanasimamia zoezi la upatikanaji wa mbolea kwa wakulima. Aidha Mkoa utaendelea kusimamia na kuimarisha mfumo stakabadhi ghalani ili kuhakikisha wakulima wanauza mazao yao kwa bei nzuri kama ambavyo tumefanya katika msimu uliopita wa kilimo.

Katika msimu wa **2021/2022** mkoa ulivuna tani **1,256,362** za mazao ya chakula, mahitaji ya chakula katika mkoa ni tani **469,172,** hivyo kuwa na ziada ya tani **787,190** ambazo zimeendelea kuuzwa kwa lengo la kuwaongezea wananchi kipato. Kutokana na uzalishaji huo mkoa wetu umeendelea kushika nafasi ya kwanza Kitaifa katika uzalishaji wa mazao ya nafaka. Nitoe wito kwa wakulima kujitahidi kutumia mvua zilizoanza kunyesha kupanda mazao kwa wakati.

Nitumie fursa hii pia kuwakumbusha kuwa suala la kusimamia Mapato yatokanayo na kodi pamoja na Ushuru ni la kila mmoja kwani fedha hiyo hutumika katika kujenga miradi ya maendeleo, hivyo ni wajibu wetu sote kusimamia vyema ukusanyaji wa

maduhuli na mapato ya serikali, kubuni vyanzo vipya na kupanua wigo wa Mapato na kuhimiza watu kudai risiti au kutoa risiti wanapouza na kununua bidhaa. Niwapongeze Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kusimamia ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka wa fedha **2021/2022** ambapo Halmashauri zote zimekusanya shilingi **21,422,972,707.68** sawa na asilimia **110.8** ya lengo la kukusanya shilingi **19,333,322,006**

Mwenyekiti alizipongeza Halmashauri zilizofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato na kuzitaka Halmashauri zote kusimamia na kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo yaliyowekwa, aidha alizitaka Halmashauri kuziba mianya yote ya upotevu na ukwepaji wa kulipa mapato.

Vilevile Mwenyekiti alimpongeza Meneja wa Mkoa na watumishi wote wa TRA kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya Mapato ndani ya Mkoa ambapo mwaka **2021/2022** mkoa umeweza kukusanya shilingi **19,850,805,877.61** ya lengo la makusanyo ya shilingi **19,553,627,572.74** sawa na asilimia **101.52.**

Mkoa pia unaendelea kuimarika kiuchumi kwa kuimarika kwa miundombinu, shughuli za uzalishaji mali, biashara na uwekezaji shughuli za uchimbaji madini hasa makaa ya mawe, maboresho ya uwanja wa Ndege wa Songea na pamoja na biashara na mikoa na nchi jirani za Msumbiji na Malawi.

Kwa upande wa Miundombinu ya elimu**,** Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa Sisi sote ni mashahidi wa namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt.Samia Suluhu Hassan alivyoamua kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa miundombinu ya elimu ambapo tumeshuhudia kwa mwaka **2021/2022** Mkoa ulipokea kiasi cha shilingi **7,700,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya **11** za Sekondari katika Halmashauri zote **8** za Mkoa wa Ruvuma. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa shule ya Mkoa ya Wasichana inayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi **bilioni 3,000,000,000.00**. Ujenzi wa shule hizi upo katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi mwezi Januari **2023**. Aidha mwezi **Oktoba, 2022** Serikali ilitoa kiasi cha sh. **3,120,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **156** ya wanafunzi wa Kidato cha kwanza kwa mwaka **2023** ambapo yamekamilika na yako tayari kupokea wanafunzi wa mwezi **Januari, 2023**.

Haya ni mafanikio makubwa kwa kuwa sasa tuna uhakika wa utoshelevu wa miundombinu ya shule kwa ajili ya kupokea wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2023 bila changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa pamoja na viti na meza. Hivyo Mwenyekiti alitoa maelekezo kuwa watoto wote wanaostahili kuanza darasa la kwanza wakiwemo wa watoto wa kike ifikapo Januari, **2023** waandikishwe na kuanza masomo bila kukosa. Kwa upande wa wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza mwaka **2023** nao hakuna kikwazo tena cha uhaba wa vyumba vya madarasa hivyo wote waripoti bila kukosa.

Pia alieleza mafanikio katika sekta ya afya ambapo Mkoa umefanikiwa kujenga Vituo vya Afya **12** kupitia fedha za Tozo, Serikali Kuu na Wafadhili kwa gharama ya shilingi **Bilioni. 7,845**, nyumba **9** za watumishi wa Afya **(3 in 1)** kwa gharama ya shilingi **Milioni 856.585**, majengo **matatu (3)** ya huduma za dharura (EMD) Kwa gharama ya Shilingi Milioni **900**, jengo moja **(1)** la wagonjwa mahututi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa gharama ya shilingi **milioni 250**.

Mkoa unaendelea na ujenzi wa **Hospitali 5** za Wilaya ya Nyasa, Mbinga DC, Namtumbo DC, Madaba DC na Songea DC kwa gharama ya Shilingi **Bilioni 3.4**. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa awamu ya kwanza kwa gharama ya shilingi **2,700,000,000.00**. Ujenzi huu unahusisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la mionzi na nyumba ya mtumishi. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya imeendelea kuimarika, kwani upatikanaji umeongezeka na kufikia **asilimia 96**.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua kikao cha Baraza la Ushauri la Mkoa **(RCC)** mnamo saa **3: 53** asubuhi.

### 4.0 MUHTASARI NA. RCC: 02/12/2022: KURIDHIA AGENDA

Agenda za kikao zilisomwa mbele ya kikao na Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia na kuzipitisha kuwa agenda za kikao.

**5.0 MUHTASARI NA. RCC: 03/12/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) CHA TAREHE 29/12/2021**

Wajumbe wa kikao walipokea na kupitisha muhtasari ulioandaliwa ukurasa kwa ukurasa na kufanya marekebisho katika maneno machache yaliyokuwa na makosa ya kiuchapaji.

**6.0 MUHTASARI NA. RCC: 04/12/2022: UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) CHA TAREHE 29/12/2021**

Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021 iliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe walipitia yatokanayo na kujadili yafuatayo:-

**i. TANESCO Mkoa wa Ruvuma kukamilisha miradi ya usambazaji wa Umeme**

Wajumbe walihoji kuhusu kuchelewa kwa utelekezaji wa usambazaji wa umeme mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na awamu ya tatu mzunguko wa pili unaotekelezwa na Tanesco na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Meneja TANESCO alieleza kuwa kuna Vijiji **32** Mbinga na Vijiji **24** Namtumbo na Tunduru vimepata Umeme. Kikao kilielekeza kuwa taarifa ya utekelezaji wa usambazaji wa umeme ianishe upatikanaji na usamabazaji wa umeme kwa kila Halmashauri.

**ii. Mkakati wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana katika Halmashauri ya Madaba.**

Wajumbe walihoji juu ya hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana katika Halmashuri ya Wilaya ya Madaba, kwani ilielekezwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichofanyika tarehe 12/01/2021 katika ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Katibu Tawala Mkoa alielekezwa kuunda Timu ya maandiko ili kupata fedha kutoka vyanzo vingine. Pia iandaliwe taarifa ya uchangiaji kwa kila Halmashauri na ujenzi uanze kwa kutumia fedha ambazo tayari zimeshakusanywa.

Kikao kilielekeza kuwa Mkoa uongezwe wigo wa ukusanyaji wa fedha kwa kukusanya shilingi 7 kwa kilo katika mazao ya mahindi, korosho,kahawa, Tumbaku, Soya, Ufuta na Mbaazi, badala ya kukusanya katika zao moja tu ambalo ni ufuta. Lengo ni kukusanya fedha nyingi na kufanikisha ujenzi wa Shule ya Wasichana. Wajumbe waliwekezwa utaratibu wa kukusanya fedha kutoka katika zao la mahindi ufanyike kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

**iii. Kuchelewa kwa ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA).**

Wajumbe walihoji kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine SUA kuwa na kampasi yake Mkoa wa Ruvuma. Wajumbe walielekezwa kuwa kwa sasa SUA wanaendeleza maeneo yao kwa ajili ya mazoezi ya vitendo ambayo ni upandaji wa miti (Madaba), Wanyamapori (DarajaMbili Tunduru) na Utalii (Nyasa). Aidha, kikao kilijulishwa kuwa Chuo cha Uhasibu Arusha kinajenga Kampasi yake Manispaa ya Songea kupitia mradi wa BOOST kwa mikoa isiyo na vyuo vikuu. Pia kikao kiliekeza kufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini kwa wawekezaji wote waliochukua ardhi na kushindwa kuendeleza.

**iv. Wananchi kuvamia maeneo ya chanzo cha maji na hifadhi ya Mto Ruvuma na kusababisha uharibifu wa mazingira.**

Mjumbe alitoa taarifa kuwa asilimia **19** ya maji yanayoenda katika bwawa la kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere yanatoka katika Mkoa wetu hivyo basi tuagalie namna ya kupata sehemu ya CSR ili kulinda vyanzo vya maji vinavyopeleka Maji kwenye bwawa hilo hasa Mto Luegu ulioko Namtumbo. Ilielezwa kuwa ili kulinda vyanzo vya maji zoezi la upandaji miti Kimkoa litafanyika katika bonde la Mto Luegu na Bonde la Mbinga Mhalule.

## 7.0 MUHTASARI NA. RCC: 05/12/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA KWA MWAKA 2021/2022 KUISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022.

### 7.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/2022.

Taarifa iliyowasilishwa ilionyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa na Bunge kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi **244,824,103,177.53** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yalikuwa ni Shilingi **164,375,177,177.53** na miradi ya maendeleo ni Shilingi **80,448,926,000.00.** Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 246,797,526,092.16** sawa na asilimia **101.1** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 225,374,553,384.48** na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ni **Tshs 21,422,972,707.68**

**7.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2021/22**

Taarifa ilionyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri zilifanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ambapo Halmashauri ya Mji Mbinga iliongoza kwa kukusanya shilingi **2,301,641,894.14** sawa na asilimia **119.2** ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyokusanya shilingi **1,780,749,173.36** sawa na asilimia **115.8.** Aidha, Manispaa ya Songea iliongoza kwa uwingi wa mapato ambayo ilikusanya shilingi **4,912,810,519.00**, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliyokusanya shilingi **4,549,317,329.13.**

**7.3 Baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 katika kipindi cha Julai, 2021 – Juni, 2022.**

Taarifa ilionesha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika Sekta za Afya, Elimu, Utawala na Rasilimali Watu, Afya na Ustawi wa Jamii, Uchumi na Uzalishaji, Ukusanyaji wa mapato na Maduhuli ya Serikali, Usambazaji wa nishati ya Umeme, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Aidha, ziliwasilishwa Changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/2022 pamoja na Mikakati ya Kutatua Changamoto.

**Majadiliano;**

Wajumbe walipokea na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2020/2021 kuishia tarehe 30 Juni, 2022.

## 8.0 MUHTASARI NA. RCC: 06/12/2022: UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 KWA KIPINDI CHA KUISHIA NOVEMBA, 2022 (JULAI 2022 - NOVEMBA 2022)

**8.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/2023**

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2022/23 ambapo Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 271,162,170,165.83,** Kati ya fedha hizo **Tshs. 250,451,604,789.83** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu na **Tshs 20,710,565,376.00** ni makusanyo ya mapato ya ndani.

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 107,881,169,074.90** sawa na **asilimia 39.8** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 98,348,159,711.00** na makusanyo ya mapato ya ndani

ya Halmashauri ni **Tshs 9,533,009,363.90.** Matumizi hadi kufikia Novemba, 2022 yalikuwa ni **Tshs 86,096,138,613.56** sawa na **asilimia 79.8** ya fedha pokelewa.

Aidha, kiasi cha **Tshs 26,078,581,877.36** zilipelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na **Tshs. 734,295,903.05** zilipelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi katika vikundi hivyo.

Pia kikao kilijulishwa kuwa Mkoa wa Ruvuma ulipokea fedha nje ya bajeti Tshs**. 3,120,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **156 v**ya kidato cha kwanza 2023 katika shule za sekondari na kiasi cha **Tshs. 980,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vitatu na nyumba nne za watumishi wa Halmashauri.

### 8.10 TAARIFA YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Taarifa ya maandalizi ya mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliwasilishwa kwa kuainisha vipaumbele mbalimbali vya kisekta kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali iliyopo ya kimkoa na kitaifa ili kuhakikisha Mpango na Bajeti ya Mkoa unaendana na vipaumbele vya kitaifa vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Mpango wa II wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021- 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Kwa kuzingatia ukomo wa bajeti na vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Mkoa uliomba kuidhinishiwa makisio ya Mpango na bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24 fungu 82 Mkoa wa Ruvuma kiasi cha Shilingi **267,530,798,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Fedha hizo zinajumuisha Shilingi **180,932,942,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **86,497,856,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na Shughuli mbalimbali za maendeleo.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida.**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Ruvuma na Halmashauri zake iliwasilisha maombi ya kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **180,932,942,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **153,907,956,000.00** ni Mishahara ya watumishi na Shilingi **27,024,986,000.00** ni Matumizi Mengineyo. Aidha, bajeti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni Shilingi **6,419,485,740.00** na Shilingi **174,513,456,260.00** ni bajeti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo**

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zake uliwawasilisha maombi ya kuidhinishiwa makadirio ya jumla ya Shilingi. **86,497,856,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi. **34,172,550,000.00** ni fedha za ndani, Shilingi. **45,511,358,000.00** ni fedha za nje na Shilingi **6,813,948,000.00** ni Fedha za maendeleo za mapato ya ndani. Fedha maendeleo kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni Shilingi. **2,285,721,000.00** na Halmashauri ni Shilingi. **84,212,135,000.00**.

**Majadiliano**

Wajumbe wa kikao walipokea kujadili na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2022/2023 kuishia tarehe 30 Novemba, 2022. Pamoja na maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Wajumbe walijadiliana na kukumbushia kuweka kwenye bajeti au kufanya ufuatiliaji wa ahadi za viongozi ikiwemo ujenzi wa Vituo vya Afya Chiwanda na Lituhi Nyasa. Pia walishauri kuwa utengaji wa fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu uzingatie maeneo yenye uhitaji badala ya kujenga katika shule ambazo hazina mahitaji hayo.

**9.0 MUHTASARI NA. RCC: 07/12/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO VIWANDA, BIASHARA, UWEKEZAJI, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA)**

Taarifa ya sehemu ya uratibu wa shughuli za uchumi na uzalishaji iliwasililishwa kwenye kikao ambapo iliangazia utekelezaji wa Taarifa za Kilimo. Katika sekta ya kilimo taarifa ilielezea hali ya upatikanaji wa pembejeo hususani mbegu na mbolea, upimaji wa udongo pamoja na matumizi sahihi ya mbolea. Taarifa nyingine zilizowasilishwa ni pamoja na Utekelezaji wa shughuli za Mifugo, Ushirika, Uvuvi, Maliasili, Utalii, Wanyamapori na utekelezaji wa shughuli za Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**Majadiliano**

Wajumbe walijadiliana kuhusu upatikanaji wa mbolea ya Ruzuku kwenye maeneo ya vijijini hasa katika Wilaya ya Namtumbo na Tunduru ambako hakuna mawakala. Wajumbe walishauri Serikali iangalie utaratibu wa kuhakikisha wakulima wote wanapata mbolea. Maafisa Ugani wawatembelee wakulima katika maeneo yao na kuacha kuwatoza fedha pindi wanapowapatia huduma au ushauri. Kuhusu upatikanaji wa boti za mkopo wataalam wa uvuvi walihimizwa kutoa elimu ya kutosha kwa wavuvi

ili waweze kunufaika na mikopo hiyo. Wilaya ya Tunduru iliomba kupatiwa mahindi ya bei nafuu kwani uzalishaji wa korosho umekuwa sio mzuri zimezalishwa tani **15,000** tu.

Baada ya majadiliano wajumbe wa kikao walipokea na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda, Uwekezaji, Uvuvi, Maliasili na Ushirika).

## 9.0 MUHTASARI NA. RCC: 08/12/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFYA.

Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii iliwasilishwa ambapo ilikuwa inahusu utoaji wa huduma za afya, mapokezi ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya, utoaji wa huduma ya afya ya uzazi na mtoto, hali ya chanjo, huduma za vvu na ukimwi, mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa (iCHF), utoaji wa huduma za lishe na mambo yanayosababisha lishe duni.

**Majadiliano.**

Kwa upande wa afya ilisisitizwa kuendelea kuboresha eneo la lishe ambalo linasababisha udumavu wa mwili na akili, wananchi waendelee kusisitizwa kutumia maziwa, matunda na vyakula vingine kwa ajili ya lishe na kupanda miti ya matunda. Pia iongezwe nguvu kwenye eneo la iCHF kwani mwitikio wa wananchi bado uko chini.

Pia Wajumbe walipendekeza kuwa mkazo uwekwe katika kukamilisha miradi ya afya ambayo imekuwa ni ya muda mrefu kama zahanati ya Mdundualo Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

## 11.0 MUHTASARI NA. RCC: 9/12/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI.

Taarifa ya elimu iliyowasilishwa ilihusu Idadi ya taasisi za elimu katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Novemba, 2022, Elimu ya Awali na Msingi, Elimu ya Sekondari, Walimu wa Shule za Sekondari hadi Novemba, 2022 na Walimu wa Ajira Mpya. Taarifa nyingine ni hali ya ufaulu wa kidato cha nne, Miundombinu ya shule za sekondari na Msingi, Utekelezaji wa Programu ya Elimu Bila Malipo, Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Mendeleo Sekta ya Elimu, Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Ufundi Stadi na Michezo

**Majadiliano;**

Wajumbe walitaka kufahamu kuhusu mkakati wa uliopo wa ujenzi wa Tawi la Chuo kikuu cha Sokoine katika wilaya ya Tunduru, Madaba na Nyasa. Aidha Wajumbe walisisitiza Wilaya na Halmashauri kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanye umri stahiki wanaandikishwa bila kukosa. Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya Mbunge wa Jimbo la Nyasa alileta ombi la maalum la kuomba kusaidiwa kujenga uwanja wa michezo katika Wilaya ya Nyasa. Wajumbe waliridhia kuchangia ujenzi huo na kumtaka Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya kuwaalika kwenye kuchangia atakapoandaa hafla ya uchangiaji.

## 12.0 MUHTASARI NA. RCC: 10/12/2022: TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA.

**Upande wa taarifa za Taasisi na Mashirika zilizowasilishwa zilihusu: -**

- Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wakala wa Hifadhi ya Chakula – NFRA kuanzia Julai 1, 2022 hadi 30 Novemba 2022;
- Taarifa ya Utendaji Kazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Ruvuma;
- Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Mkoa wa Ruvuma - Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022;
- Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Shirika la Umeme (TANESCO);
- Taarifa ya Mamlaka ya Maji Vijiji – RUWASA kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Novemba, 2022
- Taarifa ya utendaji kazi kutoka Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Songea kwa kipindi cha Julai 2021 – Novemba 2022;
- Taarifa ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) - Taarifa ya Shamba la Miti Wino na Mpepo,
- Taarifa ya Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) - Likuyusekamaganga,
- Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Ardhi Mkoa wa Ruvuma;
- Taarifa ya Utendaji Kazi wa Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani;
- Taarifa Mapambano Dhidi ya Rushwa kwa Maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma;
- Taarifa Fupi ya Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Songea - Disemba, 2022.

Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ikielezea Chimbuko la udhibiti, Majukumu ya EWURA na nyenzo za udhibiti kazi na kazi zilizofanyika Mkoa wa Ruvuma kati ya Januari 2022 mpaka Disemba 2022 na

- Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Bandari kwa Kipindi cha Julai 2021 Hadi Juni 2022.

**Majadiliano**

Wajumbe walijadiliana kuhusu taarifa za Mashirika ambapo TANESCO walitakiwa wanapotoa taarifa za utekelezaji wa mradi wa REA zioneshe utekelezaji kwa kila Wilaya/Halmashauri. EWURA walitakiwa kuendelea kutoa elimu ya fursa ya mikopo ya kujenga vituo vya mafuta katika maeneo ya Vijijini. Taarifa ya Utekelezaji wa Idara na Taasisi.

## 13.0 MUHTASARI NA. RCC: 11/12/2022: TAARIFA ZA KAMATI ZA USHAURI ZA WILAYA (DCC)

Taarifa za Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) ziliwasilishwa ambapo kwa upande wa Wilaya ya Songea taarifa zilizojadiliwa zilihusu miradi ya maendeleo, upatikanaji wa mbolea, utunzaji wa mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuomba eneo la TANROAD lililopo Kijiji cha Mtepa – Madaba litumike kama Soko la Mazao, Pia waliwasilisha Maombi ya kubadilisha eneo la maonyesho ya Nanenane kutoka Kata ya Msamala kwenda Kata ya Mwengemshindo ambapo wajumbe waliridhia ombi hilo na kuwataka wataalam kukamilisha mchakato wa mabadiliko hayo.

Taarifa ya Wilaya ya Tunduru ilihusu maombi ya kuanzisha Halmashauri mpya wilayani Tunduru hoja ya wafugaji wa ng'ombe holela, changamoto ya tembo na upatikanaji wa mbolea ya ruzuku.

Taarifa ya Wilaya ya Mbinga ilihusu Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Matumizi wa Halmashauri Mbinga Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Taarifa za utekelezaji wa Taasisi na Mamlaka na Mashirika na Chama Kikuu cha Ushirika – MBIFACU.

Taarifa ya Wilaya ya Namtumbo ilihusu Mapendekezo ya uundaji wa maeneo mapya ya Kiutawala, kitarafa, kikata, na vijiji pamoja na mapendekezo ya kugawa jimbo la

Namtumbo. Ombi maalum la kuongezewa eneo la utawala mamlaka ya mji mdogo wa Lusewa na pendekezo la kuligawa jimbo la Namtumbo.

Taarifa ya Wilaya pamoja na mambo mengine ilijulisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa 2022/2023, Mrejesho wa Bajeti 2022/2023, Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 cha Robo ya kwanza 2022/2023, Taarifa ya Utekelezaji wa mango na bajeti ya mwaka 2022/2023 cha Robo ya kwanza 2022/2023

**Majadiliano**

Kuhusu kubadilisha matumizi ya eneo la nanenane wajumbe walielekeza mchakato uendelee na eneo mbadala la maonyesho lipatikane. Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ilielekezwa kuwa eneo walilloomba kwa ajili ya ujenzi wa soko kwa sasa limekabidhiwa kwa TBA hivyo kama wanalihitaji waombe kwa TBA.

**14.0 MUHTASARI NA. RCC: 12/12/2022: MENGINEYO**

Hakukuwa na mengineyo yaliyowasilishwa kwenye kikao.

**15.0 MUHTASARI NA. RCC: 13/12/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti kabla ya kufunga kikao alieleza mambo yafuatayo; kufikia tarehe **05 Januari 2022** Halmashauri zote zinatakiwa kukamilisha ujenzi na kukabidhi madarasa **500** yanayojengwa kupitia fedha za maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya **UVICO – 19. (Mradi Na. 5441 TCRP).** Vilele mabweni matatu yanayojengwa kupitia mpango huo ujenzi wake ukamilike kufikia tarehe **20 Machi 2022.** Mwenyekiti alieleza pia juu ya changamoto zilizopo katika maendeleo na uendelezaji wa timu ya majimaji, alieleza kuwa timu ya majimaji haiwezi kusonga mbele bila kuwa na mkakati wa kuindeleza hususani kifedha, hivyo Mkoa pamoja na wadau wote tunatakiwa kutafuta namna ya kuifanya timu ijiendeshe kama Kampuni. Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa **9:46 Alasiri**

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| **…………………………..** | **……………………………** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

……………………………………………

**4.0 A. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28 DISEMBA 2022.**

| NA | AGENDA | HOJA | MUHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Ndogo Matumizi Mengineyo SK** | **15,940,597,552.90** | **15,568,824,080.88** | **97.7** | **15,240,004,495.05** | **97.9** | **328,819,585.83** |
| | | | | | | | |
| **D** | **Matumizi Mengineyo Mapato ya Ndani** | | | | | | |
| 1. | MBINGA DC | 1,962,632,046.94 | 1,962,632,046.94 | 100.0 | 1,365,846,743.10 | 69.6 | 596,785,303.84 |
| 2. | MADABA DC | 801,471,600.00 | 801,471,600 | 100.0 | 801,471,600 | 100.0 | 0 |
| 3. | SONGEA DC | 1,402,500,000.00 | 1,373,215,988.04 | 97.9 | 1,373,215,988.04 | 100.0 | 0 |
| 4. | SONGEA MC | 3,773,113,194.40 | 3,305,349,234.00 | 87.6 | 3,291,076,338.64 | 99.6 | 14,272,895.36 |
| 5. | NYASA DC | 1,032,120,256 | 938,452,401 | 90.9 | 938,452,401 | 100.0 | 0 |
| 6. | MBINGA TC | 1,033,630,200.90 | 1,033,630,201 | 100.0 | 1,009,377,589 | 97.7 | 24,252,612.07 |
| 7. | NAMTUMBO DC | 1,474,400,000 | 1,586,317,574 | 107.6 | 1,087,926,601 | 68.6 | 498,390,973.00 |
| 8. | TUNDURU DC | 2,797,240,000 | 2,565,540,517.02 | 91.7 | 2,410,546,142.96 | 94.0 | 154,994,374.06 |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/2023 | Kiasi Kilichotolewa hadi Juni, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Juni, 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Juni, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Mapato Ndani** | **14,277,107,298.24** | **13,566,609,561.90** | **95.02** | **12,277,913,403.57** | **90.50** | **1,288,696,158.33** |
| | **Jumla Matumizi Mengineyo (SK na OSR)** | **30,217,704,851.14** | **29,135,433,642.78** | **96.42** | **27,517,917,898.62** | **94.45** | **1,617,515,744.16** |
| | **Jumla Kuu** | **183,020,034,042.64** | **182,113,389,879.28** | **99.50** | **180,492,969,375.12** | **99.11** | **1,620,420,504.16** |

### 5.1.3 BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

Katika mwaka wa fedha **2022/23,** Mkoa wa Ruvuma Fungu 82 uliidhinishiwa shilingi **94,463,460,527.72** kwa ajili kutekeleza miradi/shughuli za Maendeleo, kati ya fedha hizo **shilingi 37,331,740,829.**66 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu, shilingi **48,567,936,557.31** ni fedha za Nje ( Foreighn) na **shilingi 8,563,783,140.75 ni** Mapato ya ndani ya Halmashauri.

Hadi kufikia **30 Juni, 2023** Mkoa na Halmashauri umepokea kiasi cha shilingi **86,110,799,310.23** sawa na asilimia **91.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi **38,381,893,637.26** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu, shilingi **39,620,412,741.88** ni fedha za nje na mapato ya ndani ya Halmashauri ni shilingi **8,108,492,931.09.**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, Mkoa na Halmashauri ulitumia shilingi **63,995,797,040.20** sawa na asilimia **74.3** ya fedha pokelewa na kubaki na jumla ya shilingi **22,115,002,270.03**. Jedwali Na. 04 linaonesha mchanganuo wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 5.1.4 Bajeti na Mapokezi ya Fedha hadi Juni, 2023

**Jedwali Na. 4: Bajeti, Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Maendeleo Halmashauri Hadi Juni 2023 kwa mwaka wa fedha 2022/223**

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/2023 | Kiasi Kilichotolewa hadi Juni 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Juni 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Juni 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | **Fedha za Maendeleo kutoka Serikali Kuu** | | | | | | |
| 1. | **RS** | 1,699,695,000.00 | 1,699,695,000.00 | 100.0 | 1,699,695,000.00 | 100.0 | 0.00 |
| 2. | MBINGA DC | 6,438,895,714.42 | 6,438,895,714.42 | 100.0 | 4,797,091,062.42 | 74.5 | 1,641,804,652.00 |
| 3. | MADABA DC | 2,696,899,000.00 | 2,512,625,059.36 | 93.2 | 1,559,477,664.91 | 62.1 | 953,147,394.45 |
| 4. | SONGEA DC | 3,425,999,000.00 | 4,389,935,000.00 | 128.1 | 3,185,240,500.11 | 72.6 | 1,204,694,499.89 |
| 5. | SONGEA MC | 6,877,161,030.24 | 6,877,161,030.24 | 100.0 | 6,351,120,330.24 | 92.4 | 526,040,700.00 |
| 6. | NYASA DC | 4,110,371,000.00 | 3,382,539,210.27 | 82.3 | 2,578,161,410.27 | 76.2 | 804,377,800.00 |
| 7. | MBINGA TC | 2,278,369,000.00 | 2,245,452,364.66 | 98.6 | 2,163,172,518.25 | 96.3 | 82,279,846.41 |
| 8. | NAMTUMBO DC | 2,876,434,000.00 | 3,772,117,447.12 | 131.1 | 1,974,763,447.12 | 52.4 | 1,797,354,000.00 |
| 9. | TUNDURU DC | 6,927,917,085.00 | 7,063,472,811.19 | 102.0 | 4,548,507,664.52 | 64.4 | 2,514,965,146.67 |
| | **Jumla ya Fedha za Maendeleo kutoka Serikali Kuu** | **37,331,740,829.66** | **38,381,893,637.26** | **102.8** | **28,857,229,597.84** | **75.2** | **9,524,664,039.42** |
| | | | | | | | |
| **B** | **Fedha za Maendeleo kutoka Nje** | | | | | | |
| 1. | RS | 695,972,679.00 | 301,926,507.65 | 43.4 | 295,868,351.65 | 98.0 | 0.00 |
| 2. | MBINGA DC | 8,850,305,837.75 | 6,321,215,775.34 | 71.4 | 4,477,592,366.64 | 70.8 | 1,843,623,408.70 |
| 3. | MADABA DC | 3,369,317,000.00 | 2,497,293,930.45 | 74.1 | 1,785,293,930.45 | 71.5 | 712,000,000.00 |
| 4. | SONGEA DC | 5,852,680,000.00 | 3,755,020,502.86 | 64.2 | 2,197,840,225.25 | 58.5 | 1,557,180,277.61 |
| 5. | SONGEA MC | 4,557,064,867.00 | 3,338,877,569.54 | 73.3 | 2,559,065,230.54 | 76.6 | 779,812,339.00 |
| 6. | NYASA DC | 5,957,811,000.00 | 4,921,681,754.80 | 82.6 | 3,855,327,022.30 | 78.3 | 1,066,354,732.50 |
| 7. | MBINGA TC | 3,437,948,000.00 | 2,422,596,993.00 | 70.5 | 1,791,594,878.00 | 74.0 | 631,002,115.00 |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/2023 | Kiasi Kilichotolewa hadi Juni 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Juni 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Juni 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8. | NAMTUMBO DC | 7,171,504,250.00 | 5,705,191,439.52 | 79.6 | 3,176,835,319.54 | 55.7 | 2,528,356,119.98 |
| 9. | TUNDURU DC | 8,675,332,923.56 | 10,356,608,268.72 | 119.4 | 8,273,130,987.76 | 79.9 | 2,083,477,280.96 |
| | **Jumla Maendeleo Nje** | **48,567,936,557.31** | **39,620,412,741.88** | **81.6** | **28,412,548,312.13** | **71.7** | **11,207,864,429.75** |
| **C** | **Maendeleo Mapato ya Ndani** | | | | | | |
| 1. | MBINGA DC | 2,222,120,602 | 2,222,120,602 | 100.0 | 1,962,632,046.94 | 88.3 | 259,488,555.06 |
| 2. | MADABA DC | 324,054,550.40 | 169,722,000.00 | 52.4 | 168,605,500.00 | 99.3 | 1,116,500.00 |
| 3. | SONGEA DC | 730,400,000.00 | 819,609,600.00 | 112.2 | 748,636,200.00 | 91.3 | 70,973,400.00 |
| 4. | SONGEA MC | 1,931,857,892.35 | 1,931,857,892.35 | 100.0 | 1,472,031,719.95 | 76.2 | 459,826,172.40 |
| 5. | NYASA DC | 329,144,044.00 | 388,958,596.17 | 118.2 | 359,958,596.17 | 92.5 | 29,000,000.00 |
| 6. | MBINGA TC | 608,046,000.00 | 531,075,913.00 | 87.3 | 434,124,629.17 | 81.7 | 96,951,283.83 |
| 7. | NAMTUMBO DC | 509,600,000 | 306,138,189 | 60.1 | 271,315,000 | 88.6 | 34,823,189.00 |
| 8. | TUNDURU DC | 1,908,560,052 | 1,739,010,138.57 | 91.1 | 1,308,715,438 | 75.3 | 430,294,700.57 |
| | **Jumla Maendeleo Mapato Ndani** | **8,563,783,140.75** | **8,108,492,931.09** | **94.7** | **6,726,019,130.23** | **83.0** | **1,382,473,800.86** |
| | **Jumla ya Fedha za Miradi ya Maendeleo** | **94,463,460,527.72** | **86,110,799,310.23** | **91.2** | **63,995,797,040.20** | **74.3** | **22,115,002,270.03** |

**5.1.5 Miradi/shughuli Muhimu zilizotekelezwa kwa Kipindi cha Julai, 2022 Hadi Juni 2023.**

**SEKTA YA ELIMU**

i. Ujenzi wa shule mpya 12 za Msingi za kisasa zenye madarasa ya awali na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule za Msingi 44 kwa gharama ya shilingi **7.291,000,000.00.**

ii. Ujenzi wa shule mpya **9** za Sekondari kwa gharama ya Shilingi **5,044,975,443.00** kupitia programu ya SEQUIP mzunguko wa pili (Tunduru 2, Mbinga DC 1, Mbinga TC 1, Songea DC 1, Songea MC 1, Nyasa 1, Madaba 1, Namtumbo 1).

iii. Upanuzi wa shule za sekondari nane (8) za Emmanuel Nchimbi, Mpitimbi, Jenesta Mhagama, Pamoja, Msonya, Mchoteka, Mataka na Tunduru kwa gharama ya shilingi **4,447,300,000.00;**

iv. Upanuzi wa Shule za Sekondari Kidato cha 5 na 6 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule ya sekondari Maposeni, Namabengo na Nandembo ili ziweze kupokea wanafunzi wa kidato cha Tano kwa mwaka 2023. Mradi huu huu unahusisha ujenzi wa madarasa 13, mabweni 5 na vyoo matundu 20 kwa ufadhili wa kampuni ya Barick Gold Mine kwa Gharama ya shilingi **986,000,000.00;**

v. Ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Walimu 12 kupitia GPE LANES II kwa Gharama ya shilingi milioni **264,000,000.00;**

vi. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa ya elimu ya awali, matundu 18 ya vyoo vya wanafunzi na samani katika shule ya msingi Kifaguro, Ndirima na Luhindo kupitia GPE LANES kwa gharama ya shilingi **173,475,000.00;**

vii. Ujenzi wa Vyumba **156** vya madarasa katika shule za sekondari kwa gharama ya shilingi **3,120,000,000.00** na kufanikiwa kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na hiyo kufanya wanafunzi wote wanafaulu kujiunga kidato cha kwanza;

viii. Ujenzi wa Bweni moja katika Sekondari ya Darajambili kwa gharama ya Tshs. **142,934,332.00** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA);

ix. Ujenzi wa shule ya wasichana ya Mkoa ya Dkt.Samia Suluhu Hassan awamu ya pili kwa gharama ya shilingi **1,100,000,000.00**. Awamu hii inahusisha ujenzi wa vyumba 4 vya madadara na ofisi moja, chumba cha TEHAMA, Maktaba, nyumba 3 za walimu na mabweni 4 ya wanafunzi;

x. Serikali imeanza ujenzi wa chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu katika Halmashauri ya wilaya ya Songea Kata ya Liganga awamu ya kwanza kwa gharama ya Tshs. **1,000,000.00.** Mradi huu unahusisha ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 40, madarsa 10, na nyumba moja ya Walimu (3 in 1);

xi. Ujenzi wa nyumba **10** za walimu kwa gharama ya shilingi **950,000,000.00**

xii. Kujenga miundombinu ya elimu katika shule ya sekondari Maposeni na Pambazuko, kwa gharama ya shilingi **573,649,131.00**. Ujenzi huu unajumuisha ujenzi wa majengo mawili ya utawala, madarasa 4, maabara moja, maktaba 1, chumba cha TEHEMA kimoja, matundu ya vyoo 8 na ukamilishaji wa madarasa manne (4);

xiii. Ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi (2) na matundu 20 ya vyoo vya wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari kwa gharama ya shilingi **290,000,000.00** kwa ajili ya kuongeza miundombinu ya kidato cha tano kwa Halmashauri zilizoshinda vigezo vya **EP4R.**

xiv. Ugawaji wa vishikwambi **9,079** kwa walimu wote wa shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya kuboreshaji ufundishaji.

**SEKTA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

- Ukarabati wa hospitali kongwe ya Tunduru kwa Gharama shilingi **900,000,000.00**
- Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa katika eneo la Mwengemshindo kwa gharama ya Shilingi **3,075,831,600.24**
- Ujenzi wa jengo moja (**1)** la wagonjwa mahututi kwa gharama ya shilingi milioni **250,000,000.00** katika Halmashauri ya Mbinga DC.
- Kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kwani upatikanaji umeongezeka kutoka **93% (2021)** hadi **96%** mwaka, 2023.
- Mkoa umepokea mashine ya CT scan na digital X-ray kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa na mashine ya X-Ray kwa ajili ya hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.
- Mkoa umepokea magari matatu **(7)** ya wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa (**1**), Tunduru (**2**), Songea DC (**1**), Namtumbo (**1**) na hospitali ya rufaa ya Mkoa (1)
  (i) Ukamilishaji wa Ujenzi wa Hospitali **ya** Halmashauri ya Wilaya Nyasa, Mbinga na Madaba kwa gharama ya Shilingi **2,700,000,000.00**

- Ujenzi wa nyumba 6 za Watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa gharama ya Shilingi **440,000,000.00**
- Kujenga vituo vya afya **14** kwa gharama ya shilingi Bilioni **9.345** ambayo vina majengo ya huduma ya mama na mtoto pamoja na majengo ya upasuaji.
- Ujenzi umekamilisha zahanati **21** kwenye Halmashauri saba (**7**) kwa gharama ya shilingi bilioni 1**.05.**
- Ujenzi wa nyumba **9** za watumishi wa Afya kwa gharama ya shilingi Milioni **856.585.**
- Utekelezaji wa mradi endelevu wa usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini (SRWSSP) katika zahanati **11** kwa gharama ya Shilingi milioni **569**.

**UBORESHAJI WA MAKAZI YA VIONGOZI NA OFISI**

- Ujenzi wa ya majengo **2** ya Utawala ya Halmashauri kwa gharama ya shilingi **1,488.402,504.81** (Mbinga DC, Nyasa DC);
- Ujenzi wa Nyumba za viongozi na watumishi wa Mkoa na Halmashauri kwa gharama ya shilingi **665,000,000.00** ikiwemo nyumba ya makazi ya Katibu Tawala wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Songea na Mbinga;
- Ukarabati wa nyumba **2** za makazi ya Mkuu wa wilaya ya Tunduru na Namtumbo kwa gharama ya Shilingi **200,000,000.00**
- Ujenzi wa ofisi **2** za Maafisa Tarafa ya Nakapanya na Madaba kwa gharama ya Shilingi **160,000,000.00** Tunduru na Madaba;
- Ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa Songea club kwa gharama ya shilingi **250,000,000.00;**

## 5.2 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/24.

### 5.2.1 BAJETI YA MKOA

Mkoa na Halmashauri zake kwa mwaka wa fedha 2023/24 uliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi **278,982,735,095.16** katika matumizi ya kawaida na maendelo. Kati ya fedha hizo shilingi **192,490,045,567.00** ni fedha za matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi **86,492,689,528.16** ni fedha za maendeleo. Katika fedha za matumizi ya kawaida shilingi **161,149,790,479.00 ni** fedha za mishahara na shilingi **31,340,255,088.00** ni matumizi mengineyo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi **43,389,815,000.00** ni ruzuku toka serikali kuu, shillingi **35,094,935,915.76** toka kwa

wafadhili wa maendeleo na shilingi **8,007,938,612.40** kutoka makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023 Mkoa na Halmashauri zake umepokea na kukusanya shilingi **153,037,944,010.47 sawa** na asilimia **54.86** ya makisio ya bajeti. Kati ya fedha hizo shilingi **84,823,179,532.89** ni fedha za mishahara, shilingi **18,795,956,073.59** ni fedha za matumizi mengineyo kutoka serikali kuu na mapato ya ndani, shilingi **49,418,808,403.99** ni fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo **shilingi 32,631,674,108.48** ni fedha za miradi kutoka serikali kuu, shilingi **11,331,554,686.17** ni fedha za miradi kutoka kwa wafadhili na shilingi **5,455,579,609.34** ni fedha za miradi kutoka mapato ya ndani yua Halmashauri.

Kwa upande wa matumizi hadi Desemba 31, 2023 jumla ya shilingi **129,177,635,716.57** zimetumika sawa asilimia **84.41** ya fedha pokelewa**.** Kati ya fedha hizo shilingi **84,807,763,532.49** ni fedha za mishahara, shilingi **14,693,709,228.61** ni fedha za matumizi mengineyo kutoka serikali kuu na mapato ya ndani, shilingi **29,676,162,955.47** ni fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo **shilingi 17,449,660,318.65** ni fedha za miradi kutoka serikali kuu, shilingi **8,673,650,538.60** ni fedha za miradi kutoka kwa wafadhili na shilingi **3,552,852,098.22** ni fedha za miradi kutoka mapato ya ndani yua Halmashauri.

**Jedwali Na 4: Bajeti, Mapokezi na Matumizi ya Fedha mwaka wa Fedha 2023/24**

| Na | Aina ya Bajeti | Fedha idhinishwa | Kiasi pokelewa | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi | Asilimia ya Fedha Zilizotumika | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | **Bajeti ya Matumizi ya Kawaida** | | | | | | |
| 1 | Mishahara | 161,149,790,479.00 | 84,823,179,532.89 | 52.64 | 84,807,763,532.49 | 99.98 | 15,416,000.40 |
| 2 | Matumizi mengineyo | 31,340,255,088.00 | 18,795,956,073.59 | 59.97 | 14,693,709,228.61 | 78.17 | 4,102,246,844.98 |
| | **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **192,490,045,567.00** | **103,619,135,606.48** | **53.83** | **99,501,472,761.10** | **96.03** | **4,117,662,845.38** |
| **B** | **Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo** | | | | | | |
| 4 | Fedha za Maendeleo toka Serikali Kuu | 43,389,815,000.00 | 32,631,674,108.48 | 75.21 | 17,449,660,318.65 | 53.47 | 15,182,013,789.83 |
| 5 | Fedha za Maendeleo toka Nje | 35,094,935,915.76 | 11,331,554,686.17 | 32.29 | 8,673,650,538.60 | 76.54 | 2,502,139,022.90 |
| 6 | Fedha za Maendeleo Mapato ya Ndani | 8,007,938,612.40 | 5,455,579,609.34 | 68.13 | 3,552,852,098.22 | 65.12 | 1,903,136,615.44 |
| | **Jumla Fedha za Maendeleo** | **86,492,689,528.16** | **49,418,808,403.99** | **57.14** | **29,676,162,955.47** | **60.05** | **19,587,289,428.17** |
| | **JUMLA KUU** | **278,982,735,095.16** | **153,037,944,010.47** | **54.86** | **129,177,635,716.57** | **84.41** | **23,704,952,273.55** |

### 5.2.2 MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

Katika mwaka 2022/23 Mkoa na Halmashauri ulipangiwa kukusanya kiasi cha shilingi **27,870,822,000.00** na uliidhinishiwa kutumia shilingi **27,867,014,000.00** toka kwenye vyanzo mbalimbali vya fedha za mapato ya ndani. Kati ya fedha hizo, shilingi **6,447,987,969.00** ni Mapato lindwa, na shilingi **21,419,026,031.00** ni Mapato halisi. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023 Mkoa na Halmashauri imekusanya shilingi **16,674,061,141.15 (**shilingi **3,130,405,241.05** ni Mapato lindwa, na shilingi **13,543,655,900.10** ni Mapato halisi). Aidha, kwa asilimia ya ukusanyaji wa mapato ya ndani Halmashauri ya wilaya ya Tunduru inaongoza (**84.32%)** ikufuatiwa na Nyasa **(79.01%),** na Halmbashauri ya wilaya ya Mbinga (**62.59),** wakati Sekretarieti ya Mkoa ikiwa ya mwisho kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani (**23.63 %),** ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Songea (**42.58%)** na Madaba (**43.77%).** Kwa upande wa uwingi wa mapato yaliyokusanywa Halmashauri ya wilaya ya Tunduru inaongoza (shilingi **4,106,655,698.38**), ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga (shilingi **3,943,355,844.60**) na Halmashauri ya Manispaa ya Songea (shilingi **2,584,589,248.43**).

**Jedwali Na 6: Maduhuli ya Mkoa na Mapato ya Ndani ya Halmashauri hadi Desemba 31, 2023**

| Na. | Mkoa/Halmashauri | Bajeti idhinishwa 2023/24 | Makusanyo hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya makusanyo | Nafasi kwa asilimia | Nafasi kwa uwingi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Tunduru DC | 4,870,503,000.00 | 4,106,655,698.38 | 84.32 | 1 | 1 |
| 2. | Nyasa DC | 1,444,005,000.00 | 1,140,919,479.26 | 79.01 | 2 | 7 |
| 3. | Mbinga DC | 6,300,000,000.00 | 3,943,355,844.60 | 62.59 | 3 | 2 |
| 4. | Mbinga TC | 2,476,487,000.00 | 1,459,654,161.32 | 58.94 | 4 | 4 |
| 5. | Songea DC | 2,468,957,000.00 | 1,452,115,414.13 | 58.81 | 5 | 5 |
| 6. | Namtumbo DC | 2,747,631,000.00 | 1,333,731,850.78 | 48.54 | 6 | 6 |
| 7. | Madaba DC | 1,489,777,000.00 | 652,139,444.25 | 43.77 | 7 | 8 |
| 8. | Songea MC | 6,069,654,000.00 | 2,584,589,248.43 | 42.58 | 8 | 3 |
| 9. | RS | 3,808,000.00 | 900,000.00 | 23.63 | 9 | 9 |
| | **JUMLA** | **27,870,822,000.00** | **16,674,061,141.15** | **59.83** | | |

### 5.2.3 BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2023/24

Katika mwaka wa fedha **2023/24,** Mkoa na Halmashauri uliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida kiasi cha **shilingi 192,490,045,567.00** Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi 161,149,790,479.00**, ikiwa shilingi **161,054,521,999.00** toka serikali kuu na shilingi **95,268,480.00** toka mapato ya ndani ya halmashauri na Matumizi Mengineyo ni **shilingi 31,340,255,088.00,** ikiwa shilingi **13,550,881,000.00** toka serikali kuu na shilingi **17,789,374,088.00** toka mapato ya ndani ya halmashauri**.**

Hadi kufikia **31 Desemba , 2023** Mkoa na Halmashauri umepokea na kukusanya kiasi cha **shilingi 103,619,135,606.48** sawa na asilimia **53.83** ya bajeti. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi 84,823,179,532.89**, ikiwa shilingi **84,783,855,841.90** toka serikali kuu na shilingi **39,323,690.99** toka mapato ya ndani ya halmashauri na Matumizi Mengineyo ni **shilingi 18,795,956,073.59,** ikiwa shilingi **7,514,453,195.50** toka serikali kuu na shilingi **11,281,502,878.09** toka mapato ya ndani ya halmashauri**.**

Aidha, hadi kufikia **31 Desemba, 2023** Mkoa na Halmashauri umetumia kiasi cha **shilingi 99,501,472,761.10** sawa na asilimia **96.03** ya fedha pokelewa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi 84,807,763,532.49**, ikiwa shilingi **84,768,439,841.50** toka serikali kuu na shilingi **39,323,690.99** toka mapato ya ndani ya halmashauri na Matumizi Mengineyo ni **shilingi 14,693,709,228.61,** ikiwa shilingi **6,334,000,943.75** toka serikali kuu na shilingi **8,359,708,284.86** toka mapato ya ndani ya halmashauri**.**
**Jedwali Na. 03**: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia Desemba 31, 2023.

**Jedwali Na. 7. Bajeti, Mapokezi na Matumizi ya Fedha ya Kawaida hadi Desemba 31, 2023**

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | **Mishahara Serikali Kuu** | | | | | | |
| 10. | RS | 3,014,498,000.00 | 1,473,683,990.50 | 48.89 | 1,472,113,990.5 0 | 99.89 | 1,570,000.00 |
| 11. | Mbinga DC | 23,249,317,999.00 | 12,534,748,101.00 | 53.91 | 12,534,748,101.00 | 100.00 | - |
| 12. | Madaba DC | 7,555,560,000.00 | 3,935,457,000.00 | 52.09 | 3,935,457,000.00 | 100.00 | - |
| 13. | Songea DC | 16,127,854,000.00 | 9,225,982,750.00 | 57.21 | 9,225,982,750.00 | 100.00 | - |
| 14. | Songea MC | 32,950,316,000.00 | 17,238,076,200.40 | 52.32 | 17,238,076,200.00 | 100.00 | 0.40 |
| 15. | Nyasa DC | 15,755,790,000.00 | 7,917,170,200.00 | 50.25 | 7,917,170,200.00 | 100.00 | - |
| 16. | Mbinga TC | 17,202,144,000.00 | 9,012,628,500.00 | 52.39 | 8,998,782,500.00 | 99.85 | 13,846,000.00 |
| 17. | Namtumbo DC | 20,505,300,000.00 | 10,318,193,600.00 | 50.32 | 10,318,193,600.00 | 100.00 | - |
| 18. | Tunduru DC | 24,693,742,000.00 | 13,127,915,500.00 | 53.16 | 13,127,915,500.00 | 100.00 | - |
| | **Jumla Ndogo** | **161,054,521,999.00** | **84,783,855,841.90** | **52.64** | **84,768,439,841.50** | **99.98** | **15,416,000.40** |
| | | | | | | | |
| **B** | **Mishahara Mapato ya Ndani** | | | | | | |
| 2. | SONGEA MC | 95,268,480.00 | 39,323,690.99 | 41.28 | 39,323,690.99 | 100.00 | - |
| | **Jumla Ndogo** | **95,268,480.00** | **39,323,690.99** | **41.28** | **39,323,690.99** | **100.00** | **-** |
| | **Jumla Kuu** | **161,149,790,479.00** | **84,823,179,532.89** | **52.64** | **84,807,763,532.49** | **99.98** | **15,416,000.40** |
| | | | | | | | |
| **C** | **Matumizi Mengineyo Serikali Kuu** | | | | | | |
| 10. | RS | 4,467,636,000.00 | 2,448,058,695.50 | 54.80 | 2,438,073,500.00 | 99.59 | 9,985,195.50 |
| 11. | Mbinga DC | 1,163,116,000.00 | 729,955,000.00 | 62.76 | 416,778,000.00 | 57.10 | 313,177,000.00 |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | Madaba DC | 1,047,933,000.00 | 595,850,000.00 | 56.86 | 564,051,043.75 | 94.66 | 31,798,956.25 |
| 13. | Songea DC | 1,120,508,000.00 | 553,402,000.00 | 49.39 | 553,402,000.00 | 100.00 | - |
| 14. | Songea MC | 1,218,849,000.00 | 633,672,000.00 | 51.99 | 439,627,500.00 | 69.38 | 194,044,500.00 |
| 15. | Nyasa DC | 1,047,366,000.00 | 624,650,000.00 | 59.64 | 624,650,000.00 | 100.00 | - |
| 16. | Mbinga TC | 911,560,000.00 | 489,512,500.00 | 53.70 | 229,814,800.00 | 46.95 | 259,697,700.00 |
| 17. | Namtumbo DC | 1,286,833,000.00 | 640,624,000.00 | 49.78 | 268,875,100.00 | 41.97 | 371,748,900.00 |
| 18. | Tunduru DC | 1,287,080,000.00 | 798,729,000.00 | 62.06 | 798,729,000.00 | 100.00 | - |
| | **Jumla Ndogo Matumizi Mengineyo SK** | **13,550,881,000.00** | **7,514,453,195.50** | **55.45** | **6,334,000,943.75** | **84.29** | **1,180,452,251.75** |
| | | | | | | | |
| **D** | **Matumizi Mengineyo Mapato ya Ndani** | | | | | | |
| 9. | Mbinga DC | 4,116,860,388.00 | 2,434,274,796.00 | 59.13 | 1,757,659,949.00 | 72.20 | 676,614,847.00 |
| 10. | Madaba DC | 945,284,000.00 | 588,407,747.03 | 62.25 | 588,407,747.03 | 100.00 | - |
| 11. | Songea DC | 1,418,696,000.00 | 808,614,488.90 | 57.00 | 745,210,300.00 | 92.16 | 63,404,188.90 |
| 12. | Songea MC | 4,039,382,000.00 | 2,233,158,488.42 | 55.28 | 1,313,312,356.31 | 58.81 | 919,846,132.11 |
| 13. | Nyasa DC | 724,480,000.00 | 851,484,930.92 | 117.53 | 699,576,172.72 | 82.16 | 151,908,758.20 |
| 14. | Mbinga TC | 1,128,220,200.00 | 730,601,950.20 | 64.76 | 397,355,013.00 | 54.39 | 333,246,937.20 |
| 15. | Namtumbo DC | 2,347,497,000.00 | 1,192,898,386.57 | 50.82 | 950,003,766.55 | 79.64 | 242,894,620.02 |
| 16. | Tunduru DC | 3,068,954,500.00 | 2,442,062,090.05 | 79.57 | 1,908,182,980.25 | 78.14 | 533,879,109.80 |
| | **Jumla Mapato Ndani** | **17,789,374,088.00** | **11,281,502,878.09** | **63.42** | **8,359,708,284.86** | **74.10** | **2,921,794,593.23** |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba, 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Matumizi Mengineyo (SK na OSR)** | **31,340,255,088.00** | **18,795,956,073.59** | **59.97** | **14,693,709,228.61** | **78.17** | **4,102,246,844.98** |
| | **Jumla Kuu Matumizi ya Kawaida** | **192,490,045,567.00** | **103,619,135,606.48** | **53.83** | **99,501,472,761.10** | **96.03** | **4,117,662,845.38** |

### 5.2.4 BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/24

Katika mwaka wa fedha **2023/24,** Mkoa na Halmashauri uliidhinishiwa kutumia fedha za Maendeleo kiasi cha shilingi **86,492,689,528.16** **kati** ya fedha hizo **shilingi 43,389,815,000.00** kutoka Serikali Kuu, shilingi **35,094,935,915.76** kutoka Nje na **shilingi 8,007,938,612.40** toka Mapato ya ndani ya halmashauri. Hadi kufikia **31 Desemba, 2023** Mkoa na Halmashauri umepokea kiasi cha shilingi **49,418,808,403.99** sawa na asilimia **57.14** ya bajeti. Kati ya fedha hizo shilingi **32,631,674,108.48** kutoka Serikali Kuu, shilingi **11,331,554,686.17** kutoka nje na mapato ya ndani ya halmashauri ni shilingi **5,455,579,609.34.** Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023, Mkoa na Halmashauri ulitumia shilingi **29,676,162,955.47** sawa na asilimia **60.05** ya fedha pokelewa na kubaki na jumla ya shilingi **19,587,289,428.17**. Jedwali Na. 08 linaonesha mchanganuo wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/24

### 5.2.5 Bajeti, Mapokezi na Matumizi ya Fedha hadi Desemba, 2023

**Jedwali Na.8 Bajeti, Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Maendeleo RS na Halmashauri Hadi Desemba, 2023 kwa mwaka wa fedha 2023/24**

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desesmba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | **Fedha za Maendeleo kutoka Serikali Kuu** | | | | | | |
| 1. | RS | 1,890,982,000.00 | 1,760,882,000.00 | 93.12 | 290,882,000.00 | 16.52 | 1,470,000,000.00 |
| 2. | Mbinga DC | 6,773,722,000.00 | 3,214,918,810.64 | 47.46 | 978,918,810.64 | 30.45 | 2,236,000,000.00 |
| 3. | Madaba DC | 2,896,998,000.00 | 2,176,321,120.87 | 75.12 | 2,176,321,120.87 | 100.00 | - |
| 4. | Songea DC | 4,695,638,000.00 | 4,368,955,091.90 | 93.04 | 1,080,234,400.00 | 24.73 | 3,288,720,691.90 |
| 5. | Songea MC | 7,301,709,000.00 | 4,713,864,668.51 | 64.56 | 1,826,134,151.51 | 38.74 | 2,887,730,517.00 |
| 6. | Nyasa DC | 4,664,725,000.00 | 4,024,105,749.16 | 86.27 | 2,561,744,749.16 | 63.66 | 1,462,361,000.00 |
| 7. | Mbinga TC | 3,503,552,000.00 | 3,030,755,077.59 | 86.51 | 1,452,837,240.59 | 47.94 | 1,577,917,837.00 |
| 8. | Namtumbo DC | 5,857,927,000.00 | 4,687,919,494.64 | 80.03 | 4,655,586,101.71 | 99.31 | 32,333,392.93 |
| 9. | Tunduru DC | 5,804,562,000.00 | 4,653,952,095.17 | 80.18 | 2,427,001,744.17 | 52.15 | 2,226,950,351.00 |
| | **Jumla ya Fedha za Maendeleo kutoka Serikali Kuu** | **43,389,815,000.00** | **32,631,674,108.48** | **75.21** | **17,449,660,318.65** | **53.47** | **15,182,013,789.83** |
| | | | | | | | |
| **B** | **Fedha za Maendeleo kutoka Nje** | | | | | | |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desesmba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | RS | 757,931,000.00 | 301,939,233.27 | 39.84 | 221,814,682.87 | 73.46 | |
| 2. | Mbinga DC | 4,600,945,915.76 | 2,038,795,880.56 | 44.31 | 1,852,213,465.81 | 90.85 | 186,582,414.75 |
| 3. | Madaba DC | 2,863,320,000.00 | 499,920,585.02 | 17.46 | 428,030,010.95 | 85.62 | |
| 4. | Songea DC | 3,841,364,000.00 | 1,856,859,991.09 | 48.34 | 1,395,856,473.40 | 75.17 | 461,003,517.69 |
| 5. | Songea MC | 3,351,975,000.00 | 1,384,192,154.20 | 41.29 | 458,603,050.20 | 33.13 | 925,589,103.80 |
| 6. | Nyasa DC | 4,354,248,000.00 | 1,948,533,961.82 | 44.75 | 1,944,783,961.82 | 99.81 | - |
| 7. | Mbinga TC | 2,689,737,000.00 | 309,074,300.00 | 11.49 | 271,063,555.55 | 87.70 | 38,010,744.45 |
| 8. | Namtumbo DC | 4,952,913,000.00 | 392,316,000.00 | 7.92 | 392,316,000.00 | 100.00 | |
| 9. | Tunduru DC | 7,682,502,000.00 | 2,599,922,580.21 | 33.84 | 1,708,969,338.00 | 65.73 | 890,953,242.21 |
| | **Jumla Maendeleo Nje** | **35,094,935,915.76** | **11,331,554,686.17** | **32.29** | **8,673,650,538.60** | **76.54** | **2,502,139,022.90** |
| **C** | **Maendeleo Mapato ya Ndani** | | | | | | |
| 1. | Mbinga DC | 2,183,139,612.40 | 1,474,025,632.45 | 67.52 | 1,299,689,170.88 | 88.17 | 174,336,461.57 |
| 2. | Madaba DC | 236,321,000.00 | 228,344,760.34 | 96.62 | 228,344,760.34 | 100.00 | |
| 3. | Songea DC | 423,256,000.00 | 632,085,780.68 | 149.34 | 183,853,173.00 | 29.09 | 448,232,607.68 |
| 4. | Songea MC | 2,030,272,000.00 | 961,855,082.78 | 47.38 | 961,855,082.78 | 100.00 | - |
| 5. | Nyasa DC | 181,120,000.00 | 170,296,986.18 | 94.02 | 133,605,039.22 | 78.45 | 37,101,051.28 |
| 6. | Mbinga TC | 752,147,000.00 | 374,987,904.12 | 49.86 | 343,025,435.00 | 91.48 | 31,962,469.12 |
| 7. | Namtumbo DC | 400,134,000.00 | 151,876,775.71 | 37.96 | 98,652,037.00 | 64.96 | 53,224,738.71 |
| 8. | Tunduru DC | 1,801,549,000.00 | 1,462,106,687.08 | 81.16 | 303,827,400.00 | 20.78 | 1,158,279,287.08 |

| Na | Aina ya Bajeti | Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24 | Kiasi Kilichotolewa hadi Desesmba, 2023 | Asilimia ya Fedha Zilizotolewa | Matumizi hadi Desemba 2023 | Asilimia ya Matumizi hadi Desemba, 2023 | Bakaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Maendeleo Mapato Ndani** | **8,007,938,612.40** | **5,455,579,609.34** | **68.13** | **3,552,852,098.22** | **65.12** | **1,903,136,615.44** |
| | **Jumla ya Fedha za Miradi ya Maendeleo** | **86,492,689,528.16** | **49,418,808,403.99** | **57.14** | **29,676,162,955.47** | **60.05** | **19,587,289,428.17** |

### 5.2.6 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

i. Kupanda mara kwa mara kwa bei za bidhaa na huduma hasa vifaa vya ujenzi vya viwandani, hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na bajeti iliyopangwa;

ii. Upungufu wa watumishi hususan katika Sekta ya Elimu Ujenzi, Afya, Kilimo, Mifugo, Fedha na Wathamini, kwa sasa Mkoa una mahitaji ya watumishi **21,918** waliopo ni **14,424** na upungufu ni **7,494.**

### 5.2.7 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

i. Mkoa umeendelea kuchukua hatua za kupunguza gharama za ujenzi kwa kuagiza vifaa vya ujenzi kwa wingi (bulk procurement) moja kwa moja viwandani kwa bidhaa kama saruji, mabati nk.

ii. Mkoa unaendelea kuwasilisha maombi ya vibali vya ajira mpya na ajira mbadala OR MUUB pamoja na kufanya masawazo wa ndani ya mkoa kwa ajili kupunguza ukubwa wa tatizo katika maeneo ambayo yana changamoto kubwa zaidi ya upungufu wa watumishi;

## 6.0 MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mkoa unaendelea na maandalizi ya mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika mipango, dira na miongozo mbalimbali iliyopo ya kimkoa, kitaifa na kikanda. Baadhi ya nyaraka zilizozingatiwa ni pamoja na: -

- ✓ Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;
- ✓ Mpango wa Mwaka Mmoja wa Maendeleo ya Taifa;
- ✓ Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025;
- ✓ Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030;
- ✓ Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020;
- ✓ Mpango Mkakati wa Mkoa na Halmashauri;
- ✓ Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/23;
- ✓ Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; na
- ✓ Maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, Chama na Wizara.

Baadhi ya Vipaumbele vilivyozingatiwa katika Mpango na Bajeti ya 2024/2025 ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

### 6.1 Vipaumbele vya Mkoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2024/25

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE | |
|---|---|---|---|
| **1.** | **Utawala** | (i) | Kuendelea kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama ndani ya Mkoa pamoja na usimamizi wa mipaka kwa kuratibu vikao vya ujirani mwema. |
| | | (ii) | Kuimarisha utawala bora kupitia uratibu na uendeshaji wa vikao vya kisheria, kiutawala, uboreshaji wa Serikali mtandao na ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa Umma (D by D); |
| | | (iii) | Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWA) |
| | | (iv) | Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kutenga fedha kwa ajili kujenga,kukamilisha na kukarabati nyumba na Ofisi za wakuu wa |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| | | Wilaya,Wakurugenzi wa Halmashauri,Tarafa, Kata na Vijiji na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi; |
| 2 | **Afya na Ustawi wa Jamii** | (i) Kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa tiba na dawa.<br>(ii) Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga bajeti ya uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe sambamba na kutenga katika bajeti shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe.<br>(iii) Kusimamia na kufuatilia ubora (Quality) na utoaji wa huduma za Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati<br>(iv) Kuendelea kutoa elimu ya kupambana na na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa hatari ya kuambukiza ikiwemo ugonjwa wa UVIKO 19, na Ukimwi na kuendelea kutoa elimu kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.<br>(v) Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Jamii ulioboreshwa (iCHF).<br>(vi) Kuwajengea uwezo watumishi wa Idara ya Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya katika Halmashauri (mafunzo ya muda mfupi na marefu). |
| 3. | **Elimu na Mafunzo ya Ufundi** | (i) Kundelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule.<br>(ii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo; |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| | | (iii) Kuuwezesha mafunzo kazini kwa walimu katika ufundishaji wa mada mbalimbali.<br>(iv) Kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi na ufundi kwa kusambaza vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi na kujenga maabara na karakana za ufundi. |
| **4** | **Kilimo na Mifugo** | (i) Kuendelea kuongeza uzalishaji na tija (production and productivity) kwa mazao ya chakula na biashara ili kuongeza kiwango cha utoshelevu na ziada ya chakula.<br>(ii) Kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kupata utaalam na mbinu bora za kilimo na ufugaji kwa watalam wa kilimo na wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa ambao wapo kwenye maeneo yao ili kukuza uwezo na kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara;<br>(iii) Kuendelea kusimamia upatikanaji na matumizi saahihi ya pembejeo na zana bora za kilimo ili kuongeza tija katika uzalishaji;<br>(iv) Kuwezesha uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja (**block farming**) kwa ajili ya kilmo cha mazao ya kimkakati kama ufuta, korosho,kahawa na soya).<br>(v) Kuanzisha Kongani za Kilimo na mazao ya Kilimo<br>(vi) Kuhamasisha ujenzi wa Maghala makubwa ya kuhifadhia mazao ya kilimo |
| **5** | **Usafiri na Usafirishaj i (barabara)** | (i) Kuimarishaji usafiri na usafirishaji kwa kuendelea na Ujenzi wa barabara na madaraja, kukarabati na matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020,Mpango Mkakati wa Mkoa pamoja maeneo ya kimkakati ndani ya Mkoa (kilimo,madini, maeneo mapya ya makazi na huduma. |
| **6** | **Nishati (Umeme)** | (i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na mijini inayotekelezwa na REA na TANESCO pamoja na kuendelea |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| | | kuwaunganishia nishati ya umeme wananchi ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme kwa ujumla (overall electricity access level) |
| **7** | **Fedha na tehama** | (ii) Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mifumo ya Kielektroniki ya Ukusanyaji wa Mapato (TAUSI), mifumo ya matumizi (MUSE,FFARS etc) ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya serikali sambamba na kuendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya malipo Serikalini (GePG).<br>(ii) Kuendelea kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vilivyopo. |
| **8** | **Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi** | (i) Kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa mikopo yenye mashariti nafuu inayotokana na **10%** ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu **(4:4:2).**<br>(iii) Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mpango wa Kunusuru kaya Masikini (Social Welfare Benefits) unaotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF II).<br>(iii) Kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali kama viwanda, kilimo cha kimkakati, biashara nk. |

## 6.2 MAKADIRIO YA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

### 6.2.1 Bajeti ya Mkoa na Halmashauri kwa Mwaka wa fedha 2024/25

Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri kwa kuzingatia ukomo wa bajeti wa 2023/24 uliotolewa na Wizara ya Fedha inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 272,771,649,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Fedha hizo zinajumuisha Shilingi **194,348,658,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **78,422,991,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo. Muhtasari wa bajeti ni kama inavyoonesha katika jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 01 Muhtasari wa makisio ya bajeti ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25**

| NA | MATUMIZI YA KAWAIDA | KIASI TENGWA (194,353,658,000) |
|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 161,216,761,000 |
| 2 | Matumizi Mengineyo (Mapato ya ndani) | 19,861,536,000 |
| 3 | Matumizi Mengineyo (Ruzuku) | 13,275,361,000 |
| | Jumla Ndogo | 194,348,658,000 |
| **NA** | **MPANGO WA MAENDELEO** | **KIASI TENGWA (78,422,991,000)** |
| 1 | Fedha za Ndani (Ruzuku) | 37,003,185,000 |
| 2 | Fedha za Nje | 33,409,327,000 |
| 3 | Fedha za Ndani (Mapato ya ndani) | 8,010,479,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **78,422,991,000** |
| **JUMLA KUU** | | **272,771,649,000.00** |

### 6.3 Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

Kwa mwaka wa fedha 2024/25 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 194,348,658,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **161,216,761,000.00** ni Mishahara na **Shilingi 33,131,897,000.00** ni Matumizi Mengineyo (OC). Bajeti ya ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni Shilingi **7,292,134,000** na **Shilingi 187,056,524,000** ni bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM).

### 6.4 Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inaomba kuidhinishiwa makadirio ya jumla ya **Shilingi 78,422,991,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 45,013,664,000** ni fedha za ndani za Serikali (Local) na **Shilingi 33,409,327,000** ni fedha za wahisani wa maendeleo kutoka nje ya nchi (Foreign)**.** Bajeti ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni **Shilingi 3,006,342,000** na **Shilingi 75,416,649,000** ni bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**6.5 Makisio ya Makusanyo ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2024/25**

Kwa mwaka wa Fedha 2024/25 Mamlaka za Serikali za Mitaa za mkoa wa Ruvuma zinakisia kukusanya shilingi **27,883,161,500.00** kutoka katika vyanzo vya makusanyo ya mapato ya ndani. Kati ya makisio hayo shilingi **22,072,212,500.00** ni mapato yasiyolindwa na shilingi **5,810,949,000.00** ni mapato ya vyanzo lindwa.

**Jedwali Na. 2 Makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024/25**

| NA | HALMASHAURI | MAKISIO YA MAPATO YASIYOLINDWA | MAKISIO YA MAPATO LINDWA | JUMLA MAKISIO YA MAPATO YOTE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea MC | 5,075,680,000 | 993,974,000.00 | 6,069,654,000 |
| 2 | Mbinga TC | 1,880,367,000 | 596,120,000.00 | 2,476,487,000 |
| 3 | Mbinga DC | 5,725,642,000 | 574,358,000.00 | 6,300,000,000 |
| 4 | Tunduru DC | 3,285,958,500 | 1,584,545,000.00 | 4,870,503,500 |
| 5 | Songea DC | 1,841,952,000 | 627,005,000.00 | 2,468,957,000 |
| 6 | Namtumbo DC | 2,176,908,000 | 588,370,000.00 | 2,765,278,000 |
| 7 | Nyasa DC | 905,600,000 | 538,405,000.00 | 1,444,005,000 |
| 8 | Madaba DC | 1,180,105,000 | 308,172,000.00 | 1,488,277,000 |
| | **JUMLA** | **22,072,212,500.00** | **5,810,949,000.00** | **27,883,161,500.00** |

## Jedwali Na. 3 Mchanganuo wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Mkoa na Halmashauri kwa Mwaka 2024/25

| Taasisi | Mishahara | Matumizi Mengineyo | | | Bajeti ya Maendeleo | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Serikali Kuu | Mapato ya Ndani | Jumla | Serikali Kuu | Mapato ya Ndani | Fedha za Nje | Jumla | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (2+3+4) | 6 | 7 | 8 | 9 (8+7) | 10 (5+9) |
| **Mkoa** | 3,014,498,000 | 4,277,636,000 | 0 | 7,292,134,000 | 2,270,982,000 | 0 | 735,360,000 | 3,006,342,000 | 10,298,476,000 |
| Jumla | **3,014,498,000** | **4,277,636,000** | **0** | **7,292,134,000** | **2,270,982,000** | **0** | **735,360,000** | **3,006,342,000** | **10,298,476,000** |
| **Halmashauri** | | | | | | | | | |
| Songea MC | 32,735,300,000 | 1,218,849,000 | 4,039,382,000 | 37,993,531,000 | 6,383,709,000 | 2,030,272,000 | 3,265,836,000 | 11,679,817,000 | 49,673,348,000 |
| Mbinga TC | 17,338,302,000 | 911,560,000 | 1,791,652,000 | 20,041,514,000 | 2,975,552,000 | 684,835,000 | 2,711,668,000 | 6,372,055,000 | 26,413,569,000 |
| Songea DC | 16,458,233,000 | 1,120,508,000 | 2,100,567,000 | 19,679,308,000 | 3,079,638,000 | 368,390,000 | 3,709,399,000 | 7,157,427,000 | 26,836,735,000 |
| Tunduru DC | 24,737,788,000 | 1,287,080,000 | 2,868,954,000 | 28,893,822,000 | 4,611,932,000 | 2,001,549,000 | 7,072,477,000 | 13,685,958,000 | 42,579,780,000 |
| Mbinga DC | 23,283,160,000 | 1,163,116,000 | 4,116,860,000 | 28,563,136,000 | 6,345,722,000 | 2,183,140,000 | 4,086,689,000 | 12,615,551,000 | 41,178,687,000 |
| Namtumbo DC | 20,454,972,000 | 1,201,313,000 | 2,408,555,000 | 24,064,840,000 | 4,329,927,000 | 339,076,000 | 4,609,946,000 | 9,278,949,000 | 33,343,789,000 |
| Nyasa DC | 15,615,948,000 | 1,047,366,000 | 1,277,110,000 | 17,940,424,000 | 4,236,725,000 | 166,896,000 | 4,275,282,000 | 8,678,903,000 | 26,619,327,000 |
| Madaba DC | 7,578,560,000 | 1,047,933,000 | 1,253,456,000 | 9,879,949,000 | 2,768,998,000 | 236,321,000 | 2,942,670,000 | 5,947,989,000 | 15,827,938,000 |
| **Jumla ya Halmashauri** | **158,202,263,000** | **8,997,725,000** | **19,856,536,000** | **187,056,524,000** | **34,732,203,000** | **8,010,479,000** | **32,673,967,000** | **75,416,649,000** | **262,473,173,000** |
| **Jumla Kuu** | **161,216,761,000** | **13,275,361,000** | **19,856,536,000** | **194,348,658,000** | **37,003,185,000** | **8,010,479,000** | **33,409,327,000** | **78,422,991,000** | **272,771,649,000** |

## 7.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KISEKTA

## 7.1 UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA)

### 7.1.1 SEKTA YA KILIMO

#### 7.1.1.1 HALI YA SEKTA YA KILIMO RUVUMA:

**a) Eneo linalofaa kwa Kilimo**

Mkoa wa Ruvuma una Jumla ya Hekta **4,007,746** zinafaa kwa kilimo, hadi sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **897,171** sawa na asilimia **22** ya eneo lote**,** na kufanya Mkoa kuwa na ziada ya hekta **3,110,575** sawa na asilimia **78.**

**b) Eneo la Kilimo cha Umwagiliaji**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya hekta 197,108.2 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta 7,388.3 zimeendelezwa,hii ni sawa na asimilia 3.7. Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa skimu **23** zinafanya kazi na **19** hazifanyi kazi. Skimu 23 zinazofanya kazi zina ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili, eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji **hekta 5,420** na eneo linalomwagiliwa lenye ukubwa wa **hekta 1,182.**

**c) Mazao ya Chakula**

Mazao ya chakula yanayolimwa Mkoani Ruvuma yanajumuisha Mahindi, Mpunga, Muhogo na Maharage. Mazao mengine ni Mtama, Ulezi, Mbaazi, Viazi Vitamu na Jamii ya Mikunde.

**d) Mazao ya Biashara**

Mazao makuu ya biashara yanayolimwa Mkoani Ruvuma ni Tumbaku, Kahawa na Korosho. Pia Mkoa wa Ruvuma unalima ufuta, alizeti, karanga, tangawizi, parachichi, ndizi, mpunga, maharage, mbaazi na soya kwa ajili ya biashara. Aidha, kwa upande wa zao la mahindi pamoja na kuwa ni zao la chakula lakini wananchi wanalitumia kama zao la biashara.

**e) Maafisa Ugani**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Watumishi Maafisa Kilimo **300** kati ya mahitaji ya Maafisa Kilimo **900** na upungufu wa Maafisa Kilimo **570**. Tuaishukuru serikali kwa kuwa imejiwekea utaratibu wa kuajiri mara kwa mara katika ngazi za Halmashauri. Jedwali linaonesha idadi ya Maafisa Kilimo katika ngazi ya mkoa na Halmashauri.

**Jedwali: Idadi ya wataalamu wa kilimo kwa kila Halmashauri**

| Halmashauri/ *RS* | Wanaohitajika | Waliopo | Mapungufu | Waliopo kwenye mpango wa kuajiriwa 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|
| **RS** | 3 | 3 | 0 | |
| Tunduru DC | 203 | 62 | 141 | |
| Namtumbo DC | 94 | 65 | 9 | |
| Mbinga DC | 153 | 40 | 113 | |
| Nyasa DC | 111 | 20 | 91 | 6 |
| Songea DC | 79 | 40 | 29 | |
| Madaba DC | 30 | 17 | 13 | |
| Songea MC | 123 | 27 | 96 | |
| Mbinga TC | 104 | 26 | 78 | |
| **Jumla** | **900** | **300** | **570** | |

Nb: Kila Kata, Kijiji na Mtaa na Makao Makuu inatakiwa kuwa na afisa mmoja.

### 7.1.1.2 HALI YA MAENDELEO YA SEKTA YA KILIMO

**a) Malengo na uzalishaji wa mazao;**

**i. Utekelezaji wa malengo ya kilimo msimu wa mwaka 2022/2023**

Mkoa umefanikiwa kulima jumla ya hekta **897,171** za mazao ya Chakula, Biashara na mazao ya Bustani (sawa na asilimia **97** ya lengo). Katika hekta zilizolimwa Mkoa ulipata mavuno ya tani **1,870,800** (sawa na asilimia **95** ya lengo la mavuno). Kati ya hekta hizo za kilimo cha mazao ya Chakula zililimwa jumla ya hekta **550,310** zilitoa mavuno ya tani **1, 598,163** na mazao ya Biashara hekta zilizolimwa zilikuwa ni **332,459** na zilitoa jumla ya tani **94,741**.

**ii. Malengo ya Kilimo kwa msimu wa kilimo 2023/2024**

Mkoa umelenga kulima hekta **1, 006,325** za mazao ya Chakula, Biashara na mazao ya Bustani zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **2,168,041**, kati ya hekta hizo kilimo cha mazao ya Chakula ni hekta **642,906** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,882,473** na kilimo cha mazao ya Biashara hekta **348,441** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **100,557.** Mazao ya Bustani jumla ya hekta **14,978** zitalimwa na matarajio ni kupata mavuno ya tani **185,012.**

### 7.1.1.3 Mpango wa kuendeleza Mazao

**(a) Parachichi**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani **1,768** zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani **37,500** ifikapo mwaka **2025.** Mpaka sasa

makampuni mbalimbali yameonesha nia ya kununua Parachichi katika Mkoa wa Ruvuma. Zao hili ni fursa kwani linahitajika ndani na nje ya nchi. Msimu wa uvunaji wa parachichi kwa Mkoa wa Ruvuma unatofautiana na Mikoa mingine kama Njombe na hivyo kutoa uhakika wa soko.

**(b) Kahawa**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani **23,355.00** hadi kufikia Tani **55,000** za kahawa safi ifikapo mwaka **2025.**

**(c) Soya**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la Soya kutoka **tani 5,510** kwa **msimu wa 2022/23** hadi kufikia **tani 10,000** kwa msimu wa **2023/24.** Mkoa na Wizara ya kilimo inaendelea kusimamia na kuhamasisha wananchi waongeze uzalishaji wa zao hili. Kwa sasa Shirika la Southern Agricultura Growth Corridor of Tanzania (**SAGCOT) linaendelea kutekeleza** mradi wa kuedeleza zao la soya katika Halmashauri zinazolima soya unaoitwa **TSSI**-Tanzania Sustainable Soybean Initiatives.

**(d) Korosho**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la Korosho kutoka tani **28,014.00 kwa msimu wa 2022/23** hadi kufikia tani **29,135 kwa msimu wa 2023/24.** Kupitia Taasisi ya

**(e) Ufuta**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la Ufuta kutoka **tani 9,649 kwa msimu wa 2022/23** hadi kufikia tani **12,061** kwa msimu wa **2023/24.**

### 7.1.1.4 UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO

### MBOLEA ZA CHUMVICHUMVI

**i. Upatikanaji wa Mbolea Msimu 2023/2024**

Kwa Mkoa wa Ruvuma katika Msimu wa kilimo **2023/2024** kuanzia mwezi Julai hadi kufikia **tarehe 15 Januari, 2023** zimeingizwa jumla ya tani **90,000.00** na kusambazwa kwa wakulima kiasi cha tani **62,540.225** kati ya mahitaji ya tani **112,692**. Hadi sasa kiasi cha tani **27,459.775** (Stock) zinapatikana katika maghala ya makampuni na maduka ya mawakala. Jedwali (a) linajieleza hapo chini.

**Jedwali(a): Upatikanaji wa Mbolea kutoka msimu 2020/2021 hadi 2023/2024**

| Msimu | Mahitaji (Tani) | Uingizaji (Tani) | Asilimia ya uingizaji |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 50,910 | 43,000 | 84.5 |
| 2021/2022 | 50, 524.50 | 33,501.07 | 66 |
| 2022/2023 | 80,000 | 71,000 | 87.5 |
| 2023/2024 | 112,692 | 90,000 | 79 *Usambazaji unaendelea* |

i. **Bei za Mbolea**

Bei za sokoni za mbolea ni kati ya sh.60,000 hadi sh.132,000 na bei za ruzuku za mbolea ni kati ya sh.50,000 hadi sh.70,000. Tunaipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea ambayo imempunguzia mzigo wa gharama za uzalishaji mkulima. Majejwali (b-c) ni bei za mbolea za soko zisizo na ruzuku kwa misimu mitatu 2020/2021 hadi 2022/2023 na jedwali (d) ni bei za mbolea za ruzuku kwa msimu wa 2023/2024

**Jedwali(b): Bei za Mbolea Sokoni bila ruzuku kwa misimu 2020/2021 hadi 2022/2023**

| Msimu | **UREA** | **SA** | **CAN** | **DAP** | **NPKs** |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 99,000.00 | 60,000.00 | 70,000.00 | 105.000.00 | |
| 2021/22 | 126,000 | 84,000.00 | 110,000.00 | 132.000.00 | |
| 2022/23 | 126,000.00 | 84,000.00 | 110,000.00 | 132,000.00 | 124,000.00 |

**Jedwali(c): Bei za Mbolea za Ruzuku kwa misimu 2020/2021 hadi 2022/2023**

| Msimu | **UREA** | **SA** | **CAN** | **DAP** | **NPKs** |
|---|---|---|---|---|---|
| **2020/2021** | 70,000.00 | 50,000.00 | 60,000.00 | 70,000.00 | |
| **2021/22** | 70,000.00 | 50,000.00 | 60,000.00 | 70,000.00 | |
| **2022/23** | 70,000.00 | 50,000.00 | 60,000.00 | 70,000.00 | |

**Jedwali(d): Bei za Mbolea kwa msimu wa 2023/24**

| **Na.** | **Aina ya mbolea** | **Bei (Tsh)** |
|---|---|---|
| 01 | DAP | 70,000 - 85,000 |
| 02 | UREA | 65,000 – 70,000 |
| 03 | SA | 45,000 – 50,000 |
| 04 | CAN | 60,000 - 65,000 |
| 05 | NPK | 70,000 – 85,000 |

NB: Bei za msimu 2023/2024 zinatofautiana kwa kuzingatia umbali.

ii. **Usajili wa Wakulima**

Serikali Kupitia Wizara ya Kilimo ilizindua rasmi mfumo wa mbolea za Ruzuku Agosti, 2022 ambapo zoezi la usajili kwa wakulima lilianza tarehe 01 Agosti, 2022. Hadi kufikia tarehe **15 Januari, 2024** Mkoa wa Ruvuma umesajili jumla ya wakulima **370,431** kati ya lengo la kusajili wakulima **428,288.00** sawa na asilimia **86.5**.

iii. **Idadi ya Vituo vya Kuuza na Kusambaza Mbolea**

Mpaka kufikia tarehe 15 Januari,2024, Jumla ya vituo **201** vimesajiliwa na Taasisi ya Udhibiti wa mbolea.

### 7.1.1.5 MBEGU BORA

i. **Mahitaji ya mbegu**

Mkoa wa Ruvuma unahitaji mbegu bora za nafaka, mikunde na mazao ya mafuta jumla ya tani 19,530.34 kati ya hizo mahindi tani **10,431.95**, mpunga tani **1,576.05**, Maharage tani **6,360**, Soya tani **536.06**, mbaazi tani **449.85**, ufuta tani **119.8** na alizeti tani **56.63**.

ii. **Upatikanaji wa Mbegu mbalimbali za mazao**

**Mbegu ya ufuta;** mkoa umepata mgao wa mbegu za ufuta zenye ruzuku ya Serikali jumla ya tani **2** ambazo zimegawiwa bure kwa wakulima wa ufuta kwenye Halmashauri.

iii. **Mbegu za mahindi zinapatikana kupitia soko huru; ambapo Serikali kupitia** Wizara ya Kilimo imetoa bei elekezi ya mbegu zote za mahindi, bei ya juu ni **Tsh. 16,000** kwa aina zote za mbegu za mahindi chotara. Lengo la serikali ni kumpunguzia mkulima gharama za kununua mbegu bila kuathiri Wafanyabiashara (Makampuni na Mawakala wa Pembejeo) wanaozalisha/ kusambaza mbegu.

i. **MICHE BORA - Miche ya Kahawa**

Hadi kufikia tarehe 31 Januari 2024, Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Bodi ya kahawa Tanzania, TACRI, Halmashauri na wadau wengine wa kahawa umesambaza jumla ya **miche 2,353,504** na zoezi la usambazaji wa miche hiyo linaendelea.

#### 7.1.1.6 Hatua ya Ujenzi wa Maghala 28 ya Kuhifadhia Mazao

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo unaendelea na zoezi la ujenzi wa maghala **28** yatakayotumika kuhifadhi mazao ya wakulima kwenye vijiji na miji. Hadi kufikia Mwezi Januari 2024, jumla ya maghala **16** yapo katika hatua ya kuezeka paa na kujenga kuta za bati ("roofing and cladding"), Maghala **10** yapo katika hatua ya kuchimba na ujenzi wa msingi na maghala **2** yapo katika hatua ya kufungwa vyuma ("frames"). Kwa ujumla hatua ya ujenzi na maandalizi ya vifaa umefikia asilimia sitini na tano (**65%**).

#### 7.1.1.7 Vitendea kazi kwa Maafisa Ugani

**Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** alitoa pikipiki **7000** kwa maafisa ugani wa nchi nzima ambapo katika Mkoa wetu wa Ruvuma tulipata mgao wa pikipiki **281**. Hivyo maafisa ugani wote wa Kata na Vijiji waliopo katika Mkoa wa Ruvuma kila mmoja alipata pikipiki moja.

Pia, Serikala imeleta mashine 7 za kupima udogo na kuzingawa kwenye Halmashauri za Mbinga Mji, Songea Vijijini, Mbinga Vijijini, Nyasa, Madaba na Tunduru ambazo zinaendelea kutumika kupima udongo. Wizara inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na vitendea kazi vya kutosha.

#### 7.1.1.8 Mafanikio ya Sekta ya Kilimo

**(a) Kuwepoo kwa mfumo wa ruzuku ya Serikali ya mbolea kumesaidia kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji** na manufaa mengine kama ifuatavyo;

i. Kupunguza gharama za mbolea kwa mkulima kwa asilimia 50
ii. Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea yanayoashiria kuongeza uzalishaji wa mazao;
iii. Kuongezeka kwa matumizi ya simu katika Sekta ya kilimo, hii ni kutokana na zoezi la usajili wa wakulima.
iv. Wakulima kuongeza ukubwa wa mashamba yao na kuongeza uzalishaji wa mazao.
v. Mfumo umesaidia kutambua idadi ya wakulima

vi. Mfumo umewezesha kuibua mpango wa vyama vya Ushirika kusajiliwa na kufanya kazi ya kusambaza mbolea kwa wakulima wake kama mawakala, lengo ni kusogeza huduma kwa wakulima wanaowahudumia.
vii. Kupitia mfumo huu Serikali imeweza kusimamia uchakachuaji (uuzaji wa mbolea zisizokuwa na kiwango.
viii. Kupitia mfumo huu Serikali imeweza kusimamia bei za mbolea kwa wakulima.
ix. Kupitia mfumo Mkoa na nchi kwa ujumla imeweza kupata Takwimu sahihi za mahitaji na matumizi ya mbolea.

**(b) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao** kutoka msimu 2020/2021 **tani 1,623,509.57** hadi msimu 2022/2023 **tani 1,823,509.57;**

**(c) Maafisa ugani kupewa Vitendea kazi** hasa pikipiki, mashine za kupima afya ya udongo, makoti ya mvua na Mabuti ambavyo vimeboresha utendaji wa kazi kwenye vituo vyao.

### 7.1.2 SEKTA YA USHIRIKA

#### 7.1.2.1 Hali ya Ushirika katika Mkoa wa Ruvuma

Mkoa una jumla ya Vyama vya Ushirika **297**, kati ya hivyo AMCOS **225**, Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) **63**, Vyama vingine **6** na Vyama Vikuu (UNIONS) vitatu (**3)** ambavyo ni TAMCU Ltd, SONAMCU Ltd, na MBIFACU Ltd.

Ofisi ya Mrajisi Msaidizi wa Mkoa inaendelea na jukumu la Usajili wa Vyama vya Ushirika ambavyo vinawasilisha maombi kupitia Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri. Kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia mwezi Novemba, 2023, jumla ya Vyama saba (AMCOS 6 na SACCOS 1) vya msingi vimeandikishwa ambavyo ni **Umami, Kimaki, Ukilimasi, Uwamaso, Ifinga, Miembeni pamoja na Ruvuma Coal SACCOS.**

#### 7.1.2.2 Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika

Jukumu la Usimamizi na ukaguzi wa shughuli za Vyama vya Ushirika limeendelea kutekelezwa ambapo kuishia Disemba 31, 2023 usimamizi umefanyika kwa Vyama **205.** Shughuli zilizofanyika ni:

- Kusimamia Mikutano Mikuu na Chaguzi za SACCOS 07 na AMCOS 3
- Kusimamia wa makusanyo na mauzo ya Kahawa

- Kusimamia minada ya mazao na masoko ya mikataba
- Kukagua usafi wa zao
- Kusimamia masafirisho
- Uhakiki wa malipo ya wakulima
- Ukusanyaji wa takwimu
- Ukaguzi wa ndani ambapo Vyama 21 vimekaguliwa
- Kufoa na kufuatilia matumizi ya komo za madeni
- Kufuatilia Vyama vilivyoshiriki kusambaza mbolea za ruzuku

**7.1.2.3 Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani**

Uendeshaji wa masoko ya mazao ya Ufuta, Mbaazi na Soya hufanyika kupitia wakulima kukusanya mazao kupitia Vyama vya Msingi **101** na Vyama Vikuu **2,** kati ya hivyo Namtumbo vyama **45**, Songea **15**, Mbinga **5**, Nyasa **1** na Tunduru **35**.

**a) Zao la Ufuta**

Kwa msimu wa masoko 2023/2024 minada ya Ufuta ilianza katika AMCOS ya Limamu Namtumbo tarehe 25/05/2023. Hadi kufikia tarehe 27/07/2023 jumla ya minada 21 imefanyika ambapo Songea na Namtumbo (chini ya SONAMCU) minada **14** na Tunduru (TAMCU) **7**. Jumla ya kilo zilizouzwa ni **8,621,167.00** zenye thamani ya shilingi **31,830,735,234.40.** Minada imemalizika

**Jedwali namba 1 linachanganua Mwenendo wa Mauzo ya Ufuta Kwa Misimu Mitano Kupitia Vyama Vya Ushirika**

**Jedwali Na.1: Mwenendo wa Mauzo ya Ufuta Kwa Misimu Mitano Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha kwa kulima (Tshs) Bilioni |
|---|---:|---:|---:|
| 2019/2020 | 8,428,268 | 2,952 | 24,882,415,441 |
| 2020/2021 | 12,234,757 | 2,050 | 23,153,671,988.58 |
| 2021/2022 | 8,326,686 | 2,157 | 17,221,852,087.00 |
| 2022/2023 | 7,970,176.60 | 2,874 | 22,703,978,627.45 |
| 2023/2024 | **8,621,167.00** | 3,692 | 31,830,735,234.40 |
| **JUMLA** | **45,581,055** | **2,746** | **119,792,653,378** |

**(b) Zao la Soya**

Kwa msimu wa masoko **2023/2024** imefanyika minada **kumi na tatu (13)** ambapo mnada wa kwanza ulianza tarehe 13/06/2023. Hadi kufikia tarehe 26/07/2023 jumla

ya kilo **5,023,309.00** zenye thamani ya kiasi cha shilingi **4,479,676,110.50.** Minada imemalizika.

Mchanganuo wa Mwenendo wa Mauzo ya Soya kupitia Vyama vya Ushirika kwa misimu mitano.

**Jedwali Na.02: Mwenendo wa Mauzo ya Soya Kwa Misimu Mitano Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha za Mkulima (Tshs) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 2,643,944 | 765 | 2,021,697,476.00 |
| 2020/2021 | 1,297,821 | 1,283 | 1,665,196,005.00 |
| 2021/2022 | 1,090,199 | 1,327 | 1,547,202,688.00 |
| 2022/2023 | 5,119,431 | 1238 | 5,973,969,447.90 |
| 2023/2024 | 5,023,309 | 1,238 | 4,114,766,594.00 |
| **JUMLA** | **15,174,704** | **1,170** | **15,322,832,210.90** |

**(c) Zao la Mbaazi**

Kwa msimu wa masoko 2023/2024 imefanyika minada kumi na moja **(11)** ambapo mnada wa kwanza ulianza tarehe 12/08/2023 Wilayani Tunduru. Hadi kufikia tarehe 20/09/2023 jumla ya kilo **9,244,050.50** zenye thamani ya shilingi **18,458,575,311**. Zimeuzwa kupitia vyama vya ushirika kama inavyoonyesha katika jedwali Na. 3.

**Jedwali Na.03: Mwenendo wa Mauzo ya Mbaazi Kwa Misimu Mitano Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (Tshs) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 775,543 | 724 | 561,805,805 |
| 2020/2021 | 4,280,777 | 515 | 2,205,617,364 |
| 2021/2022 | 7,109,360 | 1,310 | 9,313,114,072 |
| 2022/2023 | 5,431,983 | 805 | 4,420,536,587 |
| 2023/2024 | 9,244,050.50 | 2,003 | 18,458,575,311 |
| **JUMLA** | **26,374,210** | **1,292** | **34,078,476,689** |

**(d) Zao la Kahawa**

Kwa msimu wa masoko 2023/2024 imefanyika minada tisa (09) ambapo mnada wa kwanza ulianza tarehe 24/08/2023 huko Songwe. Minada imefanyika Songwe, Moshi na Mbinga. Hadi kufikia tarehe 19/11/2023 jumla ya kilo 3,708,824.25 za kahawa Safi zenye thamani ya kiasi cha Dola **6,409,931.27** sawa na shilingi **16,057,868,898.94** ziliuzwa**. (Jedwali Na.4).**

Mpaka kuishia tarehe 30/11/2023 makusanyo ya kahawa kavu kutoka kwenye Vyama yalifikia kilo **19,717,483.** Kilo za parchment zilizouzwa mnadani ni **4,392,295**. Kwa wastani wa bei ya shilingi **4,599** kabla ya makato. Aidha, wakulima wa Mbinga wameendelea kuuza kahawa katika masoko mbalimbali yakiwemo ya awali (kwa Makampuni ya ununuzi), mnadani na soko la moja kwa moja. Hii ni kwa sababu bei ya kahawa mnadani msimu huu zimeshuka ukilinganisha na msimu uliopita.

Vyama vinne ambavyo ni Kimuli, Ngaka, Kinjolu vimeuza kilo 254,474.21 katika soko la moja kwa moja (Direct Sales). Chama cha Mahenge kinaendelea na maandalizi ya kuuza soko la moja kwa moja mchanganuo wa mauzo kwa miaka sita (6) umeoneshwa katika jedwali Na. 4.

**Jedwali Na.04: Kahawa Zilizouzwa na Fedha Iliyopelekwa kwa Wakulima**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (Tshs) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 15,393,500 | 4,300 | 66,192,050,000 |
| 2019/2020 | 20,162,900 | 3,700 | 74,602,730,000 |
| 2020/2021 | 15,675,100 | 4,086 | 64,048,458,600 |
| 2021/2022 | 12,676,844 | 4,000 | 50,707,376,000 |
| 2022/2023 | 13,756,583.75 | 7103 | 97,712,977,942.45 |
| 2023/2024 | 3,708,824.25 | 4,330 | 16,057,868,898.94 |
| **JUMLA** | **81,373,752.00** | **4,539** | **369,321,461,441.39** |

Masoko yote ya kahawa bado yanaendelea.

### (f) Zao la Korosho

Mnada wa kwanza wa mauzo ya Korosho ulifanyika tarehe 02/11/2023 katika chama cha Namitili. Makadirio ya uzalishaji wa Korosho kwa msimu wa 2023/2024 makadirio ya uzalishaji ni tani 25,000 sawa na kilo 25,000,000. Mpaka kufikia tarehe 04/01/2024 jumla ya minada mitano (5) ilifanyika ambapo kilo **25,930,686.00** ziliuzwa kwa bei ya shilingi **45,348,730,436.00. Minada imekwisha.**

**Jedwali Na.5: Ununuzi wa Korosho Katika Misimu Sita (6) na Wastani wa Bei.**

| Msimu | Korosho Zilizonunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (Tshs) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 20,912,569 | 3,815 | 79,777,589,485.68 |
| 2019/2020 | 18,586,248 | 3,300 | 61,334,618,400.00 |
| 2020/2021 | 24,625,824 | 2,650 | 65,246,638,727.00 |
| 2021/2022 | 15,410,605 | 2,273 | 35,025,780,579.00 |

| Msimu | Korosho Zilizonunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (Tshs) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2022/2023 | 25,284,493 | 1,971 | 50,610,459,425.86 |
| 2023/2024 | 25,930,686 | 1749 | 45,348,730,436.00 |
| **JUMLA** | **130,750,425.00** | **2626** | **337,343,817,053.54** |

**3. Uendeshaji wa Zao la Tumbaku**

Kilimo cha tumbaku ni cha mkataba. Miaka ya nyuma Mkoa ulikuwa unazalisha tumbaku ya moshi. Kuanzia mwaka 2023/24 Mkoa umezalisha tumbaku ya kukaushia moshi, mvuke na hewa. Hii imepelekea kupanda kwa uzalishaji ukilinganisha misimu iliyopita.

Kwa msimu **2023/2024** masoko yalifunguliwa tarehe 24 Mei, 2023. Mpaka kuishia tarehe 23/10/2023 jumla ya kilo za tumbaku **2,358,871.29** zenye thamani ya Dola **4,237,885.20** ziliuzwa **(Jedwali Na.5). Masoko yamemalizika.**

**Jedwali Na.06: Ununuzi wa Tumbaku Katika Misimu Sita (6) na Wastani wa Bei.**

| Msimu | Tumbaku Zilizonunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei USD | Fedha Zilizopatikana USD |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 804,947.28 | 1.23 | 990,962.30 |
| 2019/2020 | 1,247,814.75 | 1.49 | 1,864,382.12 |
| 2020/2021 | 785,659.30 | 1.41 | 1,108,740.80 |
| 2021/2022 | 731,143 | 1.32 | 961,664.00 |
| 2022/2023 | 500,839 | 1.51 | 831,796.00 |
| 2023/2024 | 2,358,871.29 | 1.80 | 4,237,885.20 |
| **JUMLA** | **4,372,479.64** | **1.46** | **9,995,430.42** |

**Mafanikio Katika Usimamizi wa Mazao**

i. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya Korosho, Soya, Mbaazi na Tumbaku ukilinganisha na misimu ya nyuma.

**CHANGAMOTO**

**i.** Matumizi mabaya ya komo za madeni. Baadhi ya Vyama vya kahawa vimekuwa vikitumia komo za madeni **kwa matumizi tofauti na yaliyoidhinishwa.**

ii. Utoroshwaji wa mazao hasa zao la soya na mbaazi

iii. Baadhi ya wakulima kuchelewa kulipwa malipo yao hasa kwenye kahawa kwa sababu wakulima wengi wanaokopeshwa pembejeo na mikopo ya kukusanyia wanashindwa kuleta mzigo unaotosheleza kulipia madeni.
iv. Vyama vya tumbaku kuwa na madeni ya pembejeo na kupelekea kulipa wakulima fedha kwa kuanzia asilimia **90** kushuka chini. Makusanyo ya madeni ya pembejeo toka kwa wakulima yanaendelea ili kuwalipa wakulima asilimia ya malipo iliyobakia.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

i. Ofisi ya Mrajisi Msaidizi imefanya kikao na Maafisa Ushirika na kuazimia kuanza kupunguza mikopo ya pembejeo kwa Vyama. Kabla ya kuchukua mkopo wa pembejeo msimu huu Vyama vitatakiwa kuonesha uwezo wake wa ulipaji madeni kwa msimu uliopita. Vyama visivyoweza kuhudumia madeni havitapewa idhini ya kukopa ingawa vilishapewa komo za madeni. Pia kwa msimu ujao vyama vimeelekezwa kuwa vinapaswa kubuni mbinu mbadala wa kupata pembejeo badala ya kutegemea mikopo. Lengo ni kwamba Vyama vyote vya kahawa vitumie vyanzo vya ndani kuhudumia wakulima wake kwenye pembejeo ili kupunguza gharama za uendeshaji.

i. Utoroshwaji ulidhibitiwa na mazao yaliyotoroshwa yaliuzwa kupitia mfumo wa stakabadhi.

ii. Wadaiwa wa pembejeo za tumbaku wanafuatiliwa kwa ukaribu ili waweze kulipa madeni yao.

**HITIMISHO**

Licha ya changamoto ndogondogo zinazokabili sekta ya Ushirika bado Ushirika umeendelea kuwa ni Mkombozi kwa wananchi, hivyo usimamizi wa sekta hii unaendelea kuimarishwa ili Ushirika uweze kusonga mbele kwa maendeleo ya wanachama wake.

### 7.1.3 SEKTA YA MIFUGO

Katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Mifugo Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuboresha huduma za ugani, uzalishaji wa mifugo, uendelezaji wa nyanda za malisho kwa mfumo wa ranchi ndogo, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, uboreshaji wa miundombinu ya mifugo, masoko ya mifugo pamoja na miundombinu ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

#### 7.1.3.1 Hali ya Uzalishaji

Mkoa wa Ruvuma una mifugo **3,354,927** ikijumuisha ng'ombe **235,128**, Mbuzi **293,361**, Kondoo, Nguruwe **232,710,** Kuku, Bata, Punda, Mbwa na mifugo mingine midogo midogo. Kwa kipindi cha mwezi Juni, 2023 hadi Desemba, 2023 uzalishaji wa mazao yatokanayo na Mifugo umefikia tani **1,822.014** za nyama ya ng'ombe, tani **249.54** za nyama ya mbuzi na kondoo, tani **1,270.44** za nyama ya nguruwe na tani **516.17** za nyama ya kuku. Uzalishaji wa maziwa umefikia lita **1,344,968.64** vipande vya ngozi za ng'ombe zilizozalishwa ni **13,016** vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo ni **8,318.**

Mkoa una viwanda viwili vya kusindika nyama katika Abbasia ya Peramiho na Chipole Sisters Halmashauri ya Wilaya ya Songea maarufu kwa usindikaji wa ***sausages*** za nyama wastani wa tani **100** za nyama kwa mwaka.

Kwa upande wa usindikaji wa Maziwa Mkoa una wasindikaji wadogo **6** wanaosindika wastani wa lita **201,600** kwa mwaka. Aidha ,ili kuimarisha lishe kwa jamii wananchi wanaendelea kuhamasishwa kunywa maziwa ili kufikia lengo la unywaji wa lita **200** za maziwa kwa kila mtu kwa mwaka.

#### 7.1.3.2 Minada ya Mifugo na Uongezaji Thamani Zao la Nyama

Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Nyama ulifanya ukaguzi wa wadau wa sekta ya Nyama. Lengo kuu ni Usajili na Utoaji wa Mafunzo kwa wadau wa Tasnia ya nyama Mkoa wa Ruvuma ikihusisha Halmashauri za Namtumbo, Nyasa, Mbinga Mji, Mbinga Vijijini, Songea Manispaa, Songea Vijijini na Tunduru ili waweze kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Nyama Sura ya **421** na kanuni zake.

Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa tasnia ya nyama kuhusu ufanyaji wa biashara ya nyama usiozingatia matakwa ya sheria ya tasnia ya nyama na sheria nyingine

(SOP’s). Kufanya vikao na wamiliki wa bucha, minada, nyama choma, magari ya kubebea nyama na machinjio ili kutoa elimu ya usajili na uhuishaji kwa kutumia mfumo wa usajili na utoaji wa vibali wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (MIMIS) na kuwaelekeza wadau kuhusu ratiba za uhuishaji ambazo zinaanzia tarehe 1 mwezi wa 7 kulingana na mwaka wa Serikali.

Kutoa elimu ya unenepeshaji wa mifugo hasa ng’ombe na nguruwe ili mifugo inayozalishwa iweze kukidhi soko la ndani na nje ya Nchi na kuongeza tija katika uzalishaji wa Mifugo katika kanda ya Kusini, Kukagua na kusajili kazi za wadau wa Tasnia ya nyama (bucha, machinjio, wafugaji wa kuku, minada, magari, ya kubebea nyama, sehemu za kuhifadhia nyama, n.k).

Kutoa ushauri wa kuboresha mazingira ya uzalishaji wa nyama pamoja na usajili kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya nyama Na. 10 ya mwaka 2006, kanuni zake na miongozo mbalimbali kwa wadau wa Nyama wa Mkoa wa Ruvuma;

Katika ukaguzi huo Wadau **170** walipatiwa elimu ya ufanyaji wa biashara ya nyama kwa mujibu wa Sheria ya tasnia ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006:2020 na kanuni zake, taratibu na miongozo iliyopo (mwongozo wa usafi, ujenzi na uendeshaji, madaraja ya ubora wa bucha) (SOP’s). Wafugaji **17** wamepatiwa mafunzo ya ufugaji kibiashara na unenepeshaji ili kuwezesha uzalishaji wa mifugo wenye ubora katika Halmashauri ya Mbinga Mji na Tunduru;

#### 7.1.3.3 Utoaji wa Huduma Za Mifugo

i. **Udhibiti wa Magonjwa**

Mkoa wa Ruvuma umeendelea na shughuli za udhibiti wa magonjwa ambapo kwa kipindi cha Mwezi Julai 2023 hadi Desemba, 2023 magonjwa yaliyojitokeza zaidi ni Ndigana kali, Ndigana baridi, Homa ya Mapafu kwa ng’ombe na mbuzi, ugonjwa wa Mapele ngozi, Kideri na homa ya matumbo kwa kuku na Ndui.

Ili kukabiliana magonjwa ya Mifugo, Mkoa umesimamia utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ambapo Ng'ombe **5,456** wamepatiwa chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu (CBPP), mbwa **9,567** na paka **30** wamepatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha Mbwa (Rabies), Kuku **243,765** dhidi ya Ugonjwa wa Kideri, ugonjwa wa Ndui na ugonjwa wa Gumboro.

Matokeo ya uogeshaji katika Mkoa wa Ruvuma ni kupungua kwa vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo.

Pamoja na jitihada hizi katika zoezi la uogeshaji mifugo kuna changamoto ambazo ni pamoja na;

Uchache wa mifugo inayoogeshwa kwa majosho yaliyo mengi, hivyo kupelekea ugumu wa uendeshaji wa majosho kwasababu majosho yaliyo mengi yalijengwa kwa ajili ya uogeshaji ng'ombe na mbuzi wa maziwa.

Kukosekana kwa majosho ya kuogeshea Mifugo katika vijiji 24 vyenye maeneo ya kuchungia kwa mfumo wa ranchi ndogo. Hali hii imepelekea kuendelea kuwepo kwa vifo vya Mifugo kutokana na magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo katika ranchi hizo.

**ii. Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa**

Mkoa una mbwa **43,919** ambao wako wanaofugwa kisasa na wengine wanaofugwa kiholela. Kufuatia kuwepo kwa idadi kubwa ya mbwa wanaozurura mitaani na kuwa kero kwa ustawi na afya ya jamii inayotuzunguka, kumekuwa na jitihada za kuchanja mbwa ili kudhibiti ugonjwa huu unaoathiri wanyama na binadamu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Desemba, 2023 mbwa **9,567** walichanjwa. Pia kumekuwepo na matukio **73** ya mbwa kung'ata binadamu. Pamoja na juhudi hizo Mkoa unaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa, kampeni ya uchanjaji mbwa, na kuua mbwa wote wanaozurura ili kuendelea kuilinda jamii dhidi ya ugonjwa huu.

Mkoa umepokea dozi **7,000** za chanjo ya kichaa cha Mbwa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuadhimisha wiki ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wa mbwa. Wiki hiyo iliadhimishwa kuanzia tarehe 24 Septemba, 2023 hadi tarehe 28 Septemba, 2023.

**iii. Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF)**

Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe uliripotiwa Mwezi Juni katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga, Tunduru, Nyasa, Songea, Madaba, Mbinga Mji, na Manispaa ya Songea. Ugonjwa huu ulisababisha vifo vya Nguruwe zaidi ya **1,300**. Takwimu zinaonesha ugonjwa ulivyoenea kwa kasi na kupelekea madhara makubwa ya kiuchumi kwa wafugaji na wafanyabiashara ya nguruwe mkoani Ruvuma.

Imegundulika kuwa mambo yanayosababisha ueneaji wa ugonjwa kutoka eneo moja hadi jingine ni pamoja na kuhamisha nguruwe hai kutoka eneo moja lililoathirika hadi eneo lingine lisiloathiriwa na ugonjwa, kupeana zawadi za nguruwe au nyama kutoka

kwa ndugu wa eneo lilioathirika na kupeleka eneo lingine lisiloathirika, kusafirisha nyama za nguruwe kutoka kwenye maeneo yaliyoathirika na ugonjwa, kusafirisha samadi ya nguruwe kutoka kwenye maeneo yaliyoathirika na ugonjwa.

Ili kukabiliana na ugonjwa huu hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwemo: -

- Kuitisha vikao vya wadau wa sekta ndogo ya nguruwe ambao ni wafanyabiashara ya nguruwe, wafugaji wa nguruwe, Wasafirishaji wa mabasi, Maafisa mifugo pamoja na viongozi ngazi ya Mkoa na Wilaya.
- Kuimarisha ukaguzi wa nguruwe wote wanaochinjwa kwa kuwakagua kabla ya kuchinja (Antemortem) na baada ya kuchinja (Postmortem) ili kuzuia kusambaza kwa ugonjwa kupitia machinjio.
- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu dalili za ugonjwa na hatua za kuchukua kuzuia kusambaa zaidi.
- Kuzuia usafirishaji wa nguruwe kwenye maeneo yaliyoathirika na kutumia sheria ndogo za Halmashauri kutoza faini kwa wadau wanaokiuka sheria ya magonjwa ya Mifugo hasa utaratibu wa kusafirisha nguruwe.
- Kuelimisha Maafisa Ugani juu ya namna ya kudhibiti ugonjwa pamoja na kuchukuwa tahadhari pale wanapotibu au kuhudumia mifugo pamoja na kuacha kutibu nguruwe wagonjwa.
- Halmashauri kuandaa vifaa (mabomba na dawa aina ya VIRD) na nguvu kazi ya kuangamiza mashamba yote yaliyoathirika kwa kushirikiana na chama cha wadau wa nguruwe.
- Kupulizia dawa aina ya VIRD kwenye mabanda yote yaliyoathirika
- Kufukia na kuchoma nguruwe wote waliopata ugonjwa na waliokufa ili kuzuia ueneaji wa virusi.

#### 7.1.3.4 Mashamba Darasa

**Mashamba Darasa ya Malisho**

Athari za kupungua kwa malisho zimeendelea kujitokeza mara kwa mara kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo, mabadiliko ya tabia ya nchi na mtazamo wa wafugaji kutegemea malisho ya asili tu. Athari hizo zimesababisha mifugo kudhoofika na wakati mwingine kufa kwa kukosa malisho na maji.

Katika jitihada za kukabiliana na athari hizo, Wizara imeandaa mpango wa kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha, kutunza na kuhifadhi malisho kupitia

utaratibu wa mashamba darasa ya malisho katika maeneo ya malisho. Katika utekelezaji wa mpango huu kazi zote zitakazohitaji nguvu kazi zitafanywa na vikundi vya vijana waliopo kwenye maeneo husika. Lengo la mpango huu ni kubadili mtazamo wa wafugaji kutegemea malisho ya asili tu na kuboresha maeneo ya malisho yaliyopo.

Wizara ilitoa fedha za kuanzisha mashamba darasa ya malisho 8 yenye jumla ya ukubwa wa ekari 40 katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Songea, Namtumbo na Tunduru. Lengo kuu la mpango huu ni kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha, kutunza na kuhifadhi mbegu na malisho kwa kutumia utaratibu wa mashamba darasa. Wafugaji walishiriki kikamilifu katika mpango huu kuanzia hatua maandalizi ya shamba kulima na kuhudumia mashamba hayo. Mashamba haya yalishavunwa.

Kwa mwaka 2023/24 tunategemea kuwa na mashamba darasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Madaba ambapo kutakuwa na mashamba darasa **5** yenye jumla ya ekari **35**.

#### 7.1.3.5 Fursa

Kutokana na mifugo iliyopo na mazao yake zinafungua fursa zifuatazo za kiuchumi:

- Ufugaji wa ng’ombe wa maziwa na uzalishaji wa mitamba;
- Usindikaji wa mazao ya mifugo;
- Ujenzi wa viwanda vya vyakula vya mifugo, na mashamba ya malisho; na
- Uzalishaji wa Vifaranga vya kuku wa nyama na mayai.

#### 7.1.3.6 Changamoto

- Kukosekana kwa mitamba bora ya Ng’ombe wa maziwa;
- Ukosefu wa Malisho na Viwanda vya kusindika mazao;
- Changamoto ya Magonjwa ya Mifugo.

#### 7.1.3.7 Mapendekezo/Mikakati ya Utatuzi wa Changamoto

- Kuhimiza matumizi ya kinga zaidi kuliko tiba kwa mifugo;
- Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo;
- Kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wenye tija; na
- Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya mifugo.

### 7.1.4 SEKTA YA UVUVI.

### 7.1.4.1 UTANGULIZI

Katika sekta ya uvuvi, Mkoa unategemea kupata mazao ya Uvuvi kutoka ziwa Nyasa, Mito na Mabwawa ya kufugia samaki. Hata hivyo tija itokanayo na vyanzo hivyo vya samaki haitoshelezi mahitaji ya Mkoa ambayo ni zaidi ya tani**18, 000** kwa mwaka hivyo kupata samaki kutoka nje ya Mkoa kwa wastani wa Tani **55** kwa mwezi. Uzalishaji wa samaki wa kufuga ni wastani wa tani **121.20** kwa mwaka. Watalaam wanaendelea kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ili kukidhi mahitaji ya walaji. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka **2019** hadi Septemba **2023** jumla ya wavuvi **7,635** walisajiliwa ikiwa ni pamoja na vikundi **38** vya wavuvi na vikundi **4** vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi **(BMUs**) viilivyopo mwambao wa Ziwa Nyasa. Uzalishaji wa samaki katika Ziwa Nyasa na Mito ni wastani wa tani **480** kwa mwaka zenye thamani ya **Tshs. 2, 400, 000,000.00**. Aina ya samaki wanaovuliwa katika Ziwa Nyasa na Mito ni pamoja na **Mbufu, Mbelele, Mbasa, Kambale, Vitui, Perege, Ningu, Mchali pamoja na Dagaa**.

### 7.1.4.2 IDADI YA MAAFISA UVUVI.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Watalaam wa uvuvi **17** ambapo katika ngazi ya Mkoa ni mmoja (**1**) na kumi na sita (**16**) wako katika ngazi za Halmashauri za wilaya.

**Jedwali Na 1; Jumla ya Wataalam wa Sekta Uvuvi Mkoa wa Ruvuma**

| | Wanaohitajika | Waliopo | Mapungufu | Waliopo kwenye mpango wa kuajiriwa 2022/2025 |
|---|---|---|---|---|
| Tunduru DC | 12 | 2 | 10 | 4 |
| Namtumbo DC | 21 | 2 | 19 | 8 |
| Mbinga DC | 31 | 3 | 28 | 6 |
| Nyasa DC | 22 | 4 | 18 | 10 |
| Songea DC | 18 | 0 | 18 | 14 |
| Madaba DC | 9 | 3 | 6 | 2 |
| Songea MC | 5 | 2 | 3 | 3 |
| Mbinga TC | 14 | 0 | 14 | 2 |
| **Jumla** | **132** | **16** | **116** | **49** |

### 7.1.4.3 UZALISHAJI WA SAMAKI KATIKA MABWAWA.

Mkoa una wafugaji wa samaki **4,159** wenye jumla ya mabwawa **6,582 y**enye wastani wa uzalishaji wa tani **121.20** kwa mwaka.

Ufugaji wa samaki ni shughuli ambayo wananchi wengi wamekuwa wakiifanya katika kuongeza kipato na lishe katika jamii inayowazunguka.

Kutokana na kutotosheleza kwa vyanzo vya samaki vilivyopo kwenye Mkoa, wananchi kuhamasishwa kufuga samaki kwa tija katika mabwawa ili kuweza kukidhi mahitaji hayo kwa ajili ya chakula na kwa biashara pia. Ndani ya Mkoa kuna kituo kimoja **(1)** cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki chenye uwezo wa kuzalisha vifaranga **3,000,000** kwa Mwaka,kituo hicho kipo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Ruhila (**RADC)** kilichopo Manispaa ya Songea.

### 7.1.4.4 FURSA ZILIZOPO KATIKA UFUGAJI WA SAMAKI.

- Mwamko wa wananchi wa Mkoa kuhamasika na ufugaji wa samaki;
- Uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo,mito, chemchem na mabwawa ya Asili/Malambo zaidi ya kumi na nne (**14**) katika Mkoa yenye fursa ya ufugaji kwa kupandikiza au kufuga kwa njia ya vizimba (Cage culture);
- Uwepo wa ziwa Nyasa linalofaa kwa ufugaji wa njia ya vizimba (cage culture);
- Uwepo wa mahitaji makubwa ya samaki katika Mkoa na soko la uhakika.
- Uwepo wa wafugaji wa samaki zaidi ya **4,159** na mabwawa ya samaki zaidi ya **6,582;** na
- Upatikaniji wa uhakika wa malighafi za kutengenezea chakula cha samaki.

**Jedwali Na 2: Idadi ya Mabwawa, Wafugaji na Wastani wa Hali ya Uzalishaji wa Samaki katika Mabwawa kwa Mwaka.**

| Halmashauri | Idadi ya wafugaji | Idadi ya mabwawa | Uzalishaji (tani) |
|---|---:|---:|---:|
| Tunduru DC | 315 | 463 | 3.90 |
| Namtumbo DC | 200 | 71 | 1.3 |
| Songea MC | 955 | 937 | 7.1 |
| Mbinga DC | 951 | 1,293 | 8.4 |
| Songea DC | 1,327 | 3,227 | 96.8 |
| Nyasa DC | 168 | 225 | 1.4 |
| Mbinga TC | 215 | 310 | 1.2 |
| Madaba DC | 28 | 56 | 1.1 |
| **JUMLA** | **4,159** | **6,582** | **121.20** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa.***

### 7.1.4.5. MATUMIZI YA ZANA BORA ZA UVUVI.

Katika matumizi ya zana bora za uvuvi, jitihada zimewekwa ili kujenga uwezo wa wananchi kutambua madhara yatokanayo na matumizi ya zana haramu za uvuvi , utoaji wa elimu juu ya matumizi bora ya zana za kisasa za uvuvi zinazokubalika

kisheria, kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuhamasisha ufugaji bora wa kisasa na wenye tija. Pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi (**Beach Management Units -** BMUs) doria mbalimbali hufanyika hasa katika mwambao wa ziwa Nyasa na Mto Ruvuma kwa kushirikiana na vikundi vya **BMUs** ili rasilimali za uvuvi zitunzwe, zilindwe na ziwe endelevu,na mpaka kufikia Disemba **2023** wavuvi **5,488** walisajiliwa na leseni **2,670** za Uvuvi zilitolewa.

### 7.1.4.6 HALI YA MIUNDOMBINU YA UVUVI.

Ujenzi wa karakana ya kuunda boti za uvuvi za kisasa katika kituo cha Mbamba bay umefikia hatua za mwisho za kuweka mashine,pia soko la Samaki la Mbamba bay bado alijaanza kutumika kutokana na kutokukamilika kwa miundombinu ya maji na choo ingawa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia **98.**Aidha, ujenzi wa Mwalo wa kisasa wa Kijiji cha ng'ombo utaanza mwaka huu wa fedha **2023/2024.**Mwaka **2019** Halmashauri ya Nyasa ilipata fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 200** kwa ajili ya Mradi wa utengenezaji wa boti za Uvuvi za kisasa,na mpaka kufikia Disemba **2023** boti **2** zimeshakamilika na zinafanya kazi, na boti **4** bado hazijakamilika.Aidha,katika mwaka wa fedha **2023/2024** Halmashauri ya Nyasa imepokea fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 300** kwa ajili ya utengenezaji wa Boti ya doria ya kisasa.Pia katika mwaka wa fedha wa **2022/2023** Halmashauri Songea ilipokea fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 123** kwa ajili ya ujenzi wa shamba darasa moja la ufugaji bora wa Samaki.

### 7.1.4.7 MIKAKATI YA KUENDELEZA SEKTA YA UVUVI.

- Kuhimiza matumizi ya zana bora za uvuvi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ambapo hadi kufikia Disemba **2023** zaidi ya wavuvi **5,488,** wafugaji **4,159** na wadau **470** wamefundishwa njia bora za uvuvi,ufugaji bora wa samaki na utunzaji wa mazingira.
- Kuendeleza/kuboresha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi hasa mialo(**Land stations**), na katika mwaka huu wa fedha **2023/2024** Wizara ya Mifugo na Uvuvi(sekta ya uvuvi) ina mpango wa kujenga mualo **1** katika kijiji cha Ng'ombo**.**
- Kutoa elimu endelevu ya uanzishaji wa vikundi vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi(**BMUs**) katika mwambao wa ziwa Nyasa.

- Kuhimiza uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki, ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba (***cage***) katika ziwa na mabwawa ya asili ili kupata mavuno mengi ya samaki yatakayofaa kwa ajili ya viwanda.
- Kukijengea uwezo kituo cha maendeleo ya ufugaji samaki Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga bora na vya kutosha, kwa sasa kituo kina uwezo wa kuzalisha vifaranga **3,000,000** kwa mwaka ukilinganisha na mahitaji ya vifaranga **5,000,000** kwa mwaka kwa Mkoa mzima.
- Kila Halmashauri kuwa na kituo cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki ambapo vituo hivyo vitatumika pia kama mashamba darasa.
- Kuendeleza doria za mara kwa mara ili kuzuia utumiaji na uingizaji wa zana haramu za uvuvi katika ziwa na mito pamoja na kuvikagua vyombo vyote na kuvisajili kisheria.
- Ujenzi wa soko la samaki lililopo Mbamba bay upo katika hatua za mwisho ili liweze kutumika.
- Mradi wa ujenzi wa maboti **6** za kisasa za Halmashauri bado unaendelea, mpaka kufikia Disemba **2023,** boti **2** tayari zimeshakamilika na zinafanyakazi.
- Mpaka kufikia Disemba **2023** Halmashauri ya Nyasa ilishapokea fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 300** kwa ajili ya matengenezo ya Boti ya doria ya kisasa.

**7.1.4.8 CHANGAMOTO.**

- Uvuvi wa kutumia miti yenye sumu **(Mtupa**) bado ni tatizo katika baadhi ya maeneo ya mito ya Ruhuhu, Ruhekei na Mbawa katika Wilaya ya Nyasa;
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya kufanya doria za mara kwa mara;
- Uhaba wa watumishi wa kada ya uvuvi katika Mkoa wa Ruvuma hususani mwambao wa ziwa Nyasa;
- Kusuasua kwa uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika Halmashauri za wilaya.
- Ukosefu wa elimu endelevu kwa wavuvi juu ya madhara ya matumizi ya zana haramu za Uvuvi na uvuvi haramu kwa ujumla.
- Uchache wa vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali zaUvuvi (**BMUs**), mpaka sasa kuna BMUs **4** tu kati ya **24** zinazohitajika kwa mwambao mzima.
- Ushiriki mdogo wa ulinzi shirikishi wa rasilimali za Uvuvi kwa wadau mbalimbali;

- Katika kipindi cha mwaka **2020** hadi **2023,** zana haramu za Uvuvi aina ya timba (***monofilament)*** pamoja na makokolo zenye urefu wa zaidi ya mita **8,000** na thamani ya zaidi ya shilingi **57,000,000/=**zilikamatwa na kikosi cha kulinda rasilimali za Uvuvi (**FRP)** kwa kushirikiana na Halmashauri.
- Uhaba wawataalamu wa sekta ya Uvuvi unadhoofisha shughuli za Uvuvi na hasa Ukusanyaji wa Takwimu na maduhuli ya Serikali.

#### 7.1.4.9 MAPENDEKEZO YA KUTATUA CHANGAMOTO.

i. Halmashauri za Wilaya ziendelee kuomba kuajiri watumishi wapya hususani Halmashauri ya Nyasa ambayo inamahitaji makubwa ya watumishi wa kada ya uvuvi;
ii. Kuwahusisha wadau wote katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi hasa jamii ya wavuvi wenyewe ili rasilimali za uvuvi ziwe endelevu kwa kizazi kijacho;
iii. Halmashauri za wilaya zifanye doria za mara kwa mara katika mito ili kukomesha uvuvi haramu wa kutumia miti ya sumu;
iv. Kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika kila Halmashauri ya wilaya ili kukidhi mahitaji ya wafugaji; na
v. Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki (**floating pellets)** ili viweze kuwasaidia wafugaji wa samaki kwenye vizimba.

### 7.1.5 SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

#### i. MISITU

Mkoa umekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha juu ya upandaji miti na utunzaji mazingira. Uhamasishaji huu huenda sambamba na utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti ambao hufanyika kila mwaka kwenye Halmashauri zote.
Mkoa wa Ruvuma una lengo la kupanda miti kibiashara eka 100,000 kwa muda wa miaka kumi (10) toka 2015 – 2025.Mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya serikali kuu, serikali za Mitaa, vyuo na shule.

Kwa msimu wa mwaka 2023/24 Mkoa wa Ruvuma utapanda jumla ya miche ya miti 4,099,014 ambapo itapandwa katika Halmashauri zote, miti hii ni kwa ajili ya mbao, vyanzo vya maji na matunda. Jedwali hapo chini linaonyesha uzalishaji wa miche ya miti itakayopandwa kwa msimu huu wa mvua 2023/24.

**Jedwali Na. 1 Idadi ya Miche ya Miti Mkoa wa Ruvuma Mwaka - 2024**

| | | IDADI YA MICHE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Bustani (nursery)** | | | | |
| | | **Mbao** | **Vyanzo vya maji** | **Matunda** | **Jumla** |
| Songea | Matogoro TFS | 120,000 | 5,000 | 10,000 | 135,000 |
| | Mahenge | 100,000 | 20,000 | 35,000 | 155,000 |
| | AVIV FARM | | 31,000 | | 31;000 |
| | Bombambili | 70,000 | 10,000 | 200 | 80,200 |
| Namtumbo | | 57964 | 14400 | 3572 | 75,936 |
| Mbinga DC | | 177,673 | 38,180 | 620 | 216,473 |
| Mbinga Mji | | 1,081,969 | 16,100 | 162,130 | 1,260,199 |
| Nyasa | | 152,500 | 1,060 | 9,846 | 163,406 |
| Madaba | | 100,000 | 30,000 | 300 | 130,300 |
| Wino TFS | | 1,000,000 | | | 1,000,000 |
| Tunduru | | 150,000 | 2000 | 700,000 | 852,000 |
| **Jumla** | | **3,009,606** | **167,740** | **921,668** | **4,099,014** |

### ii. HALI YA UFUGAJI NYUKI KIMKOA

Hadi sasa Mkoa una jumla ya mizinga **16,378** ambapo mizinga ya kisasa ni **10,883** na mizinga ya kienyeji ni **5,495**.

**Jedwali Na. 2 Idadi ya Mizinga ya Nyuki**

| S/N | WILAYA | IDADI YA MIZINGA | | | UZALISHAJI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KISASA | KIENYEJI | JUMLA | ASALI - kg | NTA |
| 1 | Nyasa | 1473 | 361 | 1,834 | 1986 | 65 |
| 2 | Mbinga | 3712 | 1231 | 4,943 | 7850 | 0 |
| 3 | Songea | 3492 | 523 | 4,015 | 8100 | 0 |
| 4 | Namtumbo | 1387 | 2675 | 4,062 | 209 | 0 |
| 5 | Tunduru | 819 | 705 | 1,524 | 3300 | 92 |
| | Jumla | 10,883 | 5,495 | 16378 | 21,445 | 157 |

Katika suala la uzalishaji wa asali katika mkoa wa ruvuma linakumbwa na baadhi ya changamoto hadi kupelekea kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki.changamoto ni kama zifuatazo;

i. Wafugaji nyuki wengi hawana utaalamu wa ufugaji nyuki wa kubiashara.
ii. Moto wa msituni ambao hutokea mara kwa mara hasa hasa kwenye miombo
iii. Ukosefu wa masoko ya uhakika unapelekea wafugaji nyuki kutothamini ufugaji nyuki
iv. Ukosefu wa mitaji hasa katika suala la kupata mizinga.

### 7.2 VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

#### 7.2.1 Viwanda.

**Uwekezaji Katika Viwanda.**

a) **Viwanda vikubwa**

Mkoa wa Ruvuma una viwanda vikubwa sita **(6)** kati ya hivyo viwanda vitatu ni vya kukoboa kahawa (coffee curing) ambavyo vipo katika Wilaya ya Mbinga na kiwanda kimoja ni cha kubangua korosho ambacho kipo katika Wilaya ya Tunduru. Pia Mkoa una kiwanda cha kuzalisha unga wa sembe na kufua umeme katika Wilaya ya Songea.

b) **Viwanda vya kati**

Katika Mkoa wa Ruvuma kuna viwanda vya kati ni ishirini na tano (**25)** ambavyo ni vya kuzalisha Unga wa Sembe, Maziwa, Mikate, Nyama, Samani, maji ya kunywa na Vitabu.

c) **Viwanda Vidogo**

Mkoa wa Ruvuma una viwanda vidogo **190** na viwanda vidogo sana **3,264** vya kuchakata, kusindika na kutegeneza bidhaa ambavyo ni viwanda vya useremala, viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka, kukamua mafuta ya alizeti pamoja na usindikaji wa vyakula mbalimbali ambavyo vimechangia ukuaji wa ajira katika Mkoa wa Ruvuma.

#### 7.2.2 Biashara

a) **Masoko**

Mkoa wa Ruvuma una Masoko mbalimbali ambapo Bidhaa huuzwa kwenye masoko, takwimu za masoko hayo ni kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 1: Takwimu za masoko kwa Halmashauri**

| Na. | HALMASHAURI | MASOKO | MIUNDOMBINU ILIYOPO |
|---|---|---|---|
| 1 | Songea MC | Soko kuu Manispaa, Soko la Mazao Msamala, Soko la Mjimwema, Soko la Bombambili, Soko la Mshangano, Soko Ruhuwiko, Soko la Lizaboni, Soko la Majengo, Soko la Mfaranyaki, | Umeme, maji na vyoo |
| 2 | Mbinga TC | Soko kuu, Soko la Misheni, Soko la Makita. Soko la Mbano | Umeme, maji na vyoo |
| 3 | MBINGA DC | Nyoni, Maguu, Matekela, Ilela, Mpapa, | Umeme, maji na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Luagala,Kingonsera, Matiri,Ruanda, Malindindo, Ugano | vyoo |
| 4 | MADABA | Lituta | Umeme, maji na vyoo |
| 5 | NYASA | Soko kuu Kilosa, Mbamba bay | Umeme, maji na vyoo |
| 6 | NAMTUMBO | Soko kuu Namtumbo, Soko la Litola, Soko la Lusewa, | Umeme, maji na vyoo |
| 7 | TUNDURU | Azimio, Nakapanya, Matengo | Umeme, maji na vyoo |
| 8 | SONGEA DC | Peramiho, Namihoro na Kizuka | Umeme, maji na vyoo |

**b) Upangaji wa machinga katika maeneo rasmi ya kufanyia biashara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati ikizindua Mpango wa uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022, alielekeza kuwapanga machinga na zoezi hilo, lifanyike kwa umakini kwa lengo la kuepuka vurugu, fujo na uonevu. Ambapo Mkoa wa Ruvuma kupitia maekelezo hayo tulianza kutekeleza.

**c) Hali ya utekelezaji wa maelekezo ya upangaji wa Machinga.**

I. Kuunda Uongozi wa Machinga kwa ngazi ya Mkoa na ngazi ya Halmashauri kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma haukuwa na uongozi wa machinga.

II. Kuwaunganisha Viongozi wa Machinga Mkoa na Viongozi wa Machinga Taifa na kushiriki semina mbalimbali za Viongozi wa Machinga zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika Dodoma.

III. Halmashauri zimetenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Machinga.

IV. Halmashauri zimeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya masoko na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za Machinga.

V. Halmashauri ya Manispaa ya Songea inaendelea na hatua za ujenzi wa Ofisi za Machinga

### 7.2.3 Uwekezaji

**d) Fursa za uwekezaji zilizopo Katika Mkoa wa Ruvuma.**

Mkoa wa Ruvuma una fursa kadhaa ambazo hutumiwa katika kusukuma mbele maendeleo ya Mkoa. Fursa za msingi zilizopo ni kama zifuatazo: -

(i) Eneo kubwa linalofaa kwa kilimo kwa mazao yote ya chakula na biashara;

(ii) Hali nzuri ya hewa; Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa michache nchini yenye bahati ya kupata mvua za kutosha ambazo hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Mei kila mwaka. Wastani wa kiasi cha mvua inayonyesha kwa mwaka ni mm.1100;

(iii) Mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Mkoa wa Ruvuma una jumla ya hekta **197,108.2** zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta **7,388.3** zimeendelezwa,hii ni sawa na asimilia **3.7**. Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa skimu **23** zinafanya kazi na **19** hazifanyi kazi.

(iv) Maeneo yenye jumla ya ukubwa wa ekari **57,743.35** yametambuliwa kwa ajili ya kilimo cha pamoja katika halmashauri 8 za Mkoa wa Ruvuma.

(v) Kuwepo kwa mazao ya chakula na biashara katika kila Wilaya. Mazao hayo ni pamoja na mahindi, mpunga, kahawa, korosho na tumbaku;

(vi) Uwepo wa Maliasili. Mkoa wa Ruvuma una maliasili nyingi zikiwemo madini, wanyama pori na misitu ya asili;

(vii) Kuwepo kwa nguvukazi ya kutosha. Mkoa una wananchi wenye ari kubwa ya kufanya kazi kwa bidii kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka; na

(viii) Kufunguka kwa miundombinu ya barabara, Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma zimeunganishwa na mtandao wa barabara za lami. Pia Mikoa mingine inayotuzunguka imeunganishwa na barabara ya kiwango cha lami.

(ix) Uwepo bandari ya Mbamba bay na Ndumbi kwenye ziwa Nyasa inayowezesha usafirishaji wa Mizigo na Abiria kwa njia ya maji kwenye nchi jirani ya Malawi na maeneo mengine yanayofikiwa na ziwa Nyasa.

**e) Maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za Uwekezaji.**

Mkoa wa Ruvuma kupitia Halmashauri imetenga maeneo kwa ajili ya Shughuli za uwekezaji na ujenzi wa Viwanda kama ifuatavyo:

a) **Halmashauri ya Manispaa ya Songea:** Mletele ekari **3,619.17,** Mwanamonga Ekari **3,581.68,** Lilambo Ekari **953.7,** Tanga ekari **1,659**, Mwengemshindo (EPZA) **5,000,** Ruhuwiko **117.33.**

b) **Halmashauri ya Mji Mbinga:** jumla ya Ekari 186.61 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa ujenzi wa Viwanda katika maeneo ya Lusaka – Mwembe, Lusaka Maumba, Tanki la Maji, Luponda na uteri.

c) **Halmashauri ya Madaba:** katika Halmashauri ya Madaba jumla ya Ekari 400 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji katika maeneo ya Ifungwa.

d) **Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo;** Jumla ya Ekari 89.68 zimetengwa kwa ajili ya Shughuli za uwekezaji katika maeneo ya Kituo kikuu cha Mabasi, Hospitali ya Wilaya, Mchafu Kuoga, Minazini, Mageuzi, VETA Suruti.

e) **Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru:** Jumla ya Ekari 140.12 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji katika maeneo ya Nakayaya, Nakayaya Magharibi, Ngalinje, EPZ

f) **Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa:** Jumla ya Ekari 41 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za Uwekezaji katika eneo la Kilosa.

**f) Uwekezaji katika Sekta ya Maliasili.**

**a) Misitu.**

Vipo viwanda 4 vikubwa vya kuchakata mazao ya misitu kati ya hivyo 2 za watu Binafsi zipo katika maeneo ya Madaba na Mbinga, 2 vipo katika maeneo ya Tunduru, Namtumbo na Songea ambavyo vinafanya uvunaji na uchakataji wa mbao kwenye misitu ya vijiji ambazo zimefadhiliwa na WWF (World Wide Fund- for nature) pamoja na mradi wa FORVAC.

**b) Wanyamapori.**

Katika sekta ya wanyamapori tuna wawekezaji wawili katika vitalu vya uwindaji wa kitalii 1 ni Wembere Hunting Safari aliye katika kitalu cha Mwantis B katika Kijiji cha Ifinga Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na The Best Luxury Safari aliyepo katika vitalu vilivyopo katika Hifadhi za jamii WMA za Mbarang'andu iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na Nalikailiyopo Halmashauri ya wilaya ya Tunduru.

**g) Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo.**

Mkoa wa Ruvuma una fursa ya kupata mvua nyingi, ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo na inayokubali kuzalisha takribani mazao aina zote. Mazao ya chakula yanayolimwa ni Mahindi, Mpunga, Muhogo, Maharage, Mtama, Ulezi, Mbaazi na Viazi Vitamu. Mazao ya biashara ni Tumbaku, Kahawa, Korosho, Ufuta, Soya, Alizeti, Tangawizi, Mbaazi na Karanga. Mazao ya bustani ni pamoja na Parachichi, Embe, Machungwa, Matikiti, Ndizi, Papai na Mbogamboga. Hekta **4,**

**007,746** zinafaa kwa kilimo, hadi sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **583,279** sawa na asilimia **15** ya eneo lote**,** na kufanya Mkoa kuwa na ziada ya hekta **3, 424,467** sawa na asilimia **85.**

Wawekezaji wakubwa waliojitokeza kuwekeza katika Mkoa wa Ruvuma kwenye Sekta ya Kilimo. Mkoa wa Ruvuma unawawekezaji wakubwa wawili waliowekeza katika Sekta ya Kilimo ndani ya Mkoa wa Ruvuma ambao ni Shamba la Kahawa la AVIV linalomilikiwa na kampuni ya OLAM ambayo inaendesha shughuli zake katika nchi 72 na ina aina 47 za bidhaa. Ukulima wa kahawa katika shamba hili unajulikana kama *single origin*/nchi moja shamba moja kwa maana kwamba inazingatiwa masuala makubwa matatu ambayo ni kilimo biashara, kilimo mazingira na kilimo shirikishi.

Kampuni hii inarudisha faida yao kwa jamii kiasi cha shilingi 160 ikiwa ni pamoja na utoaji wa madawati, uchimbaji wa vyoo, nyumba za walimu, zahanati na nyumba za madaktari. Jamii zilizofaidika zimechangia kiasi cha shilingi milioni 100. Na pia shamba kubwa na **Ndolela Farm** shamba kubwa lililopo katika Halmashauri ya Madaba.

Hivi karibuni amejitokeza muwekezaji mwingine Mkubwa kutoka nchini Uganda Kampuni ya **Madhvan Group Ltd** imeonesha nia ya kuwekeza katika kilimo cha Miwa na Kiwanda cha Sukari katika kijiji cha Magwamila kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma. Muwekezaji huyu ana uzoefu mkubwa katika uwekezaji wa Sekta ya Sukari na anamiliki kiwanda kingine Nchini Uganda kinachojulikana kwa jina la **Kakira Sugar Ltd** chenye uzalishaji wa tani 187,662 kwa mwaka na kimeajiri watu 12,000. Tarehe 21 – 22 Agosti, 2023 alikuwa hapa Mkoani Ruvuma kwa ajili ya kufuata taratibu mbalimbali za kisheria za umilikishwaji wa ardhi.

**h) Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo**

a) Shamba la Ng’ombe wa Nyama la Kampuni ya SOAGRO kijiji cha Muhukulu Halmashauri ya Wilaya ya Songea
b) Ufugaji wa Ng’ombe wa Nyama Ndolela Silverland Halmashauri ya Wilaya ya Madaba
c) Viwanda vya kuchakata Nyama (Sausage)
    - Abbasia Peramiho na

- Benedict Sisters Chipole

d) Kiwanda cha Kutengeneza Vyakula vya Mifugo na Samaki Ample Company Ltd Manispaa ya Songea.

e) Viwanda vya vidogo vya kusindika Maziwa

Mkoa una viwanda vidogo vya kusindika maziwa vitano ambavyo ni Rufco Ltd, Deiwaka, Peramiho, Jema na Ngosha

f) Machinjio ya Kisasa ya Tanga Manispaa ya Songea

g) Ranchi ndogozaMifugoTunduru na Madaba.

**i) Uwekezaji katika Sekta ya Madini**

Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na madini aina mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali. Wawekezaji mbalimbali wapo katika Mkoa wa Ruvuma wakijishughulisha na Shughuli za Uchimbaji wa Madini hayo ikiwepo kampuni Kubwa za Ruvuma Coal Ltd, Tancoal, Jitegemee Company Ltd na makampuni mengineyo zaidi ya 16 yanayojishuhulisha na Uchimbaji wa Makaa ya mawe.

**Jedwali Na. 2: Aina ya madini yanayopatikana katika Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | Aina ya Madini | Mahali yanapopatikana |
|---|---|---|
| 1 | Dhahabu | • **Nyasa** (Darpori, Mpepo na Nindi)<br>• **Mbinga** (Mhongozi na Lukalasi)<br>• **Namtumbo** (Kitanda)<br>• **Tunduru** (Mbesa na Mbati) |
| 2. | Shaba | • **Nyasa** (Mt. Livingstone)<br>• **Mbinga** (Ndongosi)<br>• **Tunduru** ( Mbesa na Mbati) |
| 3 | Makaa ya Mawe | • **Nyasa** (Liweta na Malini)<br>• **Mbinga** (Luanda, Mbuyula na Paradiso)<br>• **Songea** (Mhukuru) |
| 4 | Chuma | • **Namtumbo** (Mtonya) |
| 5 | Urani | • **Namtumbo** (Mtonya) |
| 6 | Madini ya Ujenzi na Viwanda *(Mchanga, Kokoto, Moramu naMawe)* | • **Nyasa**<br>• **Mbinga**<br>• **Namtumbo**<br>• **Songea** (Mhukuru na Mtyangimbole) na<br>• **Tunduru** |
| 7 | **Madini ya Vito** (*Sapphire, Ruby, Alexandrite, Chrisoberly, Spinel, Ganet, Aquamarine,* | • **Tunduru (**Ngapa, Muhuwesi, Majimaji, Mbuyula na Lukala)<br>• **Nyasa** (Maeneo ya Mwambao wa Ziwa)<br>• **Mbinga** (Maeneo ya Mkako, Masuguru, Ngembambili, Amani Makolo na Kuhagala) |

| Na. | Aina ya Madini | Mahali yanapopatikana |
|---|---|---|
| | *Tourmaline)* | • **Namtumbo**(Mputa,Lusewa,Suluti,Mtwarapachani,Mkongo na Kiburungutu) |

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Mkoa wa Ruvuma umeweza kuvutia na kupata wawekezaji wengi waliowekeza kwenye shughuli zinazohusiana na madini kama Uchimbaji wa Madini, Ununuzi wa Madini, Usafirishaji ya Madini na Uchenjuaji wa Madini. Ufuatao ni Mchango wa Sekta ya Madini katika Mkoa wa Ruvuma na kwa sehemu kubwa madini yanayopatikana kwa wingi ni Makaa ya mawe na madini haya husafirishwa maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi na kuwa na mchango mkubwa katika Mkoa wa Ruvuma ikiwa ni pamoja na;

i. Kutoa ajira na hivyo kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi
ii. Kuongeza fedha za kigeni nchini kutokana na madini hayo kuuzwa nchi za nje; na
iii. Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri mbalimbali yatokanayo na ushuru wa huduma unaotozwa kwenye madini yanayochimbwa.

Madini ya Makaa ya Mawe ndio hutoa mchango mkubwa kwenye mapato ya maduhuli yakusanywayo na ofisi hii. Hivi karibuni ongezo la uzalishaji wa makaa ya mawe umeongezeka kwa kiasi kikubwa ambapo kwa kipindi cha Mwezi Januari, 2022 hadi Disemba, 2022 uzalishaji na makusanyo yaliyotokana na mauzo ya makaa ya mawe umeoneshwa kwenye jedwali hapa chini. Madini haya huuzwa ndani ya nchi, nchi zinazotuzunguka, barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es Salaam.

**Mikakati ya uendelezaji wa sekta ya Uwekezaji katika Mkoa wa Ruvuma.**

I. **Kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma**

Tarehe 24 -26 Julai, 2019, ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tulifanya Maonesho na kongamano la Uwekezaji ambapo katika maonesho hayo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alizindua Mwongozo wa uwekezaji ambapo kupitia muongozo huo fursa mbalimbali zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma zimeainishwa na kupitia maonesho hayo Mkoa umeweza kupokea wageni mbalimbali walionesha nia ya kuwekeza katika Mkoa wetu.

II. **Kutenga na kupima maeneo maalum ya viwanda.**

Halmashauri zimeagizwa kutenga maeneo maalum, kwa ajili wawekezaji ambayo yamepimwa na yasiyohitaji fidia kwa mwekezaji na yenye huduma muhimu kama vile maji, umeme, barabara n.k, jambo hili litasaidia kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

III. **Uanzishwaji na Uimarishaji wa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na Mkoa.**

Uendelezaji wa sekta ya viwanda unategemea uwepo wa Mabaraza ya Biashara katika ngazi za Wilaya na Mkoa. Mabaraza ya Biashara ni sehemu nzuri ya kujadili fursa na kuweka mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na taarifa za Vikao vya Mabaraza zinatakiwa kuwasilishwa katika vikao vya DCC na RCC ili maeneo yenye changamoto yaweze kutatuliwa na vikao vya ngazi hizo.

IV. **Uanzishwaji wa kongano (clusters).**

Kila Halmashauri imeagizwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuhakikisha kuwa inandaa maeneo kulingana na kongano za shughuli za viwanda ili kuweza kuanzisha industrial parks.

V. **Kuimarisha Mfumo wa Kitaasisi.**

Kuweka mazingira rahisi ya upatikanaji wa vibali na ufanyaji Biashara (Ease of Doing Business) ambayo itasaidia kuvutia wawekezaji katika maeneo yetu.

VI. **Kusimamia na kuendeleza shughuli za kijasiriamali.**

Halmashauri zimetakiwa kuwajibika kikamilifu katika kuzitambua na kuziendeleza shughuli za kijasiriamali na kuhakikisha zinatenga fedha kwa ajili ya kukuza shughuli hizo.

## 7.3 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE

### 7.3.1 Huduma za Afya

Mkoa una jumla ya vituo **419** vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo Hospitali ni **17** zikiwemo **9** za serikali, vituo vya afya **50** kati ya hivyo, **39** vya Serikali na **11** ni vya mashirika ya dini, zahanati zipo **352** ambapo za serikali ni **283**, Mashirika ya dini ni **34,** na **10** ni za mashirika ya umma na **14** ni za watu binafsi.

### 7.3.2 Utekelezaji wa miradi ya Afya

Katika kipindi cha mwaka 2023/24, Mkoa umepokea kiasi cha **Tshs. 1,800,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Afya; Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba **Tshs. 800,000,000.00**, Hospitali ya Halmashauri ya Songea Manispaa **Tshs. 800,000,000.00** na kwa upande wa Zahanati zilizopokea jumla ya **Tshs. 200,000,000.00 (Zahanati ya Ifunga – Madaba DC, Zahanati ya Likuyufusi-Songea MC, Zahanati ya Litoromelo na Litindoasili).**

### 7.3.3 Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

Vituo vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na mtoto vimefikia **348** kati ya vituo **419** sawa na **83%** ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika Mkoa. Kati ya vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Vituo **325** sawa na **78%** vinatoa huduma ya chanjo. Aidha, kati ya vituo vya afya **50,** vituo **17** sawa **34%** ya vituo vya Afya vinatoa huduma kabambe za dharura za mama wajawazito na Watoto wachanga (**CEmONC**).

Kwa upande wa huduma ya wazazi, kiwango cha akina mama waliojifungulia kituoni kimeongezeka kutoka **84%** mwaka **2022** hadi **87%** Desemba **2023**. Kiwango hiki ni juu ya lengo la taifa la **85%.**

**Jedwali Na.1: kuonesha mwenendo wa vifo vya kina mama wazazi Mkoa wa Ruvuma kwa miaka minne (4) 2020-2023**

| Na | Mwaka | Idadi ya vifo |
|---|---|---|
| 1. | 2020 | 31 |
| 2. | 2021 | 25 |
| 3. | 2022 | 22 |
| 4. | 2023 | 27 |

Idadi ya vifo vya wazazi vimeongezeka kutoka vifo **22** sawa na vifo **38/100,000** vizazi hai Desemba mwaka **2022** hadi vifo **27** sawa na vifo **43 /100,000** vizazi hai Desemba mwaka 2023. Sababu zilizochangia vifo ni Kutokwa na damu nyingi **PPH, Kifafa cha mimba, madhara ya dawa za usingizi (anaethetic complication), mgando katika mishipa ya damu (Embolism), upungufu wa damu na uambukizo.**

Vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja kwa mwaka **2023** vimeendelea kupungua kutoka **232** sawa na vifo **4/1000** ya watoto waliozaliwa hai mwaka **2022** hadi vifo **137**

sawa na vifo **2/1000 Disemba** mwaka **2023** Sababu zilizochangia vifo hivyo ni magonjwa ya watoto wachanga (perinatal condition). Vifo **35** sawa na **40%** Prematurity vifo **25** sawa na **28%**, Pneumonia vifo **13** sawa na **15%**, Malaria vifo **7** sawa na **8%,** Septicemia vifo **5** sawa na **6%** na Anaemia vifo **3** sawa na **3%** ya vifo vyote.

Takwimu za vifo vya watoto chini ya **miaka mitano** vilivyotolewa taarifa ngazi ya vituo na jamii kwa mwaka **2023** vilikuwa **219** sawa na vifo **3/1000** ya watoto waliozaliwa hai. Idadi ya vifo hivi imepungua ukilinganisha na vifo **279** sawa na vifo **5/1000** ya watoto waliozaliwa hai mwaka **2022**. Sababu zinazoongoza kwa vifo hivyo ni Neonatal condition vifo **41** sawa na **33%**, Pneumonia vifo **33** sawa na **27%** malaria vifo **24** sawa na **19%**, Septicaemia vifo **15** sawa na **12%** na Anaemia vifo **11** sawa na **9%** ya vifo vyote.

### 7.3.4 Hali ya chanjo

Mafanikio kwa kipindi cha Januari hadi Mei mwaka 2023 imeonesha kuwa kiwango cha chanjo kilichofikiwa; chanjo ya Kifua kikuu (BCG) ni **166%,** chanjo ya kuzuia kupooza (Polio **135%,** chanjo ya Donda Koo, kukakamaa na kifaduro (DTP3) **135%,** chanjo ya kuzuia homa ya mapafu (Pneumonia) **135%,** chanjo ya kuzuia kuharisha (Rota virus) **127%,** chanjo ya Surua (Measles Rubella) **152%,** chanjo ya Pepopunda (Td) kwa wajawazito **106%** na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa wasichana umri wa miaka 14 ni **126%.**

### Idadi ya watu waliochanjwa chanjo ya uviko-19

Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuchanja jumla ya watu **1,163,939** kati ya hao watu **1,050,656 (110%)** wamekamilisha dozi na watu **113,283 (10%)** hawajakamilisha dozi.

Jumla ya dozi za UVIKO-19 **1,839,169** sawa na **89%** zilitumika kuwachanja watu, dozi **148,800** sawa na **7%** hazijatumika zipo stoo ya Mkoa kati ya dozi **2,055,165** zilizopokelewa. dozi zilizotumika na zilizosalia stoo ya Mkoa zinafanya jumla ya **97%.** Hivyo upotevu wa chanjo za UVIKO-19 tangu zoezi la uchanjaji kuanza tarehe 4 Agosti, 2021 hadi Desemba, 2023 ni **3%.**

### 7.3.5 Huduma za Ustawi wa Jamii

**i. Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF)**

Mkoa wa Ruvuma unatekeleza Waraka Na.1 wa Mwaka 2018 wa Maboresho ya Mfuko wa Afya ya Jamii ambao umeleta tija kubwa kwa wananchi katika kupata huduma za afya za uhakika. Hadi kufikia 30 Disemba, 2023 jumla ya kaya **28,666 (8%)** zimeandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF) kwa malipo ya Tshs. 30,000 kwa kila kaya, sawa na makusanyo ya **859,980,000.00**.

**Jedwali Na.2: Hali ya iCHF Mkoa wa Ruvuma hadi Desemba, 2023**

| NA | HALMASHAURI | IDADI YA KAYA | KAYA ZILIZOSAJILIWA | ASILIMIA | MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MADABA DC | 12,250 | 1,716 | 14 % | 51,480,000 |
| 2. | TUNDURU DC | 82,129 | 7,243 | 9 % | 217,290,000 |
| 3. | MBINGA TC | 33,256 | 2,919 | 9 % | 87,570,000 |
| 4. | NAMTUMBO DC | 45,856 | 3,817 | 8 % | 114,510,000 |
| 5. | SONGEA DC | 33,933 | 2,709 | 8 % | 81,270,000 |
| 6. | MBINGA DC | 57,738 | 4,995 | 9 % | 149,850,000 |
| 7. | SONGEA MC | 57,640 | 3,291 | 6 % | 98,730,000 |
| 8. | NYASA DC | 37,367 | 1,976 | 5 % | 59,280,000 |
| | **JUMLA** | **360,169** | **28,666** | **8 %** | **859,980,000** |

**ii. Usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya Miaka Mitano (U5BR)**

Mkoa wa Ruvuma unasimamia utekelezaji wa mpango wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano bure katika halmashauri zote za Mkoa. Lengo la Mkoa wa Ruvuma ni kusajili na kuwapatia vyeti watoto 242,140, ambapo hadi tarehe 30 Disemba, 2023 Mkoa umeandikisha na kusajili vyeti vya watoto **274,992 (114.03%)** kwenye mfumo wa eRITA, ambapo watoto **18,680 (Me 8,662** na **Ke 10,018)** ni kutoka katika familia zenye mazingira magumu.

**iii. Utambuzi na huduma kwa watoto waishio kwenye mazingira hatarishi (WWKMH)**

Mkoa unasimamia utambuzi na huduma kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na 21 ya mwaka 2009. Hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2023 Mkoa ulitambua watoto **80,101 (Me 37,660 na Ke 42,441)** na kuwapatia huduma mbalimbali zikiwemo msaada wa kisaikolojia, afya, elimu,

msaada wa kisaikolojia, malezi kwenye makao ya watoto yatima na kuimarisha uchumi wa familia.

**iv. Utambuzi na huduma kwa watu wenye ulemavu**

Mkoa umewatambua watu wazima **7,893 (Me 3,959 na Ke 3934)** wenye ulemavu wa aina mbalimbali na watoto **3,941** wenye umri chini ya miaka mitano. Kati ya watoto walitambuliwa, wenye ulemavu wa viungo ni **1,720**, wasioona **527**, ukiziwi **626**, changamoto ya ufahamu **922** na wenye ualbino **112**. Watoto wenye uwezo wa kujumuishwa kwenye afua za ujifunzaji wameandikishwa shule.

**v. Utambuzi na huduma kwa Wazee**

Katika kipindi cha Januari 2023 hadi tarehe 30 Disemba, 2023 Wazee **67, 404 (Me 32,199 na Ke 35,205)** walitambuliwa ambapo wazee **54,279 (Me 25,516, Ke 28,763)** walipata vitambulisho vya kuwawezesha kupata msamaha wa matibabu. Aidha, Mabaraza ya Ushauri ya Wazee yameundwa katika ngazi zote za vijiji, kata, halmashauri na Mkoa.

### 7.3.6 Huduma za Lishe

Katika kuendelea na kupambana na tatizo la utapiamlo nchini, Mkoa wa Ruvuma unatekeleza viashiria mbalimbali vilivyoainishwa katika mkataba wa Lishe ulioingiwa baina ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Utekelezaji wa mkataba kwa mwaka 2023 Mkoa wa Ruvuma ulishika nafasi ya 5.

Hali ya lishe kwa Mkoa wa Ruvuma kwa mujibu wa Tanzania Demographic Health Survey and -Malaria Indicator Survey 2022 **(TDHS-MIS 2022),** kiwango cha udumavu kimepungua kutoka asilimia **41** hadi **36%** upungufu wa damu kwa watoto wenye umri kuanzia miezi 6 – 59 ni **45%**. Hivyo ukondefu ni **2.8%,** watoto wanaozaliwa na uzito pungufu ni **12%,** Watoto wanaonyonya maziwa ya mama kwa muda wa miaka miwili ni **87%,** Utoaji wa matone ya Vitamin A ni **73%** na dawa za minyoo ni **57** upungufu wad amu kwa wajawazito ni **30%,** kaya zinazotumia chumvi yenye madini joto ni Mkoani Ruvuma ni **70%.**

**Mambo yanayosababisha lishe duni ni: -**

- Ulaji duni wa chakula unaotokana na kula milo michache na kiasi kisichotosheleza mahitaji ya virutubishi mwilini, hii pia hujumuisha kutowanyonyesha watoto ipasavyo.
- Magonjwa ya mara kwa mara yanayoondoa hamu ya kula na, kusababisha ufyonzaji duni wa virutubishi na huongeza mahitaji ya virutubishi mwilini.
- Matumizi mabaya ya chakula mfano kuuza chakula chote, kutumia nafaka kutengenezea pombe nk.
- Utayarishaji mbaya wa chakula unaopoteza virutubishi kama kuosha mboga za majani baada ya kukatakata.
- Imani Potofu ya kunyonyesha watoto maziwa ya mwanzo mara baada ya kujifungua.
- Upungufu katika matunzo ya makundi maalumu (watoto wadogo, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha, wazee na wagonjwa) Makundi haya yanahitaji matunzo na huduma muhimu za kiafya kama vile chanjo, kupata vidonge vya nyongeza, kutibu maradhi na huduma za kilishe.

Katika kutekeleza mkataba wa lishe katika viashiria vya ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Halmashauri mbili ndizo zilizofanya vizuri katika viashiria vyote 9. ***Jedwali Na.3: Hali halisi ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa viashiria vya Ilani ya Chama cha Mapinduzi hadi kufikia Desemba, 2023***

| Halmashauri | % of children less than six months who are Exclusively Breastfed | % of low birth weight (less than 2.5kgs) among live birth | % of children aged 0-59 months who are stunted | % of pregnant women with Anemia (Hb<8.5g/dl) | % of children 0-59 months who are wasted | % of under-five children who are overweight/obese | % of schools (Primary and Secondary) which consume fortified maize flour | % of small and medium scale food processing industries which fortify food | % of school (Primary and Secondary) health clubs that integrates nutrition activities |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madaba DC | 91.7 | 3.83 | 5.2 | 1.6 | 1.4 | 0.8 | 11.6 | 50 | 100 |
| Mbinga DC | 97.9 | 3.55 | 0.4 | 0.8 | 0 | 0 | 0.5 | 100 | 100 |
| Mbinga TC | 96.7 | 6.77 | 0.6 | 0.8 | 0.5 | 0.5 | 2.4 | 25 | 85.6 |
| Namtumbo DC | 95.4 | 4.81 | 1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 11.4 | 100 | 80.4 |
| Nyasa DC | 100 | 4.58 | 0.4 | 0.3 | 0 | 0.1 | 0 | - | 100 |
| Songea DC | 102.1 | 6.92 | 1 | 1.9 | 0 | 0.5 | 1 | 7.1 | 98.1 |
| Songea MC | 91.7 | 5.4 | 0.2 | 2 | 0.3 | 0.7 | 4.7 | 74.6 | 58 |
| Tunduru DC | 99.7 | 4.68 | 0.1 | 0.6 | 0.2 | 0.2 | 2.2 | 9.1 | - |
| Ruvuma Region | 96.3 | 5.32 | 0.8 | 1 | 0.2 | 0.2 | 3.4 | 33 | 88.3 |

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba,2023 kadi alama ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa viashiria **11** ni Halmashauri **4** tu ndizo zilizofanya vibaya katika kiashiria cha utoaji wa fedha za mapato ya ndani kwenye kutekeleza afua za lishe kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2023/2024.

***Jedwali Na.4: Utekelezaji wa kadi alama ya mkataba wa lishe kwa kipindi cha kuanzia Julai-Desemba, 2023***

| HALMASHAURI | % of Supportive supervision Visits (CSSV) conducted | % of household salt samples collected from school children tested positive for Iodine (RTK) in a Council | % of Schools (Primary and Secondary) implementing school feeding program | Domestic funds Spent on nutrition interventions per under-five child in the Council (TZS 1000) - FY | % of children aged 6-59 months supplemented with Vitamin A during CHNM campaign - FY | % of domestic funds spent on nutrition interventions (Specific, Sensitive + Enabling) | % of mothers/caregivers of children aged 0-23 months who have received counseling on IYCF from Health Care Providers (HCPs) | % of of villages/Mitaa conducted Village/Mitaa Health and Nutrition Day (V/MHND) | Domestic budget planned for nutrition per under-five child in a Council as per National Budget Guideline | % of Food Inspections conducted in the Council | % of pregnant women who received adequate Iron Folic Acid (IFA) until next visit |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madaba DC | 100 | 100 | 100 | 4632.8 | 100 | 95.06 | 98.9 | 100 | 4873.53 | 100 | 91.63 |
| Mbinga DC | 100 | 100 | 100 | 2639.7 | 100 | 94.64 | 97.1 | 98.3 | 2789.24 | 100 | 96.46 |
| Mbinga TC | 100 | 100 | 100 | 991.3 | 100 | 63.9 | 100 | 100 | 1551.28 | 100 | 100 |
| Namtumbo DC | 100 | 100 | 100 | 1624.7 | 100 | 69.98 | 100 | 98.8 | 2321.63 | 100 | 99.72 |
| Nyasa DC | 100 | 100 | 98.51 | 1767.3 | 100 | 77.71 | 100 | 100 | 2274.22 | 100 | 100 |
| Songea DC | 100 | 100 | 100 | 1806.7 | 100 | 93.87 | 99 | 100 | 1924.61 | 100 | 99.9 |
| Songea MC | 100 | 100 | 99.15 | 3749.7 | 100 | 97.42 | 95.7 | 175.5 | 3849.12 | 100 | 92.97 |
| Tunduru DC | 100 | 100 | 96.11 | 2165.1 | 100 | 79.1 | 99.6 | 99.4 | 2737.13 | 100 | 99.8 |
| Ruvuma Region | 100 | 100 | 99.02 | 2278.7 | 100 | 85.31 | 98.4 | 574.6 | 2671.1 | 100 | 98.18 |

***Jedwali Na.5: Matumizi ya fedha zilizopangwa kutekeleza afua za lishe kwa Halmashauri***

| SN | HALMASHAURI | JANUARI - JUNE 2023 | | | JULAI - DESEMBA 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KIASI CHA FEDHAPANGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | % | KIASI CHA FEDHAPANGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | % |
| 1. | MADABA DC | 11,632,024.2 | 14,550,565.9 | 125 | 19,152,963.1 | 18,207,000 | 95 |
| 2. | MBINGA DC | 47,752,415.0 | 19,765,000.0 | 41 | 59,881,389.8 | 56,150,000 | 94 |
| 3. | MBINGA TC | 12,624,314.0 | 121,261,48.0 | 96 | 16.639,000 | 10,632,500 | 64 |
| 4. | NAMTUMBO DC | 18,712,500 | 23,841,000 | 127 | 43,613,000 | 30,520,000 | 70 |
| 5. | NYASA DC | 22,516,917 | 24,390,000 | 108 | 30,119,193.9 | 24,434,000 | 81 |
| 6. | SONGEA DC | 18,712,513.8 | 22,582,060 | 121 | 21,070,630 | 19,780,000 | 94 |
| 7. | SONGEA MC | 19,751,220 | 18,486,170 | 94 | 63,437,427.3 | 61,799,426 | 97 |
| 8. | TUNDURU DC | 34,674,696.8 | 22,948,289.6 | 66 | 68,719,414.2 | 54,160,460.1 | 79 |
| | **JUMLA KUU** | **186,376,600.80** | **146,563,085.50** | **78** | **305,994,018.30** | **275,683,386.00** | **90** |

### 7.3.7 Hali ya ugonjwa wa kipindupindu

Timu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Huduma za Afya Mkoa (RHMT) ilipokea taarifa ya uwepo wa mgonjwa anayehisiwa kuwa na Ugonjwa wa kipindupindu kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mnamo tarehe 23 Desemba 2023. Mgonjwa huyo alitokea katika Kijiji cha Mtipwili kitongoji cha Undu.

Mkoa kupitia RHMT uliagiza Halmashauri kufanya ufuatiliaji wa eneo alilotoka mgonjwa na kwenda kufanya usibuaji ili kuzuia ugonjwa usiendelee kuenea. Pia watu wote waliohusiana na Mgonjwa walifuatiliwa na kupewa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu pamoja na kupewa tiba kingaya ugonjwa wa kipindupindu. Aidha, Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri ilifanya ufuatiliaji wa Haraka wa hali hatarishi za kimazingira (Environmental Risk Factors) zilizopo katika Halmashauri na kugundua uwepo wa vyoo bora kwa asilimia 5% tu katika kijiji cha Mtipwili.

Kufuatia taarifa hizo Mkoa kupitia RHMT uliamua kuungana na Halmashauri ili kuongeza nguvu ya kupambana na ugonjwa wa kipindupindu kuanzia tarehe 29, Desemba 2023 hadi Tarehe 4 Januari 2024 kwa kufanya yafuatayo: -

- Timu ilifanya ukaguzi wa kaya katika vijiji vinneambavyo ni Mtipwili, Mtupale, Malini na Chiulu ambapo Jumla ya Kaya 1354 zilikaguliwa. Katika kaya zilizokaguliwa kaya 401 zilikuwa na vyoo bora, kaya 864 zilikuwa na vyoo visivyofaa (vyoo vya kujengwa kwa makuti, vizivyoezekea, havina milango, sakafu yenye udongo nk.) na kaya 87 hazikuwa na vyoo. - Timu ilitoza faini kwa wakuu wa kaya 87 wasiokuwa na vyoo/wenye vyoo vibovu sana ambapo kila mkuu wa kaya alitozwa faini ya shilingi 50,000,000 na kufanya Jumla ya faini kufikia 4,350,000.00.
- Timu iligawa boksi saba (7) @ boxi lilikuwa na vidonge 16,000 vya dawa za kutibu maji ya kunywa (aqua tabs) kwa kaya 1860 zilizoko katika vijiji vya mwambao mwa ziwa nyasa.
- Timu alitoa elimu ya ugonjwa wa kipindupindu (namna unavyoenee, dalili za ugonjwa, njia za kujikinga na hatua za kuchukua katika jamii iwapo mgonjwa) kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara katika vijiji vitano (Mtipwili, Mtupale, Chiulu, Malini na Mbambabay.
- Mkoa umefanya ufuatiliaji wa usafi wa mazingira katika kambi mbili (2) za wavuvi zilizoko chiulu, na Mtipwili ambapo kazi ya chiulu haikuwa na choo, na BMU iliagizwa kujenga vyoo angalau matundu (8) ndani ya siku tatu, na Kambi ya Mtiwili ilikuwa na matundu nane na jumla ya watu takribani 1000, BMU iliagizwa kuongeza matundu ya vyoo angalau yafikia 20.
- Timu imeendelea na ufuatiliaji wa wagonjwa na hadi kufikia tarehe 28/12/2023 walikuwa ni watatu na hadi kufikia sasa (tarehe 17.01/2024) hakuna mgonjwa mpya aliyeripotiwa.

Mkoa unandelea kusimamia Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ili iendelee na juhudi za kupambana na ugonjwa wa kipindupindu ikiwemo kuimarisha usafi wa mazingira, kaguzi za maeneo ya vyakula, upimaji wa maji yanayotumiwa na Wananchi kwa ajili ya kuangalia kama yanatibiwa kwa clorini na ufuatiliaji wa tetesi za magonjwa.

### 7.3.8 Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya

Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya imeendelea kuimarika, kwani upatikanaji umeongezeka kutoka **40%** mwaka 2022 hadi **68%** mwezi Septemba, 2023 kulingana na mchakato wa bidhaa kwa kutumia kigezo cha idadi ya bidhaa zinazotolewa taarifa na vituo.

Upatikanaji huu umetokana na kuongezeka kwa mapato ya ukusanyaji ya mapato ya uchangiaji wa huduma za afya, ufuatiliaji na usimamizi pamoja na ruzuku ya dawa kutoka serikali kuu; ambapo jumla ya fedha zilizokusanywa kutokana na uchangiaji na zile za Serikali kuu kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 ilikuwa shilingi **10,831,384,518.04** na **4,894,718,195.08** kwa mfuatano. Sambamba na hilo, Halmashauri pia zilipokea fedha kwa ajili ya kununulia vifaa na vifaa tiba shilingi **3,515,137,094.17** pamoja na vifaa mbalimbali kwa ajili ya kutolea huduma kwa wagonjwa kupitia mradi wa Global Fund.

### 7.3.9 Huduma za UKIMWI

Mkoa una jumla ya vituo **419** kati ya **354** sawa na **84%** vinatoa huduma za unasihi na upimaji wa VVU (HTS); vituo **336** sawa na **79%** vinatoa huduma za kuzuia maambuzi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT); vituo 151 sawa na asilimia 36 vinatoa huduma za dawa za kufubaza VVU (CTC); vituo 41 sawa na 10% vinatoa huduma rafiki za makundi maalumu yalio kwenye hatari ya kupata maambukizi na dawa kinga ya kuzuia maambukizi ya VVU (KVP); na vituo 46 sawa na asilimia 11 vinatoa huduma ya tohara ya kitabibu kwa wanaume (VMMC).

Kiwango cha maambukizi ya VVU katika Mkoa wa Ruvuma ni **4.9%** (THIS 2022/23). Kiwango hiki kipo juu kwa **0.6%** ya kiwango cha kitaifa ambacho ni **4.3%.** Aidha, kiwango hiki cha maambuzi katika Mkoa kimepungua kwa **0.7%** kutoka **5.6%** kwa

mwaka 2016 (THIS-2016/17). Takwimu za Kimataifa zinaonyesha, watu **60,271** walikuwa wanaishi na maambukizi ya VVU katika Mkoa, watu wazima wenye umri zaidi ya miaka 15 walikuwa **57,639** sawa na **96%** ambapo Wanawake walikuwa **37,077** sawa na **62%** na Wanaume walikuwa **20,562** sawa na **34%**. Aidha, watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 walikuwa 2,632 sawa na **4%,** vijana balehe miaka 10-19 walikuwa **2,722** sawa na **5%,** vijana wenye miaka 20-24 walikuwa **2,811** sawa na **5%** (Spectrum,2023).

Katika utekelezaji wa malengo ya kimkakati ya kitaifa ya **95** Tatu (95-95-95) katika Mkoa kufikia mwezi September 2023, **117%** ya watu wote wanaoishi na maambukizi VVU walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ukilinganisha na **96%** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022; **99%** ya watu wanaotambua hali ya maambukizi walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU (ARVs) sawa sawa na **99%** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022 ; na **96%** ya watu wanaotumia dawa za ARV walikuwa wamefubaza VVU ukilinganisha na **95%** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

### 7.3.10 HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea ni miongoni mwa Hospitali ambazo zimetengewa fedha za IMF na Serikali kuu kupitia Wizara ya Afya na kiasi kilichopokelewa ni shilingi **6,579,063,698.20** na katika mwaka wa fedha **2023/2024 Wizara ya Afya i**metenga kiasi cha shilingi **1,000,000,000** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la OPD.

Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya, Ukarabati wa vyumba vya kutolea huduma za Afya pamoja na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya kutolea huduma bora za Afya kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla.

Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea fedha hizi zinatekeleza/zimetekeleza miradi mitano ya ujenzi kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Daktari) – Mradi umekamilika kwa asilimia 100.

2. Ujenzi wa jengo la radiolojia (kwa ajili ya CT Scan na digital X Ray) – Mradi umekamilika kwa asilimia 100.
3. Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) – ujenzi bado unaendelea.
4. Ukarabati wa wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (ICU) – Mradi umekamilika kwa asilimia 100.
5. Ukarabati wa chumba cha Tiba Masafa (Telemedicine) – Mradi umekamilika kwa asilimia 100.
6. Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ICU, EMD, Maabara na Radiolojia – Mradi umekamilika kwa asilimia 100.

**1. UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA NJE (OPD)**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kwa sasa ipo katika eneo ambalo ni finyu na halitoshi pale huduma za ziada zinapotakiwa kuongezwa; kwani italazimu kuvunja baadhi ya majengo ili kupata eneo la ujenzi. Kwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha changamoto ya utoaji wa huduma iliyokuwa ikitolewa katika majengo yanayobomolewa. Kwa mstakabali huo Mkoa wa Ruvuma uliona umuhimu wa kuwa na eneo jipya lenye nafasi ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma. Eneo ambalo litatosheleza kwa miundo mbinu na huduma zote zinazotarajiwa kuwepo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Eneo lililotengwa lipo Mwengemshindo ndani ya Manispaa ya Songea na lina ukubwa wa hekari 270. Eneo hili lilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Songea. Katika kuanzisha ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma; jengo muhimu la kuanza nalo ni la wagonjwa wa nje (OPD). Hii itaongeza wigo wa utoaji wa huduma za afya. Ujenzi huu unafanywa na Mkandarasi anayeitwa Kiure Engineering Company ya Arusha.

Mradi huu unagharimu shilingi 3,870,000,000 ambapo katika awamu ya kwanza mkataba ulioingiwa ni wa shilingi 2,700,000,000. Na katika awamu ya pili ya ujenzi mradi huu Wizara ya Afya imeutengea kiasi cha shilingi 1,000,000,000.

**TAARIFA YA FEDHA**

Fedha iliyopokelewa ni shilingi 3,000,000,000.00 na hadi tarehe 31 Julai, 2023 kiasi cha shilingi 3,000,000,000.00 kimeshalipwa kwa Mkandarasi. Na katika awamu ya pili Mkandarasi ameshalipwa kiasi cha shilingi 78,338,430 na kiasi cha shilingi 283,467,765.60 kimeombwa na Mkandarasi na kipo kwenye hatua za ufuatiliaji na utekelezaji wa malipo katika ngazi ya Wizara ya Afya.

**HALI YA HATUA YA UTEKELEZAJI**

Ujenzi wa OPD umefikia asilimia 71 ya hatua ya ujenzi. Tunategemea jengo hili kukamilika katika mwaka huu wa fedha 2023/2024.

Kazi zilizofanyika mpaka sasa ni:-

i. *Ujenzi wa kuta za vyumba vya ghorofani umefanyika.*
ii. *Uwekaji wa mifumo mbalimbali kama vile maji, umeme, TEHAMA nk*
iii. *Upigaji wa ripu kuta za vyumba vya ghorofani*
iv. *Blundering katika vyumba vya ghorofani*
v. *Kazi ya kupaua imefanyika*
vi. *Kazi ya kuezeka imefanyika*

**UJENZI WA JENGO LA RADIOLOJIA (CT SCAN NA X RAY)**

Kuna ujenzi wa jengo la kutolea huduma ya mionzi ambalo ndani yake kuna mashine mbili za CT Scan na Digital X-Ray zinazofanya kazi.

Mradi huu wa huduma ya mionzi una thamani ya shilingi **2,034,269,178** na umegawanyika katika maeneo matatu kama ifuatavyo: -

1. Ujenzi wa jengo la huduma ya mionzi lenye thamani ya shilingi 271,079,500.00

2. Ununuzi na usimikaji wa CT Scan wenye thamani ya shilingi 1,446,939,999.00

3. Ununuzi na usimikaji wa Digital X Ray wenye thamani ya shilingi 316,249,679.00

Mzabuni aliyetekeleza ujenzi wa jengo, ununuzi na usimikaji wa mashine hizi ni Computech-ICS (T) Ltd ya Dar es salaam.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Aprili, 2022 na kukamilika mwezi Machi, 2023. Huduma za CT Scan zimeanza kutolewa mwezi 8 Machi, 2023. Hii imepunguza adha kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma ambao walikuwa wanapata huduma hii katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**NB: usimikaji wa CT Scan na Digital X Ray mashine umefanyika. Kwa sasa tunatoa huduma za CT Scan.**

**HITIMISHO:**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa Serikali ya awamu ya sita chini ya Uongozi wa Mhe: Dkt. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujali afya za Watanzania kwani watu bila kuwa na afya bora hawawezi kufanya kazi ya kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Pia tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na mamlaka zake kwa kuona umuhimu wa kuwa na Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma iliyo katika eneo pana ambapo miundombinu mingi ya kuboresha huduma za Afya inaweza kujengwa na hivyo kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hii mpya.

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma tunaahidi kutumia fedha hizi kwa weledi mkubwa ili kupata thamani halisi ya fedha (value for money).

### 7.4 ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

#### 7.4.1 Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Sekta ya Elimu Mkoani inafanya kazi kwa ushirikiano na Halmashauri, Idara ya Uthibiti Ubora wa Elimu, Idara ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, vyuo vya Ualimu na Mamlaka ya vyuo vya ufundi (VETA), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Maktaba ya Mkoa.

#### 7.4.2 Idadi ya Taasisi zinazotoa Elimu katika Mkoa

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi **841**, kati ya hizo shule za za Serikali ni **800** na zisizo za Serikali ni **41**, Shule za Sekondari ni **233** zikiwemo **174** za Serikali na **59** ni shule za binafsi.

Mkoa umekuwa na ongezeko la idadi ya shule za msingi **13** kutoka idadi ya shule **828** zilizokuwepo mwaka 2022 hadi shule **841** mwaka 2023 sawa na asilimia **1.5**. Shule za sekondari zimeongezeka **15** kutoka idadi ya shule **218** mwaka 2022 hadi kufikia shule **233** mwaka 2023 **sawa** na ongezeko la asilimia **6.4.** Aidha Mkoa una Vyuo vya Maendeleo ya wananchi **9,** Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) **4,** Vyuo vya Ualimu **3** na Vyuo Vikuu **2. J**edwali lifuatalo linaainisha mchanganuo wa Taasisi za elimu zilizopo Mkoa wa Ruvuma.

**Jedwali Na.1: Idadi ya taasisi za elimu katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Juni, 2023**

| Halmashauri | Elimu ya Awali | | Elimu ya Msingi | | Elimu ya Sekondari | | Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi | | VETA | | Vyuo vya Ualimu | | Vyuo vya Elimu ya Juu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *S | *B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B |
| Madaba | 28 | 2 | 28 | 2 | 10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga DC | 164 | 3 | 164 | 3 | 34 | 16 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga TC | 72 | 10 | 72 | 10 | 16 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Namtumbo | 108 | 5 | 108 | 5 | 26 | 8 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyasa | 115 | 0 | 115 | 0 | 18 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea DC | 79 | 3 | 79 | 3 | 18 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea MC | 82 | 16 | 82 | 16 | 25 | 18 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |

| Halmashauri | Elimu ya Awali | | Elimu ya Msingi | | Elimu ya Sekondari | | Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi | | VETA | | Vyuo vya Ualimu | | Vyuo vya Elimu ya Juu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *S | *B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B |
| Tunduru | 152 | 2 | 152 | 2 | 27 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **800** | **41** | **800** | **41** | **174** | **59** | **5** | **4** | **3** | **1** | **1** | **2** | **1** | **1** |
| **Jumla Kuu** | **841** | | **841** | | **233** | | **9** | | **4** | | **3** | | **2** | |

Chanzo: *Taarifa za Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma Juni,2023*
*S – Serikali *B – Binafsi

### 7.4.3 Elimu ya Awali na Msingi

Elimu ya Awali ni hatua muhimu ya Maandalizi katika mzunguko wa elimu. Serikali ya Tanzania imeirasmisha na kujumuisha elimu hii kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuagiza kila shule ya msingi iwe na darasa la elimu ya awali litakaloandikisha watoto wenye umri wa miaka 5-6. Elimu ya Awali inachukua miaka miwili bila ya mitihani ya kuwapandisha watoto. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) ya mwaka 1995, Elimu ya Awali inakusudiwa kuhimiza maendeleo ya jumla ya haiba ya mwanafunzi, sifa za kimwili, kiakili na kimaadili na uwezo.

### 7.4.4 HALI YA UANDIKISHAJI ELIMU YA AWALI NA DARASA LA KWANZA

#### 7.4.4.1 Uandikishaji wa wanafunzi Elimu ya Awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2022 - 2023.

Uandikishaji umeongezeka na kuimarika ambapo kuna ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali kutoka wanafunzi **42,140** mwaka 2022 hadi kufikia idadi ya wanafunzi **44,853** mwaka 2023 ambapo ni sawa na 0ngezeko la asilimia **6**. Mafanikio haya yametokana na Mpango wa Utoaji wa Elimu Bila Malipo ulioanza kutekelezwa tangu Serikali ya awamu ya tano na sasa unaowezeshwa na Serikali ya awamu ya sita ya Mhe, Rais Samia suluhu Hassani. Mafanikio hayo ni pamoja na;

- Kuongezeka kwa miundombinu ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, Mabweni, vyoo, mabwalo, maabara na ujenzi wa shule mpya.

- Ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia hususan vitabu vya ziada na kiada kwa wanafunzi ambavyo vimegawiwa katika shule zote.

**Jedwali Na. 2: Uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali mwaka 2022 na 2023**

| Na | Halmashauri | Uandikishaji mwaka 2022 | | | Uandikishaji mwaka 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maoteo | Walioandikishwa | % ya Uandikishaji | Maoteo | Walioandikishwa | %ya Uandikishaji |
| 1 | MADABA | 1938 | 1775 | 91.59 | 1687 | 1670 | 97 |
| 2 | MBINGA DC | 6581 | 6492 | 98.65 | 6581 | 6622 | 100 |
| 3 | MBINGA TC | 4569 | 4520 | 98.93 | 4569 | 5259 | 115 |
| 4 | NAMTUMBO | 7632 | 7451 | 97.63 | 7637 | 7600 | 99 |
| 5 | NYASA | 5487 | 5326 | 97.07 | 5487 | 5880 | 107 |
| 6 | SONGEA DC | 4319 | 4230 | 97.94 | 4319 | 4920 | 113 |
| 7 | SONGEA MC | 6237 | 6337 | 101.6 | 6237 | 6802 | 109 |
| 8 | TUNDURU | 6094 | 6009 | 98.61 | 60.94 | 6104 | 100 |
| | **JUMLA** | **42,857** | **42,140** | **98.33** | **42,611** | **44,857** | **105.3** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa Machi, 2023***

#### 7.4.4.2 Uandikishaji wa wanafunzi darasa la Kwanza 2022 - 2023.

Uandikishaji umeongezeka na kuimarika ambapo kuna ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la Kwanza kutoka wanafunzi **44,228** mwaka 2022 hadi kufikia idadi ya wanafunzi **45,394** mwaka 2023 ambapo ni sawa na 0ngezeko la asilimia **9** kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini;

**Jedwali Na. 3: Idadi ya maoteo na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la Kwanza mwaka 2022 - 2023**

| Na | Halmashauri | Uandikishaji mwaka 2022 | | | Uandikishaji mwaka 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maoteo | Walioandikishwa | % ya Uandikishaji | Maoteo | Walioandikishwa | % ya Uandikishaji |
| 1 | MADABA | 1538 | 1728 | 112 | 1792 | 1692 | 99 |
| 2 | MBINGA DC | 5781 | 6578 | 114 | 5918 | 6545 | 111 |
| 3 | MBINGA TC | 4249 | 4176 | 98 | 4300 | 4770 | 111 |
| 4 | NAMTUMBO | 6665 | 6294 | 94 | 6665 | 7376 | 111 |
| 5 | NYASA | 5967 | 5130 | 86 | 5133 | 7376 | 105 |
| 6 | SONGEA DC | 3895 | 4145 | 106 | 4015 | 4643 | 116 |
| 7 | SONGEA MC | 7235 | 7475 | 103 | 7307 | 7583 | 104 |
| 8 | TUNDURU | 7337 | 8702 | 119 | 8070 | 7407 | 88 |

| | JUMLA | 42,667 | 44,228 | 104 | 43,200 | 45,394 | 105 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|

*Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa Machi, 2023*

### 7.4.4.3 HALI YA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI WALIOANZA ELIMU YA AWALI NA MSINGI MWAKA 2024

**Uandikishaji wa wanafunzi Elimu ya Awali na darasa la kwanza hadi Januari 19, 2023**

Uandikishaji wa wanafunzi kuanza shule mwaka 2024 ulianza rasmi mwezi Oktoba 2023. Hadi kufikia tarehe 19 Januari, 2024 hali halisi ya uandikishaji ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 4: Idadi ya maoteo na uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali mwaka 2024**

| HALMASHAURI | MAOTEO | | | WALIOANDIKISHWA (WASIO WA MAHITAJI MAALUM) | | | WALIOANDIKISHWA (MAHITAJI MAALUM) | | | JUMLA WALIOANDIKISHWA | | | ASILIMIA YA UANDIKISHAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| MADABA | 864 | 795 | **1659** | 795 | 740 | 1535 | 0 | 0 | 0 | 795 | 740 | 1535 | 92.0 | 93.1 | 92.5 |
| MBINGA DC | 3929 | 4059 | **7988** | 3359 | 3240 | 6599 | 1 | 3 | 4 | 3360 | 3243 | 6603 | 85.5 | 79.9 | 82.7 |
| MBINGA TC | 2192 | 2279 | **4471** | 1693 | 1677 | 3370 | 11 | 7 | 18 | 1704 | 1684 | 3388 | 77.7 | 73.9 | 75.8 |
| NAMTUMBO | 4061 | 4043 | **8104** | 2634 | 2645 | 5279 | 3 | 4 | 7 | 2637 | 2649 | 5286 | 64.9 | 65.5 | 65.2 |
| NYASA | 2706 | 2806 | **5512** | 2178 | 2246 | 4424 | 0 | 0 | 0 | 2178 | 2246 | 4424 | 80.5 | 80.0 | 80.3 |
| SONGEA DC | 2607 | 2490 | **5097** | 2175 | 2056 | 4231 | 2 | 0 | 2 | 2177 | 2056 | 4233 | 83.5 | 82.6 | 83.0 |
| SONGEA MC | 3843 | 3916 | **7759** | 2633 | 2411 | 5044 | 2 | 3 | 5 | 2635 | 2414 | 5049 | 68.6 | 61.6 | 65.1 |
| TUNDURU | 5708 | 5648 | **11356** | 3392 | 3496 | 6888 | 26 | 28 | 54 | 3418 | 3524 | 6942 | 59.9 | 62.4 | 61.1 |
| **JUMLA** | **25910** | **26036** | **51946** | **18859** | **18511** | **37370** | **26** | **28** | **90** | **18904** | **18556** | **37460** | **73.0** | **71.3** | **72.1** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa Januari, 2024***

**Jedwali Na. 5: Idadi ya maoteo na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la Kwanza mwaka 2024**

| HALMASHAURI | MAOTEO | | | WALIOANDIKISHWA (WASIO WA MAHITAJI MAALUM) | | | WALIOANDIKISHWA (MAHITAJI MAALUM) | | | JUMLA WALIOANDIKISHWA | | | ASILIMIA YA UANDIKISHAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| MADABA | 844 | 851 | **1695** | 807 | 825 | 1632 | 3 | 0 | 3 | 810 | 825 | 1635 | 96.0 | 96.9 | 96.5 |

| HALMASHAURI | MAOTEO | | | WALIOANDIKISHWA (WASIO WA MAHITAJI MAALUM) | | | WALIOANDIKISHWA (MAHITAJI MAALUM) | | | JUMLA WALIOANDIKISHWA | | | ASILIMIA YA UANDIKISHAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| MBINGA DC | 3823 | 3788 | **7611** | 3170 | 3240 | 6410 | 1 | 4 | 5 | 3171 | 3244 | 6415 | 82.9 | 85.6 | 84.3 |
| MBINGA TC | 2287 | 2301 | **4588** | 1790 | 1720 | 3510 | 12 | 7 | 19 | 1802 | 1727 | 3529 | 78.8 | 75.1 | 76.9 |
| NAMTUMBO | 3764 | 3779 | **7543** | 3225 | 3140 | 6365 | 4 | 7 | 11 | 3229 | 3147 | 6376 | 85.8 | 83.3 | 84.5 |
| NYASA | 2667 | 2787 | **5454** | 2396 | 2542 | 4938 | 0 | 0 | 0 | 2396 | 2542 | 4938 | 89.8 | 91.2 | 90.5 |
| SONGEA DC | 2317 | 2461 | **4778** | 2201 | 2115 | 4316 | 0 | 4 | 4 | 2201 | 2119 | 4320 | 95.0 | 86.1 | 90.4 |
| SONGEA MC | 3596 | 3788 | **7384** | 3371 | 3468 | 6839 | 5 | 6 | 11 | 3376 | 3474 | 6850 | 93.9 | 91.7 | 92.8 |
| TUNDURU | 5398 | 5417 | **10815** | 4297 | 4230 | 8527 | 72 | 54 | 126 | 4369 | 4284 | 8653 | 80.9 | 79.1 | 80.0 |
| **JUMLA** | **24696** | **25172** | **49868** | **21257** | **21280** | **42537** | **97** | **82** | **179** | **21354** | **21362** | **42716** | **86.5** | **84.9** | **85.7** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa Januari, 2024***

### 7.4.4.3 Idadi ya wanafunzi darasa la Awali-VII mwaka 2023

Kwa mujibu wa takwimu za ASC, Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Disemba, 2023 una idadi ya wanafunzi wa darasa la Awali hadi la VII **387,526** Kati yao wavulana **194,666** na wasichana **192,860** kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo :-

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Wanafunzi darasa la Awali hadi Darasa la Saba Mwaka 2023**

| NA | HALMASHAURI | Idadi ya Wanafunzi Awali hadi VII | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Wavulana** | **Wasichana** | **Jumla** |
| 1 | Madaba | 6622 | 6620 | 13,242 |
| 2 | Mbinga DC | 32,754 | 32,892 | 65,646 |
| 3 | Mbinga TC | 18,490 | 18,892 | 37,382 |
| 4 | Namtumbo | 28,210 | 29,386 | 57,596 |
| 5 | Nyasa | 23213 | 23593 | 46806 |
| 6 | Songea DC | 17,921 | 11,338 | 29,259 |
| 7 | Songea MC | 29058 | 30463 | 59521 |
| 8 | Tunduru | 38,398 | 39,676 | 78,074 |
| | **Jumla** | **194,666** | **192,860** | **387,526** |

### 7.4.4.4 Ikama ya Walimu wa Shule za Msingi hadi Disemba, 2023

Hadi kufikia Disemba, 2023 mahitaji ya walimu wa shule za msingi ni **10,029** Waliopo ni **6,214** hivyo upungufu ni walimu **3,815** sawa na asilimia **38** Mchanganuo wa idadi ya walimu imeoneshwa katika jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Na. 7. Idadi ya walimu wa shule za msingi hadi kufikia Juni, 2023**

| Halmashauri | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Asilimia ya upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Madaba DC | 318 | 202 | 116 | 36.5 |
| Mbinga DC | 1936 | 1061 | 875 | 45.2 |
| Mbinga TC | 1,046 | 573 | 473 | 45.2 |
| Namtumbo DC | 1351 | 900 | 451 | 33 |
| Nyasa DC | 1171 | 701 | 470 | 40 |
| Songea DC | 879 | 536 | 343 | 39 |
| Songea MC | 1322 | 1106 | 216 | 14 |
| Tunduru | 2006 | 1135 | 871 | 57 |
| **JUMLA** | **10,029** | **6,214** | **3815** | **38** |

#### 7.4.4.5 Hali ya ufaulu wa mtihani wa darasa la saba 2023

Mwaka **2023** wanafunzi wa darasa la saba wapatao **48,729** walisajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba. Wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walikuwa ni **46,324** sawa na asilimia **96.7.** Wanafunzi waliofaulu mtihani walikuwa **31,992** sawa na asilimia **69.06** ambapo wanafunzi wote waliofaulu wamechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

**Jedwali Na. 8: Hali ufaulu wa mtihani wa darasa la saba mwaka 2023**

| NA | HALMASHAURI | WALIOFANYA MTIHANI | | | WALIOFAULU | | | % ASILIMIA | NAFASI ZA UFAULU KIHALMASHAURI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WAS | WAV | JML | WAS | WAV | JML | | |
| 1 | SONGEA (M) | 3650 | 3637 | 7287 | 3297 | 2996 | 6293 | 86.36 | 1 |
| 2 | MADABA | 783 | 804 | 1587 | 637 | 638 | 1275 | 80.34 | 2 |
| 3 | NYASA | 2948 | 2864 | 5812 | 2343 | 2128 | 4471 | 76.93 | 3 |
| 4 | MBINGA (M) | 2175 | 1816 | 3991 | 1579 | 1223 | 2802 | 70.21 | 4 |
| 5 | NAMTUMBO | 3845 | 3565 | 7410 | 2434 | 2189 | 4623 | 62.39 | 5 |
| 6 | SONGEA (V) | 2084 | 2052 | 4136 | 1321 | 1250 | 2571 | 62.16 | 7 |
| 7 | TUNDURU | 5105 | 4674 | 9779 | 2917 | 2982 | 5899 | 60.32 | 6 |
| 8 | MBINGA (V) | 4355 | 4279 | 8634 | 2261 | 2937 | 5198 | 60.20 | 8 |
| | **JUMLA** | **24,945** | **23,691** | **48,636** | **16,789** | **16,343** | **33,132** | **68.12** | |

### 7.4.4.6 ULINGANIFU WA MATOKEO DARASA LA SABA MWAKA 2022 na 2023

Kwa kigezo cha asilimia ya ufaulu, Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Ruvuma zimeongeza ufaulu ukilinganisha na ufaulu uliopita wa mwaka 2022. Halmashauri mbili tu ndizo zimeshuka kiufaulu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chin

***Jedwali namba 9: Ulinganifu wa ufaulu Kihalmashauri kwa Miaka Miwili***

| Halmashauri | Waliosajiliwa | | Waliofanya Mtihan | | | | Waliofaulu | | | | % Mobility | % Mobility |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | **2023** | **2022** | **%** | **2023** | **%** | **2022** | **%** | **2023** | **%** | **2021 - 2022** | **2022 - 2023** |
| MADABA | 1603 | 1465 | 1587 | 99 | 1446 | 98.7 | 1275 | 80.34 | 1267 | 87.62 | -5.94 | 7.28 |
| MBINGA DC | 8983 | 8854 | 8634 | 96.11 | 8426 | 95.17 | 5198 | 60.2 | 5296 | 62.85 | -2.7 | 2.65 |
| MBINGA TC | 4086 | 4649 | 3991 | 97.67 | 4425 | 95.18 | 2802 | 70.21 | 3189 | 72.07 | 0.81 | 1.86 |
| NAMTUMBO | 7677 | 6743 | 7410 | 96.52 | 6498 | 96.37 | 4623 | 62.39 | 4399 | 67.7 | -11.47 | 5.31 |
| NYASA | 5915 | 5576 | 5812 | 98.26 | 5422 | 97.24 | 4471 | 76.93 | 4130 | 76.17 | 0.93 | -0.76 |
| SONGEA DC | 4195 | 4079 | 4136 | 98.59 | 4012 | 98.36 | 2571 | 62.16 | 2630 | 65.55 | -0.8 | 3.39 |
| SONGEA MC | 7492 | 7353 | 7287 | 97.26 | 7048 | 95.85 | 6293 | 86.36 | 6162 | 87.43 | -1.65 | 1.07 |
| TUNDURU | 10105 | 10010 | 9779 | 96.77 | 9047 | 90.38 | 5899 | 60.32 | 4919 | 54.37 | -5.67 | -5.95 |
| **MKOA** | **50056** | **48729** | **48636** | **97.16** | **46324** | **95.06** | **33132** | **68.12** | **31992** | **69.06** | **-5.05** | **0.94** |

### 7.4.4.7 Hali ya ufaulu wa mtihani wa Upimaji darasa la nne 2023

Jumla ya watahiniwa **49,991** walifanya Upimaji wa Kitaifa wa darasa la nne ambapo

**24,533** ni wavulana na **25458** ni wasichana.

Watahiniwa **37,999** wakiwa wavulana **17,603** na wasichana **20,396** wamefaulu Mtihani ambapo ni sawa na asilimia **76.01**

Kwa matokeo haya, ufaulu wa Mkoa kwa mwaka 2022 umepanda kwa asilimia **0.01** kutoka asilimia **76** mwaka 2022 hadi kufikia asilimia **76.01.** Katika ngazi ya Mkoa nafasi ya kwanza imeshikwa na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na nafasi ya mwisho imeshikwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Jedwali lifuatalo linaonesha ufaulu na nafasi ya ufaulu Kihalmashauri.

***Jedwali namba 10: Ufaulu wa Upimaji Darasa la Nne na nafasi ya ufaulu Kimkoa kiasilimia***

| H/SHAURI | WALIOSAJILIWA | | | WALIOFANYA | | | WALIOFAULU (A-D) | | | % YA UFAULU | WALIOFELI (E) | | | NAFASI KIMKOA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WV | WS | JML | WV | WS | JML | WV | WS | JML | | WV | WS | JML | |
| MADABA | 792 | 841 | 1633 | 762 | 826 | 1588 | 686 | 747 | 1433 | 90.24 | 76 | 79 | 155 | 1 |
| NYASA | 2543 | 2619 | 5162 | 2280 | 2494 | 4774 | 1988 | 2231 | 4219 | 88.37 | 292 | 263 | 555 | 2 |
| SONGEA MC | 4229 | 4263 | 8492 | 3860 | 4052 | 7912 | 3254 | 3728 | 6982 | 88.25 | 606 | 324 | 930 | 3 |
| MBINGA MJI | 2790 | 2434 | 5224 | 2489 | 2305 | 4794 | 1700 | 1916 | 3616 | 75.43 | 789 | 389 | 1178 | 4 |

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NAMTUMBO | 4043 | 4249 | 8292 | 3492 | 3982 | 7474 | 2439 | 3024 | 5463 | 73.09 | 1053 | 958 | 2011 | 5 |
| TUNDURU | 5124 | 5293 | 10417 | 4346 | 4747 | 9093 | 3088 | 3517 | 6605 | 72.64 | 1248 | 1240 | 2488 | 6 |
| MBINGA DC | 5321 | 4666 | 9987 | 4688 | 4409 | 9097 | 2939 | 3373 | 6312 | 69.39 | 1772 | 1013 | 2785 | 7 |
| SONGEA DC | 2892 | 2722 | 5614 | 2616 | 2643 | 5259 | 1509 | 1860 | 3369 | 64.06 | 1120 | 770 | 1890 | 8 |
| **JUMLA** | **27734** | **27087** | **54821** | **24533** | **25458** | **49991** | **17603** | **20396** | **37999** | **76.01** | **6956** | **5036** | **11992** | |

### 7.4.4.8 ULINGANIFU WA MATOKEO SFNA MWAKA 2021, 2022 na 2023

Kwa kigezo cha asilimia ya ufaulu, Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Ruvuma zimeshuka kiufaulu ukilinganisha na ufaulu uliopita wa mwaka 2022. Halmashauri mbili tu ndizo zimeongeza ufaulu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini;

***Jedwali Na.11: Ulinganifu wa ufaulu Kihalmashauri kwa Miaka Mitatu***

| **Sn** | **Halmashauri** | **2021** | | **2022** | | **2023** | | **MJONGEO KIASILIMIA 2022 - 2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **% ya Ufaulu** | **Nafasi Kimkoa** | **% ya Ufaulu** | **Nafasi Kimkoa** | **% ya ufaulu** | **Nafasi Kimkoa** | |
| 1 | MADABA | 93 | 2 | 90.2 | 1 | 90.24 | 1 | 0.04 |
| 2 | NYASA | 89.41 | 4 | 84.7 | 3 | 88.37 | 2 | 3.67 |
| 3 | SONGEA MC | 96 | 1 | 89.9 | 2 | 88.25 | 3 | -1.65 |
| 4 | MBINGA MJI | 84 | 7 | 81 | 4 | 75.43 | 4 | -5.57 |
| 5 | NAMTUMBO | 86.7 | 5 | 75.6 | 6 | 73.09 | 5 | -2.51 |
| 6 | TUNDURU | 85.21 | 6 | 80.9 | 5 | 72.64 | 6 | -8.26 |
| 7 | MBINGA DC | 92.57 | 3 | 72.3 | 7 | 69.39 | 7 | -2.91 |
| 8 | SONGEA DC | 72.9 | 8 | 67.7 | 8 | 64.06 | 8 | -3.64 |
| **JUMLA YA MKOA** | | 87.4 | | 76 | | **76.01** | | **0.01** |

Kwa mujibu wa jedwali Na. 2 Halmashauri sita zilishuka katika ufaulu. Hata hivyo, Halmashauri ya Tunduru na Mbinga Mji zilishuka kwa kiasi kikubwa na hivyo kuushusha Mkoa. Ufaulu wa Halmashauri ya Songea umeendelea kuwa chini na kufanya Halmashauri kuendelea kushika nafasi ya mwisho Kimkoa kwa miaka mitatu mfululizo mwaka 2021, 2022 na 2023.

#### 7.4.4.9 Hali ya samani katika shule za Msingi

Hadi kufikia Juni, 2023 Mkoa una mahitaji ya madawati **126,459** yaliyopo ni **102,060** na upungufu ni **24,399** Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake umeendelea na jitihada mbalimbali ili kuweza kuondoa upungufu uliopo.

**Jedwali Na.12. Hali ya samani katika shule za msingi hadi kufikia Machi ,2023**

| NA. | HALMASHAURI | MADAWATI | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAHIT. | YALIOPO | UPUNG. | % ya Upungufu | ZIADA |
| 1 | Madaba | 4298 | 4322 | 0 | 0 | 24 |
| 2 | Mbinga DC | 22,323 | 19,279 | 3,044 | 13.64 | - |
| 3 | Mbinga Mji | 11,739 | 8636 | 3103 | 26.4 | - |
| 4 | Namtumbo | 17115 | 15970 | 1145 | 7 | - |
| 5 | Nyasa | 15916 | 12564 | 3352 | 24.2 | - |
| 6 | Songea DC | 12265 | 10622 | 1643 | 13 | - |
| 7 | Songea MC | 17843 | 13811 | 4032 | 23 | - |
| 8 | Tunduru | 24960 | 16856 | 8104 | 32.4 | - |
|---|---|---|
| 2021 | UMITASHUMTA | 26 |
| | UMISSETA | 24 |
| 2022 | UMITASHUMTA | 24 |
| | UMISSETA | 22 |
| 2023 | UMITASHUMTA | 22 |
| | UMISSETA | 9 |

Mkoa umeendelea kuhimiza Halmashauri zote kuanzisha vitalu vya ufundishaji michezo ili kuendeleza vipaji kwa wanafunzi. Pamoja na juhudi za Mkoa katika kuendeleza vipaji kwa wanafunzi, Serikali imetupendelea kwa kutupa vituo vitatu maalum vya michezo tofauti na mikoa mingine yenye vituo viwili. Vituo hivyo ni Mahanje sekondari, Maposeni na Songea Boys. Lengo la shule hizo maalum za michezo ni kuhakikisha wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi na kufaulu masomo yao wanapelekwa katika shule hizo ili kuendelezwa vipaji vyao.

**a) Michezo kwa shule za msingi na Sekondari**

Mwaka 2023 Mkoa umeshiriki katika mashindano hayo yaliyofanyika Mkoani Tabora ambapo timu tatu ziliingia hatua ya robo fainali na timu ya Mpira wa Kikapu wavulana na Mpira wa meza wavulana timu ziliingia nusu fainali kwa UMISSETA. Timu ya mpira wa wavu wasichana ilifanikiwa kufika hatua ya fainali na kuibuka Mshindi wa Kwanza Kitaifa na kupewa zawadi ya Kikombe na kushiriki mashindano ya Afrika mashariki na kati, na kwa upande wa UMITASHUMTA timu ya Mpira wa Goal ball wavulana ndiyo iliyoingia hatua ya robo fainali. Na kutolewa katika hatua ya robo na hivyo kushindwa kupata ushindi katika UMITASHUMTA. Mkoa ulishika nafasi ya 22 kati ya 28 na katika UMISSETA Mkoa ulikuwa nafasi ya 9. Kati ya 28.

**b) Mashindano ya SHIMIWI**

Mashindano haya huhusisha watumishi wa serikali wa wizara na idara za serikali mwaka 2022 Mkoa wa Ruvuma umeshiriki kuptia michezo ya Karata, Darts, Bao, na kupata ushindi wa kwanza katika mchezo wa bao. Aidha, kwa mwaka huu wa 2023 mkoa utashiriki katika michezo ya Riadha, Bao, DraftI na Darts.

**c) Tamasha la Utamaduni la Taifa**

Mashindano haya yalifanyika mkoani Njombe ambapo jumla ya washiriki 12 wa fani ya Ngoma walishiriki na kushika nafasi ya sita. Lengo la mashindano hayo ni kuenzi utamaduni wa Mtanzania. Vikundi mbalimbali toka Tanzania bara na visiwani walishiriki katika mashindano.

**d) Hatua za kuboresha michezo**

i) Kila Halmashauri imeagizwa kuwa na vitalu ambavyo vitawaandaa wanamichezo kuepuka maandalizi ya zimamoto.

ii) Shule ya sekondari ya Mahanje ya Halmashauri ya Madaba kuwa shule inayopokea wanafunzi wenye vipaji vya michezo mbalimbali kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma ili kukuza vipaji vyao. Wanafunzi hawa ni wale waliofika ngazi ya taifa na kufaulu mitihani yao ya elimu ya msingi.

iii) Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za kuchangia na kuendeleza Michezo katika Mkoa wetu wa Ruvuma.

iv) Kuendelea kuhamasisha wananchi na watumishi kushiriki katika jogging na michezo mbalimbali ya asili ya Mtanzania ili kuimarisha afya.

v) Kuendelea kuhamasisha wananchi kutoa ushirikiano kwa timu ya Tunduru korosho ili ipande daraja

#### 7.4.5.12 Changamoto Katika Sekta ya Elimu

i) Wazazi kuhamia mashambani mbali na shule na kuwaacha wanafunzi peke yao hivyo kusababisha baadhi yao kuwa watoro na kuacha masomo.

ii) Baadhi ya wazazi kutokuchangia chakula cha mchana shuleni kwa ajili ya wanafunzi
iii) Upungufu wa Walimu hasa katika shule za Msingi
iv) Kutokuwa na shule za bweni zinazokidhi mahitaji
v) Upungufu wa miundombinu, samani na hosteli

**7.4.5.13 Mikakati ya Kuinua Ubora wa Elimu Kuongeza Taaluma**

i) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala wa elimu katika ngazi za elimu za Halmashauri na shule.
ii) Kuhimiza na kufuatilia ufanyikaji wa mtihani ya upimaji wa mara kwa mara kwenye madarasa yote.
iii) Kutoa ushauri kwa Halmashauri kufanya urekebishaji wa ikama ya walimu.
iv) Kuhimiza utoaji wa motisha kwa wanafunzi, walimu, shule na Halmashauri zinazofanya vizuri kwenye taaluma.
v) Kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa utoaji wa chakula kwa wanafunzi wawapo shuleni wakati wa mchana.
vi) Kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya shule inayoendelea kujengwa.

**7.4.5 Hitimisho**

Mafanikio katika elimu ni jukumu la pamoja la wadau wote wa elimu, kila mmoja akitimiza wajibu wake changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa huduma ya elimu zitapungua na baadhi zitakwisha kabisa.

Tunashauri Halmashauri zote ziweke suala la elimu kuwa ni agenda ya kudumu katika ngazi zote zote za Uongozi ili kutatua changamoto katika shule zetu za Msingi na Sekondari.

## 7.5 UTUMISHI NA UTAWALA

### 7.5.1 Taarifa ya Hali ya Watumishi Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma mpaka kufikia Desemba, 2023 una jumla ya watumishi **14,424** kati ya watumishi **21,918** wanaohitajika na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zote nane (8). Aidha, Mkoa una upungufu wa watumishi **7,516** kama mchanganuo unavyoonyesha kwenye Jedwali namba 70:

**Jedwali Na. 70: idadi ya watumishi waliopo na upungufu**

| IDADI YA WATUMISHI | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **JINA LA TAASISI** | **IDADI YA WATUMISHI HITAJIKA** | **IDADI YA WATUMISHI WALIOPO** | **UPUNGUFU** | **ASILIMIA YA WATUMISHI WALIOPO** |
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 340 | 172 | 168 | 50.59 |
| 2 | Tunduru DC | 3,349 | 2,417 | 932 | 72.17 |
| 3 | Namtumbo DC | 3,528 | 1913 | 1615 | 54.22 |
| 4 | Songea MC | 3,523 | 2610 | 913 | 74.08 |
| 5 | Songea DC | 1845 | 1408 | 437 | 76.31 |
| 6 | Madaba DC | 1080 | 687 | 393 | 63.61 |
| 7 | Mbinga TC | 1836 | 1464 | 372 | 79.74 |
| 8 | Mbinga DC | 4269 | 2238 | 2031 | 52.42 |
| 9 | Nyasa DC | 2148 | 1515 | 655 | 70.53 |
| | **Jumla kuu** | **21,918** | **14,424** | **7,516** | **65.97** |

### 7.5.2 Watumishi waliopandishwa Madaraja

Mkoa wa Ruvuma, uliidhinishiwa kupandisha madaraja jumla ya watumishi 3013 kwa ikama ya mwaka 2022/2023, ambapo watumishi wote **3013** walipandishwa madaraja na kubadilishiwa mishahara.

### 7.5.3 Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja

**Jedwali Na. 71: Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja**

| NA | JINA LA TAASISI | IDADI YA WATUMISHI WALIOHIDHINISHWA KUPANDISHWA/ KUBADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI WALIOPANDISHWA /BADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI AMBAO BADO HAWAJABADILISHIWA MISHAHARA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 23 | 23 | 0 | 100 |
| 2 | Tunduru DC | 643 | 643 | 0 | 100 |
| 3 | Namtumbo DC | 276 | 276 | 0 | 100 |
| 4 | Songea MC | 489 | 489 | 0 | 100 |
| 5 | Songea DC | 393 | 393 | 0 | 100 |
| 6 | Madaba dc | 185 | 185 | 0 | 100 |
| 7 | Mbinga TC | 317 | 317 | 0 | 100 |
| 8 | Mbinga DC | 455 | 455 | 0 | 100 |
| 9 | Nyasa DC | 232 | 232 | 0 | 100 |
| | **JUMLA** | **3013** | **3013** | **0** | 100 |

### 7.5.4 Ajira Mpya

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia mwezi Desemba 2023, Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuajiri jumla ya watumishi wapya **1734** kwa kada za elimu, afya, utawala na miundombinu kutoka Serikali Kuu na wale walioajiriwa na Taasisi moja kwa moja, Jedwali hapo chini linaonyesha mchanganuo wa watumishi hao:

**Jedwali Na 72: Idadi ya watumishi walioajiriwa kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia mwezi Desemba, 2023**

| Na | JINA LA TAASISI | Idadi |
|---|---|---:|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 10 |
| 2 | Tunduru DC | 367 |
| 3 | Namtumbo DC | 214 |
| | Songea DC | 275 |
| 6 | Madaba DC | 20 |
| 5 | Songea MC | 88 |
| 7 | Mbinga TC | 120 |
| 8 | Mbinga DC | 391 |
| 9 | Nyasa DC | 249 |
| **Jumla** | | **1734** |

## 8.0 TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA

### 8.1 WAKALA WA HIFADHI YA CHAKULA KANDA YA SONGEA (NFRA)

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA NFRA KANDA YA SONGEA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024 HADI 31 DISEMBA, 2023**

**UTANGULIZI**

Kanda ya Songea ni miongoni mwa Kanda nane (8) za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Kanda hii ni moja ya Kanda zinazotegemewa katika uzalishaji wa zao la mahindi kutokana na wananchi wengi wa Mkoa wa Ruvuma kutegemea Kilimo kama chanzo cha mapato. Kanda hii inahudumia mkoa mmoja wa Ruvuma.

Aidha, pale kunapokuwa kuna uhitaji mkubwa wa Chakula katika mikoa mingine, Afisa Mtendaji Mkuu anaweza kuelekeza kuhamishwa na kupeleka chakula katika maeneo mengine nje ya mkoa wa Ruvuma.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024, kanda ilipanga kutekeleza kazi mbalimbali kwa kuzingatia malengo ya wakala ikiwa kubwa zaidi ni kuhakikisha usalama wa chakula nchini unakuwepo. Kazi hizo ni pamoja na ununuzi wa zao la mahindi, hifadhi yake na n.k.

#### 8.1.1 UTEKELZAJI WA KAZI ZA WAKALA KWA MIA 2022/2023 NA 2023/2024

a) **UTEKELEZAJI WA KAZI MBALIMBALI ZILIZOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

i. **Ununuzi wa tani 25,000 za mahindi**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Kanda ya Songea ilipangiwa kununua jumla ya tani 25,000 za mahindi. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kanda ilikuwa imefanikiwa kununua jumla ya tani 7098.283 sawa na asilimia 28.4 ya utekelezaji. Ununuzi huu ulitumia kiasi cha shilingi **5,158,527,182/=**.

Ununuzi wa kiasi kidogo cha mahindi ukilinganisha na lengo lililokuwa limewekwa, ulitokana na ushindani mkubwa wa nafaka sokoni uliosababisha bei kupanda zaidi na hivyo kushindwa kufikia lengo la ununuzi lililokuwa limewekwa.

i. **Njia za ununuzi zilizopagwa na zilizotumika**

Kutokana na ushindani na upatikanaji mdogo wa nafaka ya mahindi katika soko kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kanda ya songea ilitumia njia tatu ili kuweza kununua kiasi hicho cha mahindi. Njia hizo ilikuwa ni pamoja na:

i. Kununua kwa njia ya vituo vya ununuzi
ii. Kununua kupitia vikundi vya wakulima vya ushirika na;
iii. Kununua kwa kutumia Mawakala.

ii. **Mpango wa ununuzi**

Wakala ulipanga kiwango cha ununuzi kwa Halmashauri saba za Mkoa wa Ruvuma kwa kuzingatia uwiano wa taarifa za matarajio ya uzalishaji wa ziada ya mahindi zilizokuwepo kwa kipindi cha maandalizi ya ununuzi. Aidha, kutokana na upatikanaji mdogo wa nafaka kwa msimu huo, jumla ya vituo 18 vya ununuzi vilitumika. Mchanganuo wa vituo vilivyotumika na kiasi kilichonunuliwa kwa kila kituo ni kama unavyoonekana katika Jedwali namba 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa kiasi kilichonunuliwa kwa kila kituo kilichotumika kwa mwaka 2022/2023**

| NA | JINA LA KITUO | KIASI KILICHONUNULIWA (TANI) |
|---|---|---|
| 1 | Mgazini | 1,106.500 |
| 2 | Ruhuwiko | 2,192.010 |
| 3 | Namabengo | 181.900 |
| 4 | Tingi | 98.600 |
| 5 | Mpitimbi | 93.500 |
| 6 | Magagura | 596.600 |
| 7 | Muungano zomba | 410.050 |
| 8 | Madaba | 12.850 |
| 9 | Mwanamonga | 2.750 |
| 10 | Matimila | 253.200 |
| 11 | Likuyufusi | 578.750 |
| 12 | Matiri | 254.600 |
| 13 | Kitanda | 99.600 |
| 14 | Liganga | 55.977 |
| 15 | Msamala | 56.158 |
| 16 | Nakahegwa | 336.000 |
| 17 | Mkenda | 262.050 |
| 18 | Nakahuga | 195.150 |
| 19 | Wakala | 225.372 |
| 20 | Kikundi | 86.666 |
| **JUMLA** | | **7,098.283** |

iii. **Bei za ununuzi zilizotumika**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, mahindi yalinunuliwa kwa bei za kati ya shilingi 650 na 780. Mabadiliko ya bei za kununulia yalifanyika mara kwa mara wakati wa zoezi la ununuzi kutokana na ushindani wa bei zilizokuwa sokoni ili kuongeza akiba ya chakula.

iv. **Uhamishaji wa tani 20,000 kwenda Kanda za kipawa na Dodoma**

Kati ya kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2022/2023, ilikuwa ni kuhamisha tani 20,000 za mahindi kwenda katika Kanda za Dodoma na Kipawa. Aidha, kutokana na uhitaji mkubwa uliokuwepo wa nafaka ya mahindi katika Kanda za Dodoma na Arusha hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Kanda ilikuwa imefanikiwa kuhamisha tani 20,000 za mahindi kwenda katika Kanda za Arusha na Dodoma.

v. **Uzungushaji wa tani 1,395 za mahindi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.**

Kama ilivyoelezwa awali, jukumu kuu la Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, ni kuhakikisha usalama wa Chakula nchini unakuwepo kwa kununua, kuhifadhi na kukitoa kwenda kwa walengwa kukabiliana na majanga mbalimbali.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, maeneo mengi ya nchi yalikuwa na bei kubwa za vyakula. Katika kukabiliana na hali hiyo, Kanda ya Songea ilielekezwa kupeleka kuuza tani 1,395 za nafaka ya mahindi katika Halmashauri ya wilaya ya Tunduru kwa lengo la kupunguza makali ya bei sokoni na kuhakikisha usalama wa chakula ndani ya wilaya hii. Mahindi hayo yaliuzwa kwa bei ya shilingi 770 kwa kilo.

### 8.2.2 UTEKELEZAJI WA KAZI MBALIMBALI ZILIZOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

**i. Ununuzi wa tani 36,405 za mahindi**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, kwa kuanzia kanda ya Songea ilikuwa imepangiwa kununua tani 28,000 za mahindi. Aidha, kutokana na upatikanaji mkubwa wa nafaka ya mahindi na mabadiliko ya mpango wa ununuzi wa NFRA, Kanda ya Songea iliongezewa mgao wa ununuzi na kufikia tani 36,405 za mahindi.

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023, Kanda ya Songea ilikuwa imeshanunua jumla ya tani **36,323.559** sawa na asilimia **99.78** ya lengo la kununua tani 36,405. Kiasi hiki cha mahindi kilichokuwa tayari kimenunuliwa kinakadiriwa kuwa na thamani zaidi ya shilingi **29,369,276,200.00**.

**ii. . Njia za ununuzi zilizotumika katika ununuzi wa mwaka 2023/2024**

Katika kufikia malengo ya ununuzi yaliyowekwa, njia tatu za ununuzi zilipangwa kutumika. Njia hizo zilizopangwa na kutumika ili kufanikisha malengo ilikuwa ni pamoja na:

a. Kununua kwa njia ya vituo vya ununuzi vya kudumu pamoja na vile vya kuhama hama,
b. Kununua kwa njia ya vikundi vya wakulima pamoja na vile vya ushirika na;
c. Kununua kwa kutumia Mawakala mbalimbali ambao waliingia mikataba na NFRA.

**iii. Mpango wa ununuzi**

Ili kuweza kuwafikia wakulima wote waliofanikiwa kulima, kuvuna na kupata ziada kwa ajili ya kuuza, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa kushirikiana na Mkoa, ulipanga kutekeleza zoezi la ununuzi kwa Halmashauri saba za mkoa wa Ruvuma ambazo ni Nyasa, Mbinga Mji, Mbinga DC, Songea DC, Madaba, Manispaa ya Songea na Namtumbo.

Ili kutekeleza kazi hizo, vituo 21 vya ununuzi vilifunguliwa ili kusogeza soko kwa wakulima. Mchanganuo wa kiasi kilichonunuliwa kwa kila kituo hadi kufikia tarehe 31/12/2023 ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba 2 hapa chini. Aidha, Mawakala na Vikundi vya wakulima vilitumika katika zoezi hili la ununuzi.

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa kiasi kilichonunuliwa kwa kila kituo kilichotumika hadi tarehe 31 Disemba, 2023**

| NA | JINA LA KITUO | KIASI KILICHONUNULIWA (TANI) |
|---|---|---:|
| 1 | Mgazini | 2,367.416 |
| 2 | Ruhuwiko | 2,925.041 |
| 3 | Namabengo | 1,739.300 |
| 4 | Tingi | 10.590 |
| 5 | Mpitimbi | 1,610.561 |
| 6 | Magagura | 2,445.646 |
| 7 | Muungano zomba | 1,537.746 |
| 8 | Kizuka | 2,774.888 |
| 9 | Nakahuga | 821.466 |
| 10 | Madaba | 1,072.544 |
| 11 | Mtyangimbole | 299.850 |
| 12 | Mwanamonga | 668.117 |
| 13 | Kindimba juu/chini | 334.222 |

| NA | JINA LA KITUO | KIASI KILICHONUNULIWA (TANI) |
|---|---|---|
| 14 | Mpepai | 207.210 |
| 15 | Mbinga mjini | 649.722 |
| 16 | Matiri | 577.453 |
| 17 | Kigonsera | 2,798.715 |
| 18 | Namtumbo | 1,135.269 |
| 19 | Kitanda | 857.180 |
| 20 | Hanga | 1,415.506 |
| 21 | Mawakala | 9,129.921 |
| 22 | Vikundi vya wakulima/SACCOS | 934.504 |
| 23 | Changarawe | 10.750 |
| **JUMLA** | | **36,323.559** |

Nafaka hii ya mahindi ilinunuliwa kwa bei za kati ya shilingi 540 na 840 kwa kilo. Zoezi la ununuzi katika awamu ya pili ya ununuzi kwa mwaka 2023/2024 linaendelea.

**iv. Maendeleo ya mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa kanda ya Songea**

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2023, mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi kwa kanda ya Songea kwa tani 55,000 kwa kujenga vihenge vya kisasa 12 (tani 45000) na maghala mawili (2) yenye uwezo wa kuhifadhi tani elfu kumi (tani 10,000) ulikuwa umefikia wastani wa asilimia 54.07 ya utekelezaji, ambapo kwa upande wa vihenge mradi ulikuwa umefikia asilimia 86.22.

Aidha, kutokana na kusimama kwa utekelezaji wa mradi huu, umeifanya kanda ya songea kutofikia kwa wakati lengo lake la kuongeza uwezo wa kuhifadhi kama ilivyopangwa.

### 8.2.3 Mafanikio

i. Kununua kiasi cha tani 36,323.559 hivyo kuongeza akiba ya chakula ya Taifa
ii. Kutengeneza ajira za muda takribani 1000 kwa watu mbalimbali waliotumika kwenye zoezi la ununuzi katika vituo mbalimbali vya ununuzi
iii. Kusaidia Serikali kukusanya kodi ya zuio inayotokana na mauzo ya mahindi pamoja na kodi ya mazao kwa Halmashauri.
iv. Kanda imefanikiwa kupata hati miliki za viwanja vyake vyote vilivyopo manispaa ya Songea.

### 8.2.4 Changamoto

i. Baadhi ya wakulima/ wafanyabiashara kuleta vituoni nafaka ambazo hazikidhi viwango vya ubora na hivyo kupata usumbufu wa kutakiwa kuyarudisha majumbani au kwenye stoo zao.

ii. Ufinyu wa bajeti ya fedha za kununulia nafaka na nafasi ya kuhifadhia nafaka inayonunuliwa.

iii. Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi wa wakala kulikosababisha Kanda kutoanza kunufaika na tani 55,000 zilizopangwa kuongezwa katika mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi. Hivyo, NFRA kuendelea kutegemea maghala ya watu binafsi.

## 8.2 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) MKOA WA RUVUMA

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA MAMLAKA YA MAPATO (TRA) MKOA WA RUVUMA.**

i. **UTANGULIZI:**
Kuwasilisha taarifa inayoelezea utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato **(TRA)** Mkoa wa Ruvuma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na kipindi cha **JUL**AI mpaka **DESEMBA** kwa mwaka wa fedha **2023/2024.**

ii. **MAKUSANYO JULAI 2022- JUNI 2023**
Kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2022/2023** tulikuwa na lengo la kukusanya **TZS 21,963,392,808.48/=** tuliweza kukusanya **TZS 29,508,385,703.55/=** sawa na asilimia **134%**, mchanganuo wa lengo na makusanyo kwa kila mwezi ni kama ifuatavyo: -

| Mwezi | Mwaka | Lengo la Mwezi | Makusanyo Mwezi | Utendaji |
|---|---|---|---|---|
| JULAI | 2022 | 1,605,360,000.00 | 1,259,874,491.84 | 78% |
| AGOSTI | 2022 | 1,587,042,808.48 | 1,514,231,016.24 | 95% |
| SEPTEMBA | 2022 | 1,802,700,000.00 | 2,121,824,533.23 | 118% |
| OKTOBA | 2022 | 1,765,900,000.00 | 1,903,825,444.39 | 108% |
| NOVEMBA | 2022 | 1,710,050,000.00 | 1,521,887,115.33 | 89% |
| DESEMBA | 2022 | 2,432,300,000.00 | 2,085,075,829.11 | 86% |
| JANUARI | 2023 | 1,745,740,000.00 | 1,915,801,409.87 | 110% |
| FEBRUARI | 2023 | 1,658,420,000.00 | 1,372,912,142.43 | 83% |
| MACHI | 2023 | 1,938,530,000.00 | 4,141,767,818.77 | 214% |
| APRILI | 2023 | 1,694,050,000.00 | 4,278,137,680.59 | 253% |
| MEI | 2023 | 1,702,680,000.00 | 4,067,636,353.08 | 239% |
| JUNI | 2023 | 2,320,620,000.00 | 3,325,411,868.67 | 143% |
| **JUMLA** | | **21,963,392,808.48** | **29,508,385,703.55** | **134%** |

iii. **MAKUSANYO JULAI 2023- DESEMBA 2023**
Kwa kipindi cha **JULAI,2023** mpaka **DESEMBA, 2023** tulikua na lengo la kukusanya **TSHS. 7,894,001,416.00** tulifanikiwa kukusanya **TSHS. 8,653,241,462.49** sawa na asilimia **109.62%,** mchanganuo wa lengo na makusanyo kwa kila mwezi ni kama ifuatavyo**: -**

| Mwezi | Mwaka | Lengo la Mwezi | Makusanyo Mwezi | Utendaji |
|---|---|---|---|---|
| JULAI | 2023 | 1,203,444,899.00 | 897,427,306.73 | **74%** |
| AGOSTI | 2023 | 1,141,488,574.00 | 1,211,410,316.95 | **106%** |
| SEPTEMBA | 2023 | 1,359,425,314.00 | 1,947,174,224.36 | **143.24%** |
| OKTOBA | 2023 | 1,249,588,452.00 | 1,334,089,305.66 | **106.76%** |
| NOVEMBA | 2023 | 1,185,373,720.00 | 1,303,304,069.94 | **109.95%** |
| DESEMBA | 2023 | 1,754,680,457.00 | 1,959,836,238.85 | **111.69%** |
| **JUMLA** | | **7,894,001,416.00** | **8,653,241,462.49** | **109.62%** |

## 4. UKARABATI WA JENGO LA OFISI YA MKOA

Serikali kupitia Uongozi wa juu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania iliweza kutenga fedha na kufanya ukarabati Mkubwa wa jengo la Ofisi ya Mkoa. Kwani hapo awali jengo lilikuwa chakavu na hali mbali. Hadi kufikia **Desemba, 2023** ujenzi ulikuwa katika hatua za mwisho na hadi hivi sasa jengo limekamilika na linatumika.

Kukamilika kwa jengo hili kumewezesha kuwa na nafasi ya kutosha kwa watumishi pamoja na walipakodi ambao hufika kupata huduma.

Tunaishukuru serikali hususani **Mh. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan** kwa kutoa fedha za kutosha kwa lengo la ukarabati huu ambao umeboresha mazingira yetu ya kazi.

## 5. MIKAKATI NA MALENGO

(i) Kuwatembelea walipakodi na kuwahimiza ulipaji wa malimbikizo ya madeni ya kodi wanazodaiwa.

(ii) Kuwakumbusha walipakodi kulipa kodi kwa kutumia gari la Matangazo, kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa walipakodi.

(iii) Kuwahimiza walipakodi kulipa malimbiklizo ya kodi za nyuma kwa kuingia nao Mikataba ya namna ya kulipa madeni yao.

(iv) Kusimamia utoaji wa vibali vya leseni (Tax Clearance pamoja na Stika za Magari).

(v) Kuboresha utoaji wa huduma kwa kutoa mafunzo Maalum kwa wafanyakazi.

(vi) Kusimamia matumizi ya EFD, kwa kuwaweka maafisa katika maeneo ya starehe na maeneo mengine muhimu kwa ajili ya kusimamia utoaji wa Risiti. Pia kufanya mazoezi ya Kukagua mizigo ili kuhimiza wajibu wa kudai na kutoa risiti kwa mauzo au huduma zitolewazo.

(vii) Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Stempu za kielektroniki kwa kutembelea maeneo ya mauzo ya vimiminika kuhakiki uhalali wa

stempu maeneo hayo kama, Baa, Majumba ya Starehe, Maduka ya vinywaji ya jumla na rejareja.

(viii) Kutembelea maeneo mbalimbali kama, songea vijijini, songea wilayani ili kuongeza wigo wa walipakodi.

(ix) Kusimamia ukaguzi wa bidhaa zote zinazoingia nchini, kwa kufuata utaratibu mujibu wa sheria za forodha na ushuru, ikiwa pamoja na kuthaminisha thamani ya mizigo hiyo.

(x) Kusimamia ubadilishaji umiliki wa vyombo vyote vya moto kutoka kwa wanufaika wa misamaha kwenda kwa wasio wanufaika wa misamaha.

(xi) Kufanya doria katika sehemu mbalimbali ndani ya mkoa ili kudhibiti mianya yote ya bidhaa kuingizwa kwa njia ya magendo.

(xii) Kutambua idadi ya majengo na mabango kwa kushirikiana na watendaji wa mitaa kwaajili ya utekelezaji wa kukusanya kodi za pango Pamoja na ushuru wa mabango.

(xiii) Kuwaleta karibu washikadau wa Mamlaka ya Mapato kama TCCIA na JWT, kuwakusanya wamiliki wa biashara ili wahudhurie semina stahiki za kodi;

## 8.4 BENKI KUU YA TANZANIA - TAWI LA MTWARA TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA MKOA WA RUVUMA 2022/23

### 1.0 Mwenendo wa Uchumi

### 1.1 Pato la Taifa

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, uchumi wa Kanda ya Kusini Mashariki umeendelea kuimarika. Pato la Taifa (GDP) katika Kanda hii limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka na kufanya Kanda ichangie wastani wa asilimia 10.5 ya Pato la Taifa. Katika Mkoa wa Ruvuma, Pato la Taifa liliongezeka kutoka Sh. Bilioni 2,375.5 mwaka 2012 hadi kufikia Sh. Bilioni 6,393.7 mwaka 2022. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na uzalishaji katika shughuli za kilimo na madini. Katika mwaka 2022, Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 3.8 ya Pato la Taifa na kuwa juu ya mikoa mingine ya Kanda ya Kusini Mashariki iliyochangia kati ya asilimia 2.0 na asilimia 2.8 (Jedwali Na. 1). Aidha, mkoa wa Ruvuma ni wa tisa (9) katika kuchangia kwenye Pato la Taifa, kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara.

**Jedwali Na. 1: Pato la Taifa kwa Bei za Mwaka Husika**

| Mkoa | 2012 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | Mchango Kitaifa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | 1,151.7 | 2,315.3 | 2,406.4 | 2,621.1 | 2,922.7 | 3,142.7 | 3,429.8 | 2.0 |
| Lindi | 1,176.3 | 2,351.3 | 2,424.8 | 2,661.9 | 2,898.3 | 3,126.2 | 3,384.4 | 2.0 |
| Mtwara | 1,648.6 | 3,230.1 | 3,404.9 | 3,656.7 | 3,946.3 | 4,243.3 | 4,686.3 | 2.8 |
| **Ruvuma** | **2,375.5** | **4,512.7** | **4,699.8** | **5,108.7** | **5,506.4** | **5,911.2** | **6,393.7** | **3.8** |
| **Kanda ya Kusini Mashariki** | **6,352.1** | **12,409.5** | **12,935.9** | **14,048.5** | **15,273.7** | **16,423.3** | **17,894.3** | **10.5** |
| Kitaifa | 62,318.7 | 118,731.7 | 123,989.4 | 134,383.8 | 145,429.6 | 156,375.3 | 170,255.6 | 100.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, wastani wa pato kwa mtu (*GDP per capita*) katika mkoa wa Ruvuma umeongezeka kwa zaidi ya mara dufu, na kuwa juu ya wastani wa pato kwa mtu kitaifa, na juu ya mikoa mingine ya Kanda ya Kusini Mashariki kuanzia mwaka 2012 (Jedwali Na. 2). Wastani wa pato kwa mtu kwa mwaka kwa mkoa wa Ruvuma uliongezeka kutoka shilingi 1,725,241 mwaka 2012 hadi kufikia shilingi 3,458,329 mwaka 2022, ikilinganishwa na wastani wa pato kwa mtu kitaifa la shilingi 2,844,641 kwa mwaka.

**Jedwali Na. 2: Wastani wa Pato kwa Mtu**

Shilingi

| | 2012 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | 1,048,257 | 1,872,506 | 1,901,540 | 2,023,602 | 2,204,379 | 2,315,421 | 1,693,787 |
| Lindi | 1,360,424 | 2,440,501 | 2,464,847 | 2,650,117 | 2,825,452 | 2,983,606 | 2,834,478 |
| Mtwara | 1,297,252 | 2,310,995 | 2,390,944 | 2,520,014 | 2,668,422 | 2,814,912 | 2,866,306 |
| **Ruvuma** | **1,725,241** | **2,923,011** | **2,974,926** | **3,159,417** | **3,326,252** | **3,487,302** | **3,458,329** |
| **Kitaifa** | **1,428,496** | **2,327,517** | **2,356,348** | **2,476,430** | **2,598,534** | **2,708,999** | **2,844,641** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Mfumuko wa Bei

Katika mwaka 2022/23, mfumuko wa bei wa jumla katika mikoa yote ya Kanda ya Kusini Mashariki uliongezeka isipokuwa katika mkoa wa Pwani. Kwa ujumla, mfumuko wa bei katika Kanda hii uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.7 mwaka uliotangulia (Jedwali Na. 3). Hali hii ilisababishwa zaidi na upungufu wa chakula katika mikoa inayozalisha mazao makuu ya chakula kwa wingi, uliosababishwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji ya chakula hasi kutoka katika nchi jirani. Hali hii ilijitokeza zaidi katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2022/23. Hata hivyo, mfumuko wa bei uliopungua katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 kutokana na kupungua kwa bei za vyakula.

**Jedwali Na. 3: Mfumuko wa Bei**

| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24Q1 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pwani** | **Mfumuko wa bei wa jumla** | **5.0** | **6.9** | **9.7** | **7.4** | **1.9** | **1.4** |
| | Mfumuko wa bei za vyakula | 6.4 | 10.3 | 16.1 | 3.6 | 1.6 | -3.6 |
| | Mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula | 3.9 | 4.0 | 5.3 | 10.0 | 2.1 | 4.4 |
| **Lindi** | **Mfumuko wa bei wa jumla** | **1.4** | **1.8** | **6.5** | **0.1** | **5.8** | **7.9** |
| | Mfumuko wa bei za vyakula | -0.4 | 2.2 | 10.2 | 2.1 | 11.5 | 14.4 |
| | Mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula | 4.2 | 1.3 | 3.2 | -0.6 | 3.0 | 4.7 |
| **Mtwara** | **Mfumuko wa bei wa jumla** | **4.8** | **7.2** | **4.9** | **1.9** | **4.4** | **2.3** |
| | Mfumuko wa bei za vyakula | 8.8 | 11.5 | 9.4 | 2.3 | 8.0 | 1.4 |
| | Mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula | 1.1 | 2.7 | 1.5 | 1.6 | 2.4 | 2.8 |
| **Ruvuma** | **Mfumuko wa bei wa jumla** | **6.7** | **3.3** | **3.2** | **3.2** | **4.8** | **4.6** |
| | Mfumuko wa bei za vyakula | 3.8 | 0.5 | 5.3 | 5.8 | 10.5 | 10.6 |
| | Mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula | 9.6 | 5.8 | 1.8 | 2.3 | 2.5 | 2.1 |
| **Kanda ya Kusini Mashariki** | **Mfumuko wa bei wa jumla** | **4.8** | **4.9** | **6.0** | **3.7** | **3.8** | **3.4** |
| | Mfumuko wa bei za vyakula | 4.7 | 6.0 | 10.2 | 3.5 | 6.6 | 3.3 |
| | Mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula | 4.9 | 3.8 | 2.8 | 4.0 | 2.4 | 3.4 |


Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kwa upande wa mkoa wa Ruvuma, mfumuko wa bei uliongezeka katika mwaka 2022/23 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, na kuanza kupungua katika kipindi cha

robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 (Jedwali Na. 3 na Kielelezo Na. 1). Kuongezeka kwa mfumuko wa bei mwaka 2022/23 kulitokana na kupanda kwa bei za vyakula pamoja na bei za mafuta aina ya petroli, gharama za usafiri, huduma za elimu na malazi. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula ndio uliopungua katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 (Kielelezo Na. 2).

**Kielelezo Na 1: Mfumuko wa Bei wa Jumla Katika Mkoa wa Ruvuma**


Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na 2: Mfumuko wa Bei za Vyakula na Usiojumisha Vyakula Katika Mkoa wa Ruvuma**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 1.2 Bei za Mazao ya Chakula

Kwa ujumla, bei za jumla za mazao makuu ya chakula katika Kanda ya Kusini Mashariki na katika mkoa wa Ruvuma ziliongezeka katika mwaka 2022/23

ikilinganishwa na mwaka uliotangulia kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4 na 5. kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**. Kupanda kwa bei kulisabishwa na upungufu wa chakula, uliosababishwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji hasi kutoka katika nchi jirani; pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kutokana na kupanda kwa bei za mafuta ya petroli na dizeli.

**Jedwali Na. 4: Wastani wa Bei ya Baadhi ya Mazao ya Chakula (Kwa Gunia la Kilo 100) – Kanda ya Kusini Mashariki**

| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 48,060 | 77,296 | 61,540 | 59,727 | 112,080 | 87.7 |
| Mchele | 178,940 | 192,257 | 168,071 | 182,277 | 279,055 | 53.1 |
| Maharage | 169,352 | 207,388 | 210,416 | 198,129 | 280,844 | 41.7 |
| Ulezi | 146,428 | 143,244 | 147,971 | 178,753 | 209,855 | 17.4 |
| Mtama | 101,349 | 119,837 | 131,037 | 122,963 | 178,992 | 45.6 |
| Viazi Mviringo | 94,971 | 89,731 | 86,062 | 74,732 | 112,634 | 50.7 |

Chanzo: Vizara ya Viwanda na Biashara

**Jedwali Na. 5: Wastani wa Bei ya Baadhi ya Mazao ya Chakula (Kwa Gunia la Kilo 100) – Mkoa wa Ruvuma**

| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 33,330 | 58,753 | 42,931 | 41,503 | 83,233 | 100.5 |
| Mchele | 182,924 | 182,714 | 174,500 | 184,741 | 275,910 | 49.3 |
| Maharage | 132,838 | 172,081 | 190,466 | 175,063 | 259,616 | 48.3 |
| Ulezi | 105,938 | 87,001 | 87,459 | 157,042 | 247,917 | 57.9 |
| Mtama | | 89,667 | 89,667 | 355,000 | 275,417 | -22.4 |
| Viazi Mviringo | 81,490 | 75,156 | 71,610 | 75,574 | 89,634 | 18.6 |

Chanzo: Vizara ya Viwanda na Biashara

**Bei za bidhaa za Mafuta aina ya Petroli.**

Katika mwaka 2022/23, bei za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa katika mikoa yote ya Kanda ya Kusini Mashariki zilipanda zikiakisi kupanda kwa bei katika soko la dunia (**Jedwali Na. 3)**. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji hasa baada ya nchi nyingi duniani kuanza kufungua tena shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimefungwa ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19; pamoja na kuendelea kwa vita nchini Ukraine vilivyosababisha kuwepo kwa upungufu wa mafuta, kuporomoka kwa thamani ya shilingi iliyopelekea kupanda kwa gharama za kuagiza bidhaa nje ya nchi.

**Jedwali Na. 3: Wastani wa Bei za Bidhaa za Mafuta ya Petroli**

| | Petroli | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Pwani | Lindi | **Mtwara** | Ruvuma | Kanda |
| 2019/20 | 2,083 | 2,174 | **2,107** | 2,320 | 2,171 |
| 2020/21 | 1,913 | 1,983 | **1,932** | 2,039 | 1,967 |
| 2021/22 | 2,571 | 2,624 | **2,589** | 2,691 | 2,619 |
| 2022/23 | 2,933 | 2,987 | **2,962** | 3,062 | 2,986 |
| ***Badiliko*** | ***14.1*** | ***13.8*** | ***14.4*** | ***13.8*** | ***14.0*** |
| | **Dizeli** | | | | |
| | Pwani | Lindi | **Mtwara** | Ruvuma | Kanda |
| 2019/20 | 2,040 | 2,166 | **2,054** | 2,278 | 2,134 |
| 2020/21 | 1,810 | 1,875 | **1,811** | 1,931 | 1,857 |
| 2021/22 | 2,449 | 2,562 | **2,516** | 2,619 | 2,536 |
| 2022/23 | 3,013 | 3,183 | **3,151** | 3,254 | 3,150 |
| ***Badiliko*** | ***23.0*** | ***24.2*** | ***25.2*** | ***24.3*** | ***24.2*** |
| | **Mafuta ya Taa** | | | | |
| | Pwani | Lindi | **Mtwara** | Ruvuma | Kanda |
| 2019/20 | 2,267 | 2,069 | **2,214** | 2,194 | 2,186 |
| 2020/21 | 2,093 | 1,767 | **2,073** | 1,866 | 1,950 |
| 2021/22 | 2,699 | 2,476 | **2,500** | 2,551 | 2,557 |
| 2022/23 | 4,303 | 3,299 | **3,476** | 3,318 | 3,599 |
| ***Badiliko*** | ***59.4*** | ***33.2*** | ***39.0*** | ***30.0*** | ***40.8*** |

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

## 2.0 Uzalishaji Katika Shughuli za Kiuchumi
## 2.1 Kilimo

### 2.1.1 Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

Katika mwaka 2022/23 uzalishaji wa mazao ya chakula katika Kanda ya Kusini Mashariki umezidi mahitaji kwa tani 848,347, sawa na kiwango cha utoshelevu wa chakula (Self Sufficiency Ratio – SSR) cha asilimia 145, ikiwa ni juu ya kiwango cha Kitaifa cha asilimia 124. Uzalishaji ulikuwa tani milioni 2.74 ikilinganishwa na tani milioni 2.30 mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Mkoa wa Ruvuma ulizalisha tani milioni 1.44 za mazao ya chakula, ikilinganishwa na uzalishaji wa tani milioni 1.27 mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Aidha, uzalishaji huo umezidi mahitaji ya mwaka 2023/24 kwa tani 725,820, sawa na kiwango cha

utoshelevu wa chakula cha asilimia 225. Ziada hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka ambapo mahindi yaliyochangia takriban asilimia 90% (Jedwali Na. 4 na 5). Hali hii ilisababishwa zaidi na hali nzuri ya hewa pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea (ya ruzuku).

Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mahitaji kwa mwaka 2023/24
Tani

| Mkoa | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Mahitaji 2023/24 | Badiliko (2021/22-2022/23) | Ziada (+)/Upungufu (-) | Kiwango cha Utoshelevu (SSR) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Ruvuma** | **1,341,740** | **1,268,745** | **1,436,954** | **639,323** | **13.3** | **797,631** | **225** |
| Mtwara | 417,908 | 396,987 | 430,641 | 402,412 | 8.5 | 28,229 | 107 |
| Pwani | 400,066 | 361,990 | 544,659 | 538,351 | 50.5 | 6,308 | 101 |
| Lindi | 285,168 | 273,933 | 325,310 | 308,831 | 18.8 | 16,479 | 105 |
| **Jumla** | **2,444,882** | **2,301,655** | **2,737,564** | **1,888,917** | **18.9** | **848,647** | **145** |

Chanzo: Wizara ya Kilimo
SSR inamaanisha kiwango cha utoshelevu wa chakula: ambapo asilimia 0-99 inaashiria upungufu wa chakula, asilimia 100-119 inaashiria utoshelevu wa chakula, na asilimia 120 na zaidi inaashiria ziada ya chakula.

**Jedwali Na. 5: Uzalishaji wa Mazao ya Nafaka na Yasiyo Nafaka na Mahitaji kwa mwaka 2023/24**

**Mazao ya Nafaka (Tani)**

| Mkoa | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Mahitaji 2023/24 | Badiliko (2021/22-2022/23) | Ziada (+)/Upungufu (-) | Kiwango cha Utoshelevu (SSR) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Ruvuma** | **998,550** | **1,018,889** | **1,179,154** | **453,334** | **15.7** | **725,820** | **260** |
| Mtwara | 94,063 | 85,499 | 35,786 | 244,980 | -58.1 | -209,194 | 15 |
| Pwani | 151,553 | 114,056 | 200,861 | 335,974 | 76.1 | -135,113 | 60 |
| Lindi | 156,983 | 142,706 | 113,016 | 193,048 | -20.8 | -80,032 | 59 |
| Jumla | 1,401,149 | 1,361,150 | 1,528,817 | 1,227,336 | 12.3 | 301,481 | 125 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo
SSR inamaanisha kiwango cha utoshelevu wa chakula: ambapo asilimia 0-99 inaashiria upungufu wa chakula, asilimia 100-119 inaashiria utoshelevu wa chakula, na asilimia 120 na zaidi inaashiria ziada ya chakula.

**Mazao Yasiyo ya Nafaka (Tani)**

| Mkoa | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Mahitaji 2023/24 | Badiliko (2021/22-2022/23) | Ziada (+)/Upungufu (-) | Kiwango cha Utoshelevu (SSR) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Ruvuma** | **343,190** | **249,856** | **257,800** | **185,989** | **3.2** | **71,811** | **139** |
| Mtwara | 323,845 | 311,488 | 394,855 | 157,432 | 26.8 | 237,423 | 251 |
| Pwani | 248,513 | 247,934 | 343,798 | 202,377 | 38.7 | 141,421 | 170 |
| Lindi | 128,185 | 131,227 | 212,294 | 115,783 | 61.8 | 96,511 | 183 |
| Jumla | 1,043,733 | 940,505 | 1,208,747 | 661,581 | 28.5 | 547,166 | 183 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo
SSR inamaanisha kiwango cha utoshelevu wa chakula: ambapo asilimia 0-99 inaashiria upungufu wa chakula, asilimia 100-119 inaashiria utoshelevu wa chakula, na asilimia 120 na zaidi inaashiria ziada ya chakula.

### 2.1.2 Hifadhi ya Taifa ya Chakula

Katika mwaka 2022/23, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea ilinunua tani 7,098.3 za mahindi kutoka kwa wakulima na kuhamisha tani 20,000 kwenda katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda Dodoma (tani 10,000), Babati (tani 5,000) and Arusha (tani 5,000). Hali kadhalika, tani 27,864.1 ziliuzwa katika Halmashauri zilizokuwa na upungufu wa chakula. Hali hii ilisababisha hifadhi ya mahindi yaliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Songea kupungua na kufikia tani 547.8 mwishoni mwa mwaka 2022/23 kutoka tani 41,313.6 mwishoni mwa mwaka uliotangulia (Jedwali Na. 6).

**Jedwali Na. 6: Hifadhi ya Taifa ya Chakula Katika Kanda ya Songea**

Tani

| Mwaka | Akiba Mwanzo wa Mwaka | Kiasi Kilichonunuliwa | Kiasi Kilichohamishwa (-)/Kilichoingia (+) | Matoleo | Akiba Ghalani Mwisho wa Mwaka |
|---|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | 5,182.0 | 54,068.0 | 0.0 | 3,450.1 | 55,799.9 |
| 2014/15 | 55,799.9 | 73,168.1 | 0.0 | 6,307.0 | 122,661.0 |
| 2015/16 | 122,661.0 | 0.0 | 0.0 | 113,845.1 | 8,815.9 |
| 2016/17 | 8,815.8 | 10,335.4 | 0.0 | 8,815.8 | 10,335.4 |
| 2017/18 | 10,335.4 | 11,557.5 | 0.0 | 0.0 | 21,892.9 |
| 2018/19 | 21,892.9 | 14,700.8 | -16,152.4 | 23.1 | 20,418.2 |
| 2019/20 | 20,418.2 | 3,345.9 | -11,058.9 | 3,000.0 | 9,705.1 |
| 2020/21 | 9,705.1 | 14,299.8 | -2,941.1 | 0.0 | 21,063.9 |
| 2021/22 | 21,063.9 | 40,249.8 | -19,918.9 | 81.2 | 41,313.6 |
| 2022/23 | 41,313.6 | 7,098.3 | -20,000.0 | 27,864.1 | 547.8 |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - Ofisi ya Kanda Songea
Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Songea
* chanya (+) inamaanisha kiasi cha mahindi kilichopokelewa; na hasi (-), ni kiasi kilichohamishwa

### 2.1.3 Ununuzi wa Mazao ya Biashara

Mazao makuu ya biashara katika mkoa wa Ruvuma ni pamoja, korosho, ufuta, kahawa na tumbaku. Katika mwaka 2022/23, kiasi cha tani 189,113.8 cha korosho kiliuzwa kwenye minada na soko la awali nchini, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 21.2 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia kutokana na kupungua kwa uzalishaji. Korosho iliyouzwa katika minada mkoani Ruvuma ilipungua kwa asilimia 39.5 hadi kufikia tani 15,282.7, na kufanya mkoa kuchangia asilimia 8.1 ya korosho yote iliyouzwa nchini (Jedwali Na. 7). Kupungua kwa uzalisha kulitokana na mabadiliko ya tabianchi hususan kuongezeka kwa hewa yenye unyevu (high humidity) pamoja na nyuzi joto ya chini ya centigrade 24. Hali hii iliyojitokeza kati ya mwezi Juni na Agosti na kusababisha magonjwa aina ya *blight na powdery mildew* yaliyoathiri korosho changa pamoja na maua ya korosho kupukutika.

**Jedwali Na. 7: Ununuzi wa Korosho**

Tani

| | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtwara | 172,771.1 | 194,673.9 | 123,417.8 | 133,727.1 | 118,634.3 | 131,396.9 | 101,058.5 | -23.1 |
| Lindi | 61,739.3 | 77,655.2 | 59,602.6 | 59,875.9 | 65,598.7 | 66,007.2 | 58,684.4 | -11.1 |
| **Ruvuma** | **15,429.2** | **20,876.2** | **18,528.3** | **24,624.6** | **15,342.1** | **25,242.5** | **15,282.7** | **-39.5** |
| Pwani | 13,265.9 | 19,527.6 | 22,579.8 | 9,610.4 | 8,757.0 | 16,314.1 | 13,385.8 | -17.9 |
| Mikoa mingine | 2,032.4 | 1,093.5 | 228.2 | 563.6 | 354.0 | 1,167.2 | 702.4 | -39.8 |
| Kitaifa | 264,887.5 | 313,826.4 | 224,521.1 | 228,401.5 | 208,686.1 | 240,127.9 | 189,113.8 | -21.2 |
| **Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%)** | **5.8** | **6.7** | **8.3** | **10.8** | **7.4** | **10.5** | **8.1** | |
| Wastani wa bei kwa Kilogram moja | 3,289.9 | 3,800.6 | 3,299.8 | 2,493.6 | 2,292.7 | 2,129.1 | 1,839.0 | -13.6 |

Chanzo: Bodi ya Korosho

Katika mwaka 2023, tani 94,938.9 za ufuta ziliuzwa kwenye minada iliyofanyika katika Kanda ya Kusini Mashariki, sawa na ongezeko la asilimia 20.8 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Ongezeko hili lilitokana na wakulima kuhamasika na hivyo kulima kwa wingi ufuta kufuatia bei nzuri iliyotolewa katika msimu wa mwaka 2022. Bei ya ufuta iliongezeka kwa asilimia 21.6 hadi kufikia wastani wa shilingi 3,748.4 kwa kilogramu. Hii ilichangiwa zaidi na kupungua kwa mafuta ya kupikia duniani na kupelekea kuongezeka kwa mahitaji, hali iliyosabishwa na vita ya Urusi na Ukraine. Katika mkoa wa Ruvuma, tani 8,550.1 za ufuta ziliuzwa ikilinganishwa na tani 8,286.5 za mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.2 (Jedwali Na. 8). Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 9.0 ya mauzo yote ya ufuta katika Kanda.

**Jedwali Na. 8: Ununuzi wa Ufuta – Kanda ya Kusini Mashariki**

Tani

| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Lindi | 30,728.0 | 52,600.0 | 62,230.0 | 49,885.2 | 43,472.0 | 53,519.4 | 23.1 |
| Mtwara | 5,193.0 | 6,975.3 | 13,289.9 | 11,077.0 | 9,287.2 | 17,819.0 | 91.9 |
| Pwani | 4,737.3 | 6,737.3 | 7,236.0 | 11,374.7 | 17,526.5 | 15,050.4 | -14.1 |
| **Ruvuma** | **5,867.5** | **8,283.6** | **11,706.0** | **6,107.4** | **8,286.5** | **8,550.1** | **3.2** |
| Kanda | 46,525.8 | 74,596.2 | 94,461.9 | 78,444.3 | 78,572.1 | 94,938.9 | 20.8 |
| **Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%)** | **12.6** | **11.1** | **12.4** | **7.8** | **10.5** | **9.0** | |
| Wastani wa bei kwa Kilogram moja | 3,000.0 | 2,970.0 | 1,761.7 | 2,402.5 | 3,082.2 | 3,748.4 | 21.6 |

Chanzo: Ofisi za KatibuTawala wa Mikoa

Vile vile katika mwaka 2022/23, mkoa wa Ruvuma uliuza tani 12,987.7 za kahawa na tani 354.2 ya tumbaku, ikiwa ni sawa na asilimia 15.4 ya kahawa na asilimia 0.7 ya tumbaku yote iliyouzwa nchini (Jedwali Na. 8). Hata hivyo, kiasi cha kahawa na tumbaku kilichouzwa mwaka 2022/23 kilipungua kwa asilimia 15.0 na asilimia 35.7, mutawalia kutokana na mbaya ya hali.

**Jedwali Na. 8: Ununuzi Kahawa na Tumbaku**

Tani

| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kahawa** | | | | | | |
| Jumla Kitaifa | 66,531.5 | 59,526.1 | 73,027.0 | 65,825.7 | 84,084.0 | 27.7 |
| **Ruvuma** | **15,463.9** | **10,984.3** | **12,487.7** | **15,271.0** | **12,987.7** | **-15.0** |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Jumla Kitaifa | 72,611.8 | 37,546.4 | 54,471.7 | 60,869.2 | 53,312.8 | -12.4 |
| **Ruvuma** | **1,247.8** | **785.7** | **531.8** | **550.8** | **354.2** | **-35.7** |
| Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%) | | | | | | |
| Kahawa | 23.2 | 18.5 | 17.1 | 23.2 | 15.4 | |
| Tumbaku | 1.7 | 2.1 | 1.0 | 0.9 | 0.7 | |

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania na Bodi ya Tumbaku Tanzania

## 2.2 Mifugo

Biashara ya mifugo imeendelea kuimarika katika Kanda ya Kusini Mashariki, na katika mwaka 2022/23, thamani ya mifugo (hususan ngombe, mbuzi na kondoo) iliyouzwa katika masoko yaliyosajiliwa iliongezeka hadi shilingi billioni 166.4 kutoka shilingi bilioni 118.4 mwaka uliotangulia, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama. Idadi ya ng'ombe waliouzwa walichangia asilimia 94.7 ya thamani yote ya mauzo ya mifugo katika Kanda ya Kusini Mashariki.

Uchambuzi wa thamani ya mifugo iliyouzwa kimkoa unaonyesha kuwa mkoa wa Pwani uliongoza kwa kuchangia asilimia 67.2 ya thamani yote ya mifugo iliyouzwa katika Kanda ya Kusini Mashariki, ukifuatiwa na mkoa wa Ruvuma asilimia (asilimia 16.1).

**Jedwali Na. 9: Idadi na Thamani ya Mifugo iliyouzwa Kwenye Masoko Yaliyosajiliwa**

Shilingi millioni

| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) | Mchango |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | 23,655.7 | 20,608.7 | 20,941.1 | 43,116.0 | 64,682.0 | 111,770.7 | 72.8 | 67.2 |
| **Ruvuma** | **778.1** | **2,982.4** | **19,274.4** | **23,981.6** | **30,878.0** | **26,768.0** | **-13.3** | **16.1** |
| Lindi | 7,613.1 | 4,913.3 | 6,379.2 | 10,589.2 | 12,791.4 | 22,137.6 | 73.1 | 13.3 |
| Mtwara | 2,280.5 | 9,831.8 | 6,237.5 | 8,895.2 | 10,099.4 | 5,732.7 | -43.2 | 3.4 |
| Kanda | 34,327.4 | 38,336.2 | 52,832.2 | 86,582.1 | 118,450.9 | 166,409.1 | 40.5 | 100.0 |
| **Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%)** | **2.3** | **7.8** | **36.5** | **27.7** | **26.1** | **16.1** | | |

Chanzo: Ofisi za KatibuTawala wa Mikoa

## 2.3 Uvuvi

Thamani ya samaki waliouzwa katika masoko yaliyosajiliwa katika Kanda ya Kusini Mashariki iliongezeka kwa asilimia 56.5 hadi kufikia shilingi bilioni 118.1 mwaka

2022/23, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia (Jedwali Na 10). Ongezeko hilo la thamani lilitokana zaidi na hali nzuri ya hewa kwa ajili ya shughuli za uvuvi, kuongezeka kwa idadi ya wavuvi na vyombo vya kuvulia samaki. Mkoa wa Pwani uliongoza kwa kuchangia asilimia 71.4 ya samaki wote waliouzwa, huku mkoa wa Ruvuma ukichangia asilimia 3.9.

**Jedwali Na. 10: Thamani ya Samaki waliouzwa Kwenye Masoko Yaliyosajiliwa Kimkoa**

| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) | Mchango |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | 40,318.9 | 37,646.1 | 62,245.5 | 60,902.0 | 84,388.3 | 38.6 | 71.4 |
| Mtwara | 1,461.2 | 1,404.9 | 2,915.0 | 5,529.6 | 7,534.6 | 36.3 | 6.4 |
| Lindi | 4,146.5 | 5,500.5 | 7,098.4 | 5,714.9 | 21,585.6 | 277.7 | 18.3 |
| **Ruvuma** | **1,911.1** | **1,989.7** | **2,212.4** | **3,315.5** | **4,615.0** | **39.2** | **3.9** |
| Kanda | 47,837.7 | 46,541.2 | 74,471.3 | 75,462.0 | 118,123.6 | 56.5 | 100.0 |
| **Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%)** | **4.0** | **4.3** | **3.0** | **4.4** | **3.9** | | |

Chanzo: Ofisi za KatibuTawala wa Mikoa

## 2.4 Misitu

Katika mwaka 2022/23, sekta ndogo ya misitu ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 18.3 katika Kanda ya Kusini Mashariki ikilinganishwa na shilingi bilioni 22.3 mwaka uliotangulia (Jedwali Na. 11). Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 8.3 ya mapato yote ya misitu katika Kanda ya Kusini Mashariki, wakati mkoa wa Pwani ukiongoza kwa asilimia 60 (Jedwali Na. 11). Mapato yatokanayo na mkaa na magogo yalichangia takribani asilimia 84.2 ya mapato yote ya misitu katika Kanda ya Kusini Mashariki (Jedwali Na. 12).

**Jedwali Na. 11: Thamani ya Mazao ya Misitu Kimkoa**

Shilingi milioni

| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) | Mchango |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | 11,277.7 | 13,718.5 | 15,312.6 | 10,970.8 | -28.4 | 59.9 |
| Lindi | 4,086.0 | 3,078.1 | 3,826.6 | 4,400.7 | 15.0 | 24.0 |
| Mtwara | 171.9 | 1,789.2 | 1,785.8 | 1,424.2 | -20.3 | 7.8 |
| **Ruvuma** | **706.5** | **1,159.6** | **1,415.4** | **1,523.3** | **7.6** | **8.3** |
| Kanda | 16,242.1 | 19,745.4 | 22,340.5 | 18,318.9 | -18.0 | 100.0 |

Chanzo: Ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Kanda za Kusini na Mashariki

**Jedwali Na. 12: Thamani ya Mazao ya Misitu**

Shilingi milioni

| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) | Mchango |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Magogo | 5,997.9 | 7,708.7 | 6,429.7 | 5,699.2 | -11.4 | 31.1 |
| Mbao | 108.7 | 161.3 | 239.6 | 1,512.4 | --- | 8.3 |
| Mkaa | 8,878.3 | 9,970.4 | 13,630.3 | 9,721.6 | -28.7 | 53.1 |
| Kuni | 418.4 | 536.3 | 582.0 | 505.5 | -13.2 | 2.8 |
| Nguzo | 247.6 | 370.9 | 238.2 | 144.9 | -39.2 | 0.8 |
| Mbao za kutengeneza saman | 591.3 | 990.2 | 852.5 | 580.3 | -31.9 | 3.2 |
| Mazao mengine | - | 7.7 | 368.2 | 155.0 | -57.9 | 0.8 |
| Jumla | 16,242.1 | 19,745.4 | 22,340.5 | 18,318.9 | -18.0 | 100.0 |

Chanzo: Ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Kanda za Kusini na Mashariki
---, badiliko linalozidi asilimia 100

## 2.5 Madini

Thamani ya madini yaliyochimbwa katika Kanda ya Kusini Mashariki iliongezeka kwa asilimia 81.8 mwaka 2022/23 na kufikia shilingi bilioni 1,325.0, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Ongezeko hili lilitokana zaidi na makaa ya mawe yanayochimbwa katika mkoa wa Ruvuma na kufanya mkoa wa Ruvuma uchangie asilimia 77.3 ya thamani yote ya madini katika Kanda. Kuongezeka kwa uzalishaji wa makaa ya mawe kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji kutoka katika nchi za Ulaya kufuatia kupanda kwa bei ya gesi asilia inayotumika kama chanzo cha nishati viwandani (Jedwali Na. 13).

**Jedwali Na. 13: Uchimbaji wa Baadhi ya Madini**

Shilingi Milioni

| Madini | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (%) | Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhahabu | Thamani | 16,960.4 | 27,792.2 | 28,230.7 | 24,990.4 | -11.5 | 1.9 |
| | Mapato | 1,219.3 | 1,907.9 | 2,028.7 | 1,690.5 | -16.7 | 3.3 |
| Makaa ya mawe | Thamani | 151,756.0 | 227,526.2 | 491,118.2 | 1,012,700.2 | --- | 76.4 |
| | Mapato | 6,504.8 | 8,907.1 | 19,071.2 | 36,607.4 | 92.0 | 72.5 |
| Chumvi | Thamani | 3,231.2 | 2,934.6 | 11,396.9 | 15,861.8 | 39.2 | 1.2 |
| | Mapato | 106.1 | 87.8 | 361.0 | 837.5 | --- | 1.7 |
| Chokaa | Thamani | 24,720.9 | 44,944.1 | 37,184.3 | 66,385.3 | 78.5 | 5.0 |
| | Mapato | 744.3 | 1,383.8 | 1,776.2 | 2,653.1 | 49.4 | 5.3 |
| Madini ya ujenzi | Thamani | 162,599.5 | 141,545.6 | 134,651.9 | 157,822.0 | 17.2 | 11.9 |
| | Mapato | 6,033.1 | 5,414.2 | 6,675.1 | 6,342.4 | -5.0 | 12.6 |
| Madini jasi | Thamani | 7,318.8 | 12,856.7 | 14,839.1 | 22,162.0 | 49.3 | 1.7 |
| | Mapato | 277.6 | 581.2 | 602.6 | 902.7 | 49.8 | 1.8 |
| Madini ya vito | Thamani | 1,519.7 | 1,707.1 | 6,706.6 | 6,568.8 | -2.1 | 0.5 |
| | Mapato | 105.1 | 119.0 | 464.0 | 459.5 | -1.0 | 0.9 |
| Madini mengine | Thamani | 30.8 | 1,045.8 | 4,826.0 | 18,555.6 | --- | 1.4 |
| | Mapato | 1.0 | 62.7 | 269.6 | 1,034.2 | --- | 2.0 |
| Jumla - Kanda ya Kusini Mashariki | Thamani | 368,137.4 | 460,352.1 | 728,953.7 | 1,325,046.1 | 81.8 | 100.0 |
| | Mapato | 14,991.2 | 18,463.7 | 31,248.4 | 50,527.3 | 61.7 | 100.0 |
| Mchango wa mkoa wa Ruvuma (%) | Thamani | 43.1 | 51.6 | 69.9 | 77.3 | | |
| | Mapato | 46.6 | 51.9 | 60.8 | 64.0 | | |

Chanzo: Ofisi za Madini za Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma; na Ofisi ya Madini ya Kanda ya Pwani na Dar es Salaam,
badiliko linalozidi asilimia 100

**Jedwali Na. 14: Mwenendo wa Mauzo ya Dhahabu na Vito Katika Masoko ya Madini ya Mikoa**

| 4 | Namtumbo | 13 | 101.85 | 13 | 13 | 286 |
| 5 | Tunduru | 86 | 553.012 | 86 | 86 | 1,892 |
| **JUMLA** | | **168** | **1,553.582** | **267** | **267** | **5,874** |

**Jedwali Na. 04** Mgawanyo wa vijiji kwa wilaya za mkoa wa Ruvuma katika mradi wa REA R3R2

| NA. | WILAYA | IDADI YA VIJIJI | VIJIJI VILIVYOWASHWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Songea | 32 | 14 |
| 2 | Mbinga | 99 | 41 |
| 3 | Nyasa | 35 | 20 |
| 4 | Namtumbo | 13 | 10 |
| 5 | Tunduru | 86 | 51 |
| | **TOTAL** | **267** | **136** |

### 5.1.2 MRADI WA UJAZILIZI (RURAL ELECTRIFICATION DENSIFICATION 2C).

Wakala umepanga kutekeleza mradi wa Ujazilizi 2C katika Mkoa wa Ruvuma. Lengo la mradi huu nikuongeza wigo wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo na vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu hiyo. Mradi huu utahusisha ujenzi wa 664km za mkondo mdogo wa umeme, transifoma 241 na kuunganisha wateja wa awali 13,744. Gharama za mradi huu zinatarajia kufika shilingi Bilioni 26.64.

Mchanganuo wa idadi ya vitongoji kwa kila Wilaya ni kama ifuatavyo;

**Jedwali No. 05** Vitongoji vitakavyonufaika na umeme

| NA | WILAYA | IDADI YA VITONGOJI |
|---|---|---|
| 1. | Songea DC | 50 |
| 2. | Mbinga | 42 |
| 3. | Nyasa | 19 |
| 4. | Namtumbo | 46 |
| 5. | Tunduru | 89 |
| **JUMLA** | | **246** |

### i. MRADI WA KUPELEKA UMEME KATIKA VITUO VYA AFYA NA PAMPU ZA MAJI ILI KUKABILIANA NA MAGONJWA YA KUAMBUKIZA NA UVIKO-19.

Mradi huu unahusu kusambaza umeme kwenye vituo vya afya na visima vya maji kwenye Mkoa wa Ruvuma ambapo inatarajiwa vituo vya afya, hospitali na visima vya maji 13 vitaungwa na huduma ya umeme. Serikali inatekeleza mradi huu ili kuongeza jitihada za kupambana na magonjwa ya kuambukiza ukiwemo UVIKO-19. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia shilingi milioni 848.063.

**Utekelezaji wa mradi**

Kwa sasa mradi bado upo katika hatua za awali za utekelezwaji kwa maana ya uchimbaji mashimo na usimamishwaji wa nguzo za msongo mdogo na msongo wa kati. Kwa mkoa wa Ruvuma mkandarasi anae tekeleza huu mradi ni kampuni ya STATE GRID LTD katika wilaya zote na tayari yupo eneo la kazi akiendelea na zoezi la kuwasilisha vifaa (material delivery).

**Jedwali Na.06** Maeneo ya Visima vya maji Vitakavyonufaika na mradi.

| Na | Mkoa | Wilaya | Kata | Kijiji/Eneo | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ruvuma | Namtumbo | Lusewa | Milonji | Kisima Cha Maji |
| 2 | Ruvuma | Namtumbo | Msindo | Lumecha | Kisima Cha Maji |
| 3 | Ruvuma | Namtumbo | Namabengo | Mdemwa | Kisima Cha Maji |
| 4 | Ruvuma | Songea | Litisha | Magima | Kisima Cha Maji |
| 5 | Ruvuma | Songea | Mpandangindo | Liweta | Kisima Cha Maji |
| 6 | Ruvuma | Tunduru | Nalasi | Nasomba | Kisima Cha Maji |
| 7 | Ruvuma | Tunduru | Matemanga | Ndenyende | Kisima Cha Maji |
| 8 | Ruvuma | Tunduru | Namwinyu | Daraja mbili | Kisima Cha Maji |
| 9 | Ruvuma | Tunduru | Namwinyu | Hulia | Kisima Cha Maji |
| 10 | Ruvuma | Tunduru | Ligunga | Ligunga | Kisima Cha Maji |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Ruvuma | Tunduru | Tinginya | Namatanda | Kisima Cha Maji |
| 12 | Ruvuma | Tunduru | Ligunga | Twendembele | Kisima Cha Maji |
| 13 | Ruvuma | Tunduru | Marumba | Mchekeni | Kisima Cha Maji |
| 14 | Ruvuma | Namtumbo | Ligera | Njoomlole | Kisima Cha Maji |
| 15 | Ruvuma | Namtumbo | Mchomoro | | |
| 16 | Ruvuma | Tunduru | Nandembo | Majala | Kisima Cha Maji |

**Jedwali Na.07** Maeneo ya Vituo vya afya Vitakavyonufaika na mradi.

| Na | Mkoa | Wilaya | Kata | Kijiji/Eneo | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ruvuma | Songea | Matimira | Matimira | Kituo cha Afya |
| 2 | Ruvuma | Songea | Magagula | Magagula | Kituo cha Afya |
| 3 | Ruvuma | Tunduru | Nalasi | Nalasi Lipepo | Kituo cha Afya |

**5.1.4 MRADI WA KUPELEKA UMEME VIJIJINI, KATIKA MIGODI MIDOGO, MAENEO YA VIWANDA NA MAENEO YA KILIMO.**

Mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 5 ya uchimbaji madini hususani wachimbaji wadogo, viwanda vidogo na mashamba ya kilimo katika Mkoa wa Ruvuma, lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa. Mradi utahusisha ujenzi wa 108.3km za mkondo wa kati wa umeme, 27km mkondo mdogo wa umeme na kufunga transifoma 16. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kufikia shilingi Bilioni 4.66.

**Jedwali Na. 8** Maeneo ya Migodi, Mashamba na Viwanda yatakayonufaika

| | | | Lot 26 Ruvuma | |
|---|---|---|---|---|
| NA | WILAYA | KIJIJI | MSONGO WA KATI (Km) | MSONGO MDOGO (Km) |
| 1 | Songea | Maniamba site 1 | 6.125 | 0.297 |
| 2 | Songea | Maniamba site 2 | 3.375 | 0.189 |
| 3 | Songea | Lutanga | 5.183 | 2.389 |
| 4 | Songea | Lumecha | 11.031 | 3.221 |
| 5 | Mbinga | Masuguru | 2.279 | 1.666 |
| 6 | Mbinga | Mbuyula | 6.029 | 1.307 |
| 7 | Nyasa | Kihurunga | 4.574 | 0.386 |
| 8 | Nyasa | Kizota | 0.271 | 1.013 |
| 9 | Nyasa | Liweta | 5.302 | 0.050 |
| 10 | Tunduru | Ngapa Mining site | 22.305 | 0.335 |
| 11 | Tunduru | Mbesa 1 | 1.091 | 2.044 |
| 12 | Tunduru | Mbesa 2 | 0.482 | 1.148 |

| | | | Lot 26 Ruvuma | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **MSONGO WA KATI (Km)** | **MSONGO MDOGO (Km)** |
| **NA** | WILAYA | **KIJIJI** | | |
| 13 | Tunduru | Mitwana | 6.517 | 0.299 |
| 14 | Tunduru | Tulieni | 7.597 | 0.050 |
| 15 | Tunduru | Mwangaza | 10.962 | 2.092 |
| 16 | Namtumbo | Suluti | 2.712 | 1.899 |

**Utekelezaji wa Mradi**

Mkandarasi yupo eneo la kazi akiendelea na kazi, kwasasa yupo katika hatua ya kusimamisha nguzo za msongo wa kati kwa maeneo ya Maniamba site1(6.125 Km) na Maniamba site 2(3.375 Km) na zoezi linalofuata ni uunganishaji wa nyaya za umeme kwenye nguzo (stringing) na pia anaendelea na zoezi la usimamishaji wa nguzo kuelekea maeneo ya mradi.

## 6.0 CHANGAMOTO

Mkoa wa Ruvuma unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Uchomaji wa moto wakati wa unadaaji mashamba ambao unaathiri miundombinu ya shirika.
ii. Matukio ya wizi wa waya za kwenye transfoma na vyuma vya kushikilia nguzo isianguke (base plate)
iii. Upungufu wa wafanyakazi katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa ujumla uliosababishwa na baadhi yao kuhamishwa au kustaafu
iv. Urefu wa line za kusambaza umeme 33KV na 11KV kuwa ndefu Zaidi.mfano line ya mbinga na namtumbo
v. Kutopatikana kwa vifaa kwa wakati mfano waya, nguzo, n.k kusababisha miradi mingi kuchelewa na wateja kutokujengewa kwa wakati.

### 6.1 JINSI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

i. Tumeendelea na zoezi la kupalilia visahani kwa kutumia wanavijiji na kuendelea kutoa elimu pamoja na mwaka huu tutaanza kutumia nguzo za zege kwa Mkoa wa Ruvuma
ii. Tunaendelea kushirikiana na jeshi la Polisi pamoja na viongozi wa serikali ili kuwabaini wanaofanya uharibifu huo na kuchukuahatua za kisheria.
iii. Juu ya upungufu wa wafanyakazi tumeshapeleka mahitaji makao makuu kitengo cha rasilimali watu pia tumeendelea kutumia wafungwa na wanakijiji kwa kazi ambazo sio za kiufundi.
iv. Tumeomba ngazi za juu kujengewa kituo cha kupozea umeme mbinga ili kupunguza urefu wa line na kuongeza njia nyingi badala ya kuwa na njia moja tu inayopeleka umeme mbinga na nyasa

## 7.0 MIPANGO YA UTENDAJI KAZI KWA MWAKA FEDHA 2023/24

Mkoa umejipanga kuhakikisha unatekeleza miradi yote iliyo kwenye mwaka huu wa fedha 2023/24 lengo kuu ikiwa ni: -

- Kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara ili kuongeza mapato na kuondoka karaha kwa wananchi wanayopata kwa kukatika kwa umeme.
- Kuondoa kabisa au kupunguza hitilafu zinazojitokeza kwenye mifumo ya laini ndogo za msongo 0.4kV, zinasosambaza umeme kwa wananchi kwa kuboresha maungio yote ya nyaya.
- Kuboresha mifumo ya usambazaji umeme ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la umeme hafifu linaathiri wananchi.
- Kusogeza huduma ya umeme maeneo ambayo yamejitokeza ambayo hayakuwa na umeme.
- Kuwaunganishia umeme wananchi kwa haraka kupitia mifumo mipya ya utendaji (Nikonekt).
- Kutatua matatizo yanayoripotiwa kwenye mfumo wa pamoja wa Miito (unified call center) kwa haraka kupitiwa mifumo ya uboreshaji uwajibikaji iliyoanzishwa (CRM-Customer Relation management).

## 8.0 MAFANIKIO

Mkoa wa Ruvuma baada ya kuunganishwa na grid umepata mafanikio mengi ikiwemo yafuatayo:

- Mwitikio mkubwa wa wananchi kulipia huduma ya umeme ili waunganishwe na huduma hii muhimu
- Ongezeko kubwa la wateja baada ya kuwa na umeme wa uhakika na kuridhisha
- Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya umeme, kutoka wastani wa bilioni moja (1) mwaka 2018 hadi billioni 1.5 mwaka 2023.
- Kuokoa gharama za uendeshaji baada ya kuzima vituo vinne (4) vya kuzalisha umeme kutumia mafuta baada ya Mkoa kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

## 8.5 WAKALA MAJI MIJINI NA VIJIJINI (RUWASA)

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI RUWASA MKOA WA RUVUMA HADI DISEMBA 2023

## 1.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Utangulizi**

Katika kipindi husika cha mwaka wa fedha **2022/2023** kiasi cha fedha cha Tsh. **28,758,612,824.23** kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maji katika Mkoa wa Ruvuma. Kiasi cha fedha kilichotolewa ni Tsh. **19,117,207,336.80** ambapo fedha iliyotumika ni Tsh. **19,117,207,336.80**

Hali ya utekelezaji wa miradi ni kama inavyonesha katika jedwali hapa chini

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Luharaga na Kihuruku | 1,163,502,774.00 | 946,513,301.56 | 946,513,301.56 | Umekamilika na unatoa huduma | Mradi uko kwenye hatua za uangalizi |
| 2 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Mbangamao | 1,810,439,739.89 | 1,357,463,979.97 | 1,357,463,979.97 | Mradi uko hatua za mwisho (95%),unatoa huduma | Mradi uko kwenye hatua za uangalizi |
| 3 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Ruvumachini | 1,315,905,699.80 | 773,716,605.98 | 773,716,605.98 | Mradi uko hatua za mwisho (95%),unatoa huduma | Mradi uko kwenye hatua za uangalizi na kumalizia sehemu ya kitongoji cha Changarawe |
| 4 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Maguu | 742,369,771.50 | 111,355,465.73 | 111,355,465.73 | Mradi uko asilimia 60 | Mkandarasi anasubiri bomba ili kukamilisha mtandao wa usambazaji. |
| 5 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kitanda | 473,101,856.40 | 257,555,604.00 | 257,555,604.00 | Mradi umekamilika na unatoa huduma | |
| 6 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Tanga | 817,492,457.71 | 292,623,868.00 | 292,623,868.00 | Mradi uko hatua za mwisho (95%),unatoa huduma | Ukamilishaji unaendelea |
| 7 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Utiri | 428,434,691.91 | 249,112,072.00 | 249,112,072.00 | Mradi umekamilika na unatoa huduma | |
| 8 | Mbinga | Ukarabati wa mradi wa maji Ndongosi | 665,127,081.82 | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 | Mradi uko hatua za mwisho (85%),unatoa huduma | |
| 9 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kitai | 562,000,000.00 | 321,710,650.44 | 321,710,650.44 | Mradi uko hatua za mwisho (95%),unatoa huduma | |
| 10 | Mbinga | Ukarbati wa mradi wa maji Ruanda | 396,001,772.00 | 311,974,944.10 | 311,974,944.10 | Mradi uko hatua za mwisho (95%),unatoa huduma | |
| 11 | Mbinga | Ukarabati wa Mradi wa maji kijiji cha Myangayanga | 305,412,608.94 | 135,220,396.58 | 135,220,396.58 | Mradi uko asilimia 60 | Mchakato wa ununuzi wa mabomba unaendelea. |
| 12 | Mbinga | Ukarabati wa Mradi wa maji kijiji cha Luwaita | 273,701,057.24 | 133,574,792.44 | 133,574,792.44 | Mradi uko asilimia 90 unatoa huduma | |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 13 | Songea | Ujenzi wa mradi wa maji Matimira | 1,336,625,870.00 | 772,045,503.6 | 772,045,503.6 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |
| 14 | Songea | Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Parangu | 848,133,186.73 | 591,036,470.12 | 591,036,470.12 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |
| 15 | Songea | Ukarabati wa Mradi wa maji Kijiji cha Mpitimbi 'B' | 285,000,000.00 | 285,890,215.00 | 285,890,215.00 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |
| 16 | Songea | Ukarabati wa Mradi wa maji Kijiji cha Mahanje | 250,000,000.00 | 250,000,000.00 | 250,000,000.00 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |
| 17 | Songea | Ujenzi wa Mradi wa maji Mbangamawe | 545,639,691.24 | 413,409,016.72 | 413,409,016.72 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |
| 18 | Nyasa | Upanuzi wa mradi wa maji Chimate | 390,870,000.00 | 390,870,000.00 | 390,870,000.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 19 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa maji Upolo | 256,111,111.00 | 256,111,111.00 | 256,111,111.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 20 | Nyasa | Ukarabati wa mradi wa maji Mtipwili | 233,000,000.00 | 233,000,000.00 | 233,000,000.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 21 | Nyasa | Ukarabati wa Mradi wa maji Lundo | 438,772,073.00 | 438,772,073.00 | 438,772,073.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 22 | Nyasa | Upanuzi wa mradi wa maji Lukali - Ngingama | 142,768,889.00 | 142,768,889.00 | 142,768,889.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 23 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa maji Kwambe | 332,423,658.00 | 332,423,658.00 | 332,423,658.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 24 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa maji Likwilu | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |
| 25 | Nyasa | Ujenzi wa maradi wa maji Litoromelo | 79,920,250.00 | 79,920,250.00 | 79,920,250.00 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 26 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa maji Ngumbo awamu ya kwanza | 2,209,249,910 | 2,209,249,910 | 2,209,249,910 | Mradi umekamilika | Mradi unatumika kwa upande wa awamu ya kwanza |
| 27 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa Maji wa Lituhi Group. | 2,217,871,207 | 2,217,871,207 | 2,217,871,207 | Utekelezaji umefikia 60% | Utekelezaji unaendelea |
| 28 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa Maji wa Liuli Group | 3,091,485,406.25 | 3,091,485,406.25 | 3,091,485,406.25 | Utekelezaji umefikia 85% | Utekelezaji unaendelea |
| 29 | Nyasa | Ujenzi wa mradi wa maji Nangombo - Kilosa | 620,109,686.00 | 620,109,686.00 | 620,109,686.00 | Mradi upo hatua za mwanzo za utekelezaji | Mradi upo hatua za mwanzo za utekelezaji |
| 30 | Nyasa | Ujenzi wa mradi Puulu - Songambele | - | - | - | Mradi upo hatua za mwanzo za utekelezaji | Mradi upo hatua za mwanzo za utekelezaji |
| 31 | Namtumbo | Mradi wa Maji Mgombasi | 323,145,781.90 | 323,145,781.90 | 323,145,781.90 | Utekelezaji umefikia 70% | Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 32 | Tunduru | Mradi wa maji Masuguru-Mchoteka | 2,416,574,071.52 | 362,486,101.73 | 362,486,101.73 | Utekelezaji umefikia 75% | Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 33 | Tunduru | Mradi wa maji wa Majimaji, Ligoma na Imani | 1,451,962,121.38 | 415,790,376.68 | 415,790,376.68 | Utekelezaji umefikia 85% | Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 34 | Tunduru | Uchimbaji wa visima virefu 18 | 535,460,400.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 15% | Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 35 | Tunduru | Ujenzi wa mradi wa maji Ndaje-Mbesa | 1,500,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 35% | Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| **JUMLA KUU** | | | **28,758,612,824.23** | **19,117,207,336.8** | **19,117,207,336.8** | | |

### 1.2 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Utangulizi**

Katika kipindi husika cha mwaka wa fedha **2023/2024** kiasi cha fedha cha Tsh. **26,227,930,053.31** kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maji katika Mkoa wa Ruvuma. Kiasi cha fedha kilichotolewa ni Tsh.**6,159,379,061.48** ambapo fedha iliyotumika ni Tsh. **5,821,317,694.08**

Hali ya utekelezaji wa miradi ni kama inavyonesha katika jedwali hapa chini

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Matiri | 947,006,156.67 | 369,780,000.00 | 369,780,000.00 | Mradi uko hatua za mwisho (85%),unatoa huduma. | Unaendelea kujengwa |
| 2 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kitura | 943,175,205.00 | 141,476,280.00 | 141,476,280.00 | Mradi uko (30%), unatoa huduma. | Mkandarasi amelipwa fedha ya awali. |
| 3 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Ntunduwaro | 250,000,000.00 | 120,000,000.00 | 104,014,900.00 | Mradi uko (75%), unatoa huduma | Unaendelea kujengwa |
| 4 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kambarage | 2,884,478,730.00. | 432,671,809.00 | 432,671,809.00 | Mradi uko asilimia 15 | Mkandarasi amelipwa fedha ya awali. |
| 5 | Mbinga | Upanuzi wa mradi wa maji Amanimakolo | 1,695,868,516.80 | 0.00 | 0.00 | Maandalizi ya kazi yanaendelea. | Mkandarasi amekabidhiwa eneo la kazi. |
| 6 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Mkwaya | 375,139,800.00 | 0.00 | 0.00 | Mradi uko asilimia 15 | Mradi unaendelea kutelezwa. |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Langiro asili | 400,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | Mchakato wa ununuzi wa bomba unaendelea. |
| 8 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kilindi na Barabara | 300,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utafutaji wa chanzo na usanifu | |
| 9 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Pachasita na Lipembe | 462,662,071.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | |
| 10 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Ngima | 253,988,179.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | Mchakato wa ununuzi wa bomba unaendelea |
| 11 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Linda | 450,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | |
| 12 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Tukuzi | 450,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Usanifu unaendelea | |
| 13 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Mtama | 400,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | |
| 14 | Mbinga | Ujenzi wa mradi wa maji Kipololo | 400,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utafutaji wa chanzo unafanyika na usanifu | |
| 15 | Mbinga | Ujenzi wa chujio la maji Kigonsera/Mkako | 300,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Manunuzi yanaendelea | |
| 16 | Songea | Mradi wa maji Kijiji cha Lwangweni | 618,000,000.00 | 618,000,000 | 618,000,000 | Umekamilika kwa 100% | Mradi unatoa huduma kwa wananchi |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | Songea | Mradi wa maji Kijiji cha Lipaya | 1,936,886,234.85 | 874,736,718.2 | 874,736,718.2\ | Umekamilika kwa 99% | Mradi unaendelea na unatoa huduma kwa wananchi |
| 18 | Songea | Mradi wa maji Kijiji cha Lipokela | 734,744,190.00 | 466,653,195.35 | 466,653,195.35 | Umekamilika kwa 89% | Mradi unaendelea bado haujaanza kutoa huduma ya maji |
| 19 | Songea | Mradi wa maji Kijiji cha Kizuka | 730,430,013.00 | 366,422,154.65 | 366,422,154.65 | Umekamilika kwa 85% | Mradi unaendelea bado haujaanza kutoa huduma ya maji |
| 20 | Songea | Mradi wa maji Mtyangimbole | 5,565,324,305.08 | 834,798,645.76 | 834,798,645.76 | Umekamilika kwa 65% | Mradi unaendelea bado haujaanza kutoa huduma ya maji |
| 21 | Songea | Mradi wa maji Kijiji cha Lutukila na Ndelenyuma | 1,614,363,301.70 | 562,110,151.38 | 562,110,151.38 | Umekamilika kwa 55% | Mradi unaendelea bado haujaanza kutoa huduma ya maji |
| 22 | Nyasa | Ukarabati wa mradi wa maji Ng’ombo | 130,000,000 | 0.00 | 0.00 | Mradi umefanyiwa mapitio ya usanifu | Mradi umefanyiwa mapitio ya usanifu |
| 23 | Nyasa | Ukarabati wa mradi wa maji Lunyele | 280,000,000 | 0.00 | 0.00 | Mradi umefanyiwa mapitio ya usanifu | Mradi umefanyiwa mapitio ya usanifu |
| 24 | Nyasa | Mradi wa maji Mbuyula - Ndengele | 649,864,237.30 | 0.00 | 0.00 | Mradi umefaniwa mapitio ya usanifu na umepata kibali cha utekelezaji | Mradi umefaniwa mapitio ya usanifu na umepata kibali cha utekelezaji |
| 25 | Nyasa | Mtupale | 445,000,000.00 | 100,000,000 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 5% | Utekelezaji unaendelea |
| 26 | Nyasa | Mitomoni, Mkalawa, Uhuru, Mipotopoto | 944,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Mradi upo hatua ya usanifu | Mradi upo hatua ya usanifu |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 27 | Nyasa | Mbanga | 808,800,000.00 | 0.00 | 0.00 | Usanifu wa mradi umekamilika | Usanifu wa mradi umekamilika |
| 28 | Nyasa | Luhangarasi, Luhindo | 150,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji bado haujanza | Utekelezaji bado haujaanza |
| 29 | Nyasa | Liuli | 10,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 95% | Utekelezaji unaendelea |
| 30 | Nyasa | Lituhi | 15,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 68% | Utekelezaji unaendelea |
| 31 | Nyasa | Nangombo - Kilosa | 431,135,960.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 8% | Utekelezaji unaendelea |
| 32 | Nyasa | Malungu | 322,374,419.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 75% | Utekelezaji unaendelea |
| 33 | Nyasa | Ngumbo | 419,543,568.00 | 328,000,000.00 | 328,000,000.00 | Utekelezaji wa awamu ya I umekamilika. Awamu ya II unaendelea (10%) | Utekelezaji unaendelea kwa awamu ya II |
| 34 | Nyasa | Puulu - Songambele | 200,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 12% | Utekelezaji unaendelea |
| 35 | Nyasa | Utafutaji wa vyanzo vya maji na usanifu wa miradi ya maji (Kikole,Lindi, Kigongo, Lumeme, Mtetema, Kihurunga, Mpepo, Ndonga, Malamala, Luhangarasi, Kimbango, Luhindo,Lunyele) | 267,019,825.00 | 28,617,000.00 | 18,000,000.000 | Kazi ya utafutaji wa vyanzo vya maji na usanifu wa miradi ya maji imefanyika (Mbanga, Kikole,Lindi Kigongo, Lumeme, Lunyele, , Mitomoni, Konganywita, Mkalawa, Mbuyula, ) | Utekelezaji unaendelea |
| 36 | Nyasa | Ukarabati wa mradi wa | 130,000,000 | 0.00 | 0.00 | Mradi umefanyiwa mapitio | Mradi umefanyiwa mapitio ya |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | maji Ng'ombo | | | | ya usanifu | usanifu |
| 37 | Namtumbo | Mradi wa Maji Luhimbalilo-Naikesi | 179,476,334.00 | 127,974,154.14 | 127,974,154.14 | Utekelezaji umefikia 70% | Kiasi cha fedha kilichotumika ni kwaajili ya Malipo ya Awali(Advance payment) na Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 38 | Namtumbo | Mradi wa Maji Likusanguse | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 | 109,167,042.60 | Utekelezaji umefikia 78% | Kiasi cha fedha kilichotumika ni kwaajili ya Malipo ya Awali(Advance payment) na Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 39 | Namtumbo | Mradi wa Maji Mchomoro | 320,138,953.00 | 320,138,953.00 | 320,138,953.00 | Utekelezaji umefikia 5% | Kiasi cha fedha kilichotumika ni kwaajili ya Malipo ya Awali(Advance payment) na Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 40 | Namtumbo | Mradi wa Maji Msisima-Mnalawi | 168,000,000.00 | 168,000,000.00 | 147,373,690.00 | Utekelezaji umefikia 10% | Kiasi cha fedha kilichotumika ni kwaajili ya Malipo ya Awali(Advance payment) na Utekelezaji wa mradi unaendelea |
| 41 | Tunduru | Ukarabati wa Mradi wamaji Namwinyu | 535,038,783.91 | 0.00 | 0.00 | Mradi upo kwenye hatua za kupata fundi na ununuzi wa malighafi | Taratibu za manunuzi zinaendelea |
| 42 | Tunduru | Ujenzi wa Mradi wa maji Hulia | 300,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 15% | Utekelezaji unaendelea |
| 43 | Tunduru | Ujenzi wa mradi wa maji Tuwemacho | 150,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 10% | Utekelezaji unaendelea |

| Na. | Wilaya | Jina la mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizoletwa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo kama yapo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 44 | Tunduru | Ujenzi wa mradi wa majiMsinji | 250,000.000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji bado haujaanza | |
| 45 | Tunduru | Ujenzi wa Mradi wa maji Misechela | 200,000,00.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 15% | Utekelezaji unaendelea |
| 46 | Tunduru | Ujenzi wa Mradi wa maji Nakapanya | 150,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Mradi upo kwenye hatua za kupata fundi na ununuzi wa malighafi | Taratibu za manunuzi zinaendelea |
| 47 | Tunduru | Ujenzi wa Mradi wa maji Masonya | 94,950,000.00 | 0.00 | 0.00 | Utekelezaji umefikia 80% | Utekelezaji unaendelea |
| **JUMLA KUU** | | | **26,227,930,053.31** | **6,159,379,061.48** | **5,821,317,694.08** | | |

## 3 .0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI

Mkoa wa Ruvuma umepata mafanikio yafuatayo kupitia utekelezaji wa miradi ya maji kama ifuatavyo

i. Kuongeza huduma ya upatikanaji wa Maji kutoka asilimia **58.4**, mwaka 2018 hadi kufikia asilimia **70**, mwaka **2023**
ii. Kuongeza huduma ya maji kutoka watu **891,616**, mwaka **2018** hadi kufikia watu **1,035,325**, mwaka **2023**
iii. Kuongezeka kwa vijiji vyenye huduma ya maji hadi kufikia vijiji **366** kati ya vijiji **533** vya Mkoa wa Ruvuma.

## 4. CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA MAJI KWA MKOA WA RUVUMA

Sekta ya maji Mkoa wa Ruvuma inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

| Na | CHANGAMOTO | MIKAKATI YA UTATUZI WA CHANGAMOTO |
|---|---|---|
| **1** | Uchelewashaji wa malipo ya Wakandarasi. | Tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya maji kupitia RUWASA Makao Makuu kuwalipa Wakandarasi kwa wakati ili kukamilisha miradi kwa wakati na kutoa huduma iliyokusudiwa |
| **2** | Uhalibifu wa mazingira unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa vyanzo vya maji na kupelekea kuwa na upungufu wa maji katika vyanzo vingi vya maji hasa wakati wa kiangazi, | Kuelimisha wananchi kuacha shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ya vyanzo vya maji. |
| **3** | Uendeshaji wa miradi ya maji hasa kwenye eneo la kuchangia huduma ya maji, wananchi kuwa na mwitikio mdogo wa kuchangia huduma ya maji hasa kulipia. | Kuendelea kuelimisha jamii juu ya uchangiaji wa huduma ya maji hasa kwa kulipia gharama za matumizi ya maji kulingana na bei elekezi (ukomo) |

## 8.6 MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA (SOUWASA)

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 1. Utangulizi

Manispaa ya Songea ina wakazi wapatao **286,285** kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa iliyofanyika mwaka 2022. Manispaa inakadiriwa kuwa na Wakazi **296,305**

katika mwaka 2023. Wakazi **260,733** wanapata huduma ya maji sawa na asilimia **88.0.** Mahitaji ya maji ni wastani wa lita milioni **20.593** kwa siku mwaka **2023** katika maeneo yote ya Manispaa. Uzalishaji wa maji ghafi ni wastani wa mita za ujazo **9,170** kwa siku. Jumla ya maunganisho ya maji safi ni **22,465**. Wastani wa upatikanaji wa huduma ya Majisafi ni saa **23.15** kwa siku. Mamlaka inatekeleza miradi ya maji mijini ili kiwango cha utoaji huduma kifikie asilimia **95** ifikapo mwaka 2025 kama ilani ya chama tawala inavyoelekeza

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya miradi mitano yenye thamani ya TZS **2,238,297,690.60** iliidhinishwa kutekelezwa na fedha kiasi cha TZS **1,372,742,627.50** kilitolewa na Wizara ya Maji kwa Mamlaka kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na | Jina la Mradi | Fedha zilizoidhinishwa | Fedha zilizotolewa | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Maboresho ya Uzalishaji Maji katika Mji wa Mbinga | 322,743,300.00 | 322,743,300.00 | 322,743,300.00 | 100% | Mradi umekamilika |
| 2. | Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa Maji Safi Katika Mji wa Tunduru | 596,972,005.50 | 140,660,965.00 | 140,660,965.00 | 100% | Mradi umekamilika |
| 3 | Mradi wa Maboresho ya Uzalishaji Maji Katika Mji wa Tunduru | 355,080,000.00 | 53,262,000.00 | 53,262,000.00 | 60% | Mradi Unaendelea |
| 4 | Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa Maji Safi Eneo la Mwengemshindo Katika Manispaa ya Songea | 547,521,500.00 | 530,004,000.00 | 530,004,000.00 | 100% | Mradi umekamilika |
| 5 | Ujenzi wa Mradi wa Maji Eneo la Viwanda Lilambo Katika Manispaa ya Songea | 415,980,885.10 | 326,072,362.50 | 326,072,362.50 | 100% | Mradi umekamilika |
| **Jumla** | | **2,238,297,690.60** | **1,372,742,627.50** | **1,372,742,627.50** | | |

**Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuishia Desemba 2023**

Mamlaka inatekeleza miradi ya maji kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:

| Na | Jina la Mradi | Fedha idhinishwa | Fedha zilizotolewa | Fedha zilizotumika | hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Mradi wa Maji Eneo la Subira Katika Manispaa ya Songea | 1,168,863,390.00 | 175,329,508.50 | 175,329,508.50 | 40% | Mradi Unaendelea |
| 2. | Mradi wa kimkakati wa miji 28 katika Mji wa Songea | 145,773,015,609.69 | 21,865,952,341.45 | 21,865,952,341.45 | 0% | Mradi umeanza tarehe 2 Januari 2024 |

**2. Changamoto**

i. Miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na upatikanaji wa fedha

ii. Chanzo cha maji cha bwawa kilichoainishwa katika mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa miji 28 kutokidhi mahitaji ya mji wa Songea

**3. Utatuzi wa Changamoto**

i. Mamlaka imekuwa ikiwasiliana na kuikumbusha Wizara ya maji kuhusu kutolewa kwa fedha za miradi ili ikamilike kwa wakati

ii. Mamlaka kwa kushirikiana na Bonde la mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Wizara ya Maji na Wananchi imepata chanzo cha maji cha mto Njuga katika eneo la Kijiji cha Kikunja kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea

## 8.7 TAARIFA YA OFISI YA ARDHI MKOA WA RUVUMA.

### UTANGULIZI

Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Ruvuma ilianzishwa mnamo mwezi Machi, 2020. Uanzishwaji waOfisi hizi ni moja ya mikakati ya Serikali kusogeza huduma karibu na wananchi ili kukabiliana na changamoto za Sekta hii na kukidhi mahitaji ya huduma za ardhi za Kupanga miji na vijiji, Uthamini,Upimaji, Umilikishaji na Usajili wa Hati na Nyaraka mbalimbali. Awali huduma hizi zilikuwa zinatolewa katika Ofisi ya ardhi Kanda ya Kusini (Mtwara) hivyo, wananchi walilazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita mia sita kufuata huduma hizi ambazo kwa sasa zinatolewa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.

## 2.0 KAZI ZILIZOFANYIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KUANZIA JULAI,2023 HADI DISEMBA,2023

Ofisi ya Ardhi Mkoa inaendelea kusimamia na kutekeleza kazi za upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na nyaraka mbalimbali, utatuzi wa migogoro ya Ardhi na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kama ilivyoainishwa hapo chini;

### UPIMAJI WA VIWANJA NA MASHAMBA

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya viwanja **9300** na mashamba **06** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine kwa mchanganuo ufuatao:

**Viwanja na Mashamba yaliyopimwa**

| NA | HALMASHAURI | VIWANJA | | MASHAMBA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA |
| 1 | Songea Manispaa | 4484 | 448,000,000.00 | 0 | 0 |
| 2 | Songea DC | 224 | 22,400,000.00 | 2 | 1,290,000.00 |
| 3 | Mbinga Mji | 412 | 41,200,000.00 | 0 | 0 |
| 4 | Mbinga DC | 798 | 79,800,000.00 | 3 | 1,935,000.00 |
| 5 | Tunduru | 2686 | 268,600,000.00 | 0 | 0 |
| 6 | Madaba | 264 | 26,400,000.00 | 1 | 645,000.00 |
| 7 | Nyasa | 372 | 37,200,000.00 | 0 | 0 |
| 8 | Namtumbo | 60 | 6,000,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | **9,300** | **930,000,000.00** | **6** | **3,870,000.00** |

Pia katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2023, jumla ya Viwanja **2988** na mashamba **08** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine. Aidha, jumla ya mipaka ya vijiji **45** imepimwa kama ilivyoanishwa katika jedwali hapo chini:

| NA | HALMASHAURI | VIWANJA | | MASHAMBA | | MIPAKA YA VIJIJI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA |
| 1 | Songea Manispaa | 1258 | 125,800,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2 | Songea | 122 | 12,200,000 | 1 | 645,000 | 0 | 0 |
| 3 | Mbinga Mji | 199 | 19,900,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | Mbinga | 262 | 26,200,000 | 0 | 0 | 16 | 64,000,000 |
| 5 | Tunduru | 209 | 20,900,000 | 4 | 2,580,000 | 29 | 116,000,000 |
| 6 | Madaba | 614 | 61,400,000 | 3 | 1,935,000 | 0 | 0 |
| 7 | Nyasa | 190 | 19,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 8 | Namtumbo | 134 | 13,400,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | **2988** | **298,800,000** | **6** | **5,160,000** | **45** | **180,000,000** |

**MIPANGO MIJI NA VIJIJI**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya michoro **43** ya Mipangomiji yenye jumla ya viwanja **20,189** vya matumizi mbalimbali kutoka Mamlaka za upangaji ilipokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa. Aidha jumla ya viwanja **1,577** vimerasimishwa. Mchanganuo wa taarifa hii ni kama unavyoonekana hapa chini:

| Na | Halmashauri | Idadi ya Michoro ya Mipango Miji | Idadi ya viwanja vilivyopangwa | Viwanja vilivyorasimishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga DC | 9 | 4,181 | 0 |
| 2 | Mbinga TC | 7 | 3,035 | 0 |
| 3 | Namtumbo DC | 5 | 1,391 | 0 |
| 4 | Nyasa DC | 0 | 0 | 382 |
| 5 | Madaba DC | 0 | 0 | 0 |
| 6 | Songea DC | 1 | 145 | 0 |
| 7 | Songea MC | 17 | 8,341 | 1,195 |
| 8 | Tunduru DC | 4 | 3,096 | 0 |
| | **JUMLA** | **43** | **20,189** | **1,577** |

Aidha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Disemba,2023 jumla ya michoro **39** ya Mipangomiji yenye jumla ya viwanja **11,958** vya matumizi mbalimbali kutoka Mamlaka za upangaji ilipokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa, aidha jumla ya viwanja **778** vimerasimishwa**.** Mchanganuo wa taarifa hii ni kama unavyoonekana hapa chini: -

| Na | Halmashauri | Idadi ya Michoro ya Mipangomiji | Idadi ya viwanja vilivyopangwa | Idadi ya Viwanja vilivyorasimishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga DC | 3 | 121 | 0 |
| 2 | Mbinga TC | 9 | 3,570 | 647 |
| 3 | Namtumbo DC | 2 | 156 | 0 |
| 4 | Nyasa DC | 3 | 1,098 | 131 |
| 5 | Madaba DC | 11 | 3,790 | 0 |
| 6 | Songea DC | 0 | 0 | 0 |
| 7 | Songea MC | 8 | 1,603 | 0 |
| 8 | Tunduru DC | 3 | 1,620 | 0 |
| | **JUMLA** | **39** | **11,958** | **778** |

**UMILIKISHWAJI ARDHI NA USAJILI WA HATI**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya miamala **1,455** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa pamoja na Hati Milki **1,349** zimeandaliwa na kusajiliwa. Pia kuanzia Julai 2023 hadi Disemba 2023 jumla ya miamala **614** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa pamoja na Hati Milki **1003** zimeandaliwa na kusajiliwa. Jedwali hapo chini linatoa mchanganuo wa utekelezaji Hatimiliki kwa mwaka 2022/2023 pamoja na mwaka wa fedha 2023/2024 kuanzia tarehe 1 Julai hadi Disemba 2023.

| NA | HALMASHAURI | IDADI YA HATI | |
|---|---|---|---|
| | | 2022/2023 | JULAI-DISEMBA 2023 |
| 1 | Mbinga DC | 127 | 48 |
| 2 | MbingaTC | 215 | 197 |
| 3 | Songea MC | 578 | 351 |
| 4 | Namtumbo DC | 50 | 36 |
| 5 | Madaba DC | 64 | 38 |
| 6 | Songea DC | 39 | 207 |
| 7 | Nyasa DC | 146 | 25 |
| 8 | Tunduru DC | 130 | 101 |
| | **JUMLA** | **1349** | **1,003** |

**UTHAMINI**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya taarifa za Uthamini 425 za madhumuni mbalimbali zenye thamani ya Tshs. 75,126,199,500/= zimeidhinishwa. Aidha kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Disemba,2023 jumla ya taarifa za Uthamini 1,326 za madhumuni mbalimbali zenye thamani ya Tshs**. 22,800,000,000/=** zimeidhinishwa. Jedwali hapo chini limeanisha taarifa zilizoidhinishwa;-

| NA. | HALMASHAURI | 2022/2023 | JULAI 2023 HADI NOVEMBA 2023 |
|---|---|---|---|
| 1. | Songea Manispaa | 126 | 807 |
| 2. | Songea DC | 10 | 64 |
| 3. | Mbinga Mji | 40 | 92 |
| 4. | Mbinga DC | 7 | 0 |
| 5 | Tunduru DC | 8 | 3 |
| 6 | Madaba DC | 7 | 53 |
| 7 | Nyasa DC | 10 | 162 |
| 8. | Namtumbo DC | 7 | 26 |
| 9. | Makampuni Binafsi | 210 | 119 |
| **JUMLA** | | **425** | **1,326** |

**MIGOGORO YA ARDHI**

Ofisi ya Ardhi Mkoa imepokea na kushughulikia migogoro ya Ardhi mbalimbali inayohusu mipaka ya Kijiji na Kijiji, mipaka ya Vijiji na maeneo ya Uhifadhi, Hivyo migogoro 37 kati ya maeneo ya hifadhi na mipaka ya vijiji imetatuliwa. Migogoro mingine iliyotatuliwa ni migogoro inayotokana na ucheleweshwaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi ikiwemo eneo la Mwengemshindo lililotwaliwa na EPZA, migogoro kati ya wamiliki wa ardhi na Halmashauri pamoja na migogoro kati ya Taasisi na Taasisi.

Aidha Mhe.Mkuu wa Mkoa ameunda kamati maalumu ya kusikiliza na kushughulikia malalamiko na migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Ruvuma. Ambapo jumla ya wananchi 76 wenye malalamiko na migogoro ya ardhi wamehudumiwa

**MAKUSANYO YA MADUHULI YA SERIKALI**

Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Ruvuma imeendelea kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa lengo la kukusanya jumla ya **Tshs. 3,000,000,000/=** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, jumla ya Tshs. **1,669,902,120/=** zilikusanywa sawa na asilimia **55.7** ya lengo.

Aidha katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mkoa umepangiwa kukusanya jumla ya Tshs. **3,680,000,000/=.** Hadi kufikia tarehe 30 Disemba 2023, jumla ya Tshs. **760,532,163.49/=** zimekusanywa kutokana na Kodi ya pango la Ardhi na tozo mbalimbali za Ardhi sawa na asilimia **20.7.** Mikakati ya kuongeza makusanyo ya kodi ya Ardhi pamoja na maduhuli mengine yatokanayo na Ardhi ikiwemo kutoa elimu ya ulipaji kodi, kuandaa na kusambaza ankara za umilikishaji na kutoa Hati za madai ya kodi inaendelea katika Halmashauri zote kama ilivyoelekezwa na Wizara**.**

## 3.0 MRADI WA UBORESHAJI WA MILKI SALAMA (LAND TENURE IMPROVEMENT PROJECT - LTIP)

Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni miongoni mwa Halmashauri saba (7) nchini zilizochaguliwa kutekeleza mradi wa aina hii na ulianza rasmi kutekelezwa mapema mwezi Februari 2023. Hadi kukamilika kwake Mradi huu unatarajia kufanikisha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 103 na kutoa Hati milki za kimila 44,000 kwa wnanchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 mradi umeshafanya utekelezaji katika maeneo muhimu yafuatayo;

i. Kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi wa Wilaya ya Mbinga (District Land Use Framework Project - DLUFP).
ii. Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 34 imefanyika
iii. Migogoro ya mipaka ya vijiji 14 imetatuliwa
iv. Mipaka ya vijiji 24 imeuhishwa na kupimwa upya
v. Vipande vya ardhi 28,406 vimetambuliwa na kupandishwa kwenye mfumo

wa ILMIS

vi. Mipango kina ya vitovu ya Kijiji kimoja (01) imefanyika

vii. Elimu ya sheria za ardhi, Mazingira na Utawala kwa vijiji 40 imetolewa.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa namna ya pekee tunatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuendelea kutupa ushirikiano tangu Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Ruvuma ianzishwe. Tunawashukuru pia, Wakuu wote wa Wilaya na Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), wadau mbalimbali, Taasisi mbalimbali pamoja na watumishi wote wa Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma pamoja na watu binafsi kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia tangu kuanzishwa rasmi kwa Ofisi ya Ardhi Mkoa, tunawashukuru sana. Tunaomba tuendeleena ushirikiano huu.

## 8.8 MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA - MKOA WA RUVUMA

### TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA MKOA WA RUVUMA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA JULAI –DISEMBA 2023

Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Mkoa wa Ruvuma zinahusika na utambuzi na usajili wa wananchi na wageni wakaazi wanaoishi ndani ya Mkoa wa Ruvuma.

1. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama Mamlaka tulikuwa na lengo la kuwasajili wananchi 37,067 ambapo kwa Wilaya ya Songea wananchi 11, 706, Mbinga wananchi 8,916, Namtumbo wananchi 5,413, Nyasa wananchi 3,333 na Tunduru wananchi 7,698.

Hadi kufikia tarehe 30/60/2023 Mamlaka tuliweza kuwasajili wananchi 19,597 sawa na asilimia 53%.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 tulipokea na kugawa Vitambulisho vya Taifa 636.

**Taarifa za kila Wilaya ni kama zilivyo kwenye jedwali hapo chini**:

| S/N | WILAYA | LENGO LA USAJILI | WALIOSAJILIWA | VITAMBULISHO VILIVYOGAWIWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SONGEA | 11,706 | 5,429 | 398 |
| 2 | MBINGA | 8,916 | 8,148 | 93 |
| 3 | NYASA | 3,333 | 668 | 118 |
| 4 | NAMTUMBO | 5,413 | 3,594 | 18 |
| 5 | TUNDURU | 7,698 | 1,758 | 9 |
| | **JUMLA** | **37,067** | **19,597** | **636** |

2. Shughuli zilizotekelezwa na ofisi za NIDA katika kipindi cha Julai – Disemba 2023 ni kama ifuatavyo.

Wananchi waliosajiliwa katika kipindi hicho kwa Mkoa wa Ruvuma ni 10.389 sawa na asilimia 29% katika lengo la kuwasajili Wananchi 35,800 zoezi ambalo bado linaendelea.

Vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa katika kata mbalimbali ndani ya Mkoa wa Ruvuma ni **453,867** ambapo kati ya hiyo idadi ni Vitambulisho **196,923** ambavyo vimeshachukuliwa na wananchi na zoezi la ugawaji wa vitambulisho bado linaendelea katika ngazi ya mitaa na vijiji.

**Taarifa za kila Wilaya ni kama zilivyo kwenye jedwali hapo chini**

| S/N | WILAYA | LENGO LA USAJILI | WALIOSA JILIWA | VITAMBULISHO VILIVYOSAMBAZWA NGAZI YA MITAA/VIJIJI | VITAMBULISHO VILIVYOCHUKULIWA NA WANANCHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SONGEA | 8700 | 5,992 | 139,321 | 39,120 |
| 2 | MBINGA | 8400 | 1196 | 107,577 | 61,518 |
| 3 | NYASA | 6300 | 1628 | 37,617 | 11,555 |
| 4 | NAMTUMBO | 6400 | 614 | 60,461 | 33,730 |
| 5 | TUNDURU | 6000 | 959 | 108,891 | 51,000 |
| | **JUMLA** | **35,800** | **10,389** | **453,867** | **196,923** |

## 8.9 TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA OFISI YA AFISA MADINI MKAZI RUVUMA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DISEMBA, MWAKA 2023/2024

### 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma inahudumia Mkoa wa Ruvuma wenye Wilaya tano (05). Aidha, Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma ina ofisi ndogo za madini katika maeneo ya Ngaka na Tunduru. Ofisi hizi zinasimamiwa na Maafisa Migodi Wakazi (*Mines Resident Officers – MROs*).

Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma imetekeleza kikamilifu kazi mbalimbali kama ifuatavyo;

i. Utoaji wa leseni za madini na vibali mbalimbali;
ii. Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;
iii. Usimamizi wa masoko ya madini;
iv. Usimamizi wa uzalishaji na mauzo ya Makaa ya Mawe; na
v. Utoaji wa elimu kwa wachimbaji

### 2.0 UTOLEWAJI WA LESENI MBALIMBALI ZA MADINI

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123 leseni za madini zimegawanyika katika makundi yafuatayo; (1) Leseni za Utafutaji wa Madini, (2) Leseni za Uchimbaji wa Madini, (3) Leseni za Uchenjuaji, (4) Leseni za Uyeyushaji wa Madini, (5) Leseni za Usafishaji wa Madini na (6) Leseni za Biashara ya Madini.

- Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba Mwaka 2023/2024 jumla ya leseni **21** za utafiti wa madini zilitolewa katika Mkoa wa Ruvuma.
- Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba Mwaka 2023/2024 jumla ya leseni **02** za uchenjuaji wa madini (*Processing Licence*) zilitolewa katika Mkoa wa Ruvuma.
- Hakuna leseni ya uchimbaji mkubwa *(Special Mining Licence SML)* iliyotewa kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika Mkoa wa Ruvuma kuna **leseni Moja** ya Uchimbaji Mkubwa wa madini ya Urani iliyotolewa **Mwaka 2013** iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo inayomilikiwa na kampuni ya Mantra.
- Leseni **Tatu (03)** za uchimbaji wa kati wa madini *ML (Mining License)* zilitolewa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai mpaka Disemba kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Hadi sasa kuna **leseni 8** za uchimbaji wa kati wa madini katika Mkoa wa Ruvuma. Leseni hizo ni ML 439/2011 na ML610/2020 zinazomilikiwa na Kampuni ya Tancoal Energy Ltd, ML 617/2019 na ML618/2019 zinazomilikiwa na kampuni ya Ruvuma Coal Ltd na ML 697/2023 inayomilikiwa na kampuni ya Aria Commodity Finance Fund Tz Ltd, ML724/2023, ML725/2023 na ML726/2023 zinazomilikiwa na Jitegemee Holdings Company Limited.
- Kwa upande wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini *(Primary Mining Licence-PMLs)* **Jumla ya leseni 327** zimetolewa tangu Mwezi Julai hadi Disemba kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Leseni za uchimbaji mdogo hutolewa kwa raia wa Tanzania na hudumu kwa kipindi cha miaka saba na mmiliki wa leseni anaweza kuhuisha leseni yake.
- Pia kuna Leseni za biashara kubwa ya madini (Dealers) na Leseni za biashara ndogo ya madini (Brokers) ambazo hutolewa katika Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma ambazo huisha uhai wake kila tarehe 30 Juni ya kila Mwaka. Kwa Mwezi Julai hadi Disemba Mwaka wa Fedha 2023/2024 jumla ya **leseni kubwa za biashara 106** zilitolewa na julma ya **leseni 29 za biashara ndogo** ya madini zilitolewa.

### 3.0 UKUSANYAJI WA MADUHULI YA SERIKALINI

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Moja tu (41,000,000,000.00**). Kwa

Mwezi Julai mpaka Disemba Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ilikusanya jumla ya **Shilingi Bilioni kumi na tatu Milioni mia moja ishirini na mbili Laki tatu na elfu tatu na Hamsini na Tisa Tu (13,122,303,059.00)** sawa na **asilimia 64%** ya lengo la kuanzia mwezi Julai hadi Disemba mwaka 2023/2024. Jedwali hapo chini linaonesha makusanyo ya kila mwezi kwa kipindi hicho.

***Jedwali 1: Taarifa ya mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba 2023.***

| **Mwezi** | **Makisio kwa Mwaka 2023/2024 (TZS)** | **Makusanyo Halisi Mwaka 2023/2024 (TZS)** | **% ya Makusanyo** |
|---|---|---|---|
| Jul-23 | 3,416,666,667 | 1,339,909,329 | 39% |
| Aug-23 | 3,416,666,667 | 2,989,675,356 | 88% |
| Sep-23 | 3,416,666,667 | 2,069,806,377 | 61% |
| Oct-23 | 3,416,666,667 | 2,794,188,161 | 82% |
| Nov-23 | 3,416,666,667 | 2,341,463,902 | 69% |
| Dec-23 | 3,416,666,667 | 1,587,259,934 | 46% |
| **TOTAL** | **20,500,000,000** | **13,122,303,059** | **64%** |

## 4.0 USIMAMIZI WA MASOKO YA MADINI

Ofisi ya Madini Ruvuma inasimamia masoko mawili ya madini. Soko la Madini ya dhahabu na Vito lililopo Songea pamoja na Soko la Madini ya vito katika Wilaya ya Tunduru. Masoko haya yote yanasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni za Masoko ya Madini za Mwaka 2019. **Jedwali Na. 2,** linaonyesha taarifa za madini yaliyouzwa kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***Jedwali 2: Taarifa ya mauzo ya Madini katika Masoko ya Madini Ruvuma katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba*** **Mwaka wa Fedha 2023/2024.**

| **AINA YA MADINI** | **UZITO (kg)** | **THAMANI (TZS)** | **MRABAHA (TZS)** | **ADA YA UKAGUZI (TZS)** | **KODI YA HUDUMA (TZS)** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Vito vya Thamani** | 104,991.88 | 5,349,313,877.64 | 320,958,832.66 | 53,493,138.78 | 16,047,941.63 |
| **Dhahabu** | 30.61 | 4,323,242,514.00 | 259,394,550.84 | 43,232,425.14 | 12,969,727.54 |
| **Jumla** | **105,022.49** | **9,672,556,391.64** | **580,353,383.50** | **96,725,563.92** | **29,017,669.17** |

## 5.0 UZALISHAJI WA MADINI YA MAKAA YA MAWE

Uchimbaji na uuzaji wa makaa ya Mawe Mkoani Ruvuma ulianza mwaka 2011 kukiwa na Kampuni moja tu ambayo ni *Tancoal Energy Ltd*. Mwaka 2019 wadau wengi

walijitokeza na kufanya uwekezaji katika shughuli za Makaa ya Mawe kulikopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hayo kuanzia mwaka 2020. Uzalishaji wa Madini ya Makaa ya Mawe hutoa mchango mkubwa kwenye maduhuli yanayokusanywa na Tume ya Madini Mkoani Ruvuma. Katika kipindi cha hivi karibuni, Makaa ya Mawe yamekuwa yakihitajika sana ulimwenguni kama chanzo cha nishati na hivyo kuwa moja ya chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali. Kwa Mwezi Julai hadi Septemba Mwaka wa Fedha 2023/2024 kiasi cha **Tani 1,356,249.84** kiliuzwa kikiwa na thamani ya **USD 144,930,322.79** huku serikali ikikusanya kiwango cha mrabaha wa **USD 3,937,434.98** na ada ya ukaguzi **USD 914,034.68**. Madini haya huuzwa ndani ya nchi, nchi zinazotuzunguka, barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es Salaam.

***Jedwali 4: Taarifa ya mauzo ya Madini ya Makaa ya Mawe katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2023 hadi Disemba, 2023 katika Mkoa wa Ruvuma.***

| MWEZI | UZITO(T) | THAMANI (USD) | MRABAHA (USD) | ADA YA UKAGUZI (USD) |
|---|---|---|---|---|
| Jul-23 | 114,095.48 | 16,008,532.03 | 348,903.95 | 160,085.32 |
| Aug-23 | 220,147.40 | 28,998,022.54 | 702,118.10 | 163,725.59 |
| Sep-23 | 305,815.87 | 38,175,155.73 | 972,415.28 | 164,434.75 |
| Oct-23 | 271,484.86 | 31,526,300.61 | 765,929.38 | 169,349.31 |
| Nov-23 | 275,365.33 | 30,041,364.43 | 743,550.79 | 138,041.69 |
| Dec-23 | 169,340.90 | 21,888,537.71 | 518,331.25 | 156,335.94 |
| **JUMLA** | **1,356,249.84** | **166,637,913.05** | **4,051,248.75** | **951,972.6** |

## 6.0 MCHANGO WA SEKTA YA MADINI MKOA WA RUVUMA

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Mkoa wa Ruvuma umeweza kuvutia na kupata wawekezaji wengi waliowekeza kwenye shughuli zinazohusiana na madini kama Uchimbaji wa Madini, Ununuzi wa Madini, Usafirishaji ya Madini na Uchenjuaji wa Madini. Ufuatao ni Mchango wa Sekta ya Madini katika Mkoa wa Ruvuma

iv. Kutoa ajira na hivyo kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi
v. Kuongeza fedha za kigeni nchini kutokana na madini hayo kuuzwa nchi za nje; na
vi. Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri mbalimbali yatokanayo na ushuru wa huduma unaotozwa kwenye madini yanayochimbwa.

## 7.0 CHANGAMOTO ZA SEKTA YA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA

i. Uharibifu wa mazingira kwa kukata miti na kuharibu/kuchafua vyanzo vya maji.
ii. Mabadiliko ya Sheria ya Madini, Sura 123 yaliyofanyika kipindi cha Bajeti ya Nchi ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 yaliyopunguza Mrabaha wa Madini ya Makaa ya Mawe kutoka asilimia tatu (3%) hadi asilimia moja (1%) kwa mauzo ya ndani ya Nchi;
iii. Ubovu wa barabara ya kutoka migodini (Tancoal, Jitegemee, Mbuyula n.k) kwenda kwenye vituo vya mauzo vilivyopo maeneo ya Mkeso na Amani Makolo, ubovu wa barabara unasababisha makampuni mengi kushindwa kufikia malengo ya uzalishaji;
iv. Kumekuwa na changamoto ya upimaji wa viwango vya ubora wa madini ya makaa ya mawe na kupata majibu kwa haraka.Changamoto hii imesababishwa na maabara zetu Nchini kukosa vyeti vya Ithibati na hivyo kusababisha sampuli za makaa ya mawe kupelekwa Afrika Kusini ambao ni washindani wetu wa biashara ya makaa ya mawe;
v. Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa ya kuongeza ubora wa makaa ya mawe (*Wash Plants)* ili kuweza kushindana na soko la Dunia;
vi. Kushindwa kukusanya maduhuli kutokana na kuwepo na leseni chache zinazofanya kazi. Hii inatokana na wachimbaji wadogo kutokuwa na mitaji ya kutosha kwa ajili ya shughuli za uchimbaji;
vii. Uwepo wa leseni za utafiti na uchimbaji ambazo haziendelezwi;
viii. Uelewa mdogo wa taarifa za kijiolojia, utambuzi wa aina za madini, thamani yake na masoko ya madini jambo linalopelekea; na
ix. Kusimama kwa uzalishaji wa madini ya shaba katika eneo la Mbesa – Tunduru.

## 8.0 MIKAKATI YA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO

i. Kuendelea kuhamasisha wachimbaji wa makaa ya mawe pamoja na wawekezaji wengine kuleta mitambo ya kuosha madini (*Wash Plants)* ili kuongeza ubora ambapo hadi sasa migodi ya Ruvuma Coal imeshafunga mitambo miwili ya kuoshea makaa ya mawe na BECCO inaendelea na taratibu za kusimika mtambo huo;
ii. Kusimamia kurudishwa kwa shughuli za mgodi wa TANCOAL Energy pamoja na wachimbaji wengine ili uzalishaji uweze kuongezeka;
iii. Kuendelea kutoa elimu ya Sheria ya Madini pamoja na Kanuni zake ili kuepusha migogoro katika maeneo ya uchimbaji wa madini na kupunguza kama sio kuondosha kabisa matukio ya utoroshaji na ukwepaji tozo za madini;

iv. Kuendelea kutoa *Default Notes* kwa mujibu wa Sheria kwa leseni zote zisizofanya kazi na kuzifuta ili kutoa nafasi kwa wachimbaji wenye nia ya kufanya uchimbaji wenye tija kwa serikali;
v. Ofisi kwa kushirikiana na *TANROADS* na Mkandarasi wa barabara ya Amani Makolo-Ruanda ili kuharakisha ujenzi wa barabara hiyo kukamililila mapema iwezekanavyo na
vi. Kuendelea kutoa huduma ya ugani kwa wachimbaji kwenye usimamizi wa utunzaji wa mazingira, kupunguza ajali na kuongeza uzalishaji kwenye uchimbaji.

## 8.10 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI - TAARIFA YA UMWAGILIAJI MKOA WA RUVUMA

**Hali ya Kilimo cha Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma**

Mkoa wa Ruvuma unakadiriwa kuwa na jumla ya hekta **197,108.2** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kati hizo hekta **7,388.3** zimeendelezwa, hii ni sawa na asimilia **3.7**.

### i. Skimu Za Umwagiliaji Zinazofanya Kazi

Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa, skimu **24** zinafanya kazi na **18** hazifanyi kazi. Skimu 24 zinazofanya kazi zina ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili, eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji **hekta 5,580** na eneo linalomwagiliwa lenye ukubwa wa **hekta 1,022** ambapo uzalishaji wake ni kati ya tani 2.8-5 za mpunga kwa ekari. Uzalishaji huu unaathirika kwani wakulima katika skimu za umwagiliaji hawana mbegu zilizoboreshwa na kusababisha uzalishaji kuwa chini kwa skimu nyingi za mkoa wa Ruvuma.

### ii. Skimu Za Umwagiliaji Zisizofanya Kazi kwa ufanisi

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya skimu 18 ambazo hazifanyi kazi kwa ufanisi zenye ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili, eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 3,324 na eneo linalomwagiliwa lenye ukubwa wa hekta 950 kutokana na miundombinu iliyokuwa imejengwa hapo awali kuathirika na mafuriko katika kipindi cha msimu wa mvua kwa mwaka 2019/20 kama Jedwali Na.1(b) hapo chini linavyoonyesha.

**Jedwali Na.1(a) : Skimu Za Umwagiliaji Zilizoboreshwa na Zinazofanya Kazi**

| S/NA. | Halmashauri | Jina la skimu | Eneo linalofaa kwa umwagiliaji (ha) | Eneo linalomwagiliwa (ha) | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tunduru | Kitanda | 600 | 100 | 3900 |
| | | Lekindo | 150 | 25 | 825 |
| 2 | Nyasa | Madaba na. 1 | 200 | 100 | 300 |
| | | Kimbande | 260 | 237 | 900 |
| | | Ngindo | 250 | 141 | 1,125 |
| 3 | Songea DC | Ngingama | 40 | 10 | 180 |
| | | Namatui | 220 | 100 | 636 |
| | | Mpitimbi B | 200 | 88 | 600 |
| | | Njoka | 120 | 33 | 660 |
| | | Muhukuru | 48 | 48 | 600 |
| 4 | Mbinga DC | Nakahuga | 270 | 96 | 686 |
| | | Litumbandiyosi | 250 | 82 | 750 |
| | | Msangamabuni | 300 | 70 | 700 |
| | | Msanjesi | 100 | 45 | 560 |
| | | Amani | 90 | 70 | 630 |
| 5 | Namtumbo | Njomlole | 120 | 62 | 350 |
| | | | | | |
| | | Namahoka | 150 | 30 | 780 |
| | | Kitanda | 100 | 60 | 540 |
| | | Mchomoro | 60 | 60 | 360 |
| | | Luhimbalilo | 50 | 20 | 225 |
| 6 | Madaba | Nambecha | 40 | 20 | 40 |
| | | Hanga Ngadinda | 400 | 55 | 248 |
| | | Mbangamawe | 250 | 50 | 600 |
| | Nyasa | Nyomboka | 520 | 160 | 607 |
| | **JUMLA** | **24** | **4,428** | **1,602** | **16,802** |

**Jedwali Na.1(b): Skimu Za Umwagiliaji Zisizofanya Kazi Kwa Ufanisi**

| HALMASHAURI | JINA LA SKIMU | ENEO LINALOFAA KWA UMWAGILIAJI (Ha) | ENEO LINALOMWAGILIWA (Ha) |
|---|---|---|---|
| Tunduru DC | Legezamwendo | 220 | 200 |
| | Misyaje | 200 | 175 |
| | Naikula | 250 | 200 |
| | Madaba | 600 | 350 |
| Namtumbo DC | Mtakuja | 300 | 300 |
| | Mwangaza | 250 | 250 |
| | Nambecha | 40 | 40 |
| | Liyuni | 140 | 100 |
| | Likuyuseka | 44 | 25 |
| | Mtonya | 75 | 75 |
| Songea DC | | | |
| | Ndongosi | 200 | 135 |
| Madaba DC | Luhimba | 55 | 25 |
| Mbinga DC | Luhagara | 150 | 65 |
| Nyasa DC | Kwambe | 200 | 100 |
| | Mkalachi | 150 | 100 |
| | Kimbande | 200 | 150 |
| Songea MC | Subira | 250 | 200 |
| | Kihekwa | 170 | 45 |
| **Jumla** | **18** | **3,495.00** | **2,535.00** |

**iii) Mafanikio Mwaka 2023/2024**

**a) Usajili wa Skimu**

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kusajili jumla ya skimu **63** kati ya skimu **102,** kati ya hizo skimu **56** zimesajiliwa kipindi cha mwaka **2022/2023** ili kuendana na mabadiliko ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji **Na. 4, 2013** na kanuni ya mwaka **2015** iliyopitishwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa katika mwaka **2023/2024** imejipanga kukamilisha zoezi la usajili wa **skimu 49** zilizobaki ili serikali iweze kuendelea na zoezi la kuelekeza fedha katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa skimu zilizoathiriwa na mafuriko katika vipindi vya miaka mitatu mfululizo **2019-2021.**

Katika Jedwali Na. 3 linaonesha idadi ya skimu zilizosajiliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**Jedwali Na.3: Idadi ya Skimu Zilizosajiliwa**

| Na. | Jina la Skimu | Jina la Chama cha Umwagiliaji | Namba ya Usajili | Wilaya |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Namatuhi | Umoja wa Umwagiliaji Namatuhi | NO. 081 | Songea Vijijini |
| 2. | Njoka | Umoja wa Umwagiliaji Njoka | No. 439 | Songea Vijijini |
| 3. | Madaba | Chama cha Umwagiliaji Madaba | No. 226 | Tunduru |
| 4. | Misyaje | Chama cha Wakulima Misyaje | NO. 227 | Tunduru |
| 5. | Machemba | Chama cha Wakulima Machemba | NO. 228 | Tunduru |
| 6. | Mdabwa | Chama cha Wakulima Mdabwa | NO. 229 | Tunduru |
| 7. | Chinunje | Skimu ya Chinunje | NO. 230 | Tunduru |
| 8. | Kitanda-Tunduru | Skimu ya Kitanda | No. 231 | Tunduru |
| 9. | Masonya | Umoja wa Wakulima Masonya | NO. 232 | Tunduru |
| 10. | Nambalapi | Skimu ya Nambalapi | NO. 244 | Tunduru |
| 11. | Mkalekawana | Skimu ya Mkalekawana | NO. 242 | Tunduru |
| 12. | Legezamwendo | Skimu ya Legezamwendo | NO. 234 | Tunduru |
| 13. | Lekindo | Skimu ya Lekindo | NO. 233 | Tunduru |
| 14. | Mbati | Skimu ya Mbati | NO. 243 | Tunduru |
| 15. | Kangomba | Skimu ya kangomba | NO. 235 | Tunduru |
| 16. | Mtonya | Skimu ya Mtonya | NO. 236 | Namtumbo |
| 17. | Naikula | Skimu ya Naikula | NO. 237 | Tunduru |
| 18. | Mchengamoto | Skimu ya Mchengamoto | NO. 238 | Tunduru |
| 19. | Nyomboka | Chama cha Umwagiliaji Nyomboka | NO. 239 | Nyasa |
| 20. | Lundo | Chama cha Umwagiliaji Lundo | No. 240 | Nyasa |
| 21. | Mnkalachi | Chama cha Umwagiliaji Mnkalachi | No. 241 | Nyasa |
| 22. | Lipupuma | Chama cha Umwagiliaji Lipupuma | No. | Namtumbo |
| 23. | Njoomlole | Chama cha Umwagiliaji Njomlole | No.412 | Namtumbo |
| 24. | Nasya | Chama cha Umwagiliaji Nasya | No. 418 | Tunduru |
| 25. | Naluwale | Chama cha Umwagiliaji Naluwale | No. 420 | Tunduru |
| 26. | Mkotamo | Chama cha Umwagiliaji Mkotamo | No. 419 | Tunduru |
| 27. | Luhimbalilo | Chama cha umwagiliaji Luhimbalilo | No. | Namtumbo |
| 28. | Kitanda-Tunduru | Chama cha umwagiliaji Kitanda | No. 231 | Namtumbo |
| 29. | Ndongosi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Ndongosi | NO. 090 | Songea Vijijini |

| Na. | Jina la Skimu | Jina la Chama cha Umwagiliaji | Namba ya Usajili | Wilaya |
|---|---|---|---|---|
| 30. | Morogoro | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Morogoro | NO. 089 | Songea Vijijini |
| 31. | Muhukuru Lilai | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Muhukuru Lilai | NO. 088 | Songea Vijijini |
| 32. | Nambendo | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Nambendo | NO. 088 | Songea Vijijini |
| 33. | Parangu | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Parangu | NO. 086 | Songea Vijijin i |
| 34. | Litapwasi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Litapwasi | NO. 087 | Songea Vijijini |
| 35. | Litisha | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Litisha | NO.084 | Songea Vijijini |
| 36. | Mpitimbi A | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Mpitimbi A | NO. 083 | Songea Vijijini |
| 37. | Mpitimbi B | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Mpitimbi B | NO. 082 | Songea Vijijini |
| 38. | Nakahuga | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Nakahuga | NO.080 | Songea Vijijini |
| 39. | Hanga Ngadinda | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Hanga Ngadinda | NO. 007 | Songea Vijijini |
| 40. | Amani | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Amani | NO. 049 | Namtumbo |
| 41. | Msanjesi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Msanjesi | NO. 072 | Namtumbo |
| 42 | Namahoka | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Namahoka | NO. 274 | Namtumbo |
| 43 | Sanga mabuni | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Sanga mabuni | NO.269 | Mbinga |
| 44 | Sanga Luhagara | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Sanga Luhagara | NO.272 | Mbinga |
| 45 | Kihekwa | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Kihekwa | NO.275 | Manispaa ya Songea |
| 46 | Chiulu | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Chiulu | NO. 435 | Nyasa |
| 47 | Litumbandyosi | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Litumbandyosi | No. 436 | Mbinga DC |
| 48 | Kimbande | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Kimbande | NO.437 | Nyasa |
| 49 | Njalila | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Njalila | NO.440 | Songea DC |
| 50 | Mtakuja | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Mtakuja | NO.441 | Namtumbo |
| 51 | Ruhuhu-Lituhi | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Ruhuhu-Lituhi | NO.442 | Nyasa |

| Na. | Jina la Skimu | Jina la Chama cha Umwagiliaji | Namba ya Usajili | Wilaya |
|---|---|---|---|---|
| 52 | Juhudi Luhagara | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Juhudi Luhagara | NO.443 | Mbinga DC |
| 53 | Muungano Kaula | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Muungano kaula | NO.444 | Mbinga DC |
| 54 | Naluwale | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Naluwale | NO.483 | Tunduru |
| 55 | Kimbande | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Kimbande | NO.473 | Nyasa |
| 56 | Subira | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Subira | NO.486 | Songea MC |
| 57 | Jitume nambapala | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Jitume nambapala | | Mbinga DC |
| 58 | Ngingama | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Ngingama | | Nyasa |
| 59 | Nkwambe | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Nkwambe | | Nyasa |
| 60 | Nyamilole farmers group | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Nyamilole | | Mbinga DC |
| 61 | Namasalau | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Namasalau | | Tunduru |
| 62 | Mtengashari | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Mtengashari | | Tunduru |
| 63 | Majengo | Chama cha wakulima wa umwagiliaji Majengo | | Tunduru |

**b) Skimu Zilizohuishwa Utendaji Kazi**

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma ikishirikiana na wilaya imefanikiwa kuhuisha skimu mbili za umwagiliaji zilizokuwa hazifanyi kazi ambazo ni Nyomboka iliyopo wilaya ya Nyasa na Mpitimbi B wilaya ya Songea.Pia skimu ya Muhukuru iliyokua miongoni mwa skimu zilizoathiriwa na mvua za mwaka 2019-2021 inaendelea kufanyiwa maboresho katika mwaka huu mwa fedha.

**iv. Ada ya Huduma ya Umwagiliaji na Tozo ya Urejeshaji wa Gharama za Uwekezaji katika Miundombinu ya Umwagiliaji.**

Katika kila skimu ya Umwagiliaji kila mkulima wa umwagiliaji anayemiliki eneo ndani ya skimu anawajibika kutoa Ada ya Huduma za Umwagiliaji ambayo ni asilimia tano (5%) ya wastani wa uzalishaji kwa ekari kwa msimu.

Aidha, Wamwagiliaji wanawajibu wa kurejesha gharama za uwekezaji wa ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ambayo serikali imewekeza ili kuendelea kupanua eneo la umwagiliaji katika maeneo mengine yenye uhitaji.

### v. Ukadiriaji wa Viwango Vya Ada na Tozo

Baada ya mavuno, kamati ya usimamizi, Bodi za usimamizi za vyama vya wamwagiliaji kwa kusaidiana na Wataaalamu wa kilimo, watakokotoa wastani wa uzalishaji uliopatikana kwa ekari kwa kila zao linalolimwa katika skimu na kupata kiwango cha ada ya huduma ya uendeshaji.

### vi. Ukusanyaji, Usimamizi na Matumizi ya Fedha za Ada na Tozo

Ofisi ya Umwagiliaji Mkoa ikishirikiana na Ofisi za Umwagiliaji Wilaya zimefanikiwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyama na wakulima katika skimu 63 kuhusu Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, ukusanyaji wa ada mbalimbali, usimamizi na matumizi ya fedha za ada hizo, zoezi hili bado ni endelevu tunaendelea nalo, ili kupata matokeo tunahitaji ushirikiano kwa Maafisa kilimo wa Wilaya na wale waliopo katika maeneo ambayo skimu za umwagiliaji zipo na zinaendelea kuboreshwa.

Kwa mujibu wa aya ya 84 (3) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), na kanuni ya marekebisho ya Kanuni ya mwaka 2021, Ada ya 5% ya Huduma ya Umwagiliaji zitalipwa na wakulima pia zitahifadhiwa katika akaunti maalumu ya skimu.

Katika Mkoa wa Ruvuma ni skimu **17** zilizolipa Ada ya mwaka kati ya skimu 102 kiasi cha Tshs **100,000/=** kwa kila skimu, sawa na jumla ya Tshs **1,700,000.00.** Ada ya Huduma za Umwagiliaji ambayo ni asimilia tano (5%) ya uzalishaji kwa ekari kwa msimu, skimu 15 zimelipa jumla ya kiasi cha **Tshs 14,995,000.00**/=, kiasi cha Tshs **525,000** zimelipwa kwa ajili ya usajili wa skimu.

Hivyo, mkoa umefanikiwa kukusanya jumla ya kiasi cha Tshs **17,220,000.00** kwa kipindi cha miezi 11.

### vii. Taarifa ya miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kwa bajeti 2023/24

### A. SKIMU YA UMWAGILIAJI INAYOENDELEA NA UKARABATI

| **Wilaya** | **Jina la skimu** | **Eneo (Ha)** | **Hatua za Utekelezaji** | **Kazi zinazoendelea kufanyika** |
|---|---|---|---|---|
| Songea | Muhukuru | 48 | • Mkataba: PA.137/2022-23/HQ/W/21<br>• Thamani ya Mradi: 986,267,305<br>• Mkandarasi: MS MUUNGANO GENERAL INTERPRISES JV MS SAMA CONSTRUCTION<br>• Kuanza Mradi : 01/09/2022 na kukamilika 31/12/2023<br>• Kazi imefikia 75% | Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. |

| Wilaya | Jina la skimu | Eneo (Ha) | Hatua za Utekelezaji | Kazi zinazoendelea kufanyika |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Malipo yaliyofanyika<br>-Malipo ya awali 137,361,390.75 pamoja na VAT<br>-Maombi ya malipo aliyolipwa awamu ya kwanza 156,730,173.79. Jumla ya malipo ni 294,091,864.54<br>• Kazi zilizofanyika<br>-Ujenzi wa banio na uimarishaji wa kingo za mto<br>-Uchepushaji wa mto<br>-Ujenzi wa barabara za mashambani<br>-Uchimbaji wa mfereji na umwagaji wa zege | |

**B. MABONDE YA KIMKAKATI YANAYOENDELEA UPEMBUZI YAKINIFU NA USANIFU**

Mabonde ya kimkakati ambayo yameingia katika hatua ya utekelezaji kutokana na bajeti ya mwaka 2023-2024 katika Mkoa wa Ruvuma ni matatu ambayo ni Ruvuma, Lityumbandyosi na Ruhuhu. Kati ya mabonde hayo matatu, bonde la Litumbandyosi lipo katika hatua ya utekelezaji. Kazi inayofanyika kwa sasa ni usanifu wa mradi na kazi hii inatekelezwa na Mshauri elekezi(consultant).

Jumla ya Kiasi cha fedha za kitanzania kitakachotumika katika kukamilisha kazi hii ya Usanifu ni Shilingi **Bilioni Moja, Milioni Mbili Themanini na Moja Laki Moja na Elfu Nnne Mia Sita tuu (1,281,104,600).**

Mabonde mawili yaliyosalia Washauri Waelekezi (Consultant) wameshapatikana na muda wowote kuanzia sasa watawasili katika maeneo husika kwa ajili ya utekelezaji na mara baada ya kuwasili taratibu za kuwajulisha Wakurugenzi wa Halmashauri husika utafanyika.

**Jedwali lifuatalo linaonyesha mabonde ya kimkakati yanayoendelea na shughuli za Upembuzi yakinifu na Usanifu.**

| Jina la Bonde | Wilaya | Ukubwa(Ha) | Hatua za Utekelezaji | Kazi zitakazofanyika |
|---|---|---|---|---|
| Bonde la mto Ruvuma | Songea,Tunduru, Nanyumbu, Newala, Tandahimba, Nanyamba na Mtwara | 26,066 | Hatua za manunuzi | Kukamilisha Upembuzi, Usanifu, na Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji |
| Bonde la Mto | Nyasa na Ludewa | 3,700 | Hatua za | Kukamilisha Upembuzi, Usanifu na |

| Jina la Bonde | Wilaya | Ukubwa(Ha) | Hatua za Utekelezaji | Kazi zitakazofanyika |
|---|---|---|---|---|
| Ruhuhu | | | manunuzi | Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji |
| Bonde la Litumbandyosi | Mbinga | 900 | Hatua za utekelezaji | Kukamilisha Upembuzi, Usanifu na Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji |

**C. SKIMU MPYA ZITAKAZOFANYIWA UPEMBUZI YAKINIFU NA USANIFU**

| WILAYA | HALMASHAURI | SKIMU | ENEO (Ha) | KAZI ZITAKAZOFANYIKA |
|---|---|---|---|---|
| Namtumbo | Namtumbo | Lipupuma | 250 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Nyasa | Nyasa | Chiulu | 1,000 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| | | Lundo | 600 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Tunduru | Tunduru | Mkotamo | 800 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| | | Namblapi | 1,000 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Songea | Songea Dc | Nambendo | 1,500 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| | | Kitai Prison | 7,800 | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |

**D. SKIMU ZA UKARABATI ZITAKAZOFANYIWA UPEMBUZI YAKINIFU NAUSANIFU**

| WILAYA | HALMASHAURI | SKIMU | ENEO (Ha) | AINA YA MAHITAJI |
|---|---|---|---|---|
| Namtumbo | Namtumbo | Msanjesi | 150 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| | | Mtakuja | 300 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| Mbinga | Mbinga Dc | Sanga Lugagala | 600 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| | | Sanga mabuni | 350 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| Nyasa | Nyasa | kimbande | 400 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| Tunduru | Tunduru | Madaba | 766 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| | | Kitanda | 455 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| | | Misyaje | 1,350 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |

| WILAYA | HALMASHAURI | SKIMU | ENEO (Ha) | AINA YA MAHITAJI |
|---|---|---|---|---|
| Songea | Songea Dc | Nakahuga | 250 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |
| | | Namatuhi | 350 | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ukarabati |

## E. MABWAWA YATAKAYOFANYIWA UPEMBUZI YAKINIFU, USANIFU NAUJENZI

| WILAYA | HALMASHAURI | BWAWA | KAZI ZITAKAZOFANYIKA |
|---|---|---|---|
| Mbinga | Mbinga DC | Mkungwe | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Nyasa | Nyasa | Lundo | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Tunduru | Tunduru | Mkotamo | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| | | Nambalapi | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |
| Songea | Songea DC | Nambendo | Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina |

## F. SKIMU MPYA ZA UMWAGILIAJI ZITAKAZOJENGWA

| Wilaya | Jina la Skimu | Eneo (Ha) | Kazi zilizopangwa kufanyika |
|---|---|---|---|
| Nyasa | Chiulu | 7,000 | Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji |
| Nyasa | Lundo | 600 | Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji |
| Nyasa | Kimbande | 400 | Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji |
| Tunduru | Mkotamo | 200 | Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji |
| | Nambalapi | 600 | |

## CHANGAMOTO

Licha ya kufikia mafanikio hayo bado Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mkoa wa Ruvuma tunakabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo zikitatuliwa tunaweza kufikia malengo ya makusanyo ya ada ya umwagiliaji na kuweza kusajili vyama vingi zaidi.

### Skimu ya Ndongosi

Skimu ya Ndongosi ilijengewa miundombinu na serikali ikiwemo banio na mfereji. Lakini tangu kujengwa kwake hadi sasa mradi huu haikuwahi kutumika katika shughuli za kilimo kwa madai kuwa wakulima hawana uzoefu na hivyo waliomba eneo hilo apewe muwekezaji,Ofisi ya Tume ya Taifa Umwagiliaji mkoa pamoja na wilaya wamefanya jitihada mbalimbali, kama kutafuta muwekezaji lakini ilishindikana kuendesha shughuli za kilimo ndani ya skimu. Mpaka sasa muafaka haujapatikana.

## 8.11 IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI - TAARIFA YA UTENDAJI KAZI JULAI MOSI, 2022 – JUNI 30, 2023

### UTANGULIZI

Idara ya Huduma za Uangalizi ni idara ambayo ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo inasimamia na kuratibu utekelezaji wa Adhabu Mbadala ya Gereza kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii Na.6/2002, (The Community Service Act, No 6 of 2002) na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura 247, Marejeo ya Mwaka 2002(The Probation Act, CAP. 247 RE:2002) ambapo mfungwa anatumikia adhabu yake kwenye jamii kwa kufanya kazi za kijamii katika ofisi ya serikali atakayopangiwa kwa masaa manne kwa siku kuanzia jumatatu hadi ijumaa. Lengo ni kupunguza msongamano Magerezani, hivyo kuipunguzia serikali gharama za kuwahudumia wafungwa wakiwa gerezani.

Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma ilianza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo ya idara kuanzia Desemba 2020, hii ni baada ya idara kuamua kuwa na maafisa Probesheni nchi nzima, ambapo kila mkoa kuna maafisa wanaoratibu, kutekeleza na kusimamia adhabu ya kifungo mbadala ya Gereza kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6/2002, (The Community Service Act, No. 6 of 2002) na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia (The Probation Act, CAP. 247 RE:2002).

Kwa kipindi cha Mwezi Julai Mosi, 2022 hadi Juni 30, 2023 tumefanikiwa kuingiza katika Programu wafungwa **mia moja thelathini na saba (137),** wanaume **mia moja kumi na mbili (112)**, kati yao **sita (06)** wametokea gerezani na **mia moja na sita (106)** kutoka mahakamani na Wanawake **ishirini na tano (25),** kati yao wafungwa **wawili (02)** kutoka Magereza na wafungwa **ishirini na tatu (23)** kutoka mahakamani.

Aidha kwa kipindi hicho katika Wafungwa **mia na saba (107)** wamemaliza kutumikia adhabu zao; Wanaume **sabini na nane (78)** na wanawake **ishirini na tisa (29).**

### UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA

Idadi ya Wilaya zinazotekeleza kazi za Idara katika Mkoa wa Ruvuma ni Songea Manispaa, Wilaya ya Songea Vijijini, Nyasa na Mbinga.

**Mchanganuo wa Mahakama katika Wilaya:**

- Mahakama Kuu Moja (1).

- Idadi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Moja (1).
- Idadi ya Mahakama za Wilaya- 5
- Idadi ya Mahakama za Mwanzo- 10.

**Idadi ya Watumishi katika Mkoa;**

- Waajiriwa wa Idara ya Huduma za Uangalizi = 2
- CDOs/social welfare officers - Hakuna

Taasisi zilizotambuliwa kwenye Mkoa kwa ajili ya kutoa huduma za urekebishaji. Ni taasisi za serikali tu ambazo ni

- Ofisi za Ustawi wa Jamii.
- Ofisi za Kata na Serikali za Mitaa.
- Mahakama.
- Hospitali za Wilaya na Mkoa
- Vituo vya Afya
- Taasisi za Elimu (Shule za Sekondari na Msingi).
- Zahanati.
- Vituo vya polisi
- Ofisi ya Mkoa ya Mshauri wa Mgambo

Hali ya mahusiano ya Idara na wadau wengine kama (Mahakama, Magereza, Waendesha Mashtaka, Polisi, Serikali za Mitaa na Wananchi) ni nzuri na inaridhisha

Huduma za urekebishaji zilizotolewa kwa wafungwa na Taasisi nyingine ni ushauri nasaha na kufanya kazi bila malipo kama sehemu ya adhabu.

**USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA WAFUNGWA KWENYE MAENEO YA KAZI/MAENEO WANAYOISHI.**

(a) Idadi ya wafungwa waliokiuka masharti na kupewa onyo – Wanne (04)

(b) Idadi ya wafungwa waliorudishwa gerezani kwa kukiuka masharti. Hakuna.

(c) Idadi ya wafungwa waliotoroka na kukumatwa - Hakuna.

(d) Idadi ya wafungwa waliofariki – Moja (01).

(e) Idadi ya wafungwa waliohama kwenda Wilaya nyingine - Hakuna

**MAFANIKIO.**

**Idadi ya taarifa za kijamii zilizoandaliwa ni 147**

Zilizofanikiwa ni **137**

Zisizofanikiwa na Zinazosubiri maamuzi ni **10**

**Idadi ya wafungwa walioingia = 137**

Wajaribiwa/probationers - Hakuna

Wafungwa wa Huduma kwa Jamii waliotokea

| | | |
|---|---|---|
| Mahakamani | ME =106 | KE = 23 |
| Magereza- | ME =06 | KE = 02 |

**Idadi ya wafungwa waliorudishwa kwenye Jamii baada ya Kumaliza adhabu zao:**

ME = 78

KE = 29

**JUMLA = 107**

**Idadi ya wafungwa wote wanaoendelea ni:**

ME = 32

KE = 07

**JUMLA = 39**

**Matokeo chanya yaliyopatikana kwa wafungwa baada ya kumaliza adhabu.**

- Wafungwa wamebadilika kitabia na kimatendo na hasa kutambua haki zao za kifungo cha nje.
- Familia zimeimarika, watoto wamepata fursa ya kutunzwa na wazazi wote wawili na kupata huduma zote muhimu toka kwa wazazi wawili.
- Taasisi za serikali zimefanikiwa kupata wahudumu hivyo kupunguza gharama za uendeshaji katika taasisi hizo.
- Ujuzi wa wafungwa kunufaisha Taasisi za Kiserikali kutoka kwa wafungwa wenye ujuzi.

**Taasisi zinazotoa kazi kwa wafungwa ni taasisi za serikali tu.**

Kiasi cha fedha kilichookolewa na wafungwa kwa kufanya kazi kwenye Taasisi za Serikali ni kikubwa kwani ofisi nyingi za serikali hazina wahudumu wa ofisi ambao wanaweza kutengeneza mazingira ya ofisi kuwa mazuri na masafi, kiasi hicho ni **Tsh 92,415,000/=** kwa wafungwa **137** kama malipo ya siku kwa vibarua wa kawaida ambapo kibarua mmoja hulipwa shilingi elfu **5000/=** kwa siku. Pia kiasi cha fedha

kilichookolewa kwa kuwalisha wafungwa wakiwa gerezani kwani chakula cha siku mtu mmoja ni shilingi elfu **2,500/=,** serikali imeokoa Tsh **46,207,500/=** kama gharama ya kuwalisha wafungwa kama wangekua gerezani**.**

Upatanisho miongoni mwa wafungwa, Majirani, Ndugu, waathirika wa kosa na jamii kwa ujumla, hivyo basi mpaka sasa hakuna malalamiko yoyote kuhusu wafungwa ambao wameingia kwenye program, kwa hiyo inaonyesha kuwa wafungwa hao wamebadilika kitabia na jamii imewakubali kama raia wema.

Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa Mahakama wa wilaya ya Mbinga, Songea Manispaa, Songea Vijijini na Madaba.

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI - JULAI MOSI, 2023 – DISEMBA 31, 2023**

Kwa kipindi cha Mwezi Julai Mosi, 2023 hadi Disemba 31, 2023 tumefanikiwa kuingiza katika Programu wafungwa **hamsini na nane (58),** wanaume **arobaini na nane (48),** kati yao **watano (05)** wametokea gerezani na **arobaini na tatu (43)** kutoka mahakamani na Wanawake **kumi (10),** wote kutoka mahakamani.

Aidha kwa kipindi hicho katika Wafungwa **hamsini na mbili (52)** wamemaliza kutumikia adhabu zao; Wanaume **arobaini na moja (41)** na wanawake **kumi na moja (11)**

**UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA**

Idadi ya Wilaya zinazotekeleza kazi za Idara katika Mkoa wa Ruvuma ni Wilaya ya Songea (Halmashauri ya Songea Manispaa, Halmashauri ya wilaya Songea, Mbinga na Nyasa)

**Mchanganuo wa Mahakama katika Wilaya:**

- Mahakama Kuu - 01
- Idadi ya Mahakama ya Hakimu Mkazi- 01
- Idadi ya Mahakama za Wilaya- 05
- Idadi ya Mahakama za Mwanzo- 10

**Idadi ya Watumishi katika Mkoa;**

- Waajiriwa wa Idara ya Huduma za Uangalizi = 2
- Walio kwenye Mafunzo ya utarajali (INTERN) =2
- CDOs/social welfare officers – Hakuna

Taasisi zilizotambuliwa kwenye Mkoa kwa ajili ya kutoa huduma za urekebishaji ni Taasisi za Serikali tu ambazo ni:

- Ofisi ya Ustawi wa Jamii
- Ofisi za Kata na serikali za Mitaa
- Mahakama
- Hospitali za Wilaya na Mkoa
- Vituo vya Afya
- Taasisi za Elimu (Shule za Sekondari na Msingi)
- Zahanati
- Vituo vya Polisi
- Ofisi ya Mkoa ya Mshauri wa Mgambo

Taasisi hizi zinatoa Huduma za urekebishaji kwa wafungwa kama kutoa ushauri nasaha, sehemu za kufanyia kazi na kufanya kazi bila malipo kama sehemu ya adhabu.

**USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA WAFUNGWA KWENYE MAENEO YA KAZI/MAENEO WANAYOISHI**

a) Idadi ya wafungwa waliokiuka masharti na kupewa onyo –Hakuna
b) Idadi ya wafungwa waliorudishwa gerezani kwa kukiuka masharti-Hakuna
c) Idadi ya wafungwa waliotoroka na kukumatwa – Hakuna
d) Idadi ya wafungwa waliofariki – Hakuna
e) Idadi ya wafungwa waliohama kwenda Wilaya nyingine – Hakuna

**MAFANIKIO**

**Idadi ya taarifa za kijamii zilizoandaliwa ni 66**

Zilizofanikiwa ni **58**

Zisizofanikiwa ni **08**

**Idadi ya wafungwa walioingia = 58**

**Wafungwa wa Huduma kwa Jamii waliotoka**

| | | |
|---|---|---|
| **Mahakamani** | ME = 43 | KE = 10 |
| **Magereza** | ME = 05 | KE = 00 |

**JUMLA =58**

**Idadi ya wafungwa waliorudishwa kwenye jamii baada ya kumaliza adhabu zao ni:**

ME = 41

KE = 11

**JUMLA = 52**

**Idadi ya wafungwa wote wanaoendelea ni:**

ME = 40

KE = 06

**JUMLA = 46**

**Taasisi zinazotoa kazi kwa wafungwa ni taasisi za Serikali tu**

Kwa kupitia utekelezaji wa programu ya Huduma kwa Jamii kwa kipindi cha mwezi Julai mosi,2023 hadi Disemba 31, 2023 serikali imeokoa kiasi cha **Tsh. 33,735,000/=** kwa wafungwa **58** kufanya kazi kwenye taasisi za serikali ambapo kibarua mmoja hulipwa shilingi elfu **5,000/=** kwa siku. Pia serikali imeokoa kiasi cha **Tsh. 16,867,500/=** za kuwahudumia wafungwa wakiwa gerezani ambapo mfungwa mmoja hukishwa kwa shilingi elfu **2,500/=** kwa siku.

Pia utangamanisho kwa wafungwa umefanyika miongoni mwa wafungwa, majirani, Ndugu, wathirika wa kosa na jamii kwa Ujumla, pia kupitia Idara ya Huduma za Uangalizi imewasaidia baadhi ya wafungwa kuwaunganisha na huduma ambazo walikuwa wakiziitaji mfano, wanasheria, hospitali, baraza la ardhi kwa wenye migogoro ya ardhi n.k

**UHAMASISHAJI WA KUITANGAZA IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI MKOA WA RUVUMA.**

Kwa kipindi hicho, Maafisa Probesheni walishiriki wiki ya SHERIA nchini, pia walihudhuria Vikao vya Kusukuma Mashauri (CASE FLOW MANAGEMENT COMMITTEE) ambavyo ni kikao cha Kusukuma mashauri Mahakama Kuu Kanda ya Songea, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Ruvuma na kikao cha Kusukuma mashauri Mahakama ya Wilaya ya Songea kwa nyakati tofauti kujadili masuala mbalimbali yahusuyo kumaliza mashauri kwa wakati. Pia kuhudhuria Vikao vya Haki Jinai ngazi ya Mkoa na Wilaya. Tulihudhuria kikao cha kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Baada ya kupewa mwaliko. Katika Vikao hivyo tulipata nafasi ya kuwaeleza

wajumbe wa Vikao hivyo kuhusu Idara ya Huduma za Uangalizi na kazi zinazosimamiwa na Idara yetu. Kutoa elimu kuhusu idara na kazi tunazofanya kupitia vipindi mbalimbali vya redio mfano Redio Selous FM na Redio Jogoo FM. Miongoni mwa kazi hizo ni;

i. Kuratibu na kusimamia kifungo mbadala wa gereza ambapo kwa sasa tunasimamia sheria mbili nazo ni SHERIA YA HUDUMA KWA JAMII Na. 6/2002(The Community Service Act, No. 6/2002) na sheria ya Majaribio na ujenzi wa Tabia, sura ya 247, Marejeo ya mwaka 2002. (The Probation of Offenders Act, CAP.247 RE:2002)
ii. Kutoa ushauri nasaha kwa wafungwa na kuwaunganisha wafungwa na taasisi zinazotoa huduma hasa kwa wale wenye mahitaji maalumu, kukagua sehemu wanazofanyia kazi, kuwaunganisha wafungwa na familia zao pindi wanapomaliza vifungo vyao.

Kupitia uhamasishaji huo wajumbe waliuliza maswali mbalimbali yakiwemo tofauti ya kifungo cha Huduma kwa Jamii, EML (Extra Mural Labour) na parole pia wajumbe walihitaji kufahamu sifa za mfungwa anayewenza kunufaika na kifungo cha Huduma kwa Jamii. Ambapo maswali hayo yalijibiwa na maafisa Probesheni.

Baada ya wajumbe kupata uelewa na kazi zinazofanywa na idara, tulikubaliana kuendelea kutoa elimu kwa jamii kila tunapopata nafasi na pia kuendeleza ushirikiano na taasisi nyingine ili kujenga uelewa wa pamoja.

Maafisa Probesheni walitembelea ofisi mbalimbali zikiwemo Magereza, Ofisi ya Afisa Magereza Mkoa, Ofisi za Manispaa, serikali za Mitaa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya kwa lengo la kujitambulisha pamoja na kutoa elimu kuhusu kifungo mbadala ya gerezani.

## MATARAJIO

Tunategemea kuendelea kuitangaza Idara yetu katika vyombo vya habari hasa redio zilizopo Mkoani Ruvuma. Pia tutatembelea Mahakama za wilaya ambazo bado hatujazitembelea kwa lengo la kujitambulisha na kuitambulisha idara kwa lengo la kuongeza uelewa kwa jamii inayotuzunguka. Pia kuongeza ufanisi wa kazi katika wilaya ya Tunduru, Namtumbo na Nyasa.

## CHANGAMOTO

- Hali ya Kijiografia ya Mkoa inasababisha kutowafikia wananchi kwa wakati katika kutoa Huduma ya Kifungo mbadala ya Gereza, hivyo kusababisha jamii kutokua na uelewa wa kutosha wa namna ya utekelezaji wa vifungo mbadala kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6/2002 na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura ya 247, Marejeo ya Mwaka 2002.
- Ushiriki mdogo wa Magereza katika kutekeleza programu za adhabu mbadala licha ya kutoa elimu mara kadhaa kwa wakuu wa Magereza.
- Uchache wa Watumishi ambapo kwa sasa kuna Watumishi wawili wanaofanya kazi Mkoa mzima hivyo kupunguza ufanisi hasa kwenye ukaguzi, ufuatiliaji na usimamizi wa wafungwa wanaopatikana ambapo ukaguzi unafanyika mara chache.
- Mahakimu wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha wa namna ya utekelezaji Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6/2002 na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia SURA YA 247, Marejeo ya mwaka 2002
- Pamoja na kutoa elimu kwa mahakimu katika Wilaya ya Mbinga bado wapo ambao hawatoi adhabu mbadala kwa washtakiwa.
- Kushindwa kuwafikia mahakimu walio nje ya Manispaa ya Songea kwa wakati kutokana na kutokuwa na bajeti ya kutosha katika idara

**MAPENDEKEZO**

Tunaomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutusaidia kuunganishwa na wadau wengine hasa Magereza ili kuweza kutekeleza program hii ya vifungo vya nje na kuwafikia watu wengi zaidi katika Mkoa wa Ruvuma.

**WAFUNGWA WALIOINGIA KWENYE PROGRAMU JULAI MOSI,2022 HADI JUNI 30, 2023**

| | **KUTOKA GEREZANI** | **KUTOKA MAHAKAMANI** | **JUMLA YA WAFUNGWA** | **KIASI CHA PESA KILICHOOKOLEWA KWA VIBARUA** | **KIASI CHA PESA KILICHOOKOLEWA KWA KULISHA WAFUNGWA GEREZANI** |
|---|---|---|---|---|---|
| WANAUME | 06 | 106 | 112 | | |
| WANAWAKE | 02 | 23 | 25 | | |
| **JUMLA KUU** | **08** | **129** | **137** | **92,415,000/=** | **46,207,500/=** |

**HITIMISHO**

Kwa namna ya pekee tunatoa shukrani za dhati kwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuendelea kutupa ushirikiano, wadau mbalimbali, taasisi mbalimbali na Watumishi pamoja na watu binafsi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia tangu kuanzishwa rasmi kwa Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Rruvuma, tunawashukuru sana.

## 8.12 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA BANDARI - BANDARI ZA ZIWA NYASA

**Taarifa ya Utendaji Kazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, Pamoja na Taarifa ya Miezi Sita (Julai hadi Disemba 2023) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24**

### i. Utangulizi

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inasimamia Bandari **15** katika Bandari za Ziwa Nyasa na Bandari ya Itungi ni makao makuu ya bandari zote za Ziwa Nyasa upande wa Tanzania. Bandari hizo 15 zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Mkoani Mbeya katika Wilaya ya Kyela kuna Bandari tatu (3) za Itungi, Kiwira na Matema, Mkoani Njombe katika Wilaya ya Ludewa kuna Bandari sita (6) za Lumbila, Ifungu, Nsisi, Makonde, Lupingu na Manda, na Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa kuna Bandari sita (6) za Ndumbi, Lundu, Nkili, Njambe, Liuli na Mbamba Bay.

### ii. Miradi Iliyotekelezwa Katika Bandari za Ziwa Nyasa

### a) Ujenzi wa Bandari Mpya ya Ndumbi

Maboresho makubwa yaliyofanyika katika Bandari za Ziwa Nyasa, katika awamu ya sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Rais na Jemadari Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan, ni ujenzi wa Bandari mpya ya Ndumbi kwa gharama ya TZS 12.2 bilioni. Mamlaka ya Usimamizi ya Bandari Tanzania (TPA) imetekeleza mradi huu wa ujenzi wa Bandari kubwa ya kisasa ya Ndumbi, kwa kujenga miundombinu kama ifuatavyo;

i) Gati (eneo la kuegesha meli) lenye urefu wa mita 160 kwenda Ziwani Jeti (jetty head) ya upana wa mita 20.4,

ii) Ramp (sehemu ya kupokea lango la meli) ya urefu wa mita 40 kwenda Ziwani na upana (Ramp head) wa mita 10,

iii) Ghala la kuhifadhi mizigo inayoathiriwa na mvua lenye mita za ukubwa 1,020,

iv) Eneo la sakafu ngumu (heavy duty paved yard) kwa ajili kuhifadhi mizigo isiyoathiriwa na mvua lenye mita za ukubwa 9,030,

v) Jengo la kupumzikia abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria 70,000 kwa mwaka, na;

vi) Ofisi na nyumba za watumishi.

Ujenzi wa Bandari mpya ya Ndumbi baada ya kukamilika mwezi Disemba 2022, imeongeza uwezo wa kuhudumia shehena kwa Bandari za Ziwa Nyasa kutoka tani 76,000 kwa mwaka (kabla ya kukamilika bandari ya Ndumbi) hadi kufikia tani 110,000 za sasa, wakati uwezo wa kuhudumia abiria umeongezeka kutoka abiria 56,000 kwa mwaka hadi abiria 126,000 baada ya kukamilika bandari mpya ya Ndumbi.

**Mipango Endelevu Ya Uboreshaji Wa Bandari Za Ziwa Nyasa**

Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imekamilisha ripoti ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha Bandari za Ziwa Nyasa, zikiwemo Bandari za Ndumbi, Liuli na Mbamba Bay ambazo zipo katika wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma. Taarifa ya mwisho ya upembuzi yakinifu wa namna ya kuboresha Bandari za Ziwa Nyasa imewasilishwa mwezi February 2023.

Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imepanga kutekeleza mapendokezo ya ripoti hiyo kama ifutavyo:

**a) Ujenzi wa Bandari Mpya ya Mbamba Bay**

Mojawapo ya mapendekezo ya ripoti ya upembuzi yakinifu ni kujenga Bandari kubwa ya Mbamba Bay. TPA imepanga kuanza ujenzi wa Bandari mpya ya kisasa ya Mbamba Bay kwa lengo la kuimarisha Ushoroba wa Maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor), ambayo ni njia fupi na rahisi ya kuhudumia mzigo wa Malawi kutokea Bandari ya Mtwara, ikunganishwakwa barabara hadi Bandari ya Mbamba Bay na kuunganisha hadi Bandari za Malawi kupitia majini. Ili kutekeleza mradi huu mkubwa, Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Jemedari na Rais wetu Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan ametoa TZS 70 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa Bandari kubwa na kisasa ya Mbamba Bay. Mkataba wa ujenzi huo umesainiwa tarehe 6 Disemba 2023, Mkandarasi atakabidhiwa eneo la mradi tarehe 26 Januari 2024 tayari kuanza kazi, ambapo mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24. Ujenzi wa Bandari kubwa na ya kisasa ya Mbamba Bay itakapokamilika, itaongeza uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo kwa Bandari hiyo kutoka tani 110,000 za sasa hadi 550,000 kwa mwaka.

Aidha, baada ya Bandari mpya ya Mbamba Bay kukamilika, makao makuu ya Bandari za Ziwa Nyasa yatahamia Bandari ya mbamba Bay kutoka bandari ya Kiwira iliyopo Kyela.

**b) Ujenzi wa Gati Ndogondogo Kwenye Bandari za Ziwaa Nyasa**

Ripoti ya upembuzi yakinifu ilipendekeza pia kujenga gati ndogondogo kwenye baadhi ya Bandanri, ikiwemo Bandari ya Liuli katika Wilaya ya Nyasa. Ili kutekeleza miradi hiyo, Serikali imetoa fedha **TZS 1.5 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, ambayo imepangwa kutekelezwa ndani yam waka wa fedha 2023/24.

**iii. Matokeo Chanya ya Maboresho ya Bandari za Ziwa Nyasa ni Ongezeko la Mizigo na Abiria**

Kutokana maboresho makubwa yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya Sita katika Bandari za Ziwa Nyasa, yamewezesha Bandari kuboreshwa na kupata vifaa na kuhudumia shehena, na hivyo kuweza kuhudumia shehena ya mzigo **tani 14,431**, ambao ni sawa na ongezeko la **tani 9,021** au **167%**, ikilinganishwa na mzigo wa **tani 5,410** uliohudumiwa mwaka 2021/22.

Kwa upande wa abiria waliohudumiwa mwaka 2022/23 ni **70,172**, ambao ni ongezeko la abiria **67,673**, sawa na **2,708%** ikilinganishwa na **abiria 2,499** waliohudumiwa mwaka 2021/22.

Aidha, katika **kipindi cha miezi sita ya mwaka mwaka wa fedha 202324**, Bandari za Ziwa Nyasa zimehudumia jumla ya tani **1,828.6** na abiria walihudumiwa katika kipindi hicho **7,358**.

**iv. Uendeshji Wa Meli**

Katika kuboresha huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kupitia Ziwa Nyasa na kukuza uchumi wa mikoa inayozunguka Ziwa hilo, Mamlaka inasimamia na kuendesha Meli mbili za mizigo na Meli moja ya abiria na mizigo.

- **Uendeshaji Wa Meli Za Mizigo (Mv Njombe Na Ruvuma)**

Mamlaka inasimamia na kuendesha meli mbili za mizigo (MV Ruvuma MV Njombe) zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja ambazo zinauwezo wa kutoa huduma katika Ziwa Nyasa kwa kubeba mizigo mikubwa na mizito kama makaa ya mawe na mali ghafi ya kutengenezea saruji (gypsum).

Aidha, kwa sasa mzigo mkubwa unaohudumiwa ni wa "gypsum" unaosafirishwa kutokea Bandari ya Mbamba Bay hadi bandari ya Kiwira na Kuelekea nchini Malawi kupitia njia ya barabara.

- **Uendeshaji Wa Meli Ya Abiria Na Mizigo (Mv Mbeya II)**

Meli ya MV Mbeya II inauwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo. Meli hii kwa sasa ni nzima na inaendelea kutoa huduma ya usafirishaji ndani ya Ziwa Nyasa, ikifanya safari kati ya Bandari ya Mbamba Bay na Kiwira huku ikipitia katika bandari hizo zote 15).

**v. Mwelekeo Wa Masoko**

Kufuatia uwekezaji uliofanywa kwa lengo la kuboresha Bandari za Ziwa Nyasa, Bandari zetu zimendelea kuvutia wateja na ndiyo maana shehena iliyohudumia kwa mwaka wa fedha. 2022/2023 umeongezeka mara dufu ikilinganishwa na Shehena iliyo hudumia katika mwaka 2021/2022. Pamoja na uwekezaji huo ambao umekuwa kivutio kwa wateja, Mamlaka ya usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inaendelea kutafuta Masoko kwa kuongea na wateja wanatumia Bandari zetu pamoja kufungua ofisi za TPA Jijini Lilongwe Nchini Malawi kwa lengo pia la kuvutia wateja kutafuta wateja wapya kutoka Malawi.

vi. **Changamoto Zilizopo na Mapendekezo ya Kuziondoa**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kuna changamoto chache ambazo zikiondolewa, kazi ya kuhudumia mizigo na abiria kati ya nchi zetu mbili (Tanzania na Malawi) itakuwa na ufanisi mkubwa zaidi.

Changamoto zilizopo ni kama ifutavyo:

| Na | Changamoto | Suluhisho linalopendekezwa ili kuoondoa changamoto husika |
|---|---|---|
| 1 | Bandari za Malawi hasa bandari ya Nkata Bay kutoridhia meli zetu za Mizigo ziende katika bandari hiyo. Wateja kadhaa tuliopata wanataka kusafirisha mizigo (Gypsum na Makaa ya mawe) kwenda b andari ya Nkata Bay | i) TPA inaendelea kuwasiliana na mwendeshaji wa Bandari za Malawi ili kupata ufumbuzi wa suala hilo.<br>ii) Serikali ya Tanzania inaendelea kushauriana na Serikali ya Malawi ili kuongeza eneo la kuhudumia shehena Bandarini. |
| 2 | Ubovu wa barabara inayounganisha Bandari ya Ndumbi na Ruanda kupitia Lituhi | Serikali ya Awamu ya sita chini ya uongozi mahiri ya Mheshimiwa Dr. Suluhu Hassan imetoa fedha na tayari Mkandarasi wa kujenga Barbara hiyo kwa kiwango cha lami amepatika, hivyo kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza. |

| Na | Changamoto | Suluhisho linalopendekezwa ili kuoondoa changamoto husika |
|---|---|---|
| 3 | Upungufu wa shehena kupitia Bandari za Ziwa Nyasa | Mikakati ya kutafuta wateja ili kuongeza shehena zinaendelea.<br>Mojawapo ya mikakati hiyo ni;<br>i) TPA imefungua ofisi Jijini Lilongwe kwa lengo la kusogeza huduma zake karibu na wateja<br>ii) Mazungumzo na wateja waliopo yanaendelea ili kuongeza mizigo kupitia Bandari zetu<br>iii) Jitahada za kutafuta wateja wapya ni pamoja na kutoaelimu juu ya maboresho yaliyofanywa na serikali kwenye bandari zetu ili kuwavutia, pamoja na kuwaeleza juu ya faida za kutumia usafiri wa maji ambao ni nafuu ikilinganishwa na barabara.shehena |

**HITIMISHO**

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), tunapenda kutoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi thabiti wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Mheshimiwa Dr Samia Suluhu Hassan kwa fedha ambazo ameendelea kutoa kwa ajili ya miradi mbalimbali, kwa lengo la kutekeleza kwa vitendo nia yake ya dhati ya kuifungua nchi kupitia uboreshaji wa Bandari za Tanzania, zikiwemo Bandari za Ziwa Nyasa, ili ziweze kutoa huduma bora ya viwango na ya kiushindani, hususan maboresho makubwa ya Bandari za Ndumbi na ujenzi wa Bandari kubwa na yab kisasa ya Mbamba Bay, unaotarajiwa kuanza rasmi tarehe 26 Januari 2024.

**8.13 TAARIFA YA EWURA OFISI YA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI KIKAO CHA RCC RUVUMA.**

**1.0 UTANGULIZI**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeundwa kwa Sheria ya Bunge Sura namba 414 ikiwa na majukumu ya kudhibiti sekta kuu mbili, ambazo ni **Sekta ya Nishati** na **Sekta Maji**. Kwenye sekta ya Nishati kuna sekta ndogo ya **Gesi Asilia, Sekta ndogo ya Umeme** na **Sekta ndogo ya Mafuta jamii ya Petroli**. Katika **Sekta ya Maji**, Mamlaka ya EWURA ipo katika kudhibiti Mamlaka za maji Safi na Usafi wa Mazingira.

Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inapatikana Jijini Mbeya, Mtaa wa Karume kwenye jengo la NHIF, Ghorofa ya sita. Ofisi hiyo inahudumuia Mikoa mitano (5) ya Mbeya, Songwe, Rukwai, Njombe na Ruvuma.

Majukumu ya Mamlaka yameainishwa katika Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania kuwa ni:

- Kutoa leseni kwa watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa
- Kupanga au kuidhinisha bei na tozo katika sekta zinazodhibitiwa
- Kuweka viwango vya bidhaa na huduma kwa kushirikiana na TBS
- Kusimamia utoaji huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo husika
- Kuzingatia usalama na uhifadhi wa mazingira wakati wa kutoa huduma
- Kuelimisha wananchi kuhusu masuala yanayodhibitiwa na Mamlaka.
- Kutatua migogoro kati ya mtoa huduma na mpokea huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka.

**2.0 SEKTA YA UMEME**

Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inasimamia shughuli ya Kiufundi na Kiuchumi katika Sekta ya Umeme katika Mikoa yote mitano ya kanda hii.

Katika Mkoa wa Ruvuma, mtoa huduma mkubwa wa nishati hiyo ni TANESCO kwa sehemu kubwa. TANESCO ifanyiwa ukaguzi wa huduma na miundombinu Januari na Disemba 2023. Maelekezo yalitolewa kupita taarifa ya ukaguzi iliyowasilisha makao makuu ya TANESO kwa ajili ya utekelezaji ikiwemo kufanya marekebisho katika miundombinu ya usambazaji waliyobainishwa katika taarifa hiyo. Pia, wawekezaji wawili Tulila na Andoya “hydropower plants” walikaguliwa Mei 2023 na Disemba 2023

mtawalia. Maelekezo yalitolewa kwa ajili ya uboreshaji shughuli zao katika kuhudumia wananchi.

Hata hivyo, katika kutekeleza wajibu wake, EWURA inatoa leseni kwa mafundi umeme wa kazi mbalimbali. Kwa Mkoa wa Ruvuma, katika kipindi cha 2022/23 na Julai hadi Disemba 2023, jumla ya leseni mpya zilizotolewa ni 59 (daraja A-1, dalaja B – 2, daraja C – 34, daraja D – 21, daraja W – 1) na kufanya idadi ya mafundi umeme kufikia **120 wenye leseni hadi kufikia Januari 10, 2024.** Kufikia Januari 10, 2024, jumla ya maombi ya leseni 18 yapo katika hatua mbalimbali.

**CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA UMEME**

Uwepo wa kundi kubwa la mafundi umeme (vishoka) ambao hawana vyeti vya kitaaluma vitakavyowawezesha kuomba leseni zinazotolewa na Mamlaka. Ufinyu wa bajeti ya matengenezo kwa upande wa TANESCO hivyo kupelekea uchakavu mkubwa kutoshughulikiwa kwa wakati.

## 3.0 SEKTA YA MAFUTA YA PETROLI

EWURA pia inasimamia sekta ya mazao ya mafuta ya petrol (diseli, petrol, mafuta ya taa pamoja na gesi za LPG). Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ina jumla ya Vituo vya Wauzaji mafuta wa rejareja (***Retail outlets***) 351 hadi kufikia Disemba 2023. Idadi hiyo inajumuisha Watumiaji binafsi wa mafuta (***Consumer Installation***), Viwanda vidogo vya kujazia gesi ya kupikia majumbani (***LPG refilling***) na Wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani (***LPG distributors)*** na

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 mpaka Disemba 2023, EWURA ilifanya **ukaguzi wa kawaida** (**Compliance monitoring**) kwenye mkoa wa Ruvuma na kukagua vituo 23. Kati ya hivyo vituo 18 vya mkoa wa Ruvuma havikuweza kukutwa na makosa yoyote, Kama inavyoonesha katika **jedwali namba 1** .

**Jedwali namba 1: Ukaguzi wa kawaida kwenye Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | TAREHE | JINA LA KITUO | ENEO | WILAYA | MKOA | VIGEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 21-Sep-22 | MOM CARGO COMPANY LIMITED | Msamala | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 2 | 31-Jul-22 | Ruvuma Coal Limited | Paradiso Village, Ruanda Ward, Mbinga District in Ruvuma Region | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 3 | 21-Oct-22 | MOM Cargo Company Limited | Plot No. 1, Block 'GG', Msamala Area in Songea Municipality | Songea | Ruvuma | Ukaguzi wa awali alikutwa na makossa na kupewa maelekezo ya kurekebisha. Ukaguzi wa pili ulionyesha kuwa amekidhi vigezo. |
| 4 | 21-Oct-22 | TSN Oil (T) Ltd-Lizabon | Lizabon | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 5 | 21-Oct-22 | Oryx Oil Company Limited –Peramiho Service Station | Plot No.1, Likuyufusi Village - Peramiho, Songea District in Ruvuma Region | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 6 | 21-Oct-22 | Mbamba Bay Road Filling Station | Plot No.3, Mbinga Industrial area, Mbamba bay Road | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 7 | 21-Oct-22 | Fairtech Investments Petrol Station, Mbamba Bay Road | Plot No.20, Block “Mbamba Bay”, Mbinga Municipality, Ruvuma Region | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi wa awali alikutwa na makossa na kupewa maelekezo ya kurekebisha. Ukaguzi wa pili ulionyesha kuwa amekidhi vigezo. |
| 8 | 21-Oct-22 | Lotar Marselin Nkondola - Lotar fuel service station | Kingosera Village | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 9 | 22-Oct-22 | Mpetembe Oil ( Idd Hamis Kapinga) | Plot No.3, Block'A', Mletele Area in Songea Municipality | Songea | Ruvuma | Ukaguzi wa awali alikutwa na makossa na kupewa maelekezo ya kurekebisha. Ukaguzi wa pili ulionyesha kuwa amekidhi vigezo. |
| 10 | 22-Oct-22 | Cross Road Filling Station | Plot No. 122, Block 'A', Tunduru Urban area | Tunduru | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |

| Na. | TAREHE | JINA LA KITUO | ENEO | WILAYA | MKOA | VIGEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | 22-Oct-22 | Abdillah Kassimu Mandepe – Namtumbo Petrol Station | Muungano Area, Namtumbo District in Ruvuma Region | Namtumbo | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 12 | 24-Oct-22 | A.I.A Transporters Company Limited Petrol Station | Plot No. 7, Block ‘A’, Mitawa Area, Songea District in Ruvuma Region | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 13 | 24-Oct-22 | Refuelling Solutions (T) Limited Petrol Station | Plot No. 169, Block ‘L’, Mahenge Area in Songea Municipality | Songea | Ruvuma | Ukaguzi wa awali alikutwa na makossa na kupewa maelekezo ya kurekebisha. Ukaguzi wa pili ulionyesha kuwa amekidhi vigezo. |
| 14 | 24-Oct-22 | Oryx Oil Company Limited Service Station | Plot no 51 Block F central area Songea(Sido Industrial Area) | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 15 | 26-Nov-22 | Paskal Urban Wela Filling Station | Peramiho 'A' Area | Songea | Ruvuma | Ukaguzi wa awali alikutwa na makossa na kupewa maelekezo ya kurekebisha. Ukaguzi wa pili ulionyesha kuwa amekidhi vigezo. |
| 16 | 20-Dec-22 | Mbamba Bay Road Filling Station of P.O Box 222 Mbinga | Plot No.3, Mbinga Industrial area, Mbamba bay Road | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 17 | 21-Dec-23 | ACER PETROLEUM (T) LTD- NAMTUMBO (Abdillah Kassimu Mandepe – Namtumbo Petrol Station) | Muungano Area, Namtumbo District in Ruvuma Region | Namtumbo | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 18 | 22-Dec-23 | Fountain Petroleum Limited –Songea | Plot No.58, Block ‘A’, Peramiho Urban Area | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |

| Na. | TAREHE | JINA LA KITUO | ENEO | WILAYA | MKOA | VIGEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Peramiho 'B' Petrol Station | | | | |
| 19 | 22-Dec-23 | Lake Oil Limited-Mbinga Petrol Station | Mbinga Township | Mbinga | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 20 | 21-Dec-23 | Njombe Filling Station Co. Ltd., Madaba | Madaba Area | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 21 | 22-Dec-23 | Oryx Oil Company Limited –Peramiho Service Station of P. O. Box 35537 Dar Es Salaam | Plot No.1, Likuyufusi Village - Peramiho, Songea District in Ruvuma Region | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 22 | 23-Dec-23 | Oryx Oil Company Limited Service Station | Plot no 51 Block F central area Songea(Sido Industrial Area) | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |
| 23 | 22-Dec-23 | TSN Oil (T) Ltd-Lizabon Branch of P.O Box 76085 Dar es Salaam | Lizabon | Songea | Ruvuma | Ukaguzi ulionyesha kwamba amekidhi vigezo vya matakwa ya leseni |

Mbali na matokeo ya ukaguzi huo, pia kuna kampuni nne (4) zilipewa adhabu ya kulipa faini kati ya **TZS 1,000,000/=** mpaka **TZS 10,000,000** kwa kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta bila kupata kibali kutoka EWURA.

| Na. | Jina La Kampuni | Mahali Ilipo | Wilaya | Mkoa | Kosa | Sheria iliyovunjwa | Adhabu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Nurubicco Charles Mponda -Delldelta Refueling | Mpepai | Mbinga | Ruvuma | Kujenga miundomibu binafsi ya matumizi ya mafuta bila kupata kibali EWURA | Kanuni ya uhifadhi wa Mafuta kwa matumizi ya jumla na rejareja. GN 817/2020. Sheria ya mafuta sura 392. | Faini ya TZS 1,000,000 |
| 2 | Lake Oil Limited - Tunduru Petrol Station | Tunduru Mjini | Tunduru | Ruvuma | Kujenga miundomibu binafsi ya matumizi ya mafuta bila kupata kibali EWURA | Kanuni ya uhifadhi wa Mafuta kwa matumizi ya jumla na rejareja. GN 817/2020. Sheria ya mafuta sura 392. | Faini ya TZS 10,000,000 |
| 3 | Abas Amir Kapinga - Mpetembe Oil Petrol Station | Mletele – Songea Mjini | Songea | Ruvuma | Kujenga miundomibu binafsi ya matumizi ya mafuta bila kupata kibali EWURA | Kanuni ya uhifadhi wa Mafuta kwa matumizi ya jumla na rejareja. GN 817/2020. Sheria ya mafuta sura 392. | Faini ya TZS 10,000,000 |
| 4. | KSM Filling Station | Namtumbo Mjini | Namtumb o | Ruvuma | Kujenga miundomibu binafsi ya matumizi ya mafuta bila kupata kibali EWURA | Kanuni ya uhifadhi wa Mafuta kwa matumizi ya jumla na rejareja. GN 817/2020. Sheria ya mafuta sura 392. | Faini ya TZS 1,000,000 |

Katika kanda pia kulifanyika ukaguzi kwa mwezi Julai 2022 Mpaka Disemba 2023 kwenye vituo 55 kwa kuangalia vituo vinavyouza bidhaa ya mafuta kulingana na **bei elekezi** (cap price monitoring) na vituo vyote vya Mkoa wa Ruvuma vilivyokaguliwa viliuza bidhaa zao kufikia / chini ya bei elekezi.

Pia Ofisi ya kanda ilifanya ukaguzi wa kiufundi katika mioundombinu (pre-licence) Baadhi ya Vituo vya mafuta kujengwa bila kufuata utaratibu wa ujenzi na baadhi kutokidhi mahitaji ya leseni. Ushauri wetu ni kwamba Halmashauri / Manispaa husika ziangalie namna bora ya kushirikiana na EWURA na wadau wengine katika kuhakikisha ujenzi unakuwa na vibali husika (EWURA, NEMC na Manispaa/Halmashauri wanaotoa hati ya umiliki wa ardhi) kabla ya ujenzi kutekelezwa.

## 4.0 SEKTA YA MAJI

Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inasimamia Mamlaka za Maji 19. Kati ya Mamlaka hizo 19, Mamlaka 5 ni Mamlaka za Maji zilizoko kwenye Makao Makuu ya Mikoa, Mamlaka moja ni Mamlaka ya Mradi wa Kitaifa (Wanging'ombe) na Mamlaka 13 ni za Makao Makuu ya Wilaya na Miji midogo. Mkoa wa Ruvuma una Jumla ya Mamlaka nne (4). Kati ya Mamlaka hizo, Mamlaka moja ni Mamlaka iliyopo Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma (yenye makao yake makuu hapa Manispaa ya Songea) na Mamlaka nyingine tatu ni zilizopo katika miji ya Wilaya za Mbinga, Namtumbo,na Tunduru.

Katika sekta ya Maji kuna aina tano za ukaguzi unaofanya na EWURA

- Ukaguzi maalum (**special inspection**) - kufuatilia utendaji mbovu wa Mamlaka,
- Ukaguzi wa kawaida wa utendaji wa Mamlaka (**General compliance monitoring Inspection**) – ukaguzi huu unahusisha ukaguzi wa miuodombinu ya maji na majitaka, sharia kanuni na taratibu za utoaji huduma na ubora wa huduma kwa mteja,
- Ukaguzi kwa ajili ya taratibu za utoaji wa leseni (pre-licensing Inspection) – ukaguzi huu unafanyika ili kuzipa leseni Mamlaka mpya au kuhuisha leseni kwa Mamlaka zilizomaliza muda wa leseni.
- Ukaguzi wa kuhakiki taarifa za mamlaka (**data verification**) – unafanyika kama sehemu ya maandalizi ya kuandika Taarifa ya Utendaji wa Mamlama za Maji
- Ukaguzi wa ubora wa maji (**water quality monitoring**)

Pia EWURA inawajibu wa kufanya uchambuzi na kuidhinisha bei za Mamlaka za Maji

Katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Disemba 2023 ukaguzi ulifanyika kama ifuatavyo:

i. Ukaguzi wa kawaida wa utendaji wa Mamlaka (**General compliance monitoring Inspection**) – kwa Mamlaka za Maji tatu ambazo ni Mamlaka za maji za Mbinga, Namtumbo na Tunduru
ii. Ukaguzi kwa ajili ya kuhuisha leseni kwa mamlaka za maji tatu ambazo ni Mbinga, Namtumbo na Tunduru
iii. Ukaguzi wa ubora wa maji (**water quality monitoring**) kwa Mamlaka za maji za Songea, Mbinga na Tunduru.

Katika kipindi cha Mwaka wa fedha wa 2022/23 EWURA ilipokea na kuchakata Maombi ya marekebisho ya bei za huduma kutoka kwa Mamlaka ya Maji Songea. EWURA ilifanya Mkutano wa Wananchi wote wa Manispaa ya Songea tarehe 22 Agosti 2022 ili kukusanya maoni juu ya Maombi hayo. Bei mpya kwa mamlaka ya Maji Songea ziliidhinishwa na kuchapishwa na Gazeti la Serikali Namba 6 na 7 ya tarehe 13/01/2023.

**CHANGAMOTO SEKTA YA MAJI**

Uzalishaji wa Maji wa Mamlaka zote hizo Nne (4) ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya Maji kwa maeneo hayo, hususani wakati wa kiangazi. Pia, kuna tatizo la baadhi ya Mamlaka kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha ili kutoa huduma ipasavyo.

**5.0 USULUHISHI WA MIGOGORO**

EWURA pia inashughulikia malalamiko yanayohusiana na Sekta zote tunazozidhibiti. Miongoni mwa malalamiko hayo ni ankara za maji, kuuziwa mafuta yasio na ubora, malalamiko mbalimbali ya umeme, malalamiko ya bei za bidhaa na malalamiko ya huduma nk.

Katika kipindi tajwa kulikuwa na lalamiko moja lililohusisha TANESCO na SONGEA WSSA. Hata hivyo lalamiko hilo lilitatuliwa hatua ya usuluhishi (Mediation).

Hivyo, tunaomba ushirikiano kwa wadu wote katika kuelimisha umma kwamba EWURA ndio inashughulikia malalamiko kati ya Mteja na Mtoa Huduma kwa huduma zinazodhibitiwa na EWURA. Pale panapotokea malalamiko, basi wananchi waeleweshwe kwamba wayawasilishe EWURA kupitia fomu ya malalamiko inayopatikana katika ukurasa wa Mamlaka kupitia tovuti (www.ewura.go.tz) au kwa kufika Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyopo Jijini Mbeya, Mtaa wa Karume kwenye jengo la NHIF, Ghorofa ya sita.

**8.14 WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI - TANZANIA (TARURA)**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI 2022 HADI**

**JUNI 2023 NA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI HADI DESEMBA 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

Wakala wa Barabaraza Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma una mtandao wa barabara wa jumla ya kilometa 7146.21 kati ya hizo kilometa 2312.83 ni za Mjazio (Feeder Roads) ambazo ni sawa na asilimia 32.36%, 3873.85 ni za Mkusanyo (Collector Roads) ambazo ni sawa na asilimia 54.21%, na Kilometa 959.52 ni za Jamii/Kijiji (Community Roads) ambazo ni sawa na asilimia 13.43% ya mtandao mzima.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI 2022 HADI JUNI 2023

### Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha **2022/ 2023**, Mkoa wa Ruvuma katika bajeti ya miundombinu ya barabara ulidhinishiwa jumla ya **TZS 23,757,962,850.44** ambapo mfuko wa Barabara ni **TZS. 6,918,627,877.44** Mfuko wa Barabara (Maendeleo) **TZS. 1,390,000,000** Mfuko Mkuu wa Serikali (kila Jimbo) **TZS**. **4,500,000,000** na fedha tozo ya mafuta Shilingi 100 kwa lita **TZS. 10,025,000,000.**

### Mapokezi ya Fedha

Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023, Wakala wa barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma ulipokea jumla ya fedha kiasi cha **Tshs**. **23,757,962,850.44** ambayo ni asilimia **100** ya bajeti ya matengeneao ya barabara na fedha za Maendeleo.

### Hali ya utekelezaji wa miradi ya Barabara kupitia fedha za Maendeleo (Fedha za Jimbo na Tozo)

Hadi kufikia Juni, 2023 ya mwaka wa fedha 2022/2023, TARURA Mkoa wa Ruvuma kupitia fedha za maendeleo ulifanya kazi za matengenezo ya barabara na ujenzi wa madaraja kwa asilimia **100** za utekelezaji**.**

**Jedwali hapo chini linaonesha hali halisi ya utekelezaji ya miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 (Jedwali Na.1)**

| Na | Jina la Mradi | Fedha Idhinishwa | Fedha Zilizotolewa | Fedha Zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|

| Na | Jina la Mradi | Fedha Idhinishwa | Fedha Zilizotolewa | Fedha Zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami(DSD) Barabara ya Matomondo - Mlale JKT | 4,000,000,000.00 | 4,000,000,000.00 | 4,000,000,000 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 2 | Ujenzi wa Daraja la Mto Njoka (20m) katika barabara ya Muhukuru barabarani - Mipeta -Kizuka | 700,000,000.00 | 699,892,465.00 | 699,892,465.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 3 | Maboresho ya barabara ya Luhindo-Mpepo-Darpori katika kiwango cha Changarawe | 750,000,000.00 | 712,274,500.00 | 712,274,500.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 5 | Maboresho ya barabara za Mjini za Wilaya ya Tunduru katika kiwango cha lami(DSD) | 769,600,000.00 | 769,600,000.00 | 769,600,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 6 | Ujenzi wa Daraja la Mto Libango(30m) | 650,000,000.00 | 638,921,000.00 | | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 7 | Maboresho ya barabara za Ruhuwiko -Mwengemshindo 11.0km Katika kiwango cha Changarawe | 500,000,000.00 | 492,150,000.00 | 492,150,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 8 | Maboresho ya barabara za Kizuka -Mipeta -Matama - Muhukuru barabarani Kilometa 30 Kwa kiwango kizuri | 500,000,000.00 | 469,467,500.00 | 469,467,500.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 9 | Maboresho ya barabara za Nampungu - Mbatamila (12KM) na Nandembo 2 - Naluale Mkwajuni (8KM)Katika kiwango cha Changarawe | 500,000,000.00 | 493,740,000.00 | 493,740,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 10 | Maboresho ya barabara ya Longa-Kipololo-Litoho Kilometa1.0 kwa Kiwango cha Lami (DSD) wialaya ya | 500,000,000.00 | 455,506,720.00 | 455,506,720.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |

| Na | Jina la Mradi | Fedha Idhinishwa | Fedha Zilizotolewa | Fedha Zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mbinga | | | | |
| 11 | Maboresho ya barabara ya Marumba -Mbesa (12KM), Kangomba -Marumba - Njenga (16KM) na Tunduru - Masonya - Nambarapi(4KM) Katika kiwango cha Changarawe | 650,000,000.00 | 612,000,000.00 | 612,000,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 12 | Maboresho ya barabara yab Namasakata - Naikulu - Liwanga (12KM) Katika kiwango cha Changarawe | 300,000,000.00 | 285,680,000.00 | 285,680,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 13 | 1 Bridge Construction along Lundo-Ntengule-Mapera, Periodic Maintenance along Linda-VETA 7Km, Malini - Chiulu 5.25Km and Diwani-Linda 7Km, Periodic Maintenance along Hinga-Litolomero 10.41 Km, Ngumbo-Litoho 6.59Km , Mango-Songa Mbele 3.98 and 2Bridge Construction along Mango-Songa Mbele | 900,000,000.00 | 869,783,700.00 | 869,783,700.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 14 | Periodic Maintenance of Lipembe road and Construction of Mungaka Bridge (Stone Masonry Arch Bridge) at Kivulini road in Mbinga Town Council | 500,000,000.00 | 426,399,000.00 | 426,399,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 15 | Construction of 4 Bridges along Kitumbi - Wanga road, 2 Bridges along Mpapa - Ndengu road, 2 bridges along Mbula - Mawindi road and 1 bridge along Ndengu - Nyoni road 1 Bridge along Kihangimahuka - Luikitiki road and 2 Bridges along Ndengu - Kiereketi - Kimbangu road 2bridges along Mapera - Lundo road | 300,000,000.00 | 254,776,200.00 | 254,776,200.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 16 | Libango Bridge protection Works along Minazini-Libango road | 250,000,000.00 | 232,751,500.00 | 232,751,500.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |

| Na | Jina la Mradi | Fedha Idhinishwa | Fedha Zilizotolewa | Fedha Zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 17 | Maboresho ya barabara za Heroes -Ruhuwiko 1.0km Katika kiwango cha Lami(DSD) | 500,000,000.00 | 439,550,000.00 | 439,550,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 18 | Maboresho ya barabara ya Mfuate-Msengemnengem (17.9km) na Barabara ya Rwinga-Mandepwende-Msengemnengem (7.1km) | 650,000,000.00 | 638,011,000.00 | 638,011,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 19 | Maboresho ya barabara za Mjini za Wilaya ya Nyasa(Mbamba Bay Town Roads) katika kiwango cha lami(DSD) | 500,000,000.00 | 467,793,900.00 | 467,793,900.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 20 | Maboresho ya barabara za Mjimwema Kilometa 2 za Wilaya ya Mbinga Mji katika kiwango cha lami(DSD) | 1,000,000,000.00 | 997,941,650.00 | 997,941,650.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |
| 21 | Maboresho ya barabara ya Wino-Ifinga Katika kiwango cha Changarawena Zege | 250,000,000.00 | 200,010,000.00 | 200,010,000.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 100 |

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI HADI DESEMBA 2023

### Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024

Kwa mwaka wa fedha **2023/ 2024**, Mkoa wa Ruvuma katika bajeti ya miundombinu ya barabara umeidhinishiwa jumla ya **TZS 22,594,404,503** ambapo Mfuko wa Barabara ni **TZS. 7,894,956,996.80** Mfuko wa Barabara (Maendeleo) **TZS. 200,000,000** Mfuko Mkuu wa Serikali (kila Jimbo) **TZS**. **4,500,000,000** na fedha tozo ya mafuta Shilingi 100 kwa lita **TZS. 9,999,447,506.41.**

### Mapokezi ya Fedha

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Desemba 2023, Wakala wa barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma umepokea jumla ya fedha kiasi cha **Tshs**. **1,845,933,436.18** ambayo ni asilimia **8.2** ya bajeti ya matengeneao ya barabara na fedha za Maendeleo.

**Hali ya utekelezaji wa miradi ya Barabara kupitia fedha za Maendeleo (Fedha za Jimbo na Tozo)**

Hadi kufikia Desemba, 2023 ya mwaka wa fedha 2023/2024, TARURA Mkoa wa Ruvuma kupitia fedha za maendeleo umefanya kazi za matengenezo ya barabara na ujenzi wa madaraja kwa asilimia **65** za utekelezaji hadi sasa kwa fedha zinazotokana na tozo ya Shilingi 100 kwa lita na zinazotakana na Mfuko Mkuu wa Serikali (Kila Jimbo)**.**

**Jedwali hapo chini linaonesha hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 kuanzia Julai hadi Disemba 2023 (Jedwali Na. 2)**

| Na | Jina la Mradi | Fedha Idhinishwa | Fedha Zilizotolewa | Fedha Zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Maboresho wa barabara ya Majengo-Muungano and Kilimomseto Jct-Pm House katika kiwango cha lami(DSD) na Ujenzi wa daraja la Mjimwema | 800,000,000.00 | 783,671,000.00 | 783,671,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 50 |
| 2 | Maboresho ya barabara ya Masigira-Mlilayoyo | 250,000,000.00 | 228,753,600.00 | 228,753,600.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 20 |
| 3 | Maboresho ya barabara ya Matomondo – Mlale katika Kiwango cha Lami | 1,450,000,000.00 | 1,423,057,550.00 | 1,423,057,550.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 80 |
| 5 | Maboresho ya barabara za Makwaya - Matama Kilomita 23 | 500,000,000.00 | 437,363,800.00 | 437,363,800.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 70 |
| 6 | Maboresho ya barabara za Kifagulo - Magingo Katika Kiwango cha Lami | 600,000,000.00 | 593,600,000.00 | 593,600,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 80 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Maboresho ya barabara za Kifagulo – Magingo Katika Kiwango cha Lam | 500,000,000.00 | 492,150,000.00 | 492,150,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 80 |
| 8 | Maboresho ya barabara ya Ngadinda - Mnazi Mmoja na Hanga - Darajani katika kiwango cha Changarawe | 25,000,000.00 | 214,181,000.00 | 214,181,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 25 |
| 9 | Maboresho ya barabara za Luhimba -Liweta, Mtyangimbole - Kakonko na Igawisenga – Litowa | 500,000,000.00 | 464,001,000.00 | 464,001,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 75 |
| 10 | Maboresho ya barabara ya Mbamba bay Town 0.8km kwa Kiwango cha Lami (DSD) wilaya ya Nyasa | 500,000,000.00 | 474,861,000.00 | 474,861,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 85 |
| 11 | Maboresho wa barabara ya Daniel Mjimwema katika kiwango cha lami(DSD) Wilaya ya Mbinga Mji | 500,000,000.00 | 428,703,000.00 | 428,703,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 85 |
| 12 | Upgrading of Mbinga-Lipalamba (18km) Road to Gravel Standard and Periodic Maintenance of Kitanda, Kitanda - Lupilo, Nairobi, Kiwandani, Madevu Road, Mpepai-Kihungu and Construction of Four Small Span Bridges at Nairobi, Masimeli-Njomlole and Sepukila Roads in Mbinga Town Council | 950,000,000.00 | 893,810,000.00 | 893,810,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 50 |
| 13 | Ujenzi wa Madaraja kumi na Mbili(12) Katika Wilaya ya Mbinga Vijijini | 500,000,000.00 | 488,413,300.00 | 488,413,300.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 30 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Periodic Maintenance Works in Mbinga District | 750,000,000.00 | 749,850,500.00 | 749,850,500.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 25 |
| 15 | Maboresho wa barabara ya Hospitali - Mkurugenzi katika kiwango cha lami (DSD) Wilaya ya Mbinga Vijijini | 500,000,000.00 | 466,045,158.80 | 466,045,158.80 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 85 |
| 16 | ; Periodic Maintenance and Bride Preventive Works Along Minazini - Libango (12.8Km | 500,000,000.00 | 405,762,840.00 | 405,762,840.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 55 |
| 17 | Maboresho ya barabara za Namasakata-Naikula-Liwanga (12km) na Tunduru-Amani-Misichela (15km Katika kiwango cha Changarawe | 500,000,000.00 | 488,200,000.00 | 488,200,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 80 |
| 18 | Maboresho ya barabara ya Kangomba-Marumba - Njenga | 400,000,000.00 | 350,316,000.00 | 350,316,000.00 | Mradi unaendelea, hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia 90 |
| 19 | Maboresho ya barabara ya Chemuchemu-Ligoma-Msinji(7km) Mchesi -Lukala – Mbesa (10km) na Barabara ya Ligoma-Mkapunda(7km) katika kiwango cha Changarawe | 500,000,000.00 | 420,450,000.00 | 420,450,000.00 | Mradi umetekelezwa kwa asilimia 100 |

**4.0 HITIMISHO**

Tunachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza kwa mafanikio hasa katika sekta ya Miundombinu na kuondoa vikwazo vya usafiri na usafirishaji wa mazao vijijini na kwa kipekee kwa kuongeza fedha za miradi ya maendeleo kupitia mfuko wa majimbo na fedha za Tozo za mafuta ya petrol na dizeli kwa kufanya hivyo kumetuongezea ufanisi zaidi kwenye utekelezaji wa miradi na pia kusaidia kuinua uchumi kwa wananchi wa kawaida hasa wakulima kwa kuweza

kusafirisha mazao yao kwa urahisi kuyafikia masoko na hatimaye kukidhi mahitaji yao kwa urahisi. Tunamuomba Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan kuendelea kutuwezesha TARURA ili tuweze kutimiza kauli mbiu yetu isemayo "***Tunakufungulia Barabara kufika kusiko fikika***"

## 8.15 TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY- (TANROADS) – RUVUMA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

### 1. Utangulizi

Serikali kupitia Wakala ya Barabara (TANROADS) inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa miundombinu ya barabara na madaraja mkoani Ruvuma inaimarishwa ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kuinua uchumi na kupunguza umaskini.

TANROADS mkoa wa Ruvuma ina jukumu la kusimamia matengenezo ya mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 2,166.62. Kati ya hizo barabara kuu zikiwa na Kilomita 920.98 ambapo kilomita 702.60 ni za kiwango cha lami na 218.34 ni za kiwango cha changarawe. Urefu unaobaki wa Kilomita 1,245.64 ni wa barabara za mkoa ambapo Kilomita 31.34 ni za lami na 1,432.68 ni za changarawe.

### 2. Ukarabati Mkubwa na Ujenzi wa Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege

Ujenzi wa barabara na ukarabati mkubwa unajumuisha miradi ya kitaifa na miradi ya kimkoa kama ilivyoidhinishwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha 2020 – 2025 kama ifuatavyo:

#### 2.1. Ujenzi wa Barabara ya Mbinga – Mbamba bay

Barabara hii yenye urefu wa Kilomita 66 imejengwa na mkandarasi China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kutoka China na kusimamiwa na mhandisi mshauri SMEC International (Pty). Mkandarasi alianza kazi tarehe 3 Aprili 2018 na hadi kukamilika tarehe 2 Januari 2021 kwa gharama ya jumla ya TSh 129,361,352,517.84.

#### 2.2. Ujenzi wa Daraja la Ruhuhu

Daraja hili lina urefu wa mita 98.01 na linaunganisha Wilaya za Nyasa Mkoani Ruvuma na Wilaya ya Ludewa Mkoani Njombe. Ujenzi wa daraja ulikamilika kwa 100% tarehe 15 Oktoba 2021. Mradi huu ulitekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa nguzo za daraja ambayo ilitekelezwa na mkandarasi kampuni ya Lukolo na

mhandisi Mshauri wa mradi alikuwa ni kampuni ya Crown TECH- Consult. Awamu ya pili ilihusisha ununuzi na ufungaji wa kitanda cha daraja ambapo ilitekelezwa na TANROADS kwa kushirikiana na kampuni ya Jambela Ltd. Jumla mradi uligharimu kiasi cha Tshs. 8.976 Billioni.

### 2.3. Ukarabati na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Songea

Ujenzi wa kiwanja hiki cha ndege ulianza 29 Aprili 2019 ukitekelezwa na mkandarasi China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO). Mhandisi mshauri wa mradi ni Atkins Tanzania Ltd kwa kushirikiana na Howard Humphreys na Advanced Engineering Solutions Limited. Mradi umekamilika tarehe 30 Machi 2023 kwa gharama ya Tshs 37.09 Bilioni. Kwa hivi sasa mradi upo kwenye muda wa matazamio hadi Septemba 2024.

### 2.4. Ujenzi wa Barabara ya Kitai -Lituhi - Ndumbi

Mradi huu una urefu wa Kilomita 95.3. Mradi huu unatekelezwa kwa kiwango cha lami katika awamu zifuatazo:

(i.) Kitai – Amani Makoro : Kilomita 5;

(ii.) Amani Makoro – Ruanda : Kilomita 35;

(iii.) Ruanda – Lituhi – Ndumbi : Kilomita 50.

#### 2.4.1. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Amani Makoro (Km 5)

Mradi huu ulihusisha ujenzi wa Kilomita 5 za kiwango cha lami. ulioanza kutekelezwa tarehe 6 Juni 2019 mkandarasi akiwa ni kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kutoka China na kukamilika tarehe 7 Agosti 2020 kwa gharama ya 6.957 Bilioni. Mhandisi mshauri alikuwa ni kitengo cha ushauri cha TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU).

#### 2.4.2. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Amani Makoro - Ruanda (km 35)

Mradi huu ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara ya Kitai -Lituhi - Kipingu. Ujenzi huu unatekelezwa kwa kujenga Kilomita 35 kwa kiwango cha lami kipande cha Amani Makoro - Ruanda. Mradi ulianza tarehe 15 Juni 2022 na unategemewa kukamilika mnamo Aprili 2024, Mkandarasi ni kampuni ya China Railway Seventh Group, gharama

ya mradi ni TZS TZS 60.481 Bilioni. Mhandisi mshauri wa mradi ni kampuni ya LEA Associates South Asia Pvt Ltd.

Utekelezaji wa mradi kwa hivi sasa umefikia 28%.

#### 2.4.3. Ujenzi Kiwango cha Lami Barabara ya Ruanda – Lituhi – Ndumbi (Km 50)

Barabara hii itaanzia Ruanda hadi bandari ya Ndumbi. Usanifu wa kipande hiki cha Kilomita 50 ulishakamilika. Zabuni ya mradi huu ilitangazwa tarehe 31 Oktoba 2022 na kufunguliwa tarehe 1 Desemba 2022. Tathmini ya zabuni za wakandarasi ilishakamilika na Serikali hivi karibuni imetoa kibali cha utekelezaji wa mradi huu. Kwa sasa mkandarasi wa kutekeleza mradi huu ameshapatikana na Wakala ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba.

***Fidia***

Taarifa ya Uthamini wa Fidia kwa waathiriwa na mali zao ya kiasi cha takribani TSh. 2.9 Billioni ipo katika hatua za uwekwaji wazi wa taarifa kwa waathiriwa na hatimaye kuwasilishwa makao makuu ya TANROADS kwa ajili ya mchakato wa kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua zaidi za upatikanaji wa fedha.

### 2.5. Ujenzi wa barabara ya Likuyufusi hadi Mkenda

Barabara hii ina urefu wa Kilomita 124. Usanifu wake kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ulifanyika mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na muda mrefu kupita usanifu huo ulifanyiwa marejeo na TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU) kwa gharama ya Tsh 178 Milioni na kazi hiyo kukamilika Desemba 2020.

Zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa kiwango cha lami kuanzia Likuyufusi – Mkayukayu, Kilomita 60 ilitangazwa tarehe 19 Oktoba 2022 na kufunguliwa tarehe 14 Desemba 2022.

Tathmini ya zabuni za wakandarasi ilikamilika na Serikali hivi karibuni kupitia waziri mwenye dhamana Mhe. Innocent Bashungwa kutoa kibali cha utekelezaji wa mradi huu.

Kwa sasa mkandarasi wa kutekeleza mradi huu ameshapatikana na Wakala ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba.

***Fidia***

Taarifa ya Uthamini wa Fidia kwa waathiriwa na mali zao ya kiasi cha TSh. 5,198,353,724.16 imeshawasilishwa makao makuu ya TANROADS kwa ajili ya

mchakato wa kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua zaidi za upatikanaji wa fedha.

### 2.6. Ujenzi wa Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda - Lumecha

Mradi huu ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Malinyi Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha yenye jumla ya Kilomita 512 ambayo inaunganisha mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Serikali imeshaanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mkoa wa Morogoro kuanzia Kidatu – Ifakara (66.9Km) kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

Serikali tayari imewekeana saini na mkandarasi China Civil Engineering Construction Corporation Ltd (CCECC) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea Kilomita 512 kwa ajili ya kuijenga kwa kutumia mfumo wa EPC+F. Mradi huu utakuwa wa muda wa miezi 66. Katika ujenzi huu Kilomita 123.93 kuanzia Londo (mpaka na Mkoa wa Morogoro) – Lumecha zipo mkoa wa Ruvuma.

Hivi sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya kukamilisha upatikanaji wa dhamana za benki kabla ya kukabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya utekelezaji.

### 2.7. Ujenzi wa Barabara ya Songea – Lutukira

Mradi huu ni wa Kilomita 116 ambapo utahusisha kipande cha Songea – Lutukira Kilomita 100 pamoja na kipande cha Songea *bypass* Kilomita 16. Upembuzi yakinifu, na usanifu wa kina wa awali ulifanywa na Mhandisi Mshauri BEOMAN Engineering and Architect Co. Ltd na kukamilika mwaka 2014.

Serikali imefanikiwa kupata ufadhili wa benki ya dunia kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi huu. Kutokana na muda mrefu kupita Serikali ilitangaza manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya Usanifu wa Kina pamoja na kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa mradi tarehe 17 Februari 2023 na hivi sasa mchakato upo katika hatua za mwisho. Hali kadhalika Serikali ilitangaza zabuni ya kutafuta mkandarasi tarehe 30 Novemba 2023 na inatarajiwa kufunguliwa 28 Februari 2024.

### *Fidia*

Sambamba na hilo hivi sasa Wizara ya Fedha ipo katika hatua ya kutafuta Fidia kwa waathiriwa yenye thamani ya kiasi cha TSh. 646,964,536.20 kwa upande wa barabara ya Songea – Lutukira na TSh. 4,005,567,798.36 kwa upande wa Songea *Bypass*.

### 2.8. Ujenzi wa Daraja la Mitomoni

Daraja hili litawezesha magari kuvuka Mto Mitomoni na hivyo kuunganisha wilaya za Nyasa na Songea (Vijijini). Daraja hili lilishafanyiwa usanifu na kampuni ya Advanced Engineering Solutions na kukamilishwa tarehe 3 Machi 2020. Daraja hili limesanifiwa kuwa na urefu wa mita 47.7, njia mbili za magari na njia za waenda kwa miguu kila upande zenye upana wa mita 1.9 kila moja.

Zabuni ya ujenzi wa daraja hili ilitangazwa tarehe 15 Desemba 2022 na kufunguliwa tarehe 17 Januari 2023. Hata hivyo, kutokana na kujitokeza kwa mzabuni mmoja pekee na ambaye zabuni yake ilikuwa juu ya makadirio Ofisi ya Meneja baada ya kushauriana na TANROADS Makao Makuu ilishauriwa kuitangaza upya zabuni hii, mchakato wa Manunuzi umeshaanza na upo kwenye hatua ya mwanzo ya manunuzi.

***Fidia***

Ujenzi wa Daraja hili utafanyika katika eneo ambalo ni la hifadhi ya barabara na hivyo halitohusisha wananchi kuathiriwa na kupoteza mali zao.

### 2.9. Ujenzi wa Daraja la Mkenda

Daraja hili linaunganisha nchi ya Tanzania na Msumbiji katika mto Ruvuma. Daraja hili lilishafanyiwa usanifu na kampuni ya Advanced Engineering Solutions na kukamilishwa tarehe 3 Machi 2020. Daraja hili litakuwa na urefu wa mita 144, njia ya magari kuelekea kila upande na njia za waenda kwa miguu.

Zabuni ya ujenzi wa daraja hili ilitangazwa tarehe 15 Desemba 2022 na kufunguliwa tarehe 17 Januari 2023.Hata hivyo, kutokana na kujitokeza kwa mzabuni mmoja pekee na ambaye zabuni yake ilikuwa juu ya makadirio Ofisi ya Meneja baada ya kushauriana na TANROADS Makao Makuu ilishauriwa kuitangaza upya zabuni hii, mchakato wa Manunuzi umeshaanza na upo kwenye hatua ya mwanzo ya manunuzi.

***Fidia***

Ujenzi wa Daraja hili utafanyika katika eneo ambalo ni la hifadhi ya barabara na hivyo halitohusisha wananchi kuathiriwa na kupoteza mali zao

## 3. Usanifu wa Barabara na Madaraja

### 3.1. Usanifu wa Barabara ya Mbamba bay – Lituhi

Mradi huu una urefu wa kilomita 112.4. Usanifu ulifanywa na Mhandisi Mshauri HP Gauff kwa gharama ya Tsh 672 Milioni. Usanifu ulianza mwishoni mwa mwaka 2013 na

kukamilika Juni 2019. Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha ili kuweza kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

### 3.2. Usanifu wa barabara ya Mtwarapachani – Nalasi – Tunduru

Mradi huu una urefu wa Kilomita 300. Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina na uandaaji wa Nyaraka za Zabuni wa barabara hii ulifanywa na Mhandisi Mshauri Advanced Engineering Solutions kwa kushirikiana na G.E.G Portugal kwa gharama ya Tsh 2.559 Bilioni. Kazi ilikamilika Desemba 2019. Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha ili kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

### 3.3. Usanifu wa Barabara ya Unyoni – Maguu – Kipapa

Barabara hii ya changarawe ina urefu wa Kilomita 25. Serikali ipo katika jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga barabara hii katika kiwango cha lami. Hata hivyo, hadi hivi sasa Ofisi ya Meneja imekamilisha ujenzi wa Kilomita 4.2 kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za miradi ya maendeleo.

### 3.4. Usanifu wa Barabara ya Nangombo – Chiwindi

Barabara hii ya changarawe ina urefu wa kilomita 40. Ofisi ya TANROADS, Ruvuma imeshaandaa nyaraka za manunuzi kwa ajili ya kutafuta mhandisi mshauri atakayefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii kwa ajili ya kuijenga katika kiwango cha lami.

### 3.5. Usanifu wa Barabara ya Madaba – Mundindi (Liganga) – Mkiu

Mradi huu una urefu wa Kilomita 46. Usanifu wake ulifanywa na Mhandisi Mshauri Crown Tech Consult Ltd. na kukamilika mwaka 2016. Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

## 4. Matengenezo ya barabara ya muda maalumu, kawaida na kuboresha sehemu korofi

Pamoja na hayo Ofisi ya Wakala ya Barabara pia imeendelea kutekeleza matengenezo ya barabara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 ambayo yamewezesha mtandao mzima wa Barabara Kuu na za Mikoa kupitika wakati wote hivyo kuwezesha shughuli za kijamii na za maendeleo kufanyika bila vikwazo.

## 5. Hifadhi ya Barabara na Mizani

Wakala ya Barabara mkoa wa Ruvuma pia unasimamia sheria ya kusimamia hifadhi ya barabara kuhakikisha haivamiwi. Hali kadhalika TANROADS Ruvuma pia inasimamia

mizani 4 kwa ajili ya kudhibiti magari yasizidishe uzito na kuharibu barabara. Mizani hizo zipo katika maeneo yafuatayo:

(i.) Kijiji cha Lipokela kwenye barabara ya Songea – Mbinga,

(ii.) Kijiji cha Luhimba kwenye barabara ya Songea – Lukumburu,

(iii.) Kijiji cha Sisi kwa Sisi kwenye barabara ya Tunduru – Lumesule na

(iv.) Kijiji cha Buruma katika barabara ya Mbinga – Mbamba Bay.

## 6. Hitimisho

Wakala ya Barabara mkoa wa Ruvuma itaendelea na juhudi za kuhakikisha malengo ya Serikali katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi yanafikiwa kadiri ya mipango ya Serikali.

### 8.16 WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

**I. MAOMBI YA UANZISHWAJI WA KONGANI YA VIWANDA VYA MAZAO YA MISITU MADABA.**

**1. 1.Utangulizi**

Moja ya maeneo Matano ambapo Sera ya misitu ya 1998 imependekeza ni uanzishwaji wa viwanda na biashara ya mazao ya misitu. Mpango mikakati wa Sera wa Mwaka 2021/2031 umeweka lengo la kuwa na Kongani nne za viwanda vya msitu ambayo mojawapo inapendekezwa kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Madaba

Eneo hili litaongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu, Ajira, mapato ya serikali na ongezeko la fedha za kigeni kwa kupitia viwanda endelevu vya misitu na biashara. Kupatikana au kuwepo kwa eneo la viwanda vya misitu kutasaidia matumizi ya nishati itokanayo na mabaki ya mazao ya misitu, vile vile itaongeza hasa uanzishwaji wa misitu ya kupanda, itaongeza matumizi ya aina ya miti isiyofahamika.

i. Katika kutekeleza sera ya misitu na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Ruvuma unaanzisha Kongani ya viwanda vya mazao ya misitu kwenye eneo la Kipingo hekta 250, Halmashauri ya Madaba. Sababu za kupendekeza eneo hilo ni kama ifuatavyo:-
ii. Malighafi ya misitu ya kupandwa (Teak, Pines, Eucalyptus)
iii. Mkoa wa Ruvuma una jumla misitu ya kupanda hekta 36,572 (TFS 7,397 ha, SUA 1,475 ha na TGA 26,360 ha)
iv. Mkoa wa jirani wa Njombe una jumla ya misitu ya kupanda hekta 89,843
v. Mkoa wa Ruvuma una malighafi ya misitu ya asili ambayo inaeneo la kilometa za mraba 41,567 au hekta 4,156,700 sawa na asilimia 65 ya eneo lote la mkoa.
vi. Madaba inaunganishwa na Barabara ya rami ya Makambako-Songea ambayo inaunga na Barabara ya Mtwara-Mbambabay ambayo inaunganisha bandari ya Mtwara, Mbambabay ziwa Nyasa na uwanja wa ndege wa Songea.
vii. Madaba vilevile inaunganishwa na wilaya ya Ludewa kwa barabara ya changarawe hadi ziwa Nyasa bandari ya Manda-Nsungu.

viii. Madaba imepitiwa na lini mbili za umeme, Grid ya Taifa ya Makambako-Songea 220 mw na umeme wa REA 33kv

ix. Madaba ina uhakika wa upatikanaji wa maji ya kutosha toka kwenye mito mikubwa ya Rutukila na Mgombesi ambayo vyanzo vyake vihifadhiwa vizuri.

x. Uwepo wa soko la uhakika la mazao ya misitu ya viwandani, kwa sababu Tanzania inatumia dola za kimarekani million 90 kwa miaka mitano iyopita kwa kuagiza bidhaa hizo toka nchi za nje kama karatasi, plywood, marine board, particle board, karatasi za usafi (Tissue paper, Toilet paper), Tooth sticks n.kSoko la uhakika la mazao ya misitu la kwanza litapatikana kwenye mikoa ya Jirani ya Lindi, Ruvuma na Mtwara na nchi za SADC (Msumbiji, Malawi, Zambia Africa ya kusini na Botswana) na pili ni nchi zingine za Afrika na duniani.

**2. Lengo la mradi**

Kongani ya viwanda vya mazao ya misitu kitakachoanzishwa Madaba hadi kufikia 2026, kongani hii itaongeza ajira na kuongeza fedha za kigeni kupitia viwanda na biashara ya mazao ya misitu.

Kupitia mradi huu wa kiwanda cha mazao ya misitu tunatarajia yafuatayo,

i. Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu.
ii. Kutangaza Masoko Na Biashara ya Mazao Ya Misitu.
iii. Kukuza Uvunaji Endelevu ya Mazao Ya Misitu Na Mazao Mengine Ya Misitu.
iv. Kiwanda Kitapelekea Matumizi Mazuri Ya Mazao Ya Misitu.

**3. Hitimisho**

Mhe. Mwenyekiti tuomba kikao hiki kiridhie uanzishwaji wa kongani ya viwanda vya mazao ya misitu kwenye eneo la Kipingo hekta 250 Halmashauri ya Madaba kwa faida ya wananchi wanaopanda miti ya biashara na Taifa kwa ujumal kwa kuongeza fedha za kigeni.

## II. OMBI LA MISITU YA HIFADHI YA NAMATUI NA LIHUHU KUTANGAZWA KAMA MISITU YA LINDI MAJI (CATCHMENT FOREST).

### UTANGULIZI

Msitu wa Hifadhi wa Namatui Range na Lihuhu Range ni misitu ambayo ilitengwa na kutangazwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa LGA GN 444 ya tarehe 04/11/1994 kwa lengo la kuhifadhi Nyanzo vya maji katika Bonde la Mto Ruvuma (Catchment Forest). Misitu hii inapatikana Halmashauri ya Wilaya Songea katika kata za Muhukulu na Ndongosi

Ili kuboresha usimamizi wa misitu hii mwaka 2017 misitu hii ilihamishiwa Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) na kuchorwa Ramani kwa JB No:3209(Lihuhu) JB No:3210 (Namatui), Misitu hii ina ukubwa wa 2619 Ha (Lihuhu) na 5684 Ha(Namatui).

### UMUHIMU WA MISITU HII

Mh. Mwenyekiti Misitu ya Hifadhi ya Namatui na Lihuhu Range ni muhimu sana kwa Ustawi wa Wilaya ya Songea kwa kuwa na uoto wa Asili unaosaidia;

1) Kulinda vyanzo vya Maji vinavyoanzia ndani ya Misitu hii na kupele maji Mto Ruvuma.
2) Kusaidia kuleta Mvua kwa Maeneo ya Songea na kusaidia katika mabadiliko ya Tabia nchi.
3) Kutumika kama makazi ya Wanyama na viumbe hai wengine wanaopatikana ndani ya misitu hii.
4) Kuwapatia mahitaji muhimu ya mazao ya misitu kwa vijiji vinavyozunguka misitu hii. Nk

Mh Mwenyekiti kwa umuhimu wa Misitu hii na kupitia Kikao hiki Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) inaomba Ridhaa ya kuendele na mchakato wa Kutangaza misitu hii kama Misitu ya Hifadhi ya Lindi maji (Catchment Forest) ili kuongeza usimamizi wa Maeneo haya kwa maslahi mapana ya wananchi wa kizazi cha sasa na Baadae.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

### III. OMBI LA KUREKEBISHA MPAKA WA HIFADHI YA LIHANJE ILI KUTOA ENEO KWA WANANCHI.

**UTANGULIZI**

Msitu wa Hifadhi wa Lihanje una ukubwa wa Hekari 10,565 au Kilometa za Mraba 105.65, ulitangazwa kwa Sheria za Halmashauri ya Wilaya mwaka 1994 nakuwa mali ya Halmashauri ya Wilaya Songea.

Hifadhi kwa mara ya pili ilitangazwa tena kwa sheria ya Misitu (Cap 389) Tangazo No: 333 la tarehe 05/09/2000 na mmiliki aliendelea kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea hadi mwaka 2017 umiliki ulipobadilishwa kutoka TAMISEMI kuja Serikali Kuu (TFS) kwa lengo la kuongeza Nguvu katika uhifadhi ili kukidhi madhumuni ya Kuanzishwa kwake.

Msitu wa Hifadhi wa Lihanje unapakana na vijiji vya Kilagano, Mgazini na Lugagara kwa upande wa Wilaya ya Songea na Kijiji cha Litumbandyosi Wilaya ya Mbinga.

**MAPENDEKEZO YA KUPEWA ENEO KUTOKA HIFADHI YA LIHANJE**

Kufuatia maombi ya muda mrefu ya kuongezewa eneo kutoka Msitu wa Hifadhi Lihanje kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa Vijiji vya Kilagano, Mgazini pamoja na Lugagara, tathimini ya kina iliyofanyika kwa kupitia na kuangalia maeneo yote ya Msitu wa Hifadhi kulingana na umuhimu wake na kupelekea Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Songea kutenga eneo la Hekta **1000** sawa na Ekari **2471** kwa ajili ya kuwagawia wananchi wa Vijiji vya Lugagara,Mgazini na Kilagano kwa matumizi ya kilimo.

Hivyo Mh Mwenyekiti pamoja na kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) una leta ombi kwenu kuridhia mabadiliko ya Mpaka wa Hifadhi ya Milima Lihanje ili kuondoa Jumla ya eneo la Ekari **2471** lililopendekezwa kutolewa kwa Wananchi kwa kuzingatia umuhimu wa uhifadhi bila kuleta madhara kwenye vyanzo vya Maji.

## 9.0 TAARIFA ZA VIKAO VYA KAMATI ZA WILAYA (DCC)

### 9.1 WILAYA YA NAMTUMBO

### MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI (W) DCC KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO TAREHE 24/01/2024.

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Ngollo Malenya | Mkuu wa Wilaya Namtumbo | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Ambokile Paul | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Bw. Francis Mgoloka | Katibu Tawala (W) | Mjumbe |
| 4. | Mh. Lucas Jacob Njogopa | Diwani Kata ya Rwinga | Mjumbe |
| 5. | Mh. Isdory Brown Nyati | Diwani Kata ya Limamu | Mjumbe |
| 6. | Bw. Allen Katyale | DBC – PCCB Namtumbo | Mjumbe |
| 7. | SSGT Nzota | Mshauri Mgambo (W) | Mjumbe |
| 8. | INSP Benedict Mbawala | DPO – Magereza | Mjumbe |
| 9. | Bw. James Joseph | SO | Mjumbe |
| 10. | SSGT. Emmanuel M. | SSGT – UHAMIAJI | Mjumbe |
| 11. | SSP. Osward Ntalanya | OCD – Namtumbo | Mjumbe |
| 12. | Shekh Alfajiri Mpunga | Kaimu Shehe wa Wilaya | Mjumbe |
| 13. | Fr. Bryson Kayombo | Mchungaji | Mjumbe |
| 14. | Bw. Albert Mtimba | Kaimu Meneja TARURA | Mjumbe |
| 15. | Bw. Philipho Komu | Meneja TANESCO | Mjumbe |
| 16. | Bw. Vicent Walter | Meneja – TFS | Mjumbe |
| 17. | Bw. Thobias Nangalaba | DRO – NIDA | Mjumbe |
| 18. | Mh. Paulo Kamilius Fussi | Diwani Kata ya Litola | Mjumbe |
| 19. | Mh. Sambode Petro Mhongo | Diwani Kata ya Ligera | Mjumbe |
| 20. | Mh. Juma Janati Luambano | Diwani Kata ya Luegu | Mjumbe |
| 21. | Mh. Othuman Abed Njovu | Diwani Kata ya Luchili | Mjumbe |
| 22. | Mh. Remna Adimu Nchimbi | Diwani Kata ya Msindo | Mjumbe |
| 23. | Mh. Swaleha Said Moto | Diwani Kata ya Mputa | Mjumbe |
| 24. | Mh. Charles Wilbadi Chengula | Diwani Kata ya Kitanda | Mjumbe |
| 25. | Mh. Saidi Zidadu Zidadu | Diwani Kata ya Lusewa | Mjumbe |
| 26. | Mh. Bakiri Mohammed Mawila | Diwani Kata ya Lismonji | Mjumbe |
| 27. | Mh. Kassim Burhan Gunda | Diwani Kata ya Likuyuseka | Mjumbe |
| 28. | Mh. Nestory Kondradi Nyoni | Diwani Kata ya Namabengo | Mjumbe |
| 29. | Mh. Mrisho Twaib Mbawala | Diwani Kata ya Mgombasi | Mjumbe |
| 30. | Mh. Salum Kabumaye Nyoni | Diwani Kata ya Mchomoro | Mjumbe |
| 31. | Mh. Zamania Rajab Komba | Diwani Viti Maalum Likuyuseka | Mjumbe |
| 32. | Mh. Selina Kayombo | Diwani Viti Maalum Namtumbo | Mjumbe |
| 33. | Bw. Ephrem Kawonga | Afisa Utumishi (W) | Mjumbe |
| 34. | Bw. Estery Mwinuka | Afisa Uchaguzi (W) | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35. | Bw. Jackson Mateso | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) | Mjumbe |
| 36. | Bw. Christian Msegeya | Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) | Mjumbe |
| 37. | Bw. Xvery Mwihava | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) | Mjumbe |
| 38. | Bi. Prisca Msuha | Afisa Maliasili (W) | Mjumbe |
| 39. | Bw. Michael Gambi | Kaimu Afisa Kilimo na Mifugo (W) | Mjumbe |
| 40. | Bi. Yasinta Mayemba | Afisa Tarafa Mkongo | Mjumbe |
| 41. | Bw. Straton Kavishe | Afisa Ushirika (W) | Mjumbe |
| 42. | Bw. Kevin Mlaponi | Kaimu Mganga Mkuu (W) | Mjumbe |
| 43. | Bw. Msyangi M Kruchumila | Afisa Tarafa Sasawala | Mjumbe |
| 44. | Bw. Haruni Mang'uli | Afisa tarafa Undendeule | Mjumbe |
| 45. | Bw. Michael Lyambilo | Afisa Elimu Sekondari (W) | Mjumbe |
| 46. | Bw. Alphonce Kisinini | Kaimu Afisa Mipango (W) | Mjumbe |
| 47. | Bw. Bakari Nihuka | Kaimu Mweka Hazina (W) | Mjumbe |
| 48. | Bi. Teresia Haule | Afisa Biashara | Mjumbe |
| 49. | Bw. Geofrey Kalikawe | Afisa Utumishi | Mjumbe |
| 50. | Bw. Abel Nyoni | Kaimu Afisa TSC (W) | Mjumbe |
| 51. | Bw. Ndikumana N | Kitengo cha Manunuzi | Mjumbe |
| 52. | Bw. Mozes Komba | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | Mjumbe |
| 53. | Bw. Emmanuel Lusian | Kaimu Afisa TEHAMA | Mjumbe |
| 54. | Bw. Ndikumana M | Kaimu Afisa Manunuzi | Mjumbe |
| 55. | Bi. Editha Kayombo | WEO – Mputa | Mjumbe |
| 56. | Bw. Hamis Mkata | Kaimu TEO – Lusewa | Mjumbe |
| 57. | Bw. Ased Hokororo | M/Kiti Namtumbo AMCOS | Mjumbe |
| 58. | Bw. Ally A. Bango | M/Kiti Rwinga AMCOS | Mjumbe |
| 59. | Bw. Ally A. Chemka | M/Kiti Mgombasi AMCOS | Mjumbe |
| 60. | Bi. Josephina Mapunda | M/Kiti UMANA AMCOS | Mjumbe |
| 61. | Bi. Amina H. Hambinga | Meneja NAPACOS | Mjumbe |
| 62. | Bw. Eleterius Mbawala | M/Kiti NAPACOS | Mjumbe |
| 63. | Bw. Hamis Isima | M/Kiti TUMAINI AMCOS | Mjumbe |
| 64. | Bw. Abu M. Nihamba | M/Kiti Luegu AMCOS | Mjumbe |
| 65. | Bw. Rajabu Mtihachi | M/Kiti Libango AMCOS | Mjumbe |
| 66. | Bw. Bakari M. Luena | Mhasibu LUEGU AMCOS | Mjumbe |
| 67. | Bw. Ally A. Chemka | M/Kiti Mgombasi AMCOS | Mjumbe |
| 68. | Bw. Shaibu S. Ndimbo | Mhasibu NAUWASA | Mjumbe |
| 69. | Eng. Francis Meddah | MD – NAUWASA | Mjumbe |
| 70. | Bw. Salum Nachundu | Kaimu Meneja RUWASA | Mjumbe |
| 71. | Eng. Salome Method | Mhandisi – NAUWASA | Mjumbe |
| 72. | Bw. Simon Chosa | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| 73. | FR. Charles G. Mgeni | Padre – RC | Mjumbe |
| 74. | Bw. Hassan Namwela | Katibu ACT | Mjumbe |
| 75. | Bw. Nurdin Mputa | WEO – Namtumbo | Mjumbe |
| 76. | Bw. Zuberi Nikata | Katibu wa Mbunge Jimbo la Namtumbo | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIO HUDHURIA KWA TAARIFA:-**
Hakuna

**SEKRETARIETI:**

1. Bi. Zuhura Mbeyela — Mwandishi wa kikao
2. Bw. Solomon Hyera — Mwandishi wa Kikao.

**DONDOO NA.NMT/DCC/01/2023/2024: KUFUNGUA KIKAO.**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao hicho muhimu cha kamati ya ushauri Wilaya akiwasihi kuchangia ili kuleta maendeleo ya Wilaya.Mwenyekiti pia aliwashukuru wajumbe na wananchi wa Namtumbo kwa ushirkiano katika kuleta maendeleo Mwisho alitamka kufunguliwa kikao saa 04:00 asubuhi.

**DONDOO NA.NMT/DCC/02/2023/2024: KURIDHIA AGENDA.**
Wajumbe waliwasilishiwa agenda za kikao na waliridhia jumla ya agenda 8 zilizo wasilishwa kujadiliwa katika mkutano huo amabazo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na kuridhia ajenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kamati ya ushauri wilaya cha tarehe 17/11/2021.
4. Kusoma na kujadili yatokanayo na kikao cha kamati ya ushauri wilaya cha tarehe 17/11/2021
5. Kupokea na kujadili taarifa ya Divisheni na Vitengo vya Halmashuri ya Namtumbo
6. Taarifa za Taasisi mabalimbali
7. Ombi la kurekebisha Majina ya Vitongoji Vya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewa.
8. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti

**DONDOO NA.NMT/DCC/03/2023/2024: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA DCC CHA TAREHE 17/11/2021**
Wajumbe walipitia muhtasari kwa makini na waliridhia katibu na Mwenyekiti kutia saini ili kuwa kumbukumbu sahihi za kikao.

**DONDOO NA.NMT/DCC/04/2023/2024: YATOKANAYO NA KIKAO CHA DCC CHA TAREHE 17/11/2021**
Wajumbe walipitia maagizo yote yaliotolewa katika kikao kilichopita, na waliridhishwa na utekelezaji wake.

**DONDOO NA.NMT/DCC/05/2023/2024: KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA DIVISHENI NA VITENGO VYA HALMASHURI YA NAMTUMBO.**

Taarifa iliwailishwa ikieleza utekelezaji wa Divisheni na Vitengo vya Halmashuri ya Namtumbo.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia na kutoa maoni kama ifuatavyo:-.

- Wajumbe walishauri Halmashauri kujitahidi kuezeka maboma ilikuokoa nguvu za wananchi hasa katika kipindi cha mvua ili kuondoa hansara.
- Wajumbe walishauri idara ya Mipango kuzunguka na kuangalia uhitaji na uhalisia wa miradi katika Kata na Vijiji kabla ya kugawa fedha za miradi ya maendeleo.
- Wajumbe walishauri Halmashauri kuangalia namna ya kuombea fedha inayofika kutoka serikali kuu kujenga miradi mipya kubadili matumizi kwa kukarabati maboma ambayo yametangulia katika eneo hilo.
- Wajumbe waliomba a Halmashauri kuiomba serikali kuu kuongezewa walimu kwa kuwa bado kuna uhaba mkubwa wa walimu.
- Taarifa ziwasilishwe katika mamlaka husika juu ya Walimu kutopewa jukumu la usimamizi wa miradi kwani inapelekea walimu kutotekeleza majukumu yao ya msingi ya ufundishaji
- Wajumbe walishauri halmashauri kutenga fedha kwaajili ya kuboresha miundombinu ya vituo vya elimu ya watu wenyeulemavu ili kuleta na kuboresha mazingira ya kutoa elimu
- Wajumbe walishauri kuwe na usawazo wa walimu mjini na vijijini ilikukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu vijijini licha ya kuwa na uhaba wa walimu.
- Wajumbe walishauri kutenga bajeti au kuombea fedha kwaajili ya makazi ya walimu hasa vijijini ilikuwezesha walimu kukaa katika maeneo yao ya kazi.
- Wajumbe walishauri Waheshimiwa madiwani, wataalamu, viongozi wa dini na wazazi kushirikiana kufanikisha watoto kuripoti shuleni. Aidha Mwenyekiti aliagiza maafisa Tarafa na watendaji kuhakikisha watoto wanaenda shule. Sambamba na hilo Wajumbe walishauli elimu itolewe kwa wazazi juu ya umuhimu wa elimu.
- Mwenyekiti aliagiza idadi ya madiwati yaliyopo na upungufu iainishe katika shule za msingi na sekondari na kuwasilishwa ofisi ya mkuu wa wilaya.
- Wajumbe waliomba mabadiliko ofisi ya kata Luchili kuelekezwa maeneo ilipo ili kuweza kuepusha usumbufu katika matukio kama uchaguzi.
- Wajumbe waliomba bei ya pembejeo kwa Halmashauri ya Namtumbo ipungue kwakuwa pembejeo hushushwa Namtumbo baada ya kutoka Dar es salaam. Aidha Wajumbe walipongeza mfumo wa stakabadhi ghala kufanya vyema kwa msimu wa 2022/2023.
- Wajumbe waliagiza mawakala wa mbolea za ruzuku wanapofika eneo husika kuripoti kwa Watendaji Kata kabla ya kuanza kazi ili waweze kutambulika.

**DONDOO NA.NMT/DCC/06/2023/2024: TAARIFA ZA TAASISI MABALIMBALI**

**A. TAARIFA YA WAKALA WA BARABARA VIJIJINI NA MJINI - TARURA.**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni ya maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:-

- Wajumbe walishauri kujengwa daraja Mto Langalanga kwenda Namakonde kwani eneo hilo lina wakulima wengi wa ufuta na soya.
- Wajumbe walishauri barabara kutoka Lumecha kwenda mdwema kufunguliwa. Kwa kuwa ni moja ya barabara muhimu kwa uzalishaji. Aidha Wajumbe walishauri matengenezo ya barabara za mashambani kwani ni kichocheo cha uchumi.
- Wajumbe walishauri kuweka alama na vibao vya uelekeo na tahadhari katika barabara ya makutano na mzunguko iliyopo Miembeni Kata ya Likuyuseka ili kuwawezesha watumiaji kutambua uelekeo kwa urahisi.

**TAARIFA YA WAKALA WA MAJI VIJIJINI - RUWASA**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni ya maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:-

- Wajumbe waliomba kuongezeka kwa jitihada kumaliza miradi ya maj ili wananchi waweze kupata huduma hiyo kwa ukaribu Aidha Wajumbe waliomba kata ya msindo na kupatikana visima hata viwili ili kuondoa adha ya upatikanaji wa maji.

.

**TAARIFA YA TAASISI YA KUKUSNAYA MAPATO - TRA**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

- Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walipongeza taasisi inafanya vizuri na walishauri waongezewe watumishi iliwafanye vizuri zaidi.

**TAARIFA YA WAKALA WA UZALISHAJI WA MBEGU WA SERIKALI -ASA**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:-

- Wajumbe walipongeza ASA kwa msimu wa 2022/2023 kwa kufanya vyema katika uzalishaji wa mbegu ilimo wamenunua mbegu kwa bei nzuri.
- Wajumbe aliwaomba wananchi kuisaidia serikali kuwaelimisha wananchi kuachilia maeneo ambayo serikali imeyatenga kwaajili ya uzalishaji wa mbegu.
- Wajumbe waliwataka madiwani kubadilisha mitazamo na kutokuendekeza migogoro ya mipaka ya shamba la mbegu kwani ni kwa maslahi mapana ya taifa.

**TAARIFA YA CHAMA CHA USHIRIKA SONGEA – NAMTUMBO - SONAMCU**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:-

- Wajumbe walihoji kampuni ya tumbaku (MAGEFA) inadaiwa ushuru na Halimashauri hivyo SONAMCU kama waajiri wa makampuni kuisaidia Halimashauri dhidi ya madai hayo.
- Waheshimiwa madiwani walishauriwa kuwahimiza wakulima katika maeneo yao kudai risiti zinazoonesha uzito kabla ya taratibu za malipo pindi wanapopeleka mazao.
- Wajumbe alihimiza elimu kuendelea kutolewa kwa wakulima juu ya ufunguzi wa akaunti ilikuzuia kudhulumiwa.

**TAARIFA YA WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU - TFS**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:-

- Mheshimiwa mkuu wa wilaya alimuagiza afisa wa TFS kupita kujiridhisha kama vyama vya ushirika vya Tumbaku na wakulima wa Tumbaku wanafata muongozo wa upandaji miti na kuwasilisha ripoti kwa Mkuu wa wilaya.

**TAARIFA YA MAMLAKA ZA HIFADHI ZA TAIFA - TANAPA**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

- Baada ya Taarifa kuwasilishwa Wajumbe walishauri tathimini juu ya uhalibifu wa mazao ya wakulima kwa wanyamapori kufanyika kwa muda mfupi ilifidia hiyo iwezekumfikia mkulima na kumsaidia kwa wakati.
- Wajumbe walishauri kutafuta namna ya kuboresha miundombinu ilikuvutia watalii na kuongeza mapato kupitia utalii.

**TAARIFA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAZEE**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Taasisi kwa madhumuni a maendeleo ya Wilaya ya Namtumbo.

- Baada ya Taarifa kuwasilishwa Mwenyekiti wa wazee Namtumbo aliwasihi waheshimiwa madiwani kutambua msimamo wa Mheshimiwa Rais na Mkuu wa Wilaya ilikujenga nyumba moja.

**DONDOO NA.NMT/DCC/07/2023/2024: OMBI LA KUREKEBISHA MAJINA YA VITONGOJI VYA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LUSEWA.**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza Ombi la kurekebisha Majina ya Vitongoji Vya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewa ambavyo vilikosewa majina vitongoji hivyo ni Kitongoji cha Liginga mabacho kinasomeka Igunga badala ya Ligunga na Kitongoji cha Ntungwe ambacho kinasomeka Mtumbwe Badala ya Ntungwe kwenye GN.

- Baada ya taarifa kuwasilishwa Wajumbe waliridhia ombi hilo nakusisistiza kuwasilishwa katika mamlaka husika.

**DONDOO NA.NMT/DCC/08/2023/2024: MENGINEYO KWAIDHINI YA MWENYEKITI**

Hakukuwa na mengineyo.

**DONDOO NA.NMT/DCC/09/2023/2024: KUFUNGA MKUTANO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao, kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri. Mwisho kikao kilifungwa saa 07:32 Mchana.

**UMETHIBITISHWA,**

…………………… ………………………………
**SAINI YA KATIBU SAINI YA MWENYEKITI**

**TAREHE…………………….**

**WILAYA YA NAMTUMBO**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA USHAURI (W) DCC CHA TAREHE 24/01/2024**

| DONDOO NA | HOJA/AZIMIO | MUHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| DCC/05/2023/2024: | Halmashauri kuiomba serikali kuu kuongezewa walimu kwa kuwa bado kuna uhaba mkubwa wa walimu. | **MKURUGENZI MTENDAJI (W)** | |
| DCC/05/2023/2024: | Taarifa ziwasilishwe katika mamlaka husika juu ya Walimu kutopewa jukumu la usimamizi wa miradi kwani inapelekea walimu kutotekeleza majukumu yao ya msingi ya ufundishaji | **MKURUGENZI MTENDAJI (W)** | |
| DCC/05/2023/2024: | Idadi ya madiwati yaliyopo na upungufu iainishe katika shule za msingi na Sekondari na kuwasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. | **MKURUGENZI MTENDAJI (W)** | |
| DCC/06/2023/2024: | Kujengwa daraja Mto Langalanga kwenda Namakonde kwani eneo hilo lina wakulima wengi wa ufuta na soya. | **MENEJA TARURA (W)** | |
| DCC/06/2023/2024: | Afisa wa TFS kupita kujiridhisha kama vyama vya ushirika vya Tumbaku na wakulima wa Tumbaku wanafata muongozo wa upandaji miti na kuwasilisha ripoti kwa Mkuu wa wilaya. | **MENEJA TFS (W)** | |

## 9.2 WILAYA YA SONGEA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA YA SONGEA (DCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 19/01/2024 KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA.**

**KUMB.NA.DCC/SONG/00/2022/2023 MAHUDHURIO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Kapenjama Ndile | Mhe. Mkuu wa Wilaya | Mwenyekiti |
| 2 | Neema M. Maghembe | Mkurugenzi Mtendaji (W) Songea DC | Katibu |
| 3 | Mtela Allamu Mwampamba | Katibu Tawala Wilaya | Mjumbe |
| 4 | Thomas S. Masolwa | M/Kiti CCM Songea Vijijini | Mjumbe |
| 5 | Mwinyi A. Msolomi | Mwenyekiti CCM Songea Mjini | Mjumbe |
| 6 | Dr. Frederick Sagamiko | MD Songea MC | Mjumbe |
| 7 | Sajidu Idrisa | Mkurugenzi Madaba | Mjumbe |
| 8 | Mennas C. Komba | M/Kiti H/W Songea | Mjumbe |
| 9 | Teofanes T. Mlelwa | M/Kiti H/W Madaba | Mjumbe |
| 10 | Jeremia Mlembe | N/Meya | Mjumbe |
| 11 | James Mgego | Katibu CCM (V) Mjini | Mjumbe |
| 12 | Abushehe Nondo | DSO Wilaya | Mjumbe |
| 13 | Insp. Jackson E. Mahali | DFO Wilaya | Mjumbe |
| 14 | Robert H. Mabeja | DPO Wilaya | Mjumbe |
| 15 | Lucy Ikambo | DIO Wilaya | Mjumbe |
| 16 | Maj. Mayunga B. Jacob | MJA Wilaya | Mjumbe |
| 17 | Dismas A. Komba | A/Tarafa Songea Mjini Mashariki | Mjumbe |
| 18 | Salima H. Hakimu | A/Tarafa Ruvuma | Mjumbe |
| 19 | Alkwin R. Ndimbo | A/Tarafa Songea Mjini Magharibi | Mjumbe |
| 20 | Masha Ismail | A/Tarafa Madaba | Mjumbe |
| 21 | Imani E. Kalikumbi | A/Tarafa Muhukuru | Mjumbe |
| 22 | Jacob D. Mapunda | UDP | Mjumbe |
| 23 | Nathaniel Faraja | Ag. DPPEO | Mjumbe |
| 24 | Catherine T. Kimboka | Ag. TTC Matogoro | Mjumbe |
| 25 | Furaha Mwangakala | Songea MC | Mjumbe |
| 26 | Albert L. Nchimbi | Songea UMBASO | Mjumbe |
| 27 | Jackson Matembo | Songea Umoja Boda boda | Mjumbe |
| 28 | Mponeja Mabula | Songea MC | Mjumbe |
| 29 | Sadiki Mushi | Songea MC | Mjumbe |
| 30 | Issa H. Mlela | DFC Wilaya (TFS) | Mjumbe |
| 31 | Mustapha S. Yange | PFC Wino (TFS) | Mjumbe |
| 32 | Selina E. Ngonyani | Kaimu Katibu CCM (W) | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33 | Bumi Kasege | Songea DC | Mjumbe |
| 34 | Elias Sanga | Songea Dc | Mjumbe |
| 35 | Makisio Chengula | Songea DC | Mjumbe |
| 36 | Mama Salumu Abbdalah | BAKWATA | Mjumbe |
| 37 | Hellen Shemzigwa | Songea DC | Mjumbe |
| 38 | Charles Kitaule | SOUWASA | Mjumbe |
| 39 | Steward Chack | Madaba DC | Mjumbe |
| 40 | Jeremiah Chambai | Madaba DC | Mjumbe |
| 41 | John Chinguku | SWACCO | Mjumbe |
| 42 | Nyange Athuman | Songea DC | Mjumbe |
| 43 | Fr. Wilhem Soni | Kanisa Katoliki Songea | Mjumbe |
| 44 | Yusuph Mwikoki | Wazee Songea | Mjumbe |
| 45 | Salia Magreth | NFRA | Mjumbe |
| 46 | Andrew Mwafalo | Songea MC | Mjumbe |
| 47 | Happiness Shemkunde | Songea MC | Mjumbe |
| 48 | Amina Pilly | Songea MC | Mjumbe |
| 49 | Rev. George Kihegulo | KKKT Mjini | Mjumbe |
| 50 | Rajabu Songambele | Katibu Bakwata (M) | Mjumbe |
| 51 | Abdala Ngonyani | Makini | Mjumbe |
| 52 | Lidya B. Kidulile | Songea DC | Mjumbe |
| 53 | Sunday Wahyungi | Songea DC | Mjumbe |
| 54 | Zawadi H. Nyoni | Songea DC | Mjumbe |
| 55 | Frank Mwagongo | Songea DC | Mjumbe |
| 56 | Andrea F. Shayo | Veta Songea | Mjumbe |
| 57 | Joel Mairo | Songea MC | Mjumbe |
| 58 | Betram Njelekela | Songea MC | Mjumbe |
| 59 | Mussa Rashid | Madaba DC | Mjumbe |
| 60 | Filemon Namwinga | Madaba DC | Mjumbe |
| 61 | Hampopo Wajofile | Madaba DC | Mjumbe |
| 62 | Eng. Bakari John | Tarura – Songea | Mjumbe |
| 63 | Hamadi Tarimo | Songea DC | Mjumbe |
| 64 | Salvatory Mangisila | Umoja wa Bajaji Songea | Mjumbe |
| 65 | Wilfred Lazoro | MRCO | Mjumbe |
| 66 | Zuberi Tindwa | Chadema | Mjumbe |
| 67 | Paulo M. Geho | Ada Tadea | Mjumbe |
| 68 | Juma Haule | NCCR Mageuzi | Mjumbe |
| 69 | Evergreen Mkongwa | Songea DC | Mjumbe |
| 70 | Hance Johnrom | NHIF | Mjumbe |
| 71 | Asp. E.E. Mihigo | Polisi | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 72 | Richard M. Tawe | Padre KJKT | Mjumbe |
| 73 | Hamisi H. Kaisi | Katibu CUF | Mjumbe |
| 74 | Twaibu Komba | M/Kiti ACT Wazalendo | Mjumbe |
| 75 | Oswald A. Nyoni | M/Kiti TLP | Mjumbe |
| 76 | Khashim S. Lugome | DHRMO Songea | Mjumbe |
| 77 | Mwajabu Kipande | Bakwata Mkoa | Mjumbe |
| 78 | Maternus Ndumbaro | Madaba DC | Mjumbe |
| 79 | Pendo S. Chagu | Madaba DC | Mjumbe |
| 80 | Madiya M. Magesa | Madaba DC | Mjumbe |
| 81 | Aneth Ndonde | Madaba DC | Mjumbe |
| 82 | Steven Mapunda | Songea DC | Mjumbe |
| 83 | Charles Chawala | CC Songea DC | Sekretarieti |
| 84 | Adam Methew Mlele | Afisa Tawala | Sekretarieti |
| 85 | Maryjoan Ismail Mtui | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya | Sekretarieti |
| 86 | Vicky Phidelisy Chengula | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya | Sekretarieti |

**KUMB.NA.DCC/SONG/01/2022/2023 KUFUNGUA MKUTANO**
Katibu wa kikao alimkaribisha Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kufungua kikao.

Mhe. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wa kikao ambapo alisema akidi imetimia, hivyo aliwaasa kujadili mambo mbalimbali na kupendekeza mambo ya msingi yanayogusa watu ili mradi hayavunji sheria za Nchi. Kikao kilifunguliwa saa 5:18 asubuhi.

**KUMB.NA.DCC/SONG/02/2022/2023 UTAMBULISHO.**

Katibu wa kikao aliwatambulisha wataalam wa Halmashauri tatu (3) kwa makundi na wajumbe wengine walijitambulisha mmoja mmoja kwa majina na vyeo.

**KUMB.NA.DCC/SONG/03/2022/2023 KURIDHIA AGENDA.**
Wajumbe walizipitia agenda zilizoandaliwa na kuziridhia ambazo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Utambulisho.
3. Kuridhia agenda.

4. Kusoma Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya cha tarehe 21.11.2022
5. Yatokanayo na kikao cha tarehe 21.11.2022
6. Taarifa za Utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha 2022/2023
    - Halmashauri ya Manispaa ya Songea.
    - Halmashauri ya Wilaya ya Songea.
    - Halmashauri ya Madaba.
7. Taarifa ya Miradi ya TARURA.
8. Taarifa ya Miradi ya RUWASA.
9. Taarifa ya SOUWASA.
10. Taarifa ya TANESCO.
11. Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa.
12. Taarifa ya kongani la Viwanda vya Misitu Halmashauri ya Madaba.
13. Urekebishaji mpaka wa Hifadhi ya Lihanje, kuridhia kutangazwa kwa Misitu ya Hifadhi ya Namatuhi na Lihuhu.
14. Kuwaondoa wafugaji katika eneo la mwekezaji wa Kiwanda cha sukari katika Kijiji cha Magwamila.
15. Kuongeza maeneo mapya ya Kitongoji cha Tunduma na sehemu ya Yerusalemu (Wino) kuwa sehemu ya shamba la miti Wino (Hifadhi).
16. Mengineyo.
17. Kufunga kikao.

**KUMB.NA.DCC/SONG/04/2022/2023 KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA CHA TAREHE 21.11.2022**

Muhutasari tajwa hapo juu ulisomwa na kuthibitishwa na wajumbe ili kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao**.**

**KUMB.NA.DCC/SONG/05/2022/2023 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 21.11.2022**

Kikao tajwa hapo juu hakikuwa na Yatokanayo.

**KUMB.NA.DCC/SONG/06/2022/2023 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

- **HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA.**

  Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa Manispaa ya Songea iliwasilishwa na Afisa Mipango wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea. Aidha Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa hiyo aliweza kujibu baadhi ya changamoto zilizoibuliwa na wajumbe kama vile, changamoto ya Shule ya Sekondari ya Mgulani kuhusu upungufu wa vyumba vya madarasa ambapo alisema wanategemea kujenga madarasa manne (4). Hata hivyo aliongeza kwa kusema kwamba changamoto ni wazazi ambao wamerudi nyuma katika kuchangia chakula, hivyo alitoa rai kwa Mtoa mada akahamasishe wazazi kuchangia.

  Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Songea alijibu kuhusu changamoto ya usafi ambapo alisema katika Manispaa ya Songea hali kwa sasa ni nzuri ikilinganishwa na kipindi cha miaka miwili nyuma hali ilikuwa ni mbaya, kuhusu kudhibiti hali ya usafi. Mkurugenzi Mtendaji alisema wameweka wanamgambo kwa ajili ya kuwakamata watu wanaovunja sheria ndogo, ya marufuku ya utupaji taka ovyo.

  Kuhusu mustakabali wa mradi wa ujenzi wa Soko la Manzese A na B. Mkurugenzi Mtendaji alisema siku ya tarehe 19/01/2024 limetolewa Tangazo la kuwapata wakandarasi wa miradi ya ujenzi soko la Manzese A na B pamoja na mradi wa ujenzi wa barabara ya kwenda eneo la OTC Lilambo kwenye eneo la kuongeza thamani ya mazao ya nafaka.

  Kuhusu Soko la Bombambili alisema ni Soko la muda na endapo wafanyabiashara watakao hiyari kubaki mara baada ya mradi wa Soko la Manzese kukamilika watajadili, suala la mifereji kuziba alisema tatizo ni wafanyabiashara wenyewe ambao hupikia katika eneo hilo. Hata hivyo alisema Manispaa imekuwa ikizibua mifereji lakini wafanyabiashara wamekuwa wakiendelea kutupa vipande vya nyama katika mifereji hiyo.

Changamoto ya maji ya visima vilivyojengwa na TASAF, Mkurugenzi alisema miradi ya TASAF huibuliwa na wananchi wenyewe wa sehemu husika ya mradi, hivyo aliona ni vyema ikafanyika tathimini ya kitaalam ili kuona nini kifanyike. Sambamba na hilo alijibu changamoto ya eneo la maegesho ya Bajaji la Ikweta kuwa na giza nyakati za usiku, alisema wataweka taa mbili (2) ambapo tayari bajeti ipo. Hata hivyo Mkurugenzi aliwaasa wajumbe endapo wataona kuna changamoto wasisubiri cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) wanaweza kuwaona wataalam wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

- **HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA.**

  Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliwasilishwa na Afisa Mipango wa Halmashauri tajwa hapo juu.

  Meneja wa TARURA alijibu changamoto ya barabara ya Mtomondo – Mlale yenye urefu wa kilomita ishirini na moja nukta tano (21.5km) kwamba itajengwa kwa awamu na kwa sasa iko katika awamu ya tatu urefu wa kilimita moja (1km).

  Kuhusu changamoto ya ukosefu wa Daraja la Lusonga katika Mto Ruvuma barabara inayounganisha Wilaya za Songea na Mbinga Meneja wa TARURA alisema wanafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Daraja hilo na barabara ya Ndongosi alisema imewekwa kwenye bajeti ijayo (2024/25). Pia alisema TARURA wataendelea kufungua barabara katika maeneo ya Magwamila kwa awamu pindi wapatapo bajeti.

- **HALMASHAURI YA MADABA.**

  Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa na Afisa Mipango wa Halmashauri ya Madaba. Taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/07/2022/2023 TAARIFA YA MIRADI YA TARURA.**

Taarifa iliwasilishwa na Meneja wa TARURA.

Meneja wa TARURA alijibu kuhusu changamoto ya barabara ambapo alisema wataendelea kuboresha mathani alitaja barabara ya Majengo – Muungano watatengeneza kwa kiwango cha lami na barabara ya Songea – Makambako ni ya TANROAD. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti alisema barabara hiyo kuanzia mwezi ujao (Februari, 2024) itajengwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/08/2022/2023 TAARIFA YA RUWASA.**

Taarifa iliwasilishwa na Mwakilishi wa Meneja wa RUWASA. Taarifa ilipokelewa na kupitishwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/09/2022/2023 TAARIFA YA SOUWASA.**

Taarifa ya tajwa hapo juu iliwasilishwa na Meneja Msaidizi ambapo alijibu maswali ya wajumbe kuhusu suala la maji kupelekwa kwa wanachama wa CCM ambapo alipinga kwamba maji hupeleka kwa wananchi wote bila kujali itikadi ya Chama cha Siasa, pia alikiri kuwapo na tatizo la maji kutokuwa angavu, lakini alisema maji sio kwamba ni machafu ila kama kuna tatizo aliwaomba wajumbe watoe taarifa na wao watalishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti alielekeza uwekwe mkakati wa kuondoa maji yenye tope. Sambamba na hilo Meneja wa SOUWASA alijibu swali la mjumbe kuhusu namna walivyojipanga kujenga mtandao wa maji taka pembezoni mwa Mji. Meneja alisema kuna mradi wa majitaka ambao una awamu tatu katika utekelezaji wa mradi huo.

**KUMB.NA.DCC/SONG/10/2022/2023 TAARIFA YA TANESCO.**

Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa na Mwakilishi wa TANESCO ambapo aligusia shughuli mbalimbali za utekelezaji wa Shirika hilo kwa mwaka 2022/23 pamoja na mambo mengine alizungumzia hali ya upatikanaji umeme ambayo ni nzuri, pia walifanikiwa kupata wateja 4,500 kati ya lengo la 4,180. Sambamba na hilo alizungumzia changamoto wanazopitia Shirika hilo, kama vile uchomaji wa moto nguzo, wizi wa nyaya (copper) na kuwa na laini ndefu, hivyo wameomba kituo cha kupoozea umeme.

Meneja alisema maombi ya wateja wa kuunganishiwa umeme majumbani eneo la Ruvuma chini katika Manispaa ya Songea, kufikia mwezi Februari, 2024 watapatiwa umeme, maelekezo hayo yaliwasilishwa na Mhe. Mwenyekiti baada ya kuombwa usaidizi wake baada kuona maombi yao yamechukuwa muda mrefu. Hata hivyo Meneja alitoa taarifa kwa wajumbe kwamba kuna mradi mkubwa wa kupooza umeme Songea na Tunduru jambo litalopelekea upatikanaji wa umeme wa uhakika.

**KUMB.NA.DCC/SONG/11/2022/2023 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA SHULE YA WASICHANA YA MKOA.**

Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa na Mratibu wa Mradi huo ambapo ilipokelewa na kupitishwa na wajumbe.

**KUMB.NA.DCC/SONG/12/2022/2023 KUANZISHA KONGANI LA VIWANDA VYA MISITU HALMASHAURI YA MADABA.**

Taarifa iliwasilishwa na Afisa Misitu Mkoa ambapo alizitaja sababu ya uwepo wa mradi tajwa hapo juu ni pamoja na uwepo wa maji. Taarifa ilipokelewa na kupitishwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/13/2022/2023 UREKEBISHAJI MPAKA WA HIFADHI YA LIHANJE, KURIDHIA KUTANGAZWA KWA MISITU YA HIFADHI YA NAMATUHI NA LIHUHU.**

Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa na Kaimu Mhifadhi Mkuu wa Wakala wa huduma za Misitu Tanzania katika Wilaya ya Songea (TFS).

Mhe. Mwenyekiti alitoa maelezo kuhusu dhima ya urekebishaji mpaka wa hifadhi ya Mlima Lihanje uliopo katika Kata ya Kilagano ambapo alisema kumegawiwa eneo la Ardhi lenye ukubwa wa ekari **2,000** kwa wananchi wa Kata hiyo ili waweze kulima. Aidha alisema Serikali ilifanya mazungumzo na wananchi kwa maana ya kutolima katika eneo la hifadhi ya Mlima Lihanje ambapo kuna wakati maji yalikosekana kutokana na uhalibifu wa chanzo cha maji cha Mlima Lihanje.

Mhe. Mwenyekiti alisema kutokana na mgogoro huo ulipelekea Mawaziri nane (8) wa kisekta walishafika kwa ajili ya kutaka kusuluhisha mgogoro huo. Hata hivyo alisema kuna Wananchi wachache waliobakia wanalima, lakini walishakubaliana kuhama pindi

watakavyomaliza kuvuma mahindi yao, hivyo aliwaasa wajumbe kwamba kuhifadhi Mlima Lihanje ni muhimu kwa ajili ya chanzo cha maji sehemu nyingi hasa Kata ya Peramiho. Taarifa hiyo ilipitishwa na wajumbe.

**KUMB.NA.DCC/SONG/14/2022/2023 KUWAONDOA WAFUGAJI KATIKA ENEO LA MWEKEZAJI WA KIWANDA CHA SUKARI KATIKA KIJIJI CHA MAGWAMILA.**

Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Mhe. Mwenyekiti alitoa maelezo kuhusu kuwepo kwa Mwekezaji kwa ajili ya Kiwanda cha Sukari katika Kijiji cha Magwamila ambapo alisema kumefanyika utafiti ikabainika eneo la Magwamila ni sehemu inayoweza kulimwa miwa. Aidha alisema walikubaliana kumpa Mwekezaji eneo la hekta 30,000.

Mhe. Mwenyekiti alisema kumetengwa eneo kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa kuzunguka Kiwanda hicho cha Sukari (outgrowers) ambao watauza miwa yao katika Kiwanda hicho. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti alisema limetengwa eneo la hekta 50,000 kwa ajili ya wafugaji katika Kijiji cha Mhepai, hivyo aliwataka wafugaji kuondoa mifugo yao, lakini sio kufyeka mazao yao, aliongeza kusema kwamba kuna operesheni ya kuwaondoa wafugaji inakuja. Hivyo aliwataka wafugaji kwenda Mhepai. Taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/15/2022/2023 KUONGEZA MAENEO MAPYA YA KITONGOJI CHA TUNDUMA NA SEHEMU YA YERUSALEMU (WINO) KUWA SEHEMU YA SHAMBA LA MITI WINO (HIFADHI).**

Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Mhifadhi Mkuu wa Wakala wa huduma za Misitu Tanzania, Wilaya ya Songea (TFS).

Mhe. Mwenyekiti alitoa maelezo kuhusu umuhimu na faida zitakazopatikana kutokana na uwepo wa shamba la miti Wino (hifadhi). Aidha alisema hifadhi ni kwa manufaa ya wananchi kwa nyakati za uhaba wa Ardhi kwa kipindi wanachi watakapoongezeka,

hivyo alitumai endapo wajumbe watapatisha suala hilo, litapelekea mabadiliko ya kiuchumi yatakayopatikana kutokana na misitu kwa mantiki hiyo aliamini Wino itakuwa kama Mafinga. Taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/16/2022/2023 MENGINEYO.**

Mdau mmoja wa mchezo wa mpira wa miguu aliwaomba Wakurugenzi watatu (3) wa Halmashauri za Wilaya ya Songea kutenga maeneo ya viwanja vya michezo (mpira wa miguu), hivyo aliomba wataalam wa Idara ya Ardhi kutenga viwanja vya michezo.

Mjumbe aliwaomba wataalam wa Maliasili kufuatilia vivutio vya utalii mbalimbali vilivyopo ndani ya Wilaya ya Songea kwani watu wanavivamia. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti alisema katika Wilaya ya Songea hakuna uvamizi wa viwanja, ila alisema viwanja havitunzwi, bali alikubaliana na Mtoa mada viwanja vinapaswa na kutengwa na kutunzwa.

**KUMB.NA.DCC/SONG/17/2022/2023 KUFUNGA KIKAO**.

Katibu alimkaribisha Mhe. Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao.

Mhe. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikao hicho ambapo alisema kuna haja ya kukutana tena ili kufahamu mchango wa madini ya katika Wilaya ya Songea kwa sababu kuna taarifa mbalimbali zilizo nusunusu, hivyo kuna umuhimu wa kujadili kwa kina kuhusu masuala yahusuyo misitu na fedha za mgao wa hewa ukaa. Pia alihimiza kuongezwa kwa kasi ya kupima viwanja kabla ya Mji kuongezeka. Kikao kilifungwa saa 9:35 alasiri.

**UMETHIBITISHWA**

**…………………………...** **……………………………………..**

**SAINI YA KATIBU** **SAINI YA MWENYEKITI**

**TAREHE……………………**

## 9.3. WILAYA YA MBINGA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA YA MBINGA (DCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA FDC MBINGA TAREHE 02.02.2024

**MAHUDHURIO**

1. Mhe. AZIZ A MANGOSONGO MKUU WA WILAYA - Mwenyekiti
2. Ndugu PASCHAL NDUNGURU KAIMU MKURUGENZI WA MJI
3. Ndugu MPOKI NSYENGA KAIMU MKURUGENZI WA MJI
4. Ndugu PENDO NDUMBARO KATIBU TAWALA(W)
5. Ndugu KELVIN MAPUNDA MWENYEKITI MBINGA TC
6. Ndugu DESTERIUS HAULE MWENYEKITI MBINGA DC
7. Ndugu FIDELIS MACHOTA KAIMU MENEJA TANESCO
8. Ndugu MARY KIRITA MENEJS RUWASA
9. Ndugu ISACK MWITA MENEJA TARURA
10. Ndugu IBRAHIM LIDUKE MENEJA NIDA (W)
11. Ndugu DAUSI KAPEI MWAKILISHI WA CUF
12. Ndugu LUKAS CHALE MWAKILISHI WA NCCR
13. Ndugu ERICK KANGALAWE MTENDAJI KATA-MATARAWE
14. Ndugu URSO A. NOMBO KATIBU-CHADEMA
15. Ndugu MARCUS MJENGWA KATIBU ACT
16. Ndugu ANNA O. PATA VITI MAALUM
17. Ndugu UPENDO E. CHIMGEGE KWA NIABA YA MTENDAJI KATA
18. Ndugu MALIBWA J. DASTA MTENDAJI KATA MBINGA B
19. Ndugu HASNA A. MALINZANGA MTENDAJI KATA BETHREHEMU
20. Ndugu LAURENSIA KAPINGA MTENDAJI KATA MBINGA MJINI
21. Ndugu LAMBERTHA KAMBONA DIWANI VITI MAALUMMAALUM
22. Ndugu DORIS W. MBELE MTENDAJI KATA MASUMUNI
23. Ndugu MARIAM R. SADALA MTENDAJI KATALUHUWIKO
24. Mhe. JOHN A. NDUNGURU DIWANI WA MYANGAYANGA
25. Mhe. CRESENSIA J. MAPUNDA DIWANI VITI MAALUM
26. Mhe. EVA NGATUNGA DIWANI VITI MAALUM
27. Mhe. LEONORA MWINUKA DIWANI VITI MAALUM
28. Mhe. GAUDENSIA KOMBA DIWANI VITI MAALUM
29. Mhe. TEDDY NGWENYA DIWANI VITI MAALUM
30. Mhe. KRESENSIA NCHIMBI DIWANI VITI MAALUM
31. Mhe. ANA KAPINGA DIWANI VITI MAALUM
32. Ndugu BLANKA L. NGONYANI MTENDAJI KATA MKUMBI
33. Ndugu STELLAH S. HUMBARO MTENDAJI KATA
34. Mhe. BATSON MPOGOLO DIWANI KATA YA KAGUGU
35. Mhe. AUREUS NGONYANI DIWANI KATA KITANDA

36. Mhe. JOHN MANGILIWE DIWANI KATA YA MBANGAMAO
37. Mhe. PRISCA B. HAULE DIWANI
38. Ndugu. NEEMA MBILINYI MHANDISI MD
39. Ndugu. ELIAS L. BULONGO MTENDAJI KATA AMANI MAKOLO
40. Ndugu. TADEY V.SHAYO MAKAMU MWENYEKITI (TCCIA)
41. Ndugu ALPHONCE C. MNYENYELWA MTENDAJI KATA MIKALANGA
42. Ndugu HATIBU J. IDD MTENDAJI KATA MAPERA
43. Ndugu DANIEL R. KOMBA MTENDAJI KATA LANGIRO
44. Ndugu NASIBU MAPUNDA MTENDAJI KATA RUANDA
45. Ndugu WILSON S. MWASAKUJONGA KAIMU MTENDAJI KATA
46. Ndugu MELKION B. MBELE MTENDAJI KATA LINDYOSI
47. Ndugu SILVIA A. MLELWA AFISA MANUNUZI MBINGA VIJIJINI
48. Ndugu MARTIN MWAKALINGA MENEJA CMS
49. Ndugu GODBLESS SHAO MENEJA TACRI
50. Ndugu MARTINA E. NGAHY AFISA BIASHARA MBINGA VIJIJINI
51. Ndugu ERASTO B. HYERA MTENDAJI KATA MATEKA
52. Ndugu AMOS Y. NDOMBA MTENDAJI KATA MYANGAYANGA
53. Ndugu IVO E. MSUHA MTENDAJI KATA LUWAITA
54. Ndugu BOSCO E. LUOGA MTENDAJI KATA MPEPAI
55. Ndugu AMBROCE E. MBUNDA MTENDAJI KATA MUUNGANO
56. Ndugu ISAKA F. RUSAKA MTENDAJI KATA NAMASWEA
57. Ndugu MAURUS B. HYERA AFISA MIPANGO MIJI
58. Ndugu JACOB F. POKELA MTENDAJI KATA NYONI
59. Ndugu NARZIS G. MWITUMBA MTENDAJI KATA UKATA
60. Ndugu BETRAM A. KAPINGA KATIBU WA MBUNGE MJINI
61. Ndugu ANTHONY A. BINGWA KATIBU MBINGA VIJIJINI
62. Mhe. DOUGLAS C. MWINGIRA DIWANI RUANDA
63. Mhe. NGONEPO AMANYISYE DIWANI BETHREHEM
64. Mhe. BETRAM M. KOMBA DIWANI
65. Mhe. DORIS B. NGALEKA DIWANI MBINGA “ A”
66. Mhe. ALEX N. NGUI DIWANI KITURA
67. Mhe. LAAFORD B. NDIMBO DIWANI LUWAITA
68. Mhe. AMBROSE M. NCHIMBI DIWANI AMANI MAKOLO
69. Mhe. BOSCO K. KAPELA DIWANI MPAPA
70. Mhe. METHOD D NDUNGURU DIWANI MATEKA
71. Mhe. PAULO X KAYOMBO DIWANI MUUNGANO
72. Mhe. LEONS M. NOMBO DIWANI MIKALANGA
73. Mhe. MAGRETH D. NGONGI DIWANI LUSONGA
74. Mhe. ALCA ANDOYA DIWANI KILIMANI
75. Mhe. DENIS M. KAPINGA DIWANI KILOMO

76. Mhe. ISAACK NDUNGURU DIWANI MKAKO
77. Ndugu VEDASTUS G. MWILAFI KATIBU CDCT
78. Ndugu KEFASI A. KAMAGE MAKAMU MWENYEKITI BODABODA(W)
79. Ndugu JAMES P. KIDA KWA NIABA YA MENEJA MBIWASA
80. Ndugu LOTHY A .MWANG`ONDA MKUU WA CHUO FDC MBINGA
81. Ndugu HILAL H. MAJID KWA NIABA YA MENEJA TRA MBINGA
82. Ndugu SAMWEL SHAIDI O/INCHARGE
83. Ndugu BENADETHA NDUNGURU WEO LUSONGA
84. Ndugu SADICK B. HYERA K/ KIHANGIMAKA
85. Ndugu HELENA B. LINGOWE MTENDAJI KATA KAMBARAGE
86. Ndugu CHARLES YAPESA AFISA MIPANGO MBINGA MJI
87. Ndugu PAULO D. MAWALA AFISA TARAFA TARAFA HAGATI
88. Ndugu CHARLES O. NJOVU AFISA TARAFA MKUMBI
89. Ndugu JOHNBOSCO MKANDAWILE MWENEZI CCM(W)
90. Ndugu ANDREA J. MHAGAMA KAIMU AFISA TARAFA MBINGA MJINI
91. Ndugu KARIM H. MZEE DO NAMSWEA
92. Ndugu Eng. EVANCE M. HAULE MHANDISI MBINGA MBINGA VIJIJINI
93. Ndugu Wakili JOB A. MWALUKOSYA AFISA SHERIA MBINGA MBINGA VIJIJINI
94. Ndugu HOTAY A. ILUWAY AG TLO
95. Ndugu ISIHAKA M. RAJABU C.E.O RUVUMA CARE
96. Ndugu DOMINIKUS S. KOMBA WEO MPAPA
97. Ndugu PROSPER I. NCHIMBI WEO LINDA
98. Ndugu MPILUKA KELVIN DFC-TFC
99. Ndugu SALMA A. KIPANDE A/TARAFA MBUJI
100. Ndugu LUKAS H. MAPUNDA WEO KIGONSERA
101. Ndugu ANDREW S. CHIWINGA AG TALFO
102. Ndugu ENEA S. INYEKULE WEO KIPOLOLO
103. Ndugu GRACE P. MBENA KATIBU TSC
104. Ndugu S MKANULA UTAWALA
105. Mhe. TASILO Y. NDUNGURU DIWANI
106. Ndugu CHARLES B. MAHERO HYCS
107. Ndugu JOHN J. KOMBA JOURNALIST
108. Ndugu JOACHIM C. NGAPONDA WEO MATILI
109. Ndugu OSWARD F. WEO
110. Ndugu CECILIA MBATA TCDO
111. Ndugu SOLANA HYERA AG TFAO

112. Ndugu MOHAMED HASSAN WEO KIKOLO
113. Ndugu GEMA R. MMANDA AG TNRECO
114. Ndugu FRANCE P. KAGANDA AG TPNCO
115. Ndugu CHRISTOPHER R. NTANDY AG HPRD
116. Ndugu ALEX WATSON MWANDISHI
117. Ndugu HONEST SHOKI COMMITTEE CLERK
118. Ndugu SAMWEL J. HFRS MBINGA DC
119. Ndugu GILBERT M. GOTPRID PSSNL MTC
120. Ndugu PETER M. KALIMABULALA RCDO
121. Ndugu ROBERT HYERA LIQUORER
122. Ndugu NAMALA TIIGWERA MENEJA NBC-BANK
123. Ndugu DADY ISMAILY HUSSEIN ICTO
124. Ndugu MICHAEL G. MAGORI EMQ
125. Ndugu AMAD MWALUKUNGA AG CMOH
126. Ndugu EDWARD J. ALUKO WEO KIPAPA
127. Ndugu CONDRAD A. KAWONGA Ag TSCO
128. Ndugu ARNOLD G. NGONYANI WEO MBAMBI
129. Ndugu EMMANUEL MALILA TCCIA
130. Ndugu SHEILA MBOKE Ag THESNO
131. Ndugu SHUKURU MSIMBE THS
132. Ndugu RASHID H. BUNDALAH Ag HSE
133. Ndugu SUBIRA G. KOMBA WEO KAGUGU
134. Ndugu MUSA KIPILI MCHUMI
135. Ndugu BACKLAY A.MJUARABU WEO
136. Ndugu JANUARY M. MANJI WEO KILIMANI
137. Ndugu DITRAM E. NDONDE WEO WUKIRO
138. Ndugu KASMIR F. KOMBA PLO
139. Ndugu LILIAN KWEKA CC
140. Ndugu FESTO M. KOMBA WEO KITANDA
141. Ndugu SAIDI MAJID SHE (W)
142. Ndugu FR. BEDA KOMBA PAROKO
143. Ndugu FREDERICK J. MSAE DBC
144. Ndugu HIJA HUSSEIN FOR DSO
145. Ndugu SSGT YUSTIN MSEMRA -
146. Ndugu SP. GABRIEL F. LUDERO OIC KITAI
147. Ndugu WILLIAM MWAMAPUPA OCD MBINGA
148. Ndugu SSP. BENJAMIN M. MASIKA OIC G/MAHABUSU
149. Ndugu SSP. ALOYCE A. MBONGO OIC MKWAYA
150. Ndugu DR KUNG'E NYAMURYEKUNGE
151. Ndugu CLAUD NGUNANGWA Ag.TEO(P)

**HWM/DCC/01/2023/2024 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha Wajumbe kwenye kikao na kumkaribisha Mhe. Mkuu wa Wilaya ili aweze kufungua kikao. Mhe. Mkuu wa Wilaya alitambua uwepo wa Wajumbe wote katika kikao na alipongeza kwa mahudhurio mazuri ya Wajumbe, pia aliwajulisha Wajumbe kuwa kikao kikao kimechelewa kuanza kutokana na muingiliano wa majukumu. Mhe. Mkuu wa Wilaya alifafanua kuwa hiki ni kikao cha watumishi kushauriwa na wananchi na kinajumuisha Halmashauri zote mbili katika Wilaya yetu. Baada ya hapo kikao kilifunguliwa mnamo saa 04:49 Asubuhi.

**HWM/DCC/02/2023/2024 KUPOKEA AGENDA**

Agenda 12 zilisomwa na kupokelewa

1. Kufungua kikao
2. Kupokea agenda
3. Sala/Dua
4. Utambulisho
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 14.06.2023
6. Yatokanayo na kikao cha tarehe 14.06.2023
7. Utekelezaji wa mpango wa bajeti na mapato
   - MBINGA DC
   - MBINGA TC
8. Kuongeza na kupunguza maeneo ya kiutawala katika Wilaya ya Mbinga
   - MBINGA DC
9. Taarifa za utekelezaji wa shughuli za Taasisi mbalimbali
   I. TARURA
   II. RUWASA
   III. TANESCO
   IV. TRA
   V. MBIFACU
   VI. TFS
   VII. TANROAD
   VIII. MBIUWASA
10. Taarifa ya kuwarejesha simba weupe katika hifadhi ya Lipalamba
11. Mengineyo
12. Kufunga kikao

**HWM/DCC/03/2023/2024 SALA/DUA**

Viongozi wa dini ya kikristo na kiislam walifungua kikao kwa sala

**HWM/DCC/04/2023/2024 UTAMBULISHO**

Wajumbe wote walipewa nafasi ya kujitambulisha kwa makundi

**HWM/DCC/05/2023/2024 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 14.06.2023**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 14.06.2023 ulisomwa na ulithibitishwa kuwa kumbukumbu sahihi na za kudumu za kikao.

**HWM/DCC/06/2023/2024 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 14.06.2023**

1. **Azimio:** Taa za barabarani ziwekwe katika barabara kubwa ya kuingilia stendi ili kuepusha ajali za mara kwa mara na msongamano wa magari

**Utekelezaji:** Agizo limezingatiwa kwenye makisio ya bajeti ya 2024/2025

- Ufafanuzi ulitolewa kuwa taa zitawekwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 hivyo mpaka mwakani mwezi wa saba taa zitakuwa zimeshawekwa barabarani

2. **Azimio:** katika makutano ya sheli ya DAE pawekwe makutano ya barabara (round about)

**Utekelezaji:** Hakuna

- Ufafanuzi ulitolewa kuwa tumefanya mawasiliano na TANROAD Mkoa wakasema wataangalia uwezekano wa suala hili katika mwaka ujao fedha 2024/2025

3. **Azimio:** barabara ya hagati iongezewe lami mita mia nne

**Utekelezaji:** Hakuna

- Ufafanuzi ulitolewa kuwa agizo hili pia tuliliwasilisha TANROAD na mwaka jana 2023 waliishia kwenye Kituo cha Afya cha Mapele kwahio mwaka ujao wa fedha 2024/2025 tunategemea kuongezewa lami mita 400

4. **Azimio:** Watumishi pamoja na Wananchi wahudhurie Royal Tour

**Utekelezaji:** Agizo limetekelezwa watumishi pamoja na wananchi wamehudhuria na kushiriki Royal Tour

- Wajumbe waliridhia

5. **Azimio:** Afisa wa NIDA ashiriki kikao kijachp

**Utekelezaji:** Barua ya mwaliko imetumwa tarehe 23.01.2024

- Wajumbe waliridhia

6. **Azimio:** kutokana na mgogoro wa chama cha ushirika cha mahenge iliundwa kamati ya kushughulikia ambayo ni Mwanasheria, Afisa Ushirika na Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii

**Utekelezaji:**Agizo limetekelezwa kesi iko mahakama ya Wilaya iko hatua ya kusikilizwa

- Wajumbe waliridhia

7. Azimio: REA waongeze kasi katika kusambaza umeme Vijijini

Utekelezaji: Agizo limetekelezwa mpaka sasa jumla ya Vijiji 85 kati ya 100 vimewashwa umeme na Vijiji 15 bado na Kampuni imeongezewa mpaka tarehe 30.03.2024

- Wajumbe waliagiza Meneja wa TANESCO aliyepangiwa kuja kuripoti ofisi ya TANESCO- Mbinga aje aripoti kazini hadi kufikia tarehe 19.02.2024 na kama hataki kuja kuripoti aseme ili tuweze kuomba Meneja mwingine

**HWM/DCC/07/2023/2024 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA MAPATO**

**A: MBINGA VIJIJINI**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya mpango wa bajeti na mapato kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliidhinishwa kukusanya na kutumia TSH 43,967,185,612.41 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka vyanzo vya mapato ya ndani na Ruzuzku ya Serikali Kuu. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni TSH 1,163,116,000.00 mishahara na TSH 23,249,317,999.00 na fedha za miradi ya maendeleo (TSH 13,254,751,613.41 na matumizi ya vyanzo vya ndani TSH 6,300,000,0000 ( mapato halisi ni TSH 5,457,849,031 mapato fungwa TSH 574,358,000 na nguvu za wananchi ni TSH 267,792,969)

Hadi kufikia 30 Disemba, 2023 Halmashauri imepokea kiasi cha TSH 16,261,658,868.44 kati ya fedha hizo TSH 13,264,703,101.00 ni mishahara pamoja na matumizi ya kawaida TSH 2,751,021,276.45 ni miradi ya maendeleo TSH 3,890,759,806.00 ni makusanyo ya mapato ya ndani

Wajumbe waliipkea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo:

- Ufafanuzi ulitolewa kuwa hatukuweza kukamilisha miradi kwasababu ya uchelewashwaji wa fedha na pia mapato yalikusanywa mengi Zaidi kipindi cha mwishoni mwa mwaka na katika mwaka huu wa fedha mapato yanakusanywa vizuri
- Ufafanuzi ulitolewa kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 tumepanga bajeti ya Bilioni 8.4 na tumeweka mikakati mbalimbali ya kufikia malengo

mfano tumepanga kuanzisha shule mpya ya English medium na pia tutafatilia ukusanyaji wa mapato vizuri Zaidi

- Ufafanuzi uliendelea kutolewa kuwa tumetenga fedha katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025 wa kutekeleza miradi ya viwanja na mwaka huu wa fedha 2024/2024 tunafanya upembuzi yakinifu ili kuweza kutambua maeneo ya kuuza viwanja

**B: MBINGA MJI**

Kaimu Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya mpango wa bajeti na mapato kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, Halmashauri ya Mji wa Mbinga iliidhinishiwa kukusanya na kutumia TSH 26,783,480,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka vyanzo vya mapato ya ndani na Ruzuku ya Serikali Kuu. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni TSH 18,113,704,000.00 ambapo TSH 17,202,144,000.00 mishahara na TSH 911,560,000.00 matumizi mengineyo, na fedha za miradi ya maendeleo ni TSH 6,193,289,000.00 ( TSH 3,503,552,000.00 fedha za ndani, TSH 2,689,737,000.00 fedha za nje, na TSH 2,476,487,000.00 fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri

Hadi kufikia 30 Disemba, 2023 Halmashauri imepokea kiasi cha TSH 14,292,138,951.84 sawa na asilimia 53 ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo mapokezi ya kawaida ni TSH 9,502,141,000.00 sawa na asilimia 53 (TSH 9,012,628,500.00 sawa na asilimia 52 ni mishahara na TSH 489,512,500.00 sawa na asilimia 54 ni ruzuku ya matumizi mengineyo); na miradi ya maendeleo ni TSH 3,339,829,377.59 sawa na asilimia 54 (TSH 3,030,755,077.59 sawa na asilimia 87 ni fedha za ndani, na TSH 309,074,300.00 sawa na asilimia 11 ni fedha za nje). Mapato ya ndani hadi kufikia Disemba 2023 Halmashauri imekusanya jumla ya TSH 1,450,168,574.25 sawa na asilimia 59

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo;

- Ufafanuzi ulitolewa kuwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani tumefanikiwa kukamilisha Zahanati ya Mahande na Mhekela, pia tumepokea fedha za ujenzi wa Shule Kongwe
- Ufafanuzi uliendelea kutolewa kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 tulitakiwa kukusanya bilioni 2.4 na mpaka kufikia Disemba 2023 tumekusanya kwa 58%
- Kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025 tunategemea kukusanya TSH 3,328,862,407.8 Ufafanuzi ulitolewa kuwa bajeti imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato mfano; Kodi ya mabango ya biashara, kodi ya maegesho ya magari, kodi ya pango la ardhi, kodi ya usajili wa vyombo vya moto

**HWM/DCC/08/2023/2024 KUONGEZA NA KUPUNGUZA MAENEO YA KIUTAWALA KATIKA WILAYA YA MBINGA**

- MBINGA VIJIJINI

Kaimu Mkurugenzi aliwasilisha maombi ya mapendekezo ya kuondoa Kitongoji cha Kingole juu cha Kijiji cha Mahilo Asili, kata ya Mbuji na kufuta Kitongoji cha Mtakuja na kuanzisha Kitongoji cha Mngaka katika Kijiji cha Paradiso, Kata ya Ruanda.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo;

- Mtendaji Kata wa nyoni aliridhia Kitongoji cha Kingole Juu kiwepo katika Kata ya Nyoni na Mtendaji Kata wa Mbuji alielezea kuwa wananchi hawajaridhia Kitongoji cha Kingole juu kirudishwe Kata ya Nyoni wanahitaji kiendelee kubaki Kata ya Nyoni
- Ufafanuzi ulitolewa kuwa Mkutano wa Baraza la Madiwani uliridhia kuwa Kitongoji cha Kingole juu kifutwe kisiwepo Kata ya Nyoni wala Kata ya Mbuji kibaki kinajitegemea
- Afisa Ardhi alifafanua kuwa ardhi ya Kitongoji cha Kingole juu ilikuwepo kwenye ramani ya Kata ya nyoni
- Ufafanuzi uliendelea kutolewa kuwa kitongoji cha Kingole juu kilitangazwa tangu mwaka 2008 kwahiyo tayari kuna wananchi wana maslahi na eneo hilo. Hivyo wananchi wanatakiwa washirikishwe ili waweze kufikia muafaka wa suala hili kwasababu huwezi kukiacha Kitongoji kijitegemee bila ya kuwa na Kijiji au Kata
- Wajumbe waliagiza Wananchi waende wakashirikishwe na wakae na kujadili upya kuwa kitongoji cha Kingole juu kihamishiwe katika kata ipi kati ya kata ya Nyoni au Kata ya mbuji
- Kamati ya Ushauri ya Wilaya haikuridhia Kitongoji cha Kingole juu kilichopo katika kijiji cha Mahilo Asili, Kata ya Mbuji kiondolewe katika orodha ya maeneo ya kiutawala
- Kuhusu kufuta kitongoji cha mtakuja ufafanuzi ulitolewa kuwa wananchi wote walilipwa fidia ili waweze kuhama eneo la mgodi na kuenda maeneo waliyotengewa
- Kamati ya Ushauri ya Wilaya imeridhia na kupitisha Kitongoji cha Mngaka kianzishwe

**HWM/DCC/09/2023/2024 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAASISI MBALIMBALI**
**TARURA**

Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA) Wilaya ya Mbinga inahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya Kilometa 2,037.15 ambapo kilometa 1,063.51 zipo katika Halmashauri ya mji wa Mbinga na Kilometa 973.64 ni zipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga

Katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Mtandao wa barabara umegawanyika kama ifuatavyo kilometa 216.648 ni za Mkusanyo (Collector Roads), Kilometa 519.061 ni za Jamii/Kijiji (Communitu Roads)

Mtandao wa barabara Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga umegawanyika kama ifuatavyo, kilometa 248.69 ni za mjazio (Feeder Roads) Kilometa 88.45 ni za Jamii/Kijiji (Community Roads)

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo;

- Wajumbe walihoji kuwa barabara ya mbangamao bado haijatengenezwa kwani waliahidi kuleta greda. Ufafanuzi ulitolewa kuwa mashine iliharibika hivyo tunasubiri msimu wa masika uishe kasha barabara hiyo itatengenezwa
- Wajumbe walihoji kuwa barabara ya Mkako- Amani makolo inatengenezwa kini kwani ina hali mbaya na kuna tuta limewekwa lakini linamomonyoka kutokana na mvua hivyo litengenenzwe kwasababu tuta likiharibika mawasiliano yatakatika. Ufafanuzi ulitolewa kuwa tayari walishafika eneo la tukio na wameshaweka karavati na watajenga tuta
- Wajumbe walihoji kuwa barabara ya Luwaita iliazimiwa kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami ujenzi utaanza lini. Ufafanuzi ulitolewa kuwa amelichukua hili na wataangalia namna ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025
- Wajumbe waliagiza kuwa kuna msongamano usio wa lazima wa magari kwasababu kuna wananchi wamevamia hifadhi za barabara hivyo TARURA watatue suala hili ili kupunguza msongamano.
- Wajumbe walihoji kuwa anaehusika na kutoza faini ya kuingia barabara isiyo ruhusiwa ni yupi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa hapo awali TARURA ilikuwa inahusika na kutoa faini hizi lakini kwa sasa jukumu hili la kutoza faini ya kuingia barabara isiyo ruhusiwa ni mkurugenzi wa Mji
- Wajumbe walisisitiza kuwa barabara ya sanane ina changamoto inahitaji kuchongwa. Ufafanuzi ulitolewa kuwa barabara hii itachongwa katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025

- Wajumbe walisisitiza kuwa barabara ya Howahowa kuna karavati na mfereji unaopeleka maji Matarawe inatakiwa wazibue mfereji ili wananchi wasipate tabu ya maji. Ufafanuzi ulitolewa kuwa TARURA watatembelea eneo hilo ili waweze kubaini changamoto hiyo na kuiweka katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025
- Wajumbe waliagiza daraja la Lupilinga kwenda Lukalasi lirekebishwe vizuri kwasababu halina kingo
- Wajumbe waliagiza barabara ya Shule ya Sekondari Luanga ichongwe
- Ufafanuzi ulitolewa kuwa TARURA watachukua vipaumbele vyote na watavifanyia kazi, na barabara ya Mchungaji itawekwa katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2024/2025 na itachongwa kwa kiwango cha lami na barabara ya Mbinga Liparamba itajengwa kwa bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2024/2025

**RUWASA**

RUWASA Wilaya ya Mbinga inasimamia utoaji wa huduma ya maji katika Vijiji 117 vipo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na Vijiji 49 vipo Halmashauri ya Mji wa Mbinga vyenye jumla ya wakazi 383,607 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Idadi hii ni sawa na asilimia 86.3 ya wakazi wote wa Wilaya ya Mbinga

Hadi sasa Vijiji vilivyofikiwa na huduma ya maji ni 107 kati ya Vijiji 166 vilivyopo katika Wilaya ya Mbinga saw ana asilimia 65.66. Vijiji ambavyo bado havijafikiwa na huduma ya maji ni 59

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo:

- Wajumbe walihoji kuwa mradi wa maji wa Ruanda unachangamoto maji hayatoki. Ufafanuzi ulitolewa kuwa kuna changamoto ya bomba lakini bomba tayari zimeshafika na tayari wameshazilaza
- Ufafanuzi ulitolewa kuwa kuhusu maji kukatika Kata ya Mbangamao kulikuwa na sehemu korofi maji yalikuwa yameziba
- Wajumbe waliagiza wakandarasi wanaohusika na mradi wa Mbangamao, Mateka, maguu, Amani makolo na Ruanda waripoti ofisi ya Mkuu wa Wilaya

**TANESCO**

Wajumbe waliipokea taarifa na walijadili yafuatayo:

- Wajumbe walipongeza na kushukuru kwa mradi wa REA katika Kijiji cha Kingoli na wamesisitiza kuwa nguzo za umeme ziwekwe ili wananchi waweze kupata umeme
- Wajumbe walihoji namba ya dharura ambayo wananchi wanaweza kuitumia kuwasiliana nao pale yanapotokea maafa au dharura. Ufafanuzi ulitolewa

kuwa wananchi wanaweza kuwasiliana na TANESCO wakati wa dharura/maafa kwa kutumia namba 0715 658 383

- Wajumbe walisisitiza kuwa wakati wananchi wanapofanya maombi ya kupatiwa umeme wapatiwe kumbukumbu namba ya malipo kwa wakati
- Wajumbe walihoji kuwa ni lini Kituo cha Afya cha Mkumbi kitawekewa umeme. Ufafanuzi ulitolewa kuwa walikuwa wanafanya jitihada za kutafutia Bajeti na tayari wameshapata changamoto ni kwamba malighafi zinapatikana kwa tabu sana lakini wanaendelea kushughulikia hadi kufikia mwezi wa tatu watakuwa tayari wameshawekewa umeme
- Wajumbe waliagiza Kata ya Kikolo, Kijiji cha Uzena watoe ushirikiano kwa Mhandisi TANESCO kwa kupisha line ya umeme ipite na wakate miti ili nguzo za umeme ziweze kupita

**TRA**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 TRA Mbinga ilipewa lengo la kukusanya TSH 4,796,100,000.00/= ambapo mpaka tunamaliza mwaka (mwezi juni) 2023 tulifanikiwa kukusanya kiasi cha TSH 3,950,812,758.24/= sawa na ufanisi wa asilimia 82

Pia katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Disemba 2023 Wilaya ilipewa lengo la kukusanya TSH 1,815,620,325.85/= ambapo tumefanikiwa kukusanya kiasi cha TSH 1,957,441,259.21/= sawa na ufanisi wa asilimia 107.8

- Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na waliridhia

**TFS**

Kwa kuzingatia Dira na mwelekeo wa Taasisi kwa kipindi husika katika usimamizi wa rasilimali Misitu zilizopo ndani na nje ya misitu ya hifadhi, Wakala wa huduma za Misitu Wilaya ya Mbinga tulitekeleza majukumu mbalimbali yaliyokuwepo katika mpango kazi kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023

- Doria
- Kuimarisha na kuhakiki mipaka ya misitu (boundary consolidation)
- Uzalishaji na ugawaji wa miche kwa ajili ya wananchi na Taasisi mbalimbali
- Ukusanyaji wa maduhuli
    - Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na waliridhia

**TANROADS**

Wajumbe walijadili yafuatayo;

- Wajumbe waliagiza barabara ya Kigonsera- Kilindi kuna daraja ambalo linakaribia kukatika na kuna gema ambapo gari linaweza kutumbukia mtoni hivyo barabara hiyo itengenezwe
- Wajumbe waliagiza barabara ya mjini Lugari Kata ya Mkumbi sehemu ya mlima Ndembe na Ngiti wakati wa masika haipitiki hivyo irekebishwe
- Wajumbe waliagiza kuwa gema lililopo eneo la kimbanga kwenye kona mkono wa kulia ukitokea nyoni lirekebishwe
- Wajumbe waliagiza korongo lililopo eneo la Kijiji cha Lukanzanti Kata ya Mapera daraja la pili lidhibitiwe

**MBIUWASA**

Mji wa Mbinga una Kata 19 na wakazi wapatao 166,607 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Kati ya hao wakazi 63,822 wapo katika kata 8 zinazo zunguka makao makuu ya Mji na 102,785 wapo katika kata 11 za pembezoni mwa Mji

Hadi kufikia Juni 30, 2023 MBIUWASA imekuwa ikitoa huduma kwa Kata 8 tu zinazozunguka Mji wa Mbinga ambapo huduma imefikiwa kwa asilimia 83.7. idadi ya wateja hadi Juni, 2023 ilikuwa 4,547 na idadi ya sasa ni 4,993.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na walijadili yafuatayo;

- Wajumbe walisistiza kuwa mradi wa maji wa Mbangamao haujakamilika maji hayatoki kwahio wamalizie mradi ili wananchi wasiendelee kuteseka
- Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na waliridhia

**HWM/DCC/10/2023/2024 TAARIFA YA KUWAREJESHA SIMBA WEUPE KATIKA HIFADHI YA LIPALAMBA**

Mkoa wa Ruvuma umejiwekea mikakati mbalimbali ya kukuza na kuboresha maeneo ya vivutio vyake vya utalii. Katika kutekeleza mikakati hiyo ni pamoja na kupandikiza aina za wanyamapori waliokuwa kwenye hatari ya kutoweka katika maeneo ya hifadhi zetu kwa Mkoa wa Ruvuma

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) iliyopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, imejipanga kufanya utafiti juu ya samba weupe waliowahi kuonekana katika pori la akiba la Liparamba linalozungukwa na Wilaya tatu za Mkoa wa Ruvuma ikiwemo Wilaya ya Mbinga

Mpaka sasa hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo wa kuwarejesha simba weupe tayari zimeshaanza ikiwemo kuandika maandiko ya kitaalam (concept note and proposal writing) na wasilisho la maandiko hayo unatarajiwa kufanyika ukumbi wa Manispaa Songea Tarehe 30 Januari, 2024

Baada ya zoezi hilo la kuwarejesha simba weupe utafanyika kwa kuzingatia matokeo na ushauri wa kitaalam wa utafiti huo. Idadi ya simba hao inatarajiwa kuwa sita (06) ambapo simba wanne (04) watakuwa majike na simba wawili (02) watakuwa maduma

Aidha simba hao wataboreshewa ulinzi ikiwa ni pamoja na kufungiwa mifumo ya ufuatiliaji wa tabia na mienendo yao (tracking devices)

- Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na waliridhia

**HWM/DCC/11/2023/2024 MENGINEYO**

- Wajumbe walisisitiza mpaka wa Matiri- Kihaha uainishwe kwasababu unachangamoto
- Wataalam walisisitizwa kuwa wawasaidie wazee kwa kuwaondolea kodi za umeme, ardhi na misamaha mingine ya wazee izingatiwe
- Wajumbe walisisitiza mgogoro wa Ardhi wa Kijiji cha Ukimo Kata ya Mbangamao utatuliwe
- Watendaji wa Wilaya ya Mbinga wamepongezwa kwa utendaji kazi mzuri
- Wajumbe walisisitiza mgogoro uliopo kati ta TANCOAL na wananchi Mhe. Mkuu wa Wilaya akautatue. Ufafanuzi ulitolewa kuwa tayari Mhe. Mkuu wa Wilaya ameshapata taarifa na ataenda kutatua mgogoro huo
- Wajumbe walisisitiza kuwa vituo vya bodaboda ambavyo havina choo watafutiwe choo
- Wajumbe walisisitiza meneja wa MBIUWASA akawasilishe taarifa vizuri kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ya namna ambavyo amejipanga kuhudumia kata zote 19 za Mbinga Mji na kama Baraza la Madiwani litakataa asihudumie Kata zote za Mbinga Mji Mhe. Mkuu wa Wilaya aandikiwe barua ikiambatana na Muhtasari wa Kikao kwa ajili ya hatua zaidi

**HWM/DCC/12/2023/2024 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa michango yao mizuri baada ya hapo alifunga kikao mnamo saa 08:23 Mchana

"Muhtasari huu utapokelewa kama kumbukumbu sahihi ya vikao vya Halmashauri."

**UMETHIBITISHWA**

| | | |
|---|---|---|
| .......................... | ..................... | …............. |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |

**9.4 WILAYA YA NYASA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA YA NYASA (DCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 23/01/2024 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA HALMASHAURI YA WILAYA-NYASA.**
**NDC/DCC/2022-2023/001: MAHUDHURIO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Filberto H Sanga | Mkuu wa Wilaya Nyasa | Mwenyekiti |
| 2. | Khalid A. Khalif | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Salumu M. Ismail | Katibu Tawala (W) | Mjumbe |
| 4. | Valeriana Mosha | DIO (W) | Mjumbe |
| 5. | Almas Almas | Katekista Kilosa (W) | Mjumbe |
| 6. | Adeodatus Millanzi | DSO | Mjumbe |
| 7. | Dioniz Sylvanus | DBC | Mjumbe |
| 8. | Abdul Kayeke | MJA | Mjumbe |
| 9. | Stewart Nombo | Mwenyekiti wa Halmashauri | Mjumbe |
| 10. | Walarick Kikasi | Makamu Mwenyekiti H/W | Mjumbe |
| 11. | Abel Komba | Mwenyekiti wa CCM | Mjumbe |
| 12. | Selemani pinde | Katibu wa CCm | Mjumbe |
| 13. | Nonosius Ndunguru | Diwani kata ya Luhangarasi | Mjumbe |
| 14. | Petro Mapunda | Diwani Kata ya Upolo | Mjumbe |
| 15. | Englbert Turuka | Mratibu wa TASAF | Mjumbe |
| 16. | Shanel Mbunda | Mkuu wa Divisheni ya maendeleo ya jamii | Mjumbe |
| 17. | Joseph Kihwili | Mwenyekiti wa CDM | Mjumbe |
| 18. | Ngwatta Saulo | Katibu wa CDM | Mjumbe |
| 19. | Ally Milanzi | Mwenyekiti wa ACT | Mjumbe |
| 20. | Francis Mapunda | Katibu ACT | Mjumbe |
| 21. | Abel Kawonga | Mwenyekiti wa Wazee | Mjumbe |
| 22. | Selemani Chiwaula | Mwenyekiti wa Mila | Mjumbe |
| 23. | John Chimtunga | Katibu Msaidizi wa Wazee | Mjumbe |
| 24. | Frowin nditi | Katibu wa Mila | Mjumbe |
| 25. | Elistakius Gamba | Katekista | Mjumbe |
| 26. | Ally Liungu | SHEKH | Mjumbe |
| 27. | Romuald Mhagama | Mchungaji | Mjumbe |
| 28. | Severin Munge | Mchungaji KKT | Mjumbe |
| 29. | Reusteven Mwambungu | Mchmoram | Mjumbe |
| 30. | Rogerd Mahundi | Padre Anglikana (W) | Mjumbe |
| 31. | Abas Gama | Kaimu Mtendaji Kta Liuli | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 32. Dennis Katumbi | Mchungaji | Mjumbe |
| 33. Benjamini Kusaga | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Msingi | Mjumbe |
| 34. Blancar Mhagama | Mthibiti Ubiora wa Shule | Mjumbe |
| 35. Shabanho Mwaipopo | ICT | Mjumbe |
| 36. John R. Mrina | Mkuu wa Divisheni ya Afya | Mjumbe |
| 37. Eng. Nicodemas Kapange | Meneja TANESCO | Mjumbe |
| 38. Hairu Mchora | TANESCO | Mjumbe |
| 39. Frank Kihula | Mratibu (REA) | Mjumbe |
| 40. John Hhari | TFS NYASA | Mjumbe |
| 41. Festo haule | Meneja CRDB | Mjumbe |
| 42. Emmanuel Mwasaga | Kaimu Mkuu wa Maliasili na Uhifadhi | Mjumbe |
| 43. Pasifiki Mhapa | Mkuu wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 44. Eg. Allen Mshiu | Mkuu wa Miundombinu Mjini na Vijijini | Mjumbe |
| 45. Albert Mtungi | Kaimu Mkuu wa Fedha na Uhasibu | Mjumbe |
| 46. Dominick Masla | Mtendaji wa Kijiji cha Liweta | Mjumbe |
| 47. Selemani Ndunguru | Mwenyekiti wa wafanyabiashara Nyasa | Mjumbe |
| 48. Castory Mwakatika | Katibu wa Wafanyabiashara | Mjumbe |
| 49. Samwel Mkandawile | - | Mjumbe |
| 50. Pashenle kapinga | - | Mjumbe |
| 51. Deniss Mroki | Kaimu Mkuu wa Taka na usafi | Mjumbe |
| 52. Mohamed Athuman | Kaimu Afisa Ushirika | Mjumbe |
| 53. Michael Swati | NIDA | Mjumbe |
| 54. Paulo Lugongo | Afisa Trafa Ruhekei | Mjumbe |
| 55. Said Sinani | Mtendaji Kata Kihagara | Mjumbe |
| 56. Mossud Sawila | Meneja RUWASA | Mjumbe |
| 57. Eng. Rashid Kavandama | Meneja TARURA | Mjumbe |
| 58. Moses Nchimbi | Katibu wa Mbunge | Mjumbe |
| 59. Edward Mayemba | Afisa tarafa Ruhuhu | Mjumbe |
| 60. Kenedy Nchimbi | Mtendaji Kata Lumeme | Mjumbe |
| 61. Focus Nombo | Kaimu Mkuu wa Mipango na Uratibu | Mjumbe |
| 62. Raphael Mapunda | Kaimu Tendaji Kata Kingerikiti | Mjumbe |
| 63. Ambrose Raphael | Mchumi | Mjumbe |
| 64. Dicksoni Nyoni | Mtendaji Kata Kilosa | Mjumbe |
| 65. Mathias Mallinga | Mtendaji Kata Lipingo | Mjumbe |
| 66. Alphonce Masangati | Afisa Ugavi | Mjumbe |
| 67. Siima Beebwa | Mtendaji Kata Tingi | Mjumbe |
| 68. Daniel Mbele | Mtendaji Kata LuhangarasI | Mjumbe |
| 69. David Chilagi | TASAC – L. NYASA | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 70. | Anthony Haule | - | Mjumbe |
| 71. | Silvester Matembo | Makamu Katibu BMU | Mjumbe |
| 72. | James Charles | Kaimu Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani | Mjumbe |
| 73. | Maajabu Mbogo | Mhifadhi TAWA | Mjumbe |
| 74. | Hamis Mkelle | Mkuu wa Divisheni ya Utawala | Mjumbe |
| 75. | Kenedy Chiunguile | Meneja NMB NYASA | Mjumbe |
| 76. | Osmund Ngantunga | Hakimu Mkazi Mfawidhi | Mjumbe |
| 77. | Ostina Mapunda | Diwani Viti Maalumu | Mjumbe |
| 78. | Elias Katulu | Diwani Kilosa | Mjumbe |
| 79. | Boniface sangana | Diwani Liuli | Mjumbe |
| 80. | Martin Chagala | Diwani Lipingo | Mjumbe |
| 81. | Antoni Kapinga | Diwani Kingerikiti | Mjumbe |
| 82. | Benedicto Nsindagi | Afisa Tawala | Mjumbe |
| 83. | Gideon Mwarabu | Mchungaji | Mjumbe |
| 84. | Dotto Nyankulungu | Afisa sheria | Mjumbe |
| 85. | Philemon Ngaponda | Katibu wa Kamati | Mjumbe |
| 86. | David Makombezulu | Afisa utumishi | Mjumbe |

**NDC/DCC/2022-223/002: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti wa kikao aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao mazuri na kuwataka kuwa makini katika kuchangia hoja mbalimbali zitakazo jadiliwa kwenye kikao na kueleza hali ya usalama,chakula,vipo vizuri na kuwasisitizia wajumbe kuchukua taadhali za ugonjwa wa kipindupindu na kuwahimiza wazazi kuwapeleka watoto shuleni baada ya utangulizi huo mwenyekiti Alifungua kikao mnamo saa 04:30 Asubuhi.

**NDC/DCC/2022-2023/003:KUPOKEA NA KURIDHIA AGENDA**

Kikao kilipokea na kuridhia agenda kama zinavyojieleza hapo chini;

1. Kufungua kikao
2. Kupokea na kuridhia Agenda
3. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Tarehe 08/Desemba/2022
4. Taarifa ya utekelezaji Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Mapitio ya Bajeti ya Nusu Mwaka 2023/2024,Mapendekezo ya Makadiri ya Mapato na Matumizi ya Halmashaurikwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.
5. Taarifa ya Uteelezaji wa Idara na Taasisi

a) Afya
b) Elimu
c) Kilimo,Mifugo na Uvuvi
d) RUWASA

e) NIDA
f) TANESCO
g) TARURA
h) TFS
i) TAWA- Hifadhi ya Liparamba
j) Taaarifa za Taasisi za Kibenki
k) TAKUKURU
l) VETA
m) Kisiwa cha Lundo

7. Taarifa ya mapato ya ndani ya Halmashauri

8. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti

9. Kufunga kikao

**NDC/DCC/2022-2023/004: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 12/NOVEMBA/2021**

Ulisomwa Muhtasari wa kikao cha tarehe 08/Desemba/2022 ambapo wajumbe waliupokea, waliujadili na kuridhia kuwa ni kumbukumbu halali ya kudumu.

**NDC/DCC/2022-2023/005: TAARIFA YA UTEKELEZAJI MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 NA MAPITIO YA BAJETIYA NUSU MWAKA 2023/2024, MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 ambapo ilieleza kuwa,Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiria kukusanya na kupokea jumla ya Tshs:26,052,308,000.00 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.Hata hivyo,Hadi kufikia 30 juni 2023 halmashauri imepokea kiasi cha Tsh 24,733,009,948.62 sawa na asilimia 94.94, kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni Tsh 1,327,410,997.55 sawa na asilimia 97.5, Tsh 14,417,322,170.00 ni fedha za mishahara sawa na asilimia 104.33 na Tsh 758,690,000.00 ni sawa na asilimia 94.37 ni matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ni Tsh 8,427,634,083.37 sawa na asilimia 81.0 Tsh 5,954,464,559.41 sawa na asilimia 144.86 ni fedha za ndani Tsh 2,275,122,221.66 sawa na asilimia 38.2 ni fedha za nje na Tsh 198,047,302.3 sawa na asilimia 60 ya makadirio ya fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo.Aidha yalielezwa mafanikio yaliopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwakas 2022/2023 pia changamoto zake na namna za

kuzitatua.Pia yaliwasilishwa mapitio ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo ilielezwa,Halmashauri ya wilaya ya Nyasa iliidhinishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumia jumla ya Tsh 27,266,134,000.00 kwa ajil;I ya kutekeleza shughuli mbalimbali za halmashauri. Kati yake Tsh 15,755,790,000.00 kwa ajili ya mishahara,Tsh 1,047,366,000.00 kwaajili ya matumizi mengineyo,Tsh 9,018,973,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kati ya fedha hizo Tsh 4,664,725,000.00 ni fedha za ndani (Development Local) na Tsh 4,354,248,000.00 ni fedha za maendeleo za nje (Dev Foreign) na Tsh 1,444,005,000.00 ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ikiwa kiasi cha Tsh 905,600,000.00 ni Mapato ya ndani halisi (Proper Own Source) na Tsh 538,405,000 ni mapato lindwa.Vilevile yalielezwa Mafanikio,changamoto na namna za kuzitatua.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa inakadiria kukusanya/kupokea kiasi cha shilingi 27,266,134,000.00 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbambali za Halmashauri, kati ya fedha hizo Tsh 15,755,790,000.00 kwa ajili ya mishahara, Shilingi 1,047,366,000.00 kwaajili ya matumizi mengineyo,shilingi 9,018,973,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Tsh 4,664,725,000.00 ni fedha za ndani (Development Local) na Tsh 4,354,248,000.00 ni fedha za maendeleo za nje (Dev Foreign) na Tsh 1,444,005,000.00 ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri,ikiwa kiasi cha Tsh 905,600,000.00 ni mapato ya ndani halisi (Proper Own Source) na Tsh 538,405,000.002 ni mapato lindwa.Pamoja na makisio hayo vilitajwa vipaumbe mbalimbali vya kutekeleza kipindi cha mwaka 2024/2025.

Wajumbe waliipokea, Waliijadili na kuipitisha.

**NDC/DCC/2022-2023/006: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA IDARA NA TAASISI**

Ziliwasilishwa taarifa za utekekelezaji za idara na taasisi kama ifuatavyo;

**a) AFYA**

Iliwasilishwa taarifa ya Divisheni ya Afya ,ustawi wa jamii na lishe,ambapo ilieleza hali ya utendaji kazi wa Divisheni kwa kipindi cha mwaka 2022/2023, Idara ya Afya hadi kufikia Tarehe 30 Juni 2023, ilikuwa na Watumishi **280** wa fani mbalimbali waliosambazwa katika Vituo vyote vinavyomilikiwa na Serikali na baadhi ya Vituo

vinavyomilikiwa na Mashirika ya Dini kama vile Hospitali ya Liuli, Lituhi, Kituo cha Afya Tingi na Zahanati ya Nangombo.

**Jedwali lifuatalo linaonyesha Idadi ya vituo na umiliki wake: -**

| Ngazi ya huduma | Serikali | Makanisa | Mashirikia ya Umma | Binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 1 | 2 | 0 | 0 | 3 |
| Vituo vya Afya | 4 | 1 | 0 | 0 | 5 |
| Zahanati | 25 | 6 | 0 | 0 | 31 |
| **Jumla** | **30** | **9** | **0** | **0** | **39** |

**Vituo ambavyo vinaendelea na Ujenzi ni:-**

- Kituo cha Afya Liparamba,
- Kituo cha Afya Kingirikiti
- Marekebisho kwenye Jengo la huduma za dharula Hospitali ya Wilaya(EMD)
- Zahanati ya Ndonga
- Zahanati ya Mkali

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI KITENGO CHA HUDUMA ZA CHANJO

- Usambazaji wa Chanjo za Watoto ulifanyika katika Vituo 36 vinavyotoa Huduma za Chanjo ndani ya Wilaya.
- Uwasilishaji wa Taarifa za Chanjo uliwekwa kwenye Mfumo wa VIMS
- Ulifanyika usimamizi shirikishi wa Chanjo ya UVIKO 19 katika Vituo 8 vyenye kutoa Huduma za CTC kwa WAVIU,Vituo hivyo ni Chiulu Dispensary, Kwambe Dispensary, Liparamba Health Center, Lituhi Hospital , Lundo Dispensary Lunyere Dispensary, Mbambabay Health Center na St. Annes Liuli.
- Ilifanyika Kampeni ya Chanjo ya Surua (MR) walengwa walikuwa kuanzi Miezi **9** mpaka Miezi **18.**Walengwa walikuwa **1227** waliofikiwa kupata huduma hiyo walikuwa **1830** sawa na Asilimia125.8%
- Katika kipindi chote hatujapata Taarifa ya maudhi yatokanayo na Chanjo kwa Watoto wote waliopatiwa Chanjo.

**Changamoto**

- Mwitikio mdogo wa Wazazi kuruhusu Watoto wao wapate chanjo ya HPV.
- Changamoto yakuharibika kwa Jokofu la Zahanati ya Tingi nakupelekea Chanjo hizo kutunzwa kwenye Jokofu la Zahanati ya Luhindo.

**Utatuzi**

- Elimu inaendelea kutolewa kwenye Vituo vyetu vyakutolea huduma juu ya umuhimu wa Mtoto wa kike kupata Chanjo hiyo ya HPV.
- Mawasiliano yameshafanyika Ngazi ya Divisheni kupata Jokofu lingine lakuhifadhia Chanjo.

Jedwali linaonyesha Huduma za Afya ya Mama na Mtoto zilizotolewa mpaka Juni 30 2023

| AINA YA HUDUMA | Huduma ya uzazi wa mpango | Kliniki ya wajawazito (hudhudhurio la kwanza) | Waliohudhuria Chini ya wiki 12 za ujauzito | Waliopima maambukizi | Waliokutwa na maambukizi | Waliopata dawa | Waliopima na wenza | waliojifungua | Watoto waliozaliwa hai | Watoto waliofaiki (FSB) | Waliozaliwa na mchubuko (MSB) | Wazazi waliofariki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mpaka Juni.30 2023 | 4636 | 3520 | 3311 | 3222 | 22 | 22 | 3019 | 3238 | 3302 | 3 | 6 | 1 |

**K**ati ya wamama 3238 waliojifungua Mpaka Juni 30 2023

- Akina mama 3198 walijifungulia Kituoni

- Akina mama waliojifungulia kwa Mkunga wa Jadi 0

-Akina waliojifungulia Nyumbani ni 0

- Akina mama waliojifungulia Njiani ni 20

**Utatuzi**

- Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii na watoa Huduma katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya wanaendelea kutoa Elimu juu ya umuhimu wa kuanza Kliniki ya Wajawazito chini ya Wiki kumi na mbili za Ujauzito.
- Elimu imeendelea kutolewa kwenye Vituo vyakutolea Huduma juu ya athari za Mama Mjamzito kutumia Dawa za Mitishamba ili kuongeza Uchungu
- Idara ya Afya imeendelea kutoa Elimu kupitia Redio, na kwenye Vituo vyote vinavyotoa Huduma za Uzazi juu ya umuhimu wa Mama kuwahi mapema kufika Vituoni kwaajili yakupata Huduma ili kuepusha Vifo vitokanavyo na Uzazi.

**Taarifa ya kitengo cha dawa mpaka juni 30 2023.**

- Hali ya Upatikanaji wa Dawa muhimu kwenye Vituo vyote vya kutolea Huduma za Afya ndani ya Wilaya ya Nyasa ni Asilimia 93.7%.
- Hadi Juni 30 2023 tumepokea Vifaa Tiba vya aina mbalimbali ambavyo vilisambazwa katika vituo vyakutolea huduma kutoka MSD ikiwemo Magodoro 30,Ultrasound Machine 1,na Automatic Generator Kv48.moja
- Tulipata Msaada wa Vitanda 15 vya Wagonjwa vikiwa na Magodoro yake kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania na kuvisambaza kwenye Vituo mbalimbali vyakutolea huduma za Afya ndani ya Wilaya.
- Tuliomba msaada Hospitali ya Divisheni wa Ruvuma nakupata Vifaa Tiba kwaajili ya Kituo cha Afya Kingirikiti ikiwemo na kituo cha afya Kihagara ili kituo cha afya kingirikiti kianze kutoa Huduma za Afya Ngazi ya Msingi nakufanikiwa kupata Vifaa vifuatavyo,Vitanda vya Wagonjwa 11, Vitanda vya Uchunguzi 3, Vitanda vyakujifungulia 5, Medication Troley 2, Infant Scale 1, Donation Chair 1 na Aidha upatikanaji wa Vifaa hivi umeturahisishia kutafuta Vifaa vichache vili vyobaki ili Huduma zianze kutolewa**.**

**Changamoto**

- Bado kunachangamoto ya upatikanaji wa Vifaa Tiba na Dawa kwenye Vituo vyakutolea Huduma linalochangiwa na uhaba wa Dawa kwenye Bohari ya Serikali (MSD)

**utatuzi**

- Tumeendelea kutoa Oda ya Vifaa Tiba na Dawa kwenda MSD ili kuendelea kupunguza uhaba wa Dawa na Vifaa Tiba kwenye vituo vyakutolea Huduma

**Taarifa Ya Kitengo Cha Lishe Mpaka Juni 30 2023**

- Mpaka kufikia Juni 30 2023 Kitengo cha Lishe kilifanya Kampeni ya **Matone ya Vitamini A** katika Vituo vyote vyakutolea Huduma za Afya Ndani ya Wilaya na walengwa ni Watoto wote wenye Umri kuanzia Miezi **6-11** na wengine kuanzia Miezi **12 -59.**
- Jumla ya Watoto **23503** (walengwa) walitarajia kupata **Matone ya Vitamini A** kati ya hao tulifanikiwa kutoa **Matone ya Vitamini A** kwa Watoto **23530** ambao ni Asilimia 100.
- Siku ya Afya ya Lishe ya Kijiji imefanyika katika Vijiji vyote 84 Ndani ya Kata Ishirini tulizonazo.

**Changamoto**

- Bado kuna changamoto ya baadhi ya Wazazi kutotilia mkazo wakuhudhuria Siku ya Afya ya Lishe ya Kijiji

**Utatuzi**

- Tumeendelea kutoa Elimu kupitia Vituo vyakutolea Huduma juu ya Umuhimu wa kila Mzazi kuhudhuria Siku ya Afya ya Lishe ya Kijiji.

**TAARIFA YA KITENGO CHA USTAWI WA JAMII HADIJUNI.30 2023**

**Usuluhishi wa migogoro**

- Jumla ya Mashauri 40 yalishughulikiwa kati ya hayo, Mashauri 17 ni ya utelekezaji wa Familia na yote yalipatiwa ufumbuzi,na Shauri Moja lipo katika Ngazi ya Mahakama

**Taarifa ya ugonjwa wa kipindupindu halamashauri ya wilaya ya nyasa.**

Mnamo tarehe 21 Januari 2023 Divisheni ilipokea taarifa ya kuwepo kwa wagonjwa watatu (3) wa kipindupindu toka Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa. Baada ya ufuatiliaji wa kina ilionekana kwamba wagonjwa kabla ya kuanza kuugua walishiriki mazishi ya Mwanamume mmoja aliyefariki Nchini Msumbiji na Mwili wake kusafilishwa kwa siri kupitia mpaka usiorasmi kuja nchini katika Kijiji cha kilosa Huko Nyasa.

Divisheni umeendelea kupokea taarifa za wagonjwa wanaohisiwa kuwa na kipindupindu ambapo hadi kufikia tarehe 12/02/2023 kulikuwa na jumla ya wagonjwa 12.

Vijiji ambavyo vimepata wagonjwa hadi sasa ni Kilosa, Mtupale, Ng'ombo na Lunyere. Aidha, hadi tarehe 11/02/2023 Divisheni ulipokea uwepo wa vifo viwili zaidi na kufanya jumla ya vifo kuwa vitatu.

Historia inaonesha waliofariki ni watanzania wanaofanya kazi ya uchimbaji madini katika Nchi Jirani ya Msumbiji eneo la Mianzini C ambapo Mgonjwa mmoja alifia njiani akielekea zahanati ya Lunyere kwa ajili ya matibabu na mwingine alifariki akiwa anaendelea na matibabu katika zahanati ya Lunyere

Tarehe 14/02/2022 Timu ya Uendeshaji na usimamizi wa huduma za Afya Divisheni kwa kushirikiana na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya Halmashauri ya Nyasa ilitembelea Kijiji cha Lunyere kwa ajili ya ufuatiliaji wa ugonjwa huu.\

**YALIYOJITOKEZA WAKATI WA UFUATILIAJI**

- Timu ilikutana na wataalamu wa Afya toka Nchi ya msumbiji na kufanya majadiliano ya pamoja juu ya hali ya ugonjwa unaoendelea baina ya nchi hizi Mbili.
- Timu ya Msumbiji ilieleza kwamba hada sasa Wilaya ya Nyasa Nchini Msiumbiji kuna maambukizi ya kipindupindu yanayoendelea katika maeneo mbalimbali. Aidha, walieleza kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza kwa ugonjwa wa kipindupindu kuripotiwa katika eneo la Mianzini C.
- Ilelezwa kwamba kuna hali ya Duni ya usafi wa mazingira na na Uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji katika eneo la Machimbo (Mianzini C) pamoja na Kijiji cha Lunyere.

- Kabla ya kuugua marehemu wawili (Dominicus Mgunda na Selestine Mkenda) walishirikiana na kijana mmoja aliyetokea Eneo la Chiwindi aliyekuwa akiharisha na kutapika
- Imani potofu ya wananchi juu ya ugonjwa wa kipindupindu (wanaamini ni ugonjwa wa kulogwa)

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA WAKATI WA UFUATILIAJI**

Timu za Tanzania na Msumbiji ziliweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu kama ifuatavyo

- Timu zilikubaliana kuunda group la Whatsapp la Wataalamu wa Afya na viongozi wa tarafa,kata na eneo toka msumbiji pamoja na wataalamu wa Afya ngazi ya Kituo, Halmashauri na Divisheni wa Ruvuma kwa ajili ya kupeana taarifa mbalimbali ya wagonjwa na matukio yanayojiri katika nchi hizi mbili
- Kuimarisha utoaji wa elimu ya kujikinga na kuzuia ugonjwa wa kipindupindu kwa jamii kwa pande zote mbili.
- Kusimamia usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo bora na matumizi yake kwa pande zote mbili
- Timu ilikutana na walinzi wa mpaka kwa upande wa masumbiji na kushauriana nao juu ya uanzishwaji wa kambi ya Matibabu ya kipindupindu iwapo ugonjwa utaendelea na walishauri kambi iwekwe eneo la Majimazuri.
- Timu ilifanya mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Lunyere na kukubaliana yafuatayo
    - ✓ Viongozi wa serikali ya Kijiji wasimamie usafi wa mazingira katika maeneo yao
    - ✓ Viongozi wa Kijiji wasimamie ujenzi wa vyoo bora kwa kila kaya katika Kijiji
    - ✓ Viongozi wachague eneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka
    - ✓ Viongozi na wananchi watoe taarifa mapema kwa mganga kiongozi wa zahanati au ngazi ya Halmashauri wanapoona mgonjwa wa kuharisha na kutapika au mgonjwa wa ugonjwa wowote wasiouelewa
    - ✓ Viongozi wa Kijiji wasimamie uwekaji wa vyombo vya kunawa mikono katika maeneo yote ikiwemo kwenye kaya, taasisi maeneo ya biashara, maeneo ya starehe na maeneo ya umma.

**CHANGAMOTO ZILIZOKO**

i. Kukosekana kwa miundombinu ya barabara kutoka Nchi Jirani ya msumbiji Kwenda zahanati ya Lunyere
ii. Uwepo wa mipaka mingi isiyo rasmi (pours borders) kwa upande wa Tanzania hivyo kupelekea wananchi toka msumbiji kuingia nchini bila utaratibu
iii. Ukosefu wa usafiri kutoka eneo la Mianzini C (Msumbiji) Kwenda Lunyere hivyo wagonjwa kuchelewa kufika katika kituo cha kutolea huduma
iv. Umbali kati ya vituo vya kutolea huduma za Afya kwa upande wa Msumbiji ambapo kutoka Minzini hadi kituo cha karibu ni Zaidi ya Masaa nane kwa pikipiki

v. Ukosefu wa vipeperushi na mapango kwa ajili ya elimu ya kujikinga na kipindupindu
vi. Kukosekana kwa fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi na ufuatiliaji
vii. Kukosekana kwa mafuta
viii. Kukosekana kwa waterguard kwa ajili ya kutibu maji ya kunywa
ix. Kukosekana kwa chlorine kwa ajili ya disinfection
x. Kukosekana kwa givingset gauge 16 na 18
xi. Upungufu wa matumishi hasa mafisa Afya ambapo kwa Wilaya ya Nyasa kuna Afisa Afya mmoja tu
xii. Kutomuda gharama za kupima maji kutoka kwenye vyanzo vinavyotumiwa na jamii kwa sababu ya ukosefu wa fedha

**ELIMU**

Iliwasilishwa taarifa ya Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi ambapo ilielezea hali ya miundo mbinu katika shule pia hali ya kitaaluma kwa kufafanua juu ya hali ya ufundishaji na ujifunzaji na kuelezea hali ya ufaulu kama ifuatavyo;

- Kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji katika shule za Awali na Msingi ambapo Ufuatiliaji umefanyika kwa Mwezi Oktoba, 2023
- Kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji mahiri mbalimbali ikiwemo umahiri wa somo la Kiingereza ambapo Walimu wakuu wameagizwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanamudu mahiri hizo.
- Kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ambapo Walimu wakuu wameelekezwa kuondoa tatizo la wanafunzi kutomudu stadi za KKK
- Kufanya maandalizi na ufuatiliaji wa ufanyikaji wa Mtihani wa Kuhitimu Elimu Msingi 2023 ambapo Mtihani wa Kuhitimu Elimu Msingi ulifanyika tarehe 13 – 14/09/2023.
- Kufanya maandalizi na ufuatiliaji wa ufanyikaji wa Upimaji wa Kitaifa darasa la Nne 2023 ambapo Upimaji wa Kitaifa darasa la nne ulifanyika tarehe 25–26/10/2023.
- Ufuatiliaji na ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa MEWAKA ambapo Zoezi la ufuatiliaji wa MEWAKA linaendelea
- Kupitisha Mihtasari ya Malipo ya kifedha Shuleni ambapo Kazi ya kupitisha Mihtasari ya malipo ni endelevu
- Kufanya uandikishaji wa Wanafunzi wa darasa la Awali na darasa la Pili ambapo Hadi kufikia tarehe **22/12/2023** wanafunzi walioandikishwa kwa darasa la Awali ni Wav **1856** Was **1922** Jumla **3775** sawa na asilimia **68**, na kwa darasa la Pili wameandikishwa Wav **2164** Was **2265** Jumla **4429** sawa na asilimia **81**

b) **KILIMO,MIFUGO NA UVUVI**

Iliwasilishwa taarifa ya kilimo,Mifugo na Uvuvi ambapo ilieleza shughuli zilizofanywa ni pamoja na kuendelea kuwasajili wakulima mwaka 2022/2023 ili kuwawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo na kutambua umiliki wa mashamba kwa kila mkulima ili

aweze kupata mbolea kulingana na ukubwa wa shamba anaomiliki  na hitaji lake ili kulea tija katika uzalishaji.

Wajumbe walipokea taarifa walijadili na kuiridhia

**c) RUWASA**

Iliwasilishwa taarifa ya RUWASA ambapo ilielezea utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hususani na miradi ya maji na usafi wa mazingira katika kipindi cha mwezi wa januari 2024kazi zilizofanyika katka kipindi husika ni kama kuendelea kusimamia kazi ya ujenzi wa miradi ya maji chini ya program ya lipa kwa matokeo PAYMENT FOR RESULT (**P4R**), **GOT** na **National Water Fund** pia kufanya kazi ya kutembelea na kukagua hali ya uendeshaji wa miradi (**O&M- Operation and maintenance** ) ya maji inayofanya kazi chini ya CBWSOs na kutoa ushauri wa kiufundi kwa vyombo vya watoa maji (**CBWSOs**)    pia zilielezwa changamoto kuwa RUWASA  Nyasa inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa watumishin ambapo wakala una jumla ya watumishi 8 tu ikilinganishwa na maitaji ambayo ni watumishi 22 na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 14 pamoja na changamoto ya uchakafu wa gari .Gari lillopo huhitaji matengenezo ya mara kwa mara na hivyo kuathiri shughuli za usimamizi na ufuatiliaji sambamba na changamoto zilizotajwa kuna mwamko mdogo wa jamii kuhusu kulipia huduma ya maji

Aidha taasisi imeweka mikakati ya kukabiliana na changamoto kama ifuatavyo;

- Kuendelea kushirikiana na watalamu kutoka RUWASA mkoa kutekeleza shughuli za miradi ya maji zinazoendelea wilaya ya Nyasa hasa suala la usanifu wa miradi .
- Kuwashirikisha wadau mbalimbali kuhamasisha kuhusiana na umuhimu wa kulipia huduma ya maji kwa ajili ya uendelevu wa miradi .

Wajumbe waliipokea taarifa, waliijadili na kuiridhia.

**d) NIDA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za NIDA iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa zoezi la kutoa vitambulisho vya Utaifa linaendelea na vitaendelea kutolewa kadiri ya hitaji la wakazi na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata vitambulisho vya NIDA ili kurahisisha wanafunzi kutambulika wanapo kwenda kwenye kozi mbalmbali za mafunzo na kuwapunguzia gharama wazazi ambapo wanafunzi hao wanaposhindwa kupokelewa kwenye taasisi mbalimbali kutokana na uwepo wa changamoto ya ukosefu wa

kitambulisho cha Uraia. Wajumbe walipokea taarifa, waliijadili na kutoa ushauri kuwa aongezwe Afisa wa NIDA  Nyasa ili shughuli ziende haraka

**e) TANESCO**

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji ya Taasisi ya TANESCO ya utendaji kazi kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo ilielezea shughuli zilizofanywa kwa ujumla awamu ya tatu mzunguko wa pili (REAL III Round).jimbo lina jumla ya vijiji 35 na ambavyo vimeshapata umeme ni vijiji 26 na ambavyo avijapata umeme ni vijiji 9 na hali iliyopo mpaka sasa katika vijiji 9ambavyo mkandarasi anaendelea na ukamilishaji vijiji 6 kashamaliza hatua za awali vinasubiliwa ukaguzi ili wateja waungwe na vijij na vijij 3 mkandalasi anaendelea na kazi (Pole election and strining ) Hadi sasa tumeunga jumla ya wateja 450 ambapo utekerezaji wa mradi kwa sasa ni sawa na asilimia 84 na gharama ya miradi inakadiliwa kufikia bilioni 8,799,229,136.98 TSH

Wajumbe walipokea taarifa, walijadili na kuiridhia

**f) TARURA**

Iliwasilishwa taarifa ya TARURA kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kueleza una mtandao wa barabara wa jumla ya kilometa 729.91 kati ya hizo kilometa 291.60 ni za mjazio Feeder Road) kilometa 375.83 ni za mkusanyo (Collector Roads) na kilometa 62.48 ni za jamii/kijiji (Community Roads)

**Hali ya barabara** kwa ujumla katika wilaya ya Nyasaimegawanyika katika makundi makuu matatu ambapo jumla kilometa 145.783 ni barabara za changarawe ,km 4.25 ni barabara za lami,km 579.877 ni barabara za udongo. Mtandao wa barabara wenye lami na changarawe hupitika kirahisi majira yote ya mwaka na Mtandao wa barabara za udongo hupitika kwa shidawakati wa mvua

Bajeti ya mwaka 2023/2024 katika mwaka wa fedha 2023/2024TARURA Wilaya ya nyasa imetengewa jumla ya Tsh 2949,020,300.00 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja kwa mchanganuo ufuatao kias cha Tsh 500,000,000/= za mfuko wa majimbo, kiasi cha Tsh 1,000,000,000 kutoka serikali kuu kupitia tozo za Mafutana Tsh 554,680,300 kutoka serikali kuu kupitia Wafadhili.

Wajumbe waliipokea taarifa waliijadili na waliiridhia

**g) TFS**

Iliwasilishwa taarifa ya wakala wa Mistu (TFS) ambayo iliezea utendaji wa kazi kwa mwaka 2022/2023 kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi wa misitu katika wilaya ya Nyasa kwa kutoa elimu kwa wanchi kuhusu utunzaji wa misitu kwa kuwaelezea Athari zinazoweza kujitokeza kutokana na shughuli za kibinamu mfano uchomaji wa mkaa,ukataji wa miti ovyo kwa shughuli za kilimo pamoja na uchomaji moto misitu.

wajumbe walipokea taarifa hiyo, walijadili na kuiridhia na wajumbe walisisitiza waendelea kuhamasisha watu kuhusu upandaji wa miti ili waweze kujikinga na mahafa ya upepo

h) **TAARIFA YA HIFADHI YA LIPARAMBA.**

Iliwasilishwa taarifa ya Hifadhi ya Liparamba wilaya ya Nyasa  Mkoa wa Ruvuma umejiwekea mikakati mbalimbali ya kuboresha maeneo ya vivutio vyake vya utalii.Mikakatui hiyo pamoja na kupandikiza aina ya wanyama pori walio kuwa kwenye hatari ya kutoweka katika maeneo ya hifadhi.   Mamlaka ya usimamizi wa wanyama poriTanzania (**TAWA**) Iliyopo chini ya Wizara ya Mali Asili na Utaliiimejipanga kufanya utafiti juu ya simba mweupe waliowahi kuonekana katika pori la akibaLiparamba lililopo Wilaya ya Nyasa. Baada ya utafiti huo zoezi la upandikizaji wa simba weupe utafanyika.Idadi ya Simba wawiliwatakuwa madume. Aidha simba hao wataboreshewa ulinzi ikiwa ni pamoja na kufungiwa mifumo ya ufuatiliaji wa tabia na mienendo yao (tracking device).

Kazi ya kupandikiza simba weupe itafanyika kwa ushilikiano wa **TAWA na** mashilika ya uhifadhi duniani **word wideFoundation (WWF) na Frankfut zoological society (FZS)**

Jitihada hizi zinalenga kuboresha shughuli za utalii mkoa wa Ruvuma hasa katika kuunga mkono juhudi za Mhe **Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr SAMIA SULUHU HASSAN** katika kampeni yake ya ya kukuza utalii ya "**TANZANIA THE ROYAL TOUR**".

**i) TAARIFA ZA TAASISI ZA KIBENKI**

NMB na CRDB  Ziliwasilishwa taarifa Za utendaji kazi wa taasisi za NMB na CRDB Benki kwa kushilikiana wa wananchi katika kuunga mkono jitihada mbalimbali za miradi ya maendeleo na kuwapatia mikopo ilkuweza kuinua hali ya uchumi wa kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla .

wajumbe walipokea taarifa, walijadili na kuiridhia

**j) TAKUKURU**

Iliwasilishwa taarifa ya Taasisi ya kuzuia na kupambana na  rushwa ambapo ilielezwa kuwa kwenye miradi ya maendeleo bado kuna mianya ya rushwa.pia kwenye eneo la ukusanyaji mapato na katika maeneo ya huduma.Hivyo alitoa rai watu wabadilike na wawe na uzalendo.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuiridhia.

**k) VETA**

Iliwasilishwa taarifa ya VETA ambapo Mkuu wa Chuo alieleza kuwa chuo kinatoa fani sita changamoto iliyopo katika Chuo ni miundombinu ya maji safi na maji taka

Wajumbe walipokea taarifa, waliijadili na walishauri kuwa RUWASA ishughulikie swala la maji pia walishauri kuwa zitolewe kozi fupi kwa mafundi wa mitaani ili waweze kuingia kwenye ushindani wa kazi mbalimbali zinazotolewa na serikali.

**l) TAARIFA YA KISIWA CHA LUNDO**

Iliwasilishwa taarifa ya kisiwa cha Lundo ambapo ilieleza kuwa ni sehemu nzuri ya kuvutia watalii na wajumbe walipokea taarifa na walitaka kujua maswala yafuatavyo; hali ya usafiri na hali ya usalama ambapo alitarifiwa kuwa usafiri upo ni mzuri na usalama upo. Kisha wajumbe walishauri TAWA wajitaidi kuweka mitumbwi kwa ajili ya kuwasafirishia watalii pia pawepo na dawati la utalii.

**NDC/DCC/2023-2024/07:TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI YA MWAKA 2022/202 NA 2023/2024.**

Iliwasilishwa taaarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo ilielezwa Halmashauri ya wilaya ya Nyasa ilikisia kukusanya jumla ya Tsh **1,361,264,000.00** kuanzia tarehe 01 julai 2022 hadi tarehe 30 juni 2023 hadi kufikia tarehe 30 juni 2023 Halmashauri imekusanya **Tsh 1,327,410,997.55** sawa na asilimia 97.51 ya makusanyo yote

Aidha kwa mwaka wa fedha huohuo 2022/2023 hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2022 Halmashauri iliweza kukusanya jumla ya **Tsh 622,533,070,85** sawa na asilimia 45.73 ya makusanyo yote

Pia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya wilaya ya Nyasa ilikisia kukusanya **Tsh 1,444,005,000.00** kuanzia tarehe 01 julai 2023 hadi tarehe 30 juni 2024.Hadi kufikia tarehe 31Desemba 2023 Halmashauri imekusanya jumla ya Tsh **1,140,919,479.26** sawa na asilimia 79.01 ya makusanyo yote.

Wajumbe waliipokea taarifa waliijadili nakuiridhia

**NDC/DCC/2022-2023/008 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwa na mengineyo iliyowalishwa kwa mwenyekiti.

**NDC/DCC/2022-2023/009 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuwa makini kuchangia hoja katika kikao

Mwenyekiti alifunga kikao 12:15 Jioni

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA YA NYASA (DCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 23/01/2024 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA HALMASHAURI YA WILAYA NYASA**

| AGENDA NA | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | HATUA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **NDC/DCC/2023-2024/006** | Kuhusu kuwa na Mwongozo wa chakulaambao ni sare kwa shule zote | Iliagizwa mwongozo wa chakula ambao ulitolewa na kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya usambazwe kwa shule zote.Hivyo Mkurugenzi Mtendaji Wilaya awaandikie barua Watendaji wa kata kuwajulisha watoe taarifa katika maeneo yao. | **DED** | |
| **NDC/DCC/2023-2024/006** | Kuhusu kupeleka Shule watoto wote walioandiokishwa shule na waliofaulu kujiunga kidato cha Kwanza | Wazazi wote wasiopeleka watoto shule wakamatwe na kufikishwa Mahakamani | **DED** | |
| **NDC/DCC/2023-2024/006** | Kuhusu Taasisi zote kupatiwa Umeme | Il<br><br>Kuhakikisha Taasisi zote zinapatiwa umeme | **MENEJA WA TANESCO** | |